

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Tatu – Tarehe 8 Septemba, 2016**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwakaribishe kwenye kikao chetu cha tatu cha Mkutano wa Nne leo tarehe 8 Septemba. Katibu!

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri Mkuu karibu. *(Makofi)*

Kama ilivyo ada endapo kiongozi wa upinzani ana swali tunampa kipaumbele cha kwanza. Mheshimiwa Freeman Mbowe.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza ya kumuuliza Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Spika, kwa hali ilivyo nchini sasa hivi kiuchumi, kuna mdororo mkubwa wa uchumi, na katika mdororo huu wa uchumi ambao tuna imani kabisa katika hatua za baadaye utaathiri bajeti ya Serikali, wawekezaji wengi wanasita kuwekeza katika nchi kwa sababu ya kutokuwa na uhakika kuwa Tanzania ya kesho itakuwaje. Kuna kuporomoka sana kwa *deposits* ama amana zinazowekwa katika benki zetu za biashara, mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam, mizigo katika Bandari ya Tanga, mizigo katika *border posts* za Namanga, Sirari, Horohoro na Tunduma imepungua kwa zaidi ya asilimia 60.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, baadhi ya makampuni ya usafirishaji kwa zaidi ya asilimia 40 yamefunga kazi zao au vyombo vyao vya usafirishaji, kwa maana ya malori makubwa yamesitisha safari na makampuni mengine yamehamia nchi nyingine za jirani kwa sababu ya kutokuwa na uhakika wa hali ya ndani.

Je, hali hiyo kama Serikali mnaijua? Na kama mnaijua mnachukua hatua gani za makusudi za kurekebisha hasa ikizingatiwa kwamba uchumi unapoporomoka, kama ilivyo Tanzania leo mazao ya wakulima kama mbaazi, nafaka, mpunga nao unaanguka bei na tayari umeshaanguka bei kwa kiwango kikubwa?

Mheshimiwa Waziri Mkuu, mna mkakati gani wa makusudi wa kurekebisha hali hii? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze leo kwa kujibu swali la Mheshimiwa Mbowe, Mbunge na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwa swali lake muhimu kwa sababu linagusa hali ya uchumi ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumia hali ya uchumi tunazingatia mambo mengi na nikiri kwamba maeneo yote uliyoyatamka ni sehemu kubwa ya mchango wa hali ya uchumi nchini. Na kwa kutambua kwamba uchumi unashuka, inabidi tufanye tathmini ya kutosha, ingawa maeneo uliyoyatamka kwamba yamepungua sana nayo pia kuna haja ya kujiridhisha na kupata takwimu sahihi za miaka iliyopita na hali tuliyonayo sasa ili tujue kama je, kiwango cha kushuka kimesababishwa na nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali haitaweza kulala, malengo ya Serikali wakati wote ni kuhakikisha kwamba uchumi wa nchi unaongezeka. Moja ya jitihada za Serikali ya Awamu ya Tano ni kuhakikisha kwamba uchumi unakua kupitia nyanja zote pamoja na maeneo uliyoyatamka. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kupungua kwa mizigo bandarini kumekuwa kunazungumzwa na watu wengi na juzi juzi Kamati yetu ya Bunge ya Viwanda na Biashara ilikuwa bandarani kupitia hayo na wamekaa na wadau. Lakini wadau peke yao hawatoshi, ni lazima tupate pia taarifa kutoka ndani ya Serikali na mwenendo wa uendeshaji wa bandari, mipaka yetu, lakini pia mazao yetu ndani ya nchi na mwenendo wake mzima. *(Makofi)*

Kwa hiyo, niseme kwa sasa kukupa takwimu halisi za kuporomoka au kutoporomoka si rahisi sana, lakini nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwamba Serikali itafanya jitihada wakati wote kuhakikisha kwamba uchumi wake unapanda. Serikali itakubali kukutana na wadau kuzungumzia hatma ya uchumi nchini, Serikali itapokea ushauri kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge kwa namna ambavyo wanaona kwamba kuna

udhaifu mahali ili tuweze kuhakikisha kwamba uchumi unaongezeka na pia bajeti ya mwakani inapata mafanikio makubwa ukilinganisha na bajeti ambayo tunaitekeleza sasa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo basi bado nirudie kukuhakikishia kwamba Serikali haitalala katika hili kuhakikisha kwamba uchumi wa nchi unapanda na kwa hiyo, kama changamoto ya maeneo ambayo umeyatamka tutafanya mawasiliano na Wizara ya Fedha lakini pia na Benki Kuu ili tuweze kupata takwimu halisi za hali ya uchumi nchini na tutakuja kulijulisha Bunge letu ili Wabunge wajue na wapate nafasi ya kutushauri. Kamati yetu ya Kudumu ya Biashara na Viwanda ipo, bado ina nafasi nzuri ya kuweza kutushauri kama Serikali. Ahsante sana. (Makofi)

**SPIKA:** Swali la nyongeza Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Mbowe.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, haihitaji utafiti wa ziada kujua uchumi umeshuka. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini tunatambua kwamba Benki Kuu ndiyo taasisi muhimu katika Taifa ambayo mara kwa mara kila baada miezi mitatu ina-*release data* fulani fulani kuonesha hali ya uchumi katika Taifa, na tayari hali ya uchumi katika Taifa imeshaelezwa kwenye Ripoti ya Benki Kuu ambayo inatoka *quarterly*, kila baada ya miezi mitatu kwamba kuna kushuka kwa hali ya juu katika *importation*, kuna kushuka katika *exportation*, kuna kushuka katika *construction industry*, kuna kushuka katika *circulation* ya fedha. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu hivi majuzi tulimsikia Mheshimiwa Rais akisema kwamba watu wanaweka fedha nyumbani, wanahifadhi fedha na ndiyo sababu mzunguko wa fedha umepungua katika *circulation*, kitu ambacho mimi binafsi naamini si kweli, na sijui vyanzo vya Mheshimiwa Rais ni nini kama Serikali ilikuwa haijafanya utafiti wa kina kujua kweli hali hiyo ipo.

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kamati ya Bunge ya Biashara na Uwekezaji ilikwenda Bandarini na ilitoa ripoti ambayo ni dhahiri, ni Kamati ya Bunge imedhihirisha hilo. Hao wadau mnaosema mtawashirikisha tayari wanalalamika. TATOA wanalalamika kuhusu mizigo yao, mahoteli yanafungwa, makampuni yanafungwa, watalii wamepungua, utafiti gani bado mnahitaji mjue kwamba uchumi umeanguka? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nilitegemea leo Waziri Mkuu ujue kabisa waziwazi kwamba uchumi unaanguka na uchumi umeanguka na utueleze *measures* ambazo mnachukua kurekebisha hali hii. Lakini *it seems like the government*

haina uhakika ni nini kinaendelea. Waziri Mkuu unaonaje katika mazingira hayo, mka-declare kwamba mmeshindwa kuendesha Serikali hii? (Makofi)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbowe, Mbunge na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni kwa kuanza kusema kwamba Serikali hii haijashindwa kuongoza nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote, tutaongoza nchi hii kwa mafanikio makubwa sana kwenye sekta zote. Kazi hiyo imeanza kwa kufanya marekebisho makubwa ya maeneo ambayo tunadhani yatafanya Taifa hili liweze kupata mafanikio makubwa vilevile. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani umeeleza hasa juu ya bandari. Kwanza nieleze kwamba Serikali imekuwa ikifanya mawasiliano na mataifa mengine yanayoendesha shughuli za bandari. Mwezi mmoja uliopita nilipokea timu ya wafanyabiashara maarufu duniani kutoka Singapore akiwemo mfanyabiashara anayefanya biashara za meli duniani. Alinieleza kwamba suala la mdororo wa usafirishaji wa mizigo kwa njia ya meli imeshuka duniani kote.

Mheshimiwa Spika, suala la kupungua kwa mizigo maeneo yote ni kwa sababu ya hali ya kiuchumi duniani iliyotokana na kuporomoka kwa bei ya gesi na mafuta duniani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ukanda huu wa kwetu wa Afrika Mashariki ambako bandari yetu inatumika sana, nataka nikuhakikishie, Tanzania kupitia bandari zetu tunategemea sana mizigo kutoka Congo, Rwanda, Burundi kidogo lakini pia na Zambia; na wote mnajua kwamba Congo na Zambia ni nchi ambazo zilikuwa zinaelekea kwenye uchaguzi na kulikuwa na migongano mingi ndani ya nchi na wafanyabiashara wengi walisimama kidogo kufanya biashara zao; na hiyo ikasababisha kupungua hata kwa kiasi cha mizigo. Sio tu kwa Bandari ya Dar es Salaam pia hata usafirishaji kwenda kwenye bandari nyingine kutoka kwenye nchi hizo ambazo nimezitaja. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini nataka nikupe faraja kwamba wiki moja iliyopita tumepata barua kutoka kwa timu ya wafanyabiashara wa Congo. Kutokana na hali iliyokuwepo awali na *stabilization* iliyopo sasa wametuhakikishia kwamba sasa usafirishaji wa mizigo yao yote utafanyika kupitia Bandari ya Dar es Salaam. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Rwanda wametuandikia barua kutuhakikishia kwamba kutokana na mdororo uliokuwepo awali wafanyabiashara wengine kuamua kupeleka maeneo mengine kwa sababu ya hali ya kiuchumi lakini sasa

wameamua mizigo yote itapitia Bandari ya Dar es Salaam, hasa kwa mkakati wetu wa pamoja wa ujenzi wa reli ya *standard gauge* inayotoka Dar es Salaam - Tabora mpaka Bandari kavu ya Isaka, lakini tunaunganisha pia na reli hiyo *standard gauge* kwenda nchini Rwanda na kwa hiyo jitihada za kusafirisha mizigo sasa zitaimarishwa ili kuleta motisha ya ujenzi wa reli hiyo ili iendelee kusafirisha mizigo hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge nataka nikuhakikishie, ni kwamba haya yote uliyoyaeleza kama kuna jambo ambalo tunahitaji kukaa pamoja ni jambo la uchumi na hili ni jambo endelevu na nataka nikuhakikishie kwamba tutalifanyia kazi kwa kiasi kikubwa ili sasa tujiridhishe kila eneo na yale ambayo yanatakiwa na kama kufanya kampeni zaidi ya kupata wafanyabiashara zaidi, Serikali itafanya hilo kwa lengo lile lile la kuhakikisha kwamba uchumi wa nchi yetu hauporomoki na wala hauwezi kuathiri mahusiano na nchi nyingine. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hiyo ndiyo *commitment* ambayo naweza kukupatia kwa ajii ya maeneo haya. (Makofi)

**SPIKA:** Mnaofuata sasa naomba muulize kifupi na kama si lazima usiulize swali la nyongeza ili na mwenzako aweze kupata nafasi. Nianze kumchukua Mbunge kutoka Visiwani CCM, Mheshimiwa Jaku Hashimu Ayoub.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika ahsante sana. Nami nikushukuru na vilevile nikutakie afya njema na kila zito Mwenyezi Mungu afanye jepesi kwa upande wako.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali hii isingekuweko madarakani bila kuwepo wananchi na wananchi ndiyo Serikali na Serikali ni wananchi, hata Mheshimiwa Waziri Mkuu wewe mwenyewe bila kuwepo wananchi usingepata Uwaziri Mkuu hata Mheshimiwa Rais pamoja na sisi Waheshimiwa Wabunge wote humu ndani.

Mheshimiwa Spika, swali, afya huwezi kupata bila kupata chakula, mwanzo upate chakula ili upate afya. Hivi sasa kumekuwa na harufu inaweza ikawa nzuri au ni mbaya.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na upungufu wa chakula ikiwemo bidhaa muhimu ya sukari, na sijui kama Serikali mmefanya utafiti gani kuliangalia suala hili. Msemo wa Waswahili husema, usipojenga ufa, hutajenga ukuta. Mmechukua jitihada gani kama Serikali kuangalia hali ya sukari na mchele ilivyo sasa? Na wanaoumia ni wananchi na ukizingatia kesho kutwa tuna sikukuu na inahitaji sukari kwa kiasi kikubwa. (Makofi)

Je, kuna harufu Serikali imeagiza sukari. Ni kweli suala hilo kwa ajili ya kuwajali wananchi wake?

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, nadhani umeeleweka. Tukienda na mswali mafupi tutapata nafasi wengi zaidi. Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jaku, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ameeleza maneno mengi lakini muhimu ni kwamba kuna harufu ya upungufu wa bidhaa ya sukari nchini. Ni kweli huko nyuma tulikuwa na tatizo la sukari nchini kote na Serikali ikafanya jitihada ya kutambua mahitaji ya nchi, na yale mapungufu tuliyafanyia kazi kwa kuagiza sukari nje ya nchi na kuleta ndani kwa kiwango ambacho hakitaathiri uzalishaji wa ndani ili tuweze kuendelea kutoa huduma hiyo. Tumeendelea kufanya hilo mpaka pale ambapo tumeridhika kwamba viwanda vyetu vya ndani vimeanza kuzalisha na kuona uzalishaji ule na sukari ambayo tumeingiza vinaweza kutufikisha tena msimu ujao wa uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, suala la sukari hatujaishia tu kuwa na maazimio ya kuagiza toka nje. Mkakati mkubwa tuliofanya ni kuhakikisha tunaimarisha viwanda vya ndani viweze kuzalisha. Tumekutana na wazalishaji wote wa sukari, TPC, Kilombero, Kagera pamoja na Mtibwa kupata picha ya uzalishaji kwenye viwanda vyao na mkakati walionao kuendeleza uzalishaji. Lakini bado tumegundua kwamba viwanda vyetu havitakuwa na uwezo kwa kipindi cha miaka minne ijayo kuzalisha sukari ikatosheleza nchini. Lakini pia kumekuwa na wasiwasi wa takwimu za mahitaji ya sukari nchini kwa sababu nchi jirani ya Kenya yenye watu milioni 45 mahitaji ya sukari ni tani 800,000, lakini tathmini ya Idara yetu ya Kilimo nchini kwa Tanzania yenye watu zaidi ya milioni 45 ile ile wanatuambia takwimu zile zinahitaji tani 420,000; kwa hiyo utaona tuna upungufu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, tulichokifanya; kwanza tumeagiza Wizara ya Kilimo ifanye utafiti wa kina kuona mahitaji ya sukari nchini, lakini pili kutokana na maelezo tuliyopata kutoka kwa viwanda tumewapa maelekezo ya kuzalisha zaidi ili tuongeze sukari, na tumekubaliana hilo. Tatu, tumeamua kuwekeza kwenye ujenzi wa viwanda na uhamasishaji wa kilimo cha miwa ili tuweze kuzalisha sukari inayoweza kutosheleza mahitaji ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tayari tumeshapata wawekezaji walioonesha nia ya kuwekeza kwenye ulimaji wa miwa pamoja na uzalishaji wa sukari nchini ili na sisi tufikie kiwango ambacho kitakwenda kutambulika baada ya Wizara ya Kilimo kufanya sensa yake. Lakini wakati wote huu Serikali itahakikisha kwamba nchi haikosi sukari na wananchi wanaweza kupata kinywaji ambacho kinahitaji

sukari, uendeshaji wa sukari kwenye viwanda kwa ajili ya kuzalisha mazao yanayohitaji sukari ili tuweze kuhakikisha kwamba biashara hii na zao hili linatosheleza kwa matumizi ya ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia Mheshimiwa Jaku ametaka kuzungumzia upungufu wa chakula na jana Mheshimiwa Keissy aliomba Mwongozo wa kutaka maelezo ya hali ya chakula nchini na bado Serikali tumeahidi kutoa taarifa hapa Bungeni kabla ya mwisho wa wiki hii ya hali ya chakula nchini na mkakati wa taifa kama kuna upungufu huo wa kiasi hicho ili sasa kila mmoja wetu nchini aelewe nafasi tuliyonayo ili tuweze kushirikiana kwa pamoja kuondoa tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo taarifa ambayo itatolewa na Wizara ya Kilimo juu ya hali ya chakula ikiwemo na zao la sukari inaweza kusheheneza mahitaji ya uelewa kwenye eneo hili ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jaku sina hakika kama kuna haja ya swali la nyongeza, kwa sababu taarifa itakuja ni vizuri tukawa na uvumilivu tupate hiyo taarifa kwanza lakini sitaki kukunyima nafasi, hebu tulisikie hilo swali la nyongeza kama lipo.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi niendeleo kumshukuru Waziri Mkuu kwa umakini wake wa hali ya juu kujibu suala hili nililomuuliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu hii imekuwa kama miongo ya mvua za masika. Ni sababu gani hasa Serikali kuwa haijajipanga kuonekana tatizo hili likafika pahala likamaliza kabisa suala la sukari?

Baada ya miezi mitatu, sita atakuja kiongozi mwingine atasahau kuhusu suala hili, kwa hiyo, Serikali ikajipange na suala hili, wananchi ndio muhimu na mlikuwa mkipiga kelele kuwa mtawajali wananchi, Serikali haiogopi hasara kwa ajili ya wananchi wake ni hilo tu Mheshimiwa.

**SPIKA:** Mimi naona kilichotolewa ni ushauri tu, lakini kwamba haijajipanga tusbiri ripoti ni ushauri tu. Tunaendelea Mheshimiwa Riziki Said Lulida. Niko upande wa Chama cha CUF sasa.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu swali langu linahusu suala la zao la korosho.

Mheshimiwa Spika, Serikali hivi karibuni ilifanya maamuzi mazuri ya kuhakikisha wakulima wa korosho wanaondolewa tozo na kero kubwa ambazo zilikuwa zinawasumbua kwa muda mrefu na hizo tozo tano zilitolewa maamuzi



ambayo mpaka sasa hivi hajatoa tamko zuri ambalo litawafanya wananchi wale waweze kufarijika na hilo suala.

Swali langu Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama mdau wa korosho na sisi wengine ambao ni wadau wa korosho, na mikoa mingine ya Tanzania nzima ambao ni wadau wa korosho wanataka wapate tamko lako la kuhusu suala la korosho.

Je, katika msimu huu wa korosho utaweza kusimamia na kuhakikisha zile tozo tano zinafutwa ili wananchi wafarijike? Ukizingatia kwamba hali ya sasa hivi ni mbaya, mazao ya mbaazi yako majumbani, ufuta uko majumbani, kunde ziko majumbani, njugu mawe ziko majumbani, njegere ziko majumbani, choroko ziko majumbani? Mwenyezi Mungu akikujalia kusimamia na kutupa tamko lako hapa ndani ya Bunge utawafariji Watanzania. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lulida, Mbunge na mdau wa korosho kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba zao hili la korosho limekuwa na matatizo mengi hasa kwenye masoko kufuatia mfumo unaotumika wa kuuzia zao hili wa Stabadhi za Mazao Ghalani. Lakini pia zao hili linaendeshwa kwa mfumo wa ushirika ambao una viongozi kutoka ngazi za vijiji, Chama Kikuu cha AMCOS na badaye kuundiwa Bodi.

Mheshimiwa Spika, zao la korosho lilikuwa na tozo zake za kisheria lakini pia wanaushirika waliongeza tozo nyingine nyingi za hovyoy, na mimi ndiye niliyetamka kusimamia mazao yetu ya biashara kote nchini kuhakikisha kwamba tunafanya mapitio ya kina na kwamba tunaondoa makato ya hovyoy hovyoy yaliyoingizwa tu na wanaushirika kwa maslahi yao na hatimaye kupelekea wananchi wanaolima mazao haya kukata tamaa kuendelea na uzalishaji wa zao husika likiwemo zao la korosho.

Mheshimiwa Spika, Serikali baada ya kutoa tamko jukumu letu sasa ni kusimamia na tumeshatoa maelekezo kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na viongozi wa ushirika, lakini pia hata viongozi wa taasisi yenyewe Bodi ya Korosho kuhakikisha kwamba wanasimamia maelekezo ya Serikali ya kuondoa zile tozo.

Mheshimiwa Spika, zao hili baada ya kuwa tumetoa maelekezo wajibu wa Serikali sasa ni kuhakikisha kwamba yale tuliyoyaagiza yakiwemo na yafuatayo yanaweza kukamilishwa:-

(i) Tunataka zao hili linapokusanywa na kupelekwa kwenye maghala, maghala yote ya vijijini lazima sasa yatumike kuhifadhi korosho hizo badala ya



kupeleka kwenye ghala kuu ambayo yalikuwa yanatengenezewa ushuru, huku wakulima wenyewe wakiwa wameshajijengea maghala yao; na kwa hiyo kila maeneo ya Wilaya watabaini maghala ambayo yatatunza korosho hizo ili kuwapunguzia tozo ya gharama ya ghala kwenye maghala makuu.

(ii) Kumekuwa na minada inayopelekwa makao makuu ya mkoa pekee, na kuwanyima wananchi kusimamia na kuona mwenendo wa minada. Tumeagiza kuanzia sasa minada yote itafanywa kwenye ngazi ya Wilaya ili wananchi waende kushuhudia minada hiyo. *(Makofi)*

(iii) Kulikuwa na wanunuzi wanaoenda kwenye minada wakiwa hawana fedha. Sasa ili kujihakikishia kwamba mnunuzi ananunua na analipa lazima aweke dhamana ya kiwango cha fedha benki ambacho bodi itaamua, ili tuwe na uhakika kwamba anayekuja kuweka zabuni ya kununua zao la korosho ana fedha za kulipia; kwa sababu tumegundua watu wanakuja kutafuta zabuni hawana fedha halafu wanakimbia.

Kwa hiyo, Serikali itaendelea kusimamia haya kuhakikisha kwamba mkulima anapata fedha yake kwa kipindi kifupi sana baada ya mnada na mnunuzi awe na fedha na fedha ikishatolewa inaingizwa kwenye akaunti ya benki halafu wakulima waweze kupelekewa mahali walipo.

Kwa hiyo, hiyo ndizo jitihada ambazo Serikali itahakikisha kwamba yale maelekezo yanasimamiwa na tutashuhudia kwamba yanatekelezwa vizuri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana tunaendelea na swali linalofuata sasa nahamia CHADEMA. Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Mheshimiwa Waziri Mkuu, utaratibu wa kibajeti unaanzia kwenye Serikali za vijiji mpaka inamalizikia Bungeni ndio tunapitisha bajeti ya Serikali. Lakini mpaka hapa ninapoongea kuanzia mwaka 2014 kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kuna vijiji vitatu vilisimamishwa na Ofisi ya TAMISEMI visifanye uchaguzi ingawaje vilishatangazwa kuwa vijiji. Vijiji hivyo viko katika kata ya Mofu ambapo ni Miomboni, lakini Kata ya Namohala ni Idandu na Chiwachiwa. Lakini kwa maelezo ya Serikali kwamba yale maeneo ni ya uwekezaji kwa hiyo hakuna uchaguzi wa vijiji utakaofanyika.

Je, Waziri Mkuu nini kauli ya Serikali kuhusu hatma ya vijiji hivyo na wananchi katika hilo Jimbo la Mlimba na kata na vijiji nilivyovitaja? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Susan unategemea Waziri Mkuu avijue hivyo vijiji Mlimba huko? Eeh si ungesubiri siku ya kawaida umuulize labda Mheshimiwa

Simbachawene. Mheshimiwa Waziri Mkuu labda una cha kusema kuhusu hilo, nikuruhusu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Susan Kiwanga kwa eneo lile la kisera zaidi badala ya kujikita kwenye ngazi za vijiji na hasa alipokuja kutamka kwamba kuna mwelekeo wa kibajeti kwenye ngazi za vijiji mpaka Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mchakato wa bajeti huanza kwenye ngazi za vijiji inaenda kwenye Kata, Wilaya na hatimaye Mkoa na baadaye unakuja kwenye Wizara. Hii inatoa nafasi kwa kila eneo kutengeneza mpango wake wa matumizi ya kifedha ili kuboresha masuala mbalimbali yakiwemo na mambo ya maendeleo. Na kama lipo tatizo ndani ya Halmashauri ya Wilaya linalogusa vijiji na wamekosa nafasi ya kuweka bajeti zao ngazi ya juu inawajibika kuweka bajeti ya maeneo hayo ambayo hayajapewa uongozi unaosimamia utengenezaji wa bajeti kwenye eneo hilo ili na wao waweze kupata huduma.

Mheshimiwa Spika, na kwa hiyo basi kama vijiji vile vitatu havijapata nafasi ya kuunda uongozi utakaoweka bajeti ya maendeleo yao ngazi ya kata ambako kuna Diwani ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Kata ndiye atakayewajibika kuviingiza vijiji vile kuvitengenezea bajeti kwenye kata yake na diwani atabeba kupeleka kwenye Halmashauri ya Wilaya na atalazimika kuviingiza kwenye mpango wa bajeti wa Halmashauri ya Wilaya vijiji hivyo ili wananchi wa maeneo hayo waweze kupata huduma. Hata kama vijiji hivyo havijapewa nafasi kwa sababu tu eneo hilo ni la uwekezaji. Bado Serikali inatambua kuna wananchi pale na ni lazima wahudumiwe kwa hiyo bajeti lazima pia ioneshe kwamba wananchi wale watahudumiwa kadri wanavyokwenda mpaka hapo jambo hilo litakapopata utatuzi wake.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge mchakato wa kibajeti unahusisha Watanzania wote, hata kama kwenye maeneo hayo kuna upungufu wa viongozi waliopo wanayo dhamana ya kutengeneza bajeti. Kwa hiyo basi, Wizara ya TAMISEMI na bajeti yao yote ya nchi nzima lazima vijiji hivyo viweze kushughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini suala la mgogoro wa vijiji hivyo sasa, na Waziri mwenye dhamana yuko hapa atakuwa ameshachukua jambo hilo na atawajibika sasa kufuatilia kule Ifakara na aweze kukupa jibu katika kipindi hiki cha Bunge ili utakaporudi nyumbani uwe na majibu ya hatma ya vijiji hivyo na uwekezaji uliopo maeneo hayo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Swali la mwisho la leo Mheshimiwa Hillary Ngonyani.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kumeendelea kuwa na mauaji ya mara kwa mara katika nchi yetu hasa askari pamoja na wananchi wa kawaida, hasa katika mikoa ya Mwanza, Tanga, Vikindu, je, Serikali inatoa kauli gani kuhusiana na vitendo hivi vinavyosababisha mauaji makubwa kwa wananchi wasiokuwa na makosa yoyote?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mbunge wa Korogwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upo ukweli kwamba hapa karibuni tumepata matukio mengi ya mauaji ya raia, lakini pia hata askari wetu nao wameuawa katika mfululizo wa matukio hayo hayo kwenye maeneo ya Tanga, Mwanza na hivi karibuni pale Vikindu.

Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii kwanza kutoa pole kwa wananchi wote ambao ndugu zao wamepoteza maisha kupitia mauaji hayo yaliyotokea kwenye maeneo haya yote. Lakini pili, ningependa niwahakikishie Watanzania kwamba Serikali imesikitishwa sana na jambo hili ambalo linaonekana kuna Watanzania wachache wasingependa maisha ya wenzao yaendeleo na kuamua kukatiza kwa njia ya mauaji ambayo Serikali haijaridhishwa, na Watanzania wengi wamepata uoga katika hili kwamba linaweza kuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, nataka niwatoe wasiwasi huo Watanzania kwamba Serikali iko macho, na imeendelea kuwasaka wale wote waliohusika kwenye mauaji haya, na tutahakikisha tutawakamata wote popote walipo ili tuwatie mikononi na hatimaye mkondo wa kisheria uweze kuchukua nafasi yake.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo hili kwa masikitiko ambayo nimeyaeleza napenda tuwahakikishie Watanzania kwamba vyombo vya dola viko macho, na tutaimarisha ulinzi maeneo yote, kutoka ngazi ya vitongoji na maeneo yote ambayo wananchi wanavyokuwa wanaishi na wanahitaji amani ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili niombe wananchi wote washirikiane sana na vyombo vya dola katika kuhakikisha kwamba kwenye maeneo yetu kama kuna jambo ambalo tunalitia mashaka, kama kuna mtu ambaye tunamtilia mashaka tushirikiane na vyombo vya dola kuvipa taarifa ili vyombo vya dola viweze kuchukua tahadhari kabla ya mauaji hayo hajawahi kujitokeza.

Kwa hiyo, kauli ya Serikali katika hili ni kuhakikisha Watanzania kwamba usalama wa nchi hii utaendela kwa kuhakikisha kwamba tunathibiti matukio matukio yote ya hovyoyanayopelekea wananchi kusitisha maisha yao kama ambavyo imetokea kwa askari, lakini pia kwa wananchi wetu ambao wametangulia mbele za haki kwa matukio haya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo bado nirudie kwamba Serikali itaongeza ulinzi katika nchi yetu kwenye maeneo yote, na ndio hiyo ambayo tulikuwa tunaijadili hapa juzi kuona kwamba tumeimarisha ulinzi zaidi; polisi wako wengi wanaangalia usalama katika nchi hii unaendelea. Kwa hiyo, naomba niwahakikishie kwamba nchi itaendelea kuwa salama na wale wote waliohusika katika matukio haya tutaendelea kuwasaka ili kuhakikisha tunawapata na kuwachukulia hatua. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakushukuru sana, muda wa nusu saa umeshapita ahsante sana kwa majibu ya ufasaha, niwaombe radhi wale Wabunge walitegemea wapate nafasi ya kuuliza maswali maana mlikuwa 15 na tumepata nafasi ya Wabunge watano tu, lakini *at least* tumekuwa na uwakilishi kutokana na vyama vyetu kama tulivyo humu Bungeni. *(Makofi)*

Katibu tuendeleee.

#### **NDG. ASIA MINJA - KATIBU MEZANI:**

#### **MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Maswali ya kawaida, tunaanza na swali kwa Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, swali linaulizwa na Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mbunge wa Wete.

Na. 31

#### **Tatizo la Dawa za Kulevya Nchini**

**MHE. MBAROUK SALUM ALI** aliuliza:-

Pamoja na sheria kali ya udhibiti na usimamizi wa dawa za kulevya, bado biashara hiyo ni tatizo kubwa kwa Tanzania.

Je, nini mkakati mahususi wa Serikali wa kupambana na kadhia hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mbunge wa Wete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa dhamira ya dhati, inaendelea kuhakikisha kuwa inafanya udhibiti wa kutosha wa kupambana na kadhia ya dawa za kulevya nchini.

Mheshimiwa Spika, ili dhamira ya Serikali ya kudhibiti dawa za kulevya nchini itimie serikali kupitia Sheria Namba Tano ya mwaka 2015 imeanza kutekeleza maeneo yafuatayo ya kimkakati katika vita ya dawa za kulevya nchini:-

(i) Kukamilisha muundo mpya wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ili kuongeza nguvu ya kisheria ya kuchunguza, kupeleleza na kukamata watuhumiwa wa dawa za kulevya.

(ii) Kupunguza urasimu katika utendaji kwa kuwa na watendaji wa mamlaka wanaoshiriki moja kwa moja katika kutekeleza majukumu yao.

(iii) Kuharakisha kesi za dawa za kulevya kwa kuongeza nguvu katika maeneo ya uchunguzi, upelelezi na ukamataji.

(iv) Kuongeza nguvu katika huduma za matibabu na utengamao pamoja na kuzuia matumizi haramu ya dawa za kulevya, maabara na vifaa vya kuzalisha dawa za kulevya nchini.

Mheshimiwa Spika, nilihakikishie Bunge lako tukufu kwamba baada ya kuanza kutumika kwa Sheria Namba Tano ya mwaka 2015, shughuli za udhibiti wa dawa za kulevya nchini zitasimamiwa vyema na Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mbunge wa Wete kama una swali la nyongeza.

**MHE. MBAROUK SALIM ALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini pamoja na majibu hayo nina maswali tena mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza katika awamu iliyopita kulikuwa na watu mashuhuri ambao walijilabu kwamba wanawajua watu ambao wanajishughulisha na biashara za dawa za kulevya. Je, Serikali inaonaje kuwaona watu hao au vingozi hao na kuwasihi ili wawapatie majina hayo ili Serikali ipate pa kuanzia?  
(Makofi)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, dawa za kulevya zinapiga vikali katika mishipa ya *riyakh*, na inaathiri sana nguvu za vijana ambao kwa kweli baada ya miaka 10, 15 nchi hii inaweza ikawa na mazezeta watupu. Sasa pamoja na Serikali kusema kwamba inabadilisha au ina muundo mpya wa mamlaka ya kudhibiti dawa za kulevya.

Je, Naibu Waziri anatuambiaje katika mamlaka hiyo mpya au katika mabadiliko hayo mapya kuna nini ambacho kinaweza kikakuhakikishia kwamba hali hii inapungua kwa kiasi kikubwa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, kwa kipengele cha kwanza kuhusiana na watu waliotoa taarifa kwamba wanawafahamu watu wanaojihusisha na dawa za kulevya, niseme tu kwamba Serikali iko tayari kushirikiana na mtu yeyote yule mwenye taraifa zinazohusu au zinaweza kupelekea kukamatwa kwa wafanyabiashara wa dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, japo sijalielewa vizuri niseme kwamba baada ya kupitishwa kwa sheria mpya ya mwaka 2015 kama nilivyoeleza awali Serikali itakuwa imepata nguvu katika maeneo yote ya kuchunguza kukamata na kuthibiti dawa za kulevya ikiwemo pia kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuhakikisha kwamba biashara ya dawa za kulevya inathibitiwa.

Mheshimiwa Spika, na jambo moja tu la uangalifu katika lugha hizi, watu wanaopata magonjwa ya akili kutokana na dawa za kulevya hatuwaiti mazezeta.

Mheshimiwa Spika, naomba Waheshimiwa Wabunge tuwe *very sensitive* katika lugha tunayotumia dhidi ya wagonjwa au watu wenye aina mojawapo au nyingine ya ulemavu. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ungetusaidia ili Taifa liweze kujua vizuri. Jina halisi la watu wenye matatizo hayo uliyoyaeleza ni jina gani Mheshimiwa Waziri?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, inategemea na viwango, kuna wahanga au warahibu, kuna wagonjwa wa akili wa kawaida, lakini maneno kama mateja au mazezeta ni maneno ya unyanyapaa yaani *stereo type*. (*Makofi*).

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunakushukuru sana kwa kutusaidia.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda tunaomba tuendelee na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa – TAMISEMI. Swali la Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 32

### **Unyanyasaji wa Mama Lishe na Wauzaji wa Bidhaa Wadogo Mjini**

**MHE. ZAYNABU M. VULU** aliuliza:-

Zaidi ya asilimia 30 ya wakazi wa mijini hupata chakula chao cha asubuhi, mchana na jioni kwa mama lishe, lakini mama lishe hao wananyanyaswa sana na askari wa mgambo wa majiji na miji kote nchini.

Je, kwa nini Serikali isiandae mazingira mazuri na masafi ya kufanyia kazi zao na wao wakatozwa ushuru mdogo kuliko hali ya kuendelea kuwanyanyasa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la Mheshimiwa Vulu na linajibiwa na Mheshimiwa kaka yake, wote wanatoka Kisarawe hawa. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vulu, mama yangu huyu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa wafanyabisahara wadogo walioko katika sekta isiyo rasmi katika kukuza kipato na ajira. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Halmashauri zote zimeagizwa kuhakikisha zinatenga maeneo kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo wadogo wakiwemo mama lishe karibu na maeneo walipo wateja wao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu askari mgambo wanaonyanyasa mama lishe, jambo hili halikubaliki pia ni kinyume cha Sheria ya Polisi Wasaidizi ya mwaka 1969 inayowazuia kuwapiga, kuchukua au kuharibu bidhaa au mali za wananchi. Askari mgambo kama ilivyo kwa watumishi wengine wanatakiwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na bila manyanyaso wala dhuluma wakati wa kuwaondoa wafanyabisahara katika maeneo yasiyoruhusiwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali haitasita kuchukua hatua kwa askari mgambo yoyote atakayebainika kujihusisha na vitendo vya unyanyasaji wa mama lishe na wafanyabisahara wengine wadogo, kwa sababu vitendo hivyo ni kinyume



cha sheria. Aidha, napenda kutoa wito kwa wafanyabiashara wadogo wadogo wote kufanya biashara zao katika maeneo yaliyotengwa rasmi na Halmashauri na kuacha kufanya bisahara hizo katika maeneo yasiyoruhusiwa.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Awali ya yote napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kauli yake ya kuruhusu wafanyabiashara ndogo ndogo wafanye biashara bila kubughudhiwa. Sasa naomba nijikite katika maswali yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza kutokana na majibu ya swali la msingi; naomba Serikali iniambie mama lishe na wafanyabiashara ndogo ndogo wangapi ambao walikamatwa na bidhaa zao zikaharibiwa au kuchukuliwa ambao tayari wamepewa fidia?

Mheshimiwa Spika, pia niambiwe askari mgambo wangapi, kutokana na sheria ambayo ametueleza Mheshimiwa Naibu Waziri, wameshakamatwa, wamehukumiwa au bado wako wanaendelea na kifungo?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa maswali ambayo mnataka takwimu za kusema ni wangapi kwa kumuuliza Waziri papo kwa papo, kwa kweli, majibu ya namna hii yatakuwa ni magumu sana, lakini kwa ujumla wake Mheshimiwa Naibu Waziri Jafo, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwanza Mheshimiwa Rais ametoa maelekezo ambayo haya ni lazima yazingatiwe na kila mmoja wetu katika maeneo yetu. Lakini pia kwa mujibu wa sheria hii ni kweli wafanyabisahara ambao wengine kwa kweli ni jambo baya, utakuta mtu amechukua mkopo, ameenda kufanya biashara yake, lakini kwa makusudi mtu mwingine, hata hawa mgambo wanalichukua hizi bidhaa nyingine, waliamua kuchukua na wakazitumia kwa maslahi yao binafsi hata bila kuzi-report katika Halmashauri zetu, hili limekuwa ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi siwezi kutoa takwimu ni wangapi waliokamatwa, lakini katika maeneo hayo na maeneo mbalimbali, maana yake nchi nzima hii, tukizungumzia Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya, hili limejitokeza katika maeneo mbalimbali na hata hivyo maeneo mengine hatua zimeshachuliwa. Kwa mfano ukienda katika Jiji la Arusha kwa rafiki yangu Mheshimiwa Lema, kuna baadhi ya wafanyabiashara ambao bidhaa zao zilichukuliwa na baadhi ya mgambo waliohusika kwenye hilo wameshapelekwa kwenye vyombo vya sheria.

Mheshimiwa Spika, na juzi juzi kule Mwanza ambako tukio kama hilo limetokea, na ninashukuru sana dada yangu Angelina Mabula naye alikuwepo

kule site, kuna kazi kubwa ambayo imefanyika. Wale wote ambao wameonekana kwamba wamedhulumu mali za watu, kukatakata mapanga mapapai pamoja na matikiti hivi sasa wanachukuliwa hatua zile za kisheria.

Mheshimiwa Spika, na ni kwamba katika eneo la pili ni askari mgambo wangapi ambao hivi sasa wamefikishwa; niseme hili ni suala la kitakwimu. Jukumu letu kubwa ni kusimamia sheria. Wale ambao watakiuka sheria ambazo zimewekwa ni lazima tuwachukulie hatua za kisheria. Lengo kubwa ni kwamba mwananchi wetu aweze kushiriki katika yale mazingira halali yaliyotengwa na Serikali. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, swali fupi la nyongeza.

**MHE. MARYAM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na pole sana. Mwenyezi Mungu ni mwingi wa rehema. Naomba kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri swali dogo la nyongeza

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nchi za wenzetu kama kwa mfano nchi za jirani *South Africa* na nchi nyingine wametenga maeneo kwa ajili ya mama lishe, maeneo rafiki na wanauza vyakula vyao bila kubughudhiwa.

Je, Serikali mna mikakati gani kuhakikisha mnatenga maeneo maalum kwa ajili ya wajasiriamali wadogo wadogo hasa mama lishe?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, Jafo, kwa majibu mazuri ya swali la msingi.

Mheshimiwa Spika, lakini nikuhakikishie tu kwamba Serikali inatambua mchango mkubwa katika uchumi wa nchi yetu kutoka kwa wafanyabiashara wadogo wadogo.

Hata hivyo Serikali imeweka mkakati na tumetoa waraka maalum kuwaagiza Wakuu wa Mikoa na Wilaya, kusimamia Halmashauri kutenga maeneo mahususi, maalum kabisa kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo wadogo. Na ndiyo maana Mheshimiwa Rais katika agizo lake la kwamba, wafanyabiashara wadogo wadogo hawa, wamachinga, wasibughudhiwe bali wasaidiwe. Ni agizo ambalo tunalitekeleza na tumeanza kulipa mkakati wa namna ya kulitekeleza.

Mheshimiwa Spika, lakini niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge, wao ni Wajumbe wa Mabaraza ya Madiwani na wao ni Madiwani. Hawa mgambo wameajiriwa na Halmashauri zetu, hawa mgambo si sawa na polisi, kwa hiyo, hawawezi wakapewa kazi kubwa ya kufanya *operation* hivi kwenye

Halmashauri, maeneo ambayo sisi tunayasimamia bila maamuzi ya vikao, bila kusimamiwa na wataalam au hata na kamati fulani ya madiwani wakaanzisha tu *operation* hivi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunawapa madaraka makubwa ambayo hayastahili, sisi ndio wenye Halmashauri na hawa ni waajiriwa wa Halmashauri, lazima kila *operation* inayofanyika kwa nia nzuri ya kuwatoa watu ambao wanavunja mahususi ya Halmashauri, hakika ni lazima tuhakikishe kwamba tunasimamia zoezi hilo na si kuliacha likafanyika kiholela.

Mheshimiwa Spika, yanayofanyika mengi ni makosa ya sisi Halmashauri kuwaruhusu wale kuwa na mamlaka makubwa na kufanya *operation* bila kuwasimamia.

Na.33

### **Msaada wa UNICEF kwa Halmashauri ya Mbeya**

**MHE. ORAN M. NJEZA** Aliuliza:-

Ili kuboresha elimu Serikali inashirikiana na Mashirika mbalimbali ikiwemo *UNICEF* ambao wanatoa misaada kwa sekta ya elimu:-

(a) Je, kwa mwaka 2014/2015 msaada wa *UNICEF* kwa Halmashauri ya Mbeya ulilenga mahitaji gani ya kuboresha elimu?

(b) Je, ni kiasi gani na asilimia ngapi ya msaada huo ulitumika katika miradi ya maendeleo ya elimu?

(c) Je, ni kiasi gani na asilimia ngapi ya msaada huo ulitumika katika matumizi ya kawaida?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (*UNICEF*) lilitoa msaada kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya uliolenga katika uendeshaji wa shughuli za elimu ya msingi, hususan kutoa mafunzo kwa walimu, wanafunzi, wazazi na walezi, kamati ya bodi za shule, wenyeviti wa vitongoji na vijiji, kuhusu malezi na haki za msingi za watoto kwa kupata elimu bora. Kwa kuzingatia makubaliano hayo yaliyopo kati

ya UNICEF na Serikali fedha hizo ni kwa ajili ya kujengea uwezo (*capacity building*) na hazitumiki kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule.

(b) Mheshimiwa Spika, hadi Juni, 2015 Halmashauri ilipokea shilingi milioni 308.6 sawa na asilimia 64.8 ya shilingi milioni 475.9 zilizopangwa kutolewa na UNICEF kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

(c) Mheshimiwa Spika, fedha zote zilizopokelewa sawa na asilimia 100 zilitumika kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Nashukuru pia kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na pia nashukuru kwa juhudi za misaada ya UNICEF kwa kuboresha elimu kwenye Halmashauri ya Mbeya na sehemu nyingine za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi hizo, changamoto nyingi, hasa kwa shule za vijijini ni miundombinu. Ukichukulia mfano wa Jimbo langu la Mbeya Vijijini, Shule ya Msingi Ipwizi ya ina walimu wawili na wanafunzi wanaozidi 200; Shule za Iyanga, Shule za Iwanga hazina hata mwalimu na hizo ziko karibu sana na Jiji la Mbeya.

Mheshimiwa Spika, shule nyingine kama za Kitusi na Iwanga wanafunzi wanatembea zaidi ya kilometakumi kwenda Mkoa mpya wa Songwe kwa ajili ya kujipatia elimu.

Je, ni kwa nini misaada hii haijalenga kwenye changamoto muhimu za miundombinu katika shule zetu za vijijini? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli hili jambo analolisema Mheshimiwa Mbunge lipo na juzi tarehe tano tulipokuwa katika Mkutano wa Programu ya Walimu ya Mpango wa KKK pale Rungwe miongoni mwa changamoto ambayo niliiona ni kwamba kuna mshiriki mmoja alishindwa kuhudhuria mafunzo yale kwa sababu idadi ya walimu ni chache katika shule yao. Na ndiyo maana juzi tulikubaliana kwamba RAS Mkoa wa Mbeya anaweza kupitia michakato ya mgawanyo wa walimu katika shule zote kwa sababu imebainika kwamba kuna baadhi ya walimu wamelundikwa katika baadhi ya maeneo na maeneo mengine wamekosa walimu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa hili jambo unalosema sio jambo la uongo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa Mkoa wa Mbeya jambo hilo lipo na RAS Mkoa wa Mbeya Mama yangu Mariam Mtunguja, amelibeba hili na

tumekubaliana ndani ya mwezi huu atafanya *reallocation* vizuri ya walimu katika Mkoa wake wa Mbeya.

Mheshimiwa Spika, lakini suala zima la ajenda ya miundombinu ni kweli naomba tuendeleo kushirikiana. Lakini wakati mwingine hii misaada inayotoka kwa wafadhili, inawezekana wao wana malengo yao maalum katika eneo lao.

Mheshimiwa Spika sisi kwanza tunapenda kuwashukuru sana wenzetu wa UNICEF kwa kazi kubwa wanayofanya, na tutajitahidi vile vile kuwashawishi wadau mbalimbali katika baadhi ya misaada, japokuwa itakuwa na *capacity building*, basi tutatafuta wengine ambao wataweza kutusaidia katika suala zima la *infrastructure*, jinsi gani tutawekeza miundombinu katika maeneo yetu, lengo kubwa ni kupunguza kero kwa wananchi wetu na hasa watoto wetu wanaotembea umbali mrefu.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuendeleo na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, swali litatoka Tabora, Viti Maalum Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah.

Na.34

### **Serikali Kuunganisha Wajasiriamali**

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango mkakati gani kupitia diplomasia ya uchumi na nchi ya China kuunganisha wajasiriamali wadogo, wa kati na wakubwa ili kuingia ubia wa kuimarisha viwanda vidogo na vya kati?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Munde Abdallah Tambwe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba nchi yetu ni miongoni mwa nchi nne Barani Afrika ambazo Serikali ya China imezichagua kuwekeza viwanda vyake katika miaka mitatu ijayo (2016 mpaka 2018). Kufuatia uamuzi huo Majimbo mawili ya China ya Jiangsu na Zhejiang yamekwishaelekezwa kuwekeza nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya China imeanzisha Mfuko Maalum wa Fedha kwa ajili ya kuwezesha wafanyabiashara wadogo na wa kati wa Afrika kupata

mitaji maalum. Mfuko huo umewekwa katika Benki ya Maendeleo ya China na tayari umetengewa dola za Kimarekani bilioni tano. Serikali imekwishaanza mazungumzo na benki hiyo kwa ajili ya kuwezesha mabanki nchini yaweze kukopa fedha hizo ili hatimaye yaweze kuwakopesha wajasiriamali wetu wanaotaka kuwekeza kwenye sekta ya viwanda kwa kushirikiana na wenzao wa China.

Mheshimiwa Spika, tarehe 22 Agosti, 2016 Wizara yangu iliitisha kikao cha pamoja kati ya Benki ya Maendeleo ya China na mabanki ya Tanzania ili kupewa utaratibu wa namna ya kupata fedha za mfuko huo. Matarajio yetu ni kwamba, mabanki hayo yatakidhi vigezo vya kuchukua fedha kutoka katika Mfuko huo wa China, ili Watanzania waanze kupata mitaji mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, ubalozi wetu nchini China mara kwa mara umekuwa ukiwashawishi wafanyabiashara wa China waje kuwekeza nchini na mara kadhaa umeandaa ziara za makampuni mbalimbali ya China kuja nchini kuonana na Kituo chetu cha Uwekezaji (TIC).

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa zilizopo TIC wameendelea kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi mkubwa ambao makampuni mbalimbali ya China yameingia ubia na Watanzania kuanzisha viwanda nchini. Mfano mzuri ni ujenzi wa kiwanda kikubwa cha kuzalisha nondo na bidhaa za chuma kinachojengwa Kibaha, Mkoani Pwani kwa ubia kati ya Watanzania na Wachina. Kiwanda hicho kitakapokamilika kitazalisha ajira nyingi kwa ajili ya vijana wa Kitanzania.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwanza kabisa nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini pia, niipongeze Serikali kwa kuonesha baadhi ya mikakati yao inayoendelea nayo na ninayo maswali mawili ya nyongeza. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, je, Serikali kupitia diplomasia yake ya kiuchumi nchini ina mkakati gani wa kuwashawishi wakulima wakubwa wa tumbaku nchini China waje kuingia ubia na wakulima wadogo wa tumbaku Mkoani Tabora, ili wakulima wa tumbaku Mkoani Tabora waweze kupata faida kubwa na yenye tija na kuona kilimo cha tumbaku sasa kinawasaidia, tofauti na hali ilivyo sasa? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa vijana wengi nchini wamejiajiri kwenye biashara ya bodaboda, hususan Mkoa wangu wa Tabora ambao vijana wengi wanaoendesha bodaboda hizo zisizo zao, je, Serikali kupitia diplomasia yake ya uchumi nchini inaweza leo kunihakikishia hapa kwamba,

itafanya kila liwezekanalo kuhakikisha Mkoa wa Tabora unapata kiwanda cha pikipiki kutoka kwenye viwanda vikubwa kama *SanLG*, labda *Boxer* na viwanda vingine vyovyote vilivyopo China, ili kuweza kuwapatia vijana hawa pikipiki kwa bei nzuri, ili na sisi watu wa Mikoa ya Tabora, Katavi, Sumbawanga, Kanda ya Ziwa, tuweze kujikomboa kiuchumi kwa kupitia diplomasia hii? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Suzan Kolimba, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, wape majibu wanyamwezi!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Munde kwa kufanya kazi kubwa ya kuwatetea wananchi wa Tabora. Naomba niende kujibu maswali yake mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ambalo linahusu jinsi Wizara yangu inaweza kufanya mkakati gani wa kuweza kuwezesha wakulima wakubwa wa China kujakuwekeza na kufanya kazi pamoja na wakulima wadogo wa Tabora.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Munde kwamba Wizara yangu ilifanya mkakati huo, sisi kama Wizara ni Wizara kiunganishi, tumefanya mkakati na mkakati huo ni kuwahakikishia kwamba watu wa China wanaweza wakawekeza katika zao la tumbaku na nimwambie tu kwa hali sasahivi ilivyo ni kwamba Balozi wa China nchini Tanzania pamoja na Wizara ya Kilimo wako katika mkakati wa majadiliano wa kuweza kufikia makubaliano ya kujua zao la tumbaku na bei ya tumbaku itakuwaje na sisi tumeaachia wao kama Wizara kwasababu sisi kazi yetu ni kuhakikisha kujenga mahusiano mazuri. Tukishawaleta, wakifika nchini tunawapeleka katika Wizara husika.

Mheshimiwa Spika, kwahiyo, nikuhakikishie kwamba wakulima wa Tabora pamoja na wale wakulima wa China watafanya biashara hiyo ya tumbaku lakini baada ya mazungumzo na majadiliano yatakapokwisha kati ya Wizara ya Kilimo na Balozi wa China nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili la kuhusu bodaboda na kuhusu vijana wa bodaboda waliopo Tabora na Kanda ya Ziwa, nikuhakikishie si tu Tabora na Kanda ya Ziwa lakini kwa Tanzania. Nafikiri umeshawahi kusikia ndani ya Bunge hili Waziri wa Viwanda na Biashara amezungumzia kuhusu suala la watu wa china kuwekeza katika viwanda vya kutengeneza bodaboda hapa Tanzania.

Kwa hiyo, biashara hiyo itakuwepo na watawezesha katika namna hiyo na kufundishwa pia jinsi ya kuendesha biashara ndogo ndogo kama ujasiriamali ili kusudi wasiwe tegemezi na waweze kutoka katika utegemezi na kufanya kazi yao vizuri.



Mheshimiwa Spika, niendeleo kumhakikishia Mheshimiwa Munde kwamba sisi kama Wizara kwa kutumia diplomasia ya kiuchumi tutaendelea kupambania Tanzania iende katika kuhakikisha kwamba inatimiza ahadi yake ya kuhakikisha kwamba Tanzania inatoka katika hali ya kawaida na inakwenda katika uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, tutatumia diplomasia hiyo kwa kutumia Mabalazi wetu wote waliopo nje na wale waliopo Tanzania na kutumia vijana wetu na watumishi wetu wenye ujuzi na weledi uliostahiki katika kuhakikisha kwamba miradi hii na *projects* zote ambazo tunazikuta katika mikutano na sehemu mbalimbali zinaletwa Tanzania na kuwafaidisha na kunufaisha Watanzania kwa ujumla wake, ahsante. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mchungaji Msigwa nilikuona.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru; Mheshimiwa Waziri dhana nzima ya diplomasia ya kiuchumi ni pana sana na hivi karibuni tumeona Tanzania inasita kusaini Mkataba wa EPA pamoja na Jumuiya ya Ulaya. Ni sababu zipi za kimsingi ambazo zinasabisha Tanzania iwe inasuasua, na muda mrefu Wabunge tumekuwa tukiuliza Serikali kwamba haijiandai ku-*capitalize* kwa fursa zinazotokea? Sasa Mheshimiwa Waziri unasema Serikali imejipanga, ni kwa nini hasa Serikali imekuwa ikisuasua pamoja na kwamba inaweza ikawa na sababu nzuri kusaini huu mkataba pamoja na Jumuiya za Ulaya?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu kwamba kama tunavyosema kwamba chochote sisi tunachokipigania kama Wizara na kama Serikali ni kwa manufaa ya nchi hii, ni kwa manufaa ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, tumesema kwamba hatusaini kwa sababu mkataba ule kwa namna fulani jinsi ulivyokaa uta-*affect* maslahi ya Tanzania na hasa katika suala zima la kuhakikisha kwamba viwanda vinaweza kuendelea na wewe unajua kuhusu hilo. Kwa hiyo, hatusaini kwa sababu hizo. (Makofi)

Na. 35

### Hali Mbaya ya Magereza Nchini

**MHE. SOPHIA M. SIMBA** aliuliza:-

Hali ya magereza nchini ni mbaya hivyo kufanya vigumu katika utoaji wa haki za kibinadamu licha ya kwamba nchi imekuwa ikijali sana utekelezaji wa

mikataba mbalimbali ya kikanda na ya kimataifa katika utoaji wa haki hizo za wafungwa.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha hali hiyo katika magereza nchini?

(b) Je, Serikali imejenga magereza mapya mangapi katika kipindi cha miaka 20 iliyopita?

**NAIBU WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Mathayo Simba, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango wa kuboresha hali ya magereza nchini kwa awamu kadri ya fedha zitakavyopatikana. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali imetenga fedha katika fungu la maendeleo na matumizi mengineyo kwa ajili ya ukarabati, upanuzi, ujenzi wa mabweni mapya, majengo ya utawala na ununuzi wa vifaa mbalimbali vya malazi katika magereza nchini ili kuboresha huduma kwa mahabusu na wafungwa kukidhi vigezo vya haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka 20 iliyopita Serikali imejenga magereza mapya 11 kwa mchanganuo ufuatao:-

1. Gereza la Mkuza- 1996;
2. Gereza la Mbarali - 2003;
3. Gereza la Igunga - 2003;
4. Geeza la Meatu - 2003;
5. Gereza la Mgagao - 2004;
6. Gereza la Kinegele - 2005;
7. Gereza la Mbozi - 2005;
8. Gereza la Mbinga - 2007;
9. Gereza la Chato - 2008;
10. Gereza la Kiteto - 2009; na
11. Gereza la Karatu - 2010.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo magereza hayo pamoja na ujenzi kutokamilika yanaendelea kutumika isipokuwa Gereza la Chato na Gereza la Karatu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Simba swali la nyongeza kama lipo.

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, na ninamshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini kidogo yananitatanisha.

Mheshimiwa Spika, anazungumzia ujenzi wa magereza 11 katika kipindi cha miaka 20. *Speed* hii si nzuri, na pia hayo magereza pamoja na kwamba amesema hayajamalizika lakini wanayatumia, nadhani hapo pana hitilafu kubwa.

Ningependa niulize katika hayo magereza yanayojengwa ni lini anafikiri wanaweza wakaboresha ile mahabusu ya watoto iliyopo Upanga Dar es Salaam; ni mahabusu ya miaka mingi na ni ndogo na haifanani kuwa mahabusu ya watoto? Na sidhani kama zipo mahabusu nyingi kama hizo, Waziri wa Ardhi ana viwanja vingi Dar es Salaam ni vyema akaihamisha pale, ni lini watafikiria kuiondoa ile mahabusu pale?

Mheshimiwa Spika, la pili, kumejitokeza msongamano mkubwa sana kwenye mahabusu na magereza, hasa mahabusu pale wanapokamata watu wengi kwa wakati mmoja.

Ningependa kujua hivi kule polisi au magereza wana utaratibu gani wanapokamata watu wengi kwa pamoja, wa kuweza kupunguza wengine kwenda maeneo mengine kwasababu pale ndipo kuna *gross breach* ya *human rights*, watu wanapumuliana, wale watuhumiwa wanashindwa hata kukaa na wanalala wakiwa wamesimama.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua kuna utaratibu gani kupunguza hilo tatizo kwa sababu ni la muda tu wanakamatwa kwa muda? Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi, *Engineer* Masauni.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kasi ya kuongeza idadi ya magereza ama kuboresha magereza yaliyopo, naomba tu nichukue fursa hii kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inajitahidi sana kuhakikisha kwamba magereza yetu yanaendelea kuongezeka ukubwa kwa kupanua na kujenga mabweni mapya. Na mfano mzuri wa hilo ni bajeti ya mwaka huu ambayo tumeipitisha hivi karibuni; ambapo tumetenga takribani shilingi bilioni tatu kwa ajili ya kazi hiyo ambayo itahusisha ukarabati mabweni karibu 15 katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya maeneo hayo ni kama vile Nzega, Babati, Ushora, Tarime na kadhalika. Lakini pia itahusisha kukamilisha kwa mabweni

kama saba ambayo yameshaanza kujengwa ambayo yapo maeneo mbalimbali, likiwemo hilo la Chato, Mpwapwa, Biharamulo, Mkuza, Urambo na kadhalika; pamoja na kuimalisha maeneo ya huduma katika magereza yetu ambapo itahusisha ujenzi wa jiko katika Gereza la Segerea pamoja na mazingira mengine ya magereza yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kazi hiyo inafanyika hatua kwa hatua kadiri hali ya uchumi utakavyoruhusu na tutaendelea kufanya hivyo katika bajeti ya kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusiana na lile Gereza la Watoto la Upanga ambalo Mheshimiwa Sophia Simba ameliulizia; ni kwamba kimsingi lile lipo chini ya Wizara ya Afya kwenye Idara ya Ustawi wa Jamii. Kwa hiyo, sisi tunachokifanya ni kwamba hatuna magereza ya watoto ukiachia Gereza la Vijana la Wami ambalo lipo Morogoro; linalochukua vijana wa miaka 16 mpaka 21, kimsingi watoto wanopatikana kwenye hatia katika magereza hupelekwa katika Idara ya Ustawi wa Jamii kwa ajili ya kuhudumiwa kama watoto na si wafungwa. Kwa hiyo, kimsingi jibu la swali lake lilikuwa hivyo.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili linahusu kupunguza msongamano magerezani. Kuna njia mbalimbali zimefanyika, ukiachia hizi ambazo tumezungumza za kuona jinsi gani tunapanua mabweni na kujenga magereza mapya pia kuna hatua mbalimbali ambazo zimesaidia kufanikisha kupungua kwa idadi ya wafungwa kutoka 38,000 mpaka sasa hivi takribani 34,000 tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingia madarakani.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo ilitokana na hatua mbalimbali ikiwemo kuhakikisha kwamba tunatumia njia za *parole*, huduma za jamii, *probation* na njia nyingine ili kuona sasa wafungwa ambao wana kesi ndogo ndogo ama wana hatia ndogo za miaka michache kukaa magerezani basi watumie vifungo vya nje badala ya kurundikana magerezani na kusababisha msongamano usio ulazima. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri wa Afya, sikujua kama una magereza, una mpango gani wa kuhamisha Gereza la Upanga?

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, niseme kwanza nimefurahi kukuona hapo.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani kwa majibu mazuri. Ni kweli kwamba mahabusu za watoto ziko chini ya wizara yangu, lakini nataka kumthibitishia mama Sophia Simba kwamba katika mwaka huu wa fedha tumetenga zaidi ya bilioni mbili kwa ajili ya kuboresha kwanza makazi ya wazee lakini pia tutaboresha hizo nyumba za

kuwarekebisha tabia watoto. Tunajaribu ku-avoid neno mahabusu kwa sababu tunataka kuwarekebisha tabia, ndilo neno ambalo tunapenda kulitumia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mama yangu Sophia hatukuwa na mpango wa kulihamisha lakini sasa kabla hatujaboresha naomba nichukue hoja yako tuone kama je, tuboresha au tulihamishe tulipeleke sehemu nyingine. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Naona swali la nyongeza tulipeleke Kanda Maalum, Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, napenda kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa magereza mengi nchini ni kweli miundombinu ni michakavu sana; na kwa kuwa asilimia zaidi ya 75 mahabusu waliopo magereza ni wale ambao wana kesi za kudhaminika lakini wananyimwa dhamana. Swali langu linakuja kwamba Gereza la Tarime linachukua mahabusu na wafungwa kutoka Wilaya ya Rorya na unakuta ina msongamano mkubwa kutoka 209 mpaka 560 mpaka 600.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua sasa Serikali ni lini itajenga gereza Rorya, kwa sababu ile ni Wilaya inajitegemea, ili kupunguza msongamano wa mahabusu na wafungwa Tarime ambayo inaweza ikapelekea magonjwa mbalimbali na ukizingatia miundombinu ni mibovu sana? Lakini pia kwa haki za kibinadamu wanatoka kule Rorya kufuatilia kesi Tarime, kuja kuona mahabusu Tarime, kuja kuona wafungwa Tarime. Ni lini sasa mtajenga Gereza la Rorya kupunguza msongamano katika Gereza la Tarime? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi, Kanda Maalum inaomba gereza maalum.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tunakiri kwamba kuna msongamano wa wafungwa katika Gereza la Rorya na kuna umuhimu mkubwa wa kujenga Gereza pale. Lakini changamoto ya upungufu wa magereza katika Wilaya zetu mbalimbali nchini halipo Rorya tu; kwenye maeneo mengi ya Wilaya nchini bado magereza yamekuwa ni upungufu.

Kwa hiyo tutajaribu kuhakikisha kwamba tunapunguza msongamano huo kwa kujenga magereza katika Wilaya ambazo zina upungufu katika nchi nzima, na utekelezaji wa mpango huo utategemea upatikanaji wa rasilimali fedha, kwani mpaka sasa hivi kati ya Wilaya 92 ni Wilaya 43 nchini ndio ambazo zina magereza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kimsingi tunalifahamu hili tatizo, niombe tu Mheshimiwa Mbunge awe na subira pale ambapo hali itakapo ruhusu tutashughulikia pamoja na hizo Wilaya nyingine 43 ambazo nimezitungumza zenye mapungufu hayo. (Makofi)

**SPIKA:** Kwa muda uliobakia Waheshimiwa Wabunge tuvumiliane kwa maswali yaliyobakia hatutakuwa na mswali ya nyongeza, watauliza wale wenye *basic questions* tu ili muda uweze kutosha.

Tunaenda Wizara ya Nishati na Madini, swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba.

Na. 36

### **Ujenzi wa “LNG Plant”**

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA** aliuliza:-

Kampuni ya BG-EXXON MOBIL, OPHIR na washiriki wenzao wako tayari kuanza ujenzi wa *LNGPlant*.

(a) Je, ni nini kinachokwamisha kuanza kwa utekelezaji wa mpango huo?

(b) Je, ni hatua gani za makusudi zinachukuliwa ili kuharakisha utekelezaji wa mradi huo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kusindika Gesi Asilia (*Liquefied Natural Gas – LNG*) ulibuniwa mwaka 2014 kufuatiwa ugunduzi wa gesi asilia nchini ambao umetoka katika bahari ya kina kirefu. Mradi huo unatekelezwa katika na kampuni za kimataifa ya *Statoil* ya Norway, BG ya Uingereza, *Exxon Mobil* ya Marekani pamoja na *Ophir* ya Uingereza. Kampuni nyingine *Pavilion* ya nchini Singapore pamoja na shirika la *TPDC* ambalo ni la Serikali hapa nchini. Kutokana na umuhimu wa wa mradi huo katika kujenga uchumi wa gesi asilia nchini Serikali inachukua hatua za utekelezaji wa mradi kwa awamu tofauti. Lakini Serikali inachukua tahadhari muhimu sana katika kuandaa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa utekelezaji wa mradi huo unaendelea vizuri. Hatua zilizofikiwa kwa sasa ni

pamoja na kupata eneo la LNG litakalojengwa kwa umbali wa kilometa 2,000 na katika eneo lingine ambalo litakamilika mpaka 2020.

Mradi huu unatekelezwa kama nilivyosema na TPDC ambapo kufikia mwaka 2015 Serikali ilikabidhi TPDC hatimiliki ya eneo ambalo kwa sasa tafiti mbalimbali za kihandisi, kijiolojia, kimazingira na kijamii zinaendelea kufanyika.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya mikataba mbalimbali yameanza baada ya Serikali kukamilisha uundaji wa timu ya kufanya majadiliano (*government negotiating team*). Majadiliano kati ya *government negotiation team* yameanza na yatakamilika mwezi Septemba mwaka huu. Mahojiano hayo pamoja na mambo mengine yanafanya pia ifikapo mwaka 2020 kukamilika kwa ufasaha kabisa. Aidha, Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini hukutana na wawekezaji hao kila baada ya miezi mitatu ili kutathmini maendeleo ya utekelezaji wa mradi huu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Chikota, swali la nyongeza kama lipo.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, je, Serikali ina mpango gani sasa wa kutoa elimu kwa wakati wa Mtwara na Lindi ili wapate uelewa juu ya mradi huu?

Lakini pili, waweze kujiandaa kutumia fursa zitakazopatikana baada ya ujenzi wa kiwanda hiki? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pili, maeneo ambayo yalianishwa na mradi huu ni mawili, eneo la kwanza ni kwa ajili ya ujenzi wa kile kiwanda cha LNG, eneo la pili ni *industrial park* kwa ajili ya viwanda vingine ambavyo vitajengwa hapo baadaye.

Sasa nataka nijue hatua iliyofikia katika kutwaa eneo hili ambalo litajegwa viwanda vingine yaani eneo la *industrial park* kwamba je, wananchi wameshafidiwa au bado hawajafidiwa hadi sasa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, mradi wa LNG ni mardi mkubwa sana, na nipende tu kusema kwa niaba yako na kwa niaba ya Wabunge; kati ya miradi mikubwa ambayo Serikali tumeitekeleza ni pamoja na mradi huu utakapo kamilika. Mradi huu kwa nchi za Afrika, Tanzania itakuwa ni nchi ya tatu katika kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, lakini kujibu swali la msingi ambalo Mheshimiwa Chikota anataka kujua ni hatua gani imefikiwa katika kutoa elimu kwa wananchi; hatua tatu zimeshafanyika hadi sasa.



Mheshimiwa Spika, hatua ya kwanza ilikuwa ni kuwapa ufahamu na utambuzi wa manufaa ya mradi huu kwa viongozi wa Mikoa ya Lindi pamoja na Mtwara ambao vikao vimefanyika na kikao cha mwisho kilifanyika jana pamoja na juzi.

Mheshimiwa Spika, lakini hatua ya pili kulingana na hilo TPDC pamoja na wakandarasi na wazabuni waliopewa kazi hii wameshaanza kutoa elimu katika Vijiji vinavyoambaa katika mradi huu. Vijiji ambavyo vimeshatoa elimu hadi sasa ni pamoja na Kijiji cha Likong'o ambapo mradi utachukuliwa, eneo la Kikwetu pamoja na Kijiji cha Mtomkavu. Hayo ni maeneo ambayo elimu wananchi wameshapewa kwa ajili ya umuhimu wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la pili, kwamba ni maeneo gani yamechukuliwa kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda hiki. Kwa niaba ya wananchi ni vizuri niwatangazie kwamba eneo lililochukuliwa na mradi huu kimsingi ni eneo kubwa sana, ni jumla ya ekari 20,000 zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa mradi huu, hata hivyo kwa awamu ya kwanza kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa LNG ni hekta 2,071 zitatumika.

Mheshimiwa Spika, na kwa niaba ya wananchi ni vizuri nikiwaeleza, mradi huu utakapokamilika utakuwa na manufaa mengi kwa sababu wawekezaji mbalimbali watatumia maeneo haya. Kwa mujibu wa swali la Mheshimiwa Chikota, nikushukuru sana Mheshimiwa Chikota kwa sababu mradi huu ni vizuri sana Watanzania tukaelewa. Tunapozungumza kujenga uchumi wa viwanda ni pamoja na viwanda vikubwa kama kiwanda hiki ambacho nimekieleza.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Na. 37

### **Bei Elekezi ya Mawe na Mchanga kwa Wakandarasi**

**MHE. OMARY A. BADWEL** aliuliza:-

Wananchi wanaoishi kwenye maeneo yenye rasilimali mawe, mchanga na maji inapotokea wakandarasi wanachukua rasilimali hizo au mojawapo kwa ajili ya ujenzi huchukua bure au kwa malipo kidogo na hivyo kuwakosesha wananchi haki ya kunufaika na rasilimali hizo; hali hii ni tofauti na maeneo yenye madini ambapo wananchi hunufaika na uwepo wake:-

Je, Serikali haioni haja ya kuweka bei elekezi kwa wakandarasi wanaohitaji mawe, mchanga au maji ili wananchi wanaoishi maeneo yenye rasilimali hizo waweze kunufaika?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omary Ahmad Badwel, Mbunge wa Bahi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na kanuni zake inamtaka kila mmiliki wa eneo la kuchimba madini amiliki leseni halali kutoka Wizara ya Nishati na Madini, hata hivyo leseni katika maeneo ya uchimbaji wa madini ya viwanda na ujenzi yanatakiwa pia kupata leseni bila kuchimba kiholela. Wakandarasi wanaofanya kazi ya ujenzi hulazimika pia kupata leseni za kuchimba madini ya ujenzi na kulipa mrabaha pamoja na ada nyingine kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa wakandarasi wasiokuwa na leseni za uchimbaji hununua madini ya ujenzi kwa wananchi wanaochimba na pia kufanya shughuli za ujenzi, pamoja na hayo, Wizara kwa kushirikiana na Wakala wa Ukaguzi wa Madini (TMA) hutoa matangazo kwenye Ofisi za Madini za Kanda na Maafisa Madini Wakazi yakionesha bei ya soko ya ndani ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wa madini ya ujenzi wanaweza kuwasiliana na ofisi ya madini kupata mwongozo wa bei ya soko kwa sasa ili kupata ufahamu wa bei halisi ya mazao hayo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Badwel swali la nyongeza.

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Kwa kuwa, Wakandarasi wengi wanaotumia bidhaa hizi hawafuati taratibu hizi ambazo zimeelezwa na Mheshimiwa Waziri, ama kununua mawe na bidhaa nyingine kwa watu wenye leseni, mara nyingine wamekuwa wao wenyewe wakiamua kuchukua hizo bidhaa katika maeneo yetu na bila kulipa mrabaha katika Halmashauri au bila kuwanufaisha wananchi katika maeneo yetu ambako bidhaa hizo zinatoka;

Je, Serikali iko tayari sasa kuangalia utaratibu mzuri ambao utanufaisha hizi Halmashauri zetu pamoja na wananchi husika katika maeneo husika ambayo bidhaa hizi zinapatikana?

Swali la pili, kwa kuwa wakati wa zoezi hili la uchukuaji bidhaa mbalimbali za ujenzi pia hutokea uharibifu wa mazingira katika maeneo yetu ikiwepo uchimbaji wa mashimo makubwa na kuacha hayo mashimo katika maeneo yetu, pia afya za wananchi zinaathrika kwa mavumbi na kadhalika;

Je, Serikali inachukua hatua gani madhubuti kuhakikisha kwamba inadhibiti suala la uharibifu wa mazingira pamoja na afya za wananchi katika maeneo husika?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa wachimbaji wadogo hasa wanaojihusisha na uchimbaji wa madini ya ujenzi pamoja na viwandani kwa kiwango kikubwa sana hawalipi ada pamoja na malipo mengine Serikalini. Nichukue nafasi hii kuwataka rasmi wachimbaji wadogo wote popote walipo waanze sasa kufanya hivyo.

Hata hivyo, manufaa yanayoweza kupatikana kutokana na uchimbaji wa kokoto pamoja na mchanga ni pamoja na kutakiwa kama ambavyo sheria inawataka kulipa ushuru wa Halmashauri ambao ni asilimia 0.3, haya ni matakwa ya sheria, ni vizuri sana ninakushukuru Mheshimiwa Badwel, nichukue nafasi hii kuwahamasisha viongozi wa Halmashauri ili waanze kukusanya ushuru huo kutoka kwa wakandarasi wanaochimba kokoto pamoja na mchanga kote nchini. Kwa hiyo namshukuru sana Mheshimiwa Badwel kwa kuwakumbusha wananchi ili wachukue hatua hiyo, ninawaagiza pia wakandarasi wote waanze kufanya hivyo mara moja.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, athari za mazingira, kwanza nikubaliane na Mheshimiwa Badwel kwamba uchimbaji wowote wa madini jambo la kwanza kabisa wanalotakiwa kufanya ni juu ya kutokuharibu mazingira. Huwezi kuchimba madini bila kuharibu mazingira, lakini wana jukumu kwa mujibu wa Sheria za Mazingira na kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya 2010, wana wajibu wa kisheria wa kutunza mazingira.

Mheshimiwa Spika, hatua tunazochukua kwa wakandarasi na wamiliki wa leseni wasiotunza mazingira ni pamoja na kuwafutia leseni zao lakini pia kuwachukulia hatua za kisheria kwa mujibu wa sheria hizo mbili.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Badwel pia natoa tamko rasmi, Wizara ya Nishati na Madini kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira huwa tunachukua hatua za kisheria kwa wale wasiotunza mazingira kwa mujibu wa sheria.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Gekul nakuona lakini muda hauko upande wetu, vumilia tu. Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, swali la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka Mbunge wa Same Mashariki.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nitumie nafasi hii kukupongeza, wananchi wa Jimbo la Same Mashariki wanakupongeza sana kwa kuona na kurudi.

Na. 38

### **Kituo cha Utafiti wa Malaria Same**

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA** aliuliza:-

Kituo cha Utafiti wa Malaria kilichopo Kata ya Vuje, Tarafa ya Gonja, Jimbo la Same Mashariki kimejengwa miaka ya 1960 na kina majengo ya kisasa kumi na kwamba Serikali ilikifanyia ukarabati mkubwa mwaka 2007, lakini mpaka sasa hakifanyi kazi badala yake kimegeuzwa kuwa nyumba za kulala wageni na pesa zinaingia mfukoni mwa watu.

Je, Serikali inafahamu jambo hilo na kama inafahamu inatoa kauli gani?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Jimbo la Same Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu na Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Same Mashariki kuwa ni kweli Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) inamiliki maabara, jengo la utawala na nyumba ya wageni (*rest house*) katika kituo chake cha Gonja Maore, Wilayani Same. Kulingana na jiografia ya Gonja, *rest house* hiyo ilijengwa kwa madhumuni ya kufikia wafanyakazi wa taasisi kutoka vituo vyake vingine wanaokwenda pale Gonja katika maeneo hayo kwa malengo ya kikazi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa *rest house*, licha ya kuhudumia wafanyakazi wa taasisi pia inatoa huduma kwa wananchi ikiwa pia ni mojawapo ya vyanzo vya mapato kwa taasisi. Taasisi imeweka taratibu na miongozo mahsusi inayoongoza utoaji wa huduma katika *rest house* zake zote ikiwemo ile ya Gonja, katika utaratibu huo wageni wote wanaohitaji huduma

katika *rest house* huwajibika kujisajili katika *register* ya wageni ya *rest house* na stakabadhi hutolewa kwa malipo yoyote yatakayofanyika. Hivyo, majengo yote ya kituo yanatumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli nasikitika sana kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, najua hizi habari alipewa akiwa ofisini kwake.

Mheshimiwa Spika, hii *guest house* anayoizungumzia kwanza imepitwa na wakati sana, imejengwa miaka 56 iliyopita, lakini ambacho kimempita asione ni kwamba kituo hiki ni kikubwa sana na ni kizuri sana, kina eneo takribani zaidi ya heka tatu, kina mandhari mazuri sana, kina majengo mengine yote ya maabara, nyumba ya daktari, nyumba ya manesi na wodi za wagonjwa.

Sasa swali langu ni kwamba, je, kwanza Naibu Waziri atakuwa tayari tuende akajiridhishe kwamba jibu lake hili ambalo alizungumza kana kwamba kuna nyumba tatu tu, halitoshelezi maana ya kuwa na kituo kama hiki?

Pili, nataka Waziri aniambie kutokana na kwamba kituo hiki sasa hivi hakitumiki vizuri kama kituo cha utafiti kwa vile inaweza kuisha mwaka, miaka miwili hakujaanyiwa utafiti hata mtu mmoja; je, haoni kwa nini kituo hiki kiongezewe kiwe kituo cha afya ili pale watakapopenda kufanya utafiti wafanye, lakini kwa vile kuna majengo ambayo Serikali imetumia hela nyingi sana kukitengeneza na mandhari mazuri na kuna mlinzi, kuna *gardener*, kuna msafishaji, kuna *tv*, kuna maji, kuna umeme lakini kituo hiki sidhani hata hiyo *guest house* inapata watu wawili kwa mwezi maana mwenyewe nilienda nikalala pale kujiridhisha.

Mheshimiwa Spika, naomba Naibu Waziri aniambie; je, Serikali iko tayari kukifanya kituo hiki kiwe Kituo cha Afya ili kisaidie Kata tatu za Vuje, Maore na Bombo ambazo zina wananchi zaidi ya 50,000 ukichukulia kwamba Jimbo langu ni kubwa sana na ukichukulia kwamba jiografia ya kwangu ni mbaya sana na vituo vipo viwili tu na viko mbali mno? (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naghenjwa, ujumbe umefika.

Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane, kelele ni nyingi mno hasa upande wangu wa kulia sijui kuna nini. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya. Naomba tusikilizane, tubadilishane mawazo kwa sauti za chini kidogo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka kwa maswali yake mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, majibu ya Serikali kwa swali lake la kwanza kwamba Waziri atakuwa tayari kwenda kukitembelea kituo hiki, ndiyo tupo tayari na baada ya Bunge hili tutakwenda na tutamtaarifu Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo hili aongozane na sisi tutakapokwenda kukitembelea kituo hicho.

Mheshimiwa Spika, jibu la pili ni kwamba ninachokiona Mheshimiwa Kaboyoka ana uchu wa kupata kituo cha afya zaidi kuliko matatizo yaliyopo pale kwenye Kituo hiki cha Utafiti cha Gonja. Sasa mahitaji ya vituo vya afya huwa yanaibuliwa na wananchi kwenye Halmashauri yao wenyewe. Ninamshauri Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na Watendaji kwenye Halmashauri yake na wananchi kwenye Halmashauri yake waweze kuanzisha mchakato wa namna ya kupata Kituo cha Afya kwa ajili ya kukidhi mahitaji yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kwamba kituo hiki kimekaa kwa muda mrefu na kwamba hakitumiki, hapana siyo kweli. Nakubaliana na yeye kimejengwa zaidi ya miaka 50 iliyopita lakini mwaka 2007/2008 kituo hiki kilifanyiwa ukarabati mkubwa kwa ajili ya maandalizi ya utafiti wa mabadiliko ya *prevalence* ya ugonjwa wa malaria ambao unaendana na tabia nchi. Wakati mchakato wa kuanza utafiti ule ikaonekana kwamba *prevalence* ya malaria imeshuka kwa kiasi kikubwa katika nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara na kwa maana hiyo utafiti ule haukuendelea. Kwa sasa utafiti mwingine unaendelea kwenye kituo kile unaendeshwa na Taasisi yetu ya Utafiti ya NIMR kupitia kituo chake cha Amani kilichopo Tanga kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Muhimbili kuhusiana na namna ya kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano katika kufikisha ujumbe unaohusiana na kupambana na maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI.

Kwa hiyo, siyo kwamba kituo kile hakitumiki, kituo kile kinatumika kwa matumizi yake ya awali ya utafiti, kama nitakapokitembelea kutakuwa kuna haja ya kuangalia namna ya kuweza kukifanya kitoe huduma nyingine mbali na zile huduma mahsusni tutashauriana ndani ya Serikali kuona kama tunaweza tukulichukua wazo hilo.

Na. 39

### **Uanzishaji wa Duka la Dawa la MSD Singida**

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE** aliuliza:-

Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli, iliagiza Bohari Kuu ya Dawa (MSD) kuanzisha maduka ya dawa kwenye hospitali kubwa nchini.

(a) Je, ni lini Serikali itaagiza MSD kufungua duka la dawa katika Hospitali ya Mkoa wa Singida ili kuwasaidia wananchi kununua dawa kwa bei nafuu tofauti na zile zinazouzwa kwenye maduka ya mitaani?

(b) Je, lini Serikali itasambaza vifaa tiba vya kutosha kama vitanda vya wajawazito katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa na Hospitali za Wilaya za Mkoa wa Singida?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika hospitali zetu, Serikali iliagiza maduka ya dawa yafunguliwe kwenye Hospitali za Kanda na Taifa nchini. Aidha, ikumbukwe kwamba siyo jukumu la Bohari ya Dawa kuuza dawa kwa rejareja moja kwa moja kwa wateja, kuruhusu hili litokee ni kujaribu kunyakuwa fursa ya hospitali husika kupata mapato kwa kuuza dawa kwa wateja hivyo kuzichelewesha kuanza kujitegemea. Ili kutekeleza agizo hilo kwa Tanzania nzima ilionekana itahitajika rasilimali watu na fedha nyingi sana ambapo Bohari ya Dawa peke yake isingeweza kumudu. Kwa hiyo basi, Bohari ya Dawa ilikubaliana na TAMISEMI kuwa hospitali zilizo chini yake basi zifungue maduka yao wenyewe na MSD itakuwa tayari kutoa ushauri wa kitaalam pamoja na kuziuzia dawa na vifaa tiba.

(b) Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Rufaa ya Singida inashauriwa kutenga fedha kwenye mgao unaoletwa na Wizara kila robo mwaka pamoja na makusanyo kutoka vyanzo vingine kama Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ili iweze kununua vifaa, vitendea kazi pamoja na vitanda vya wajawazito.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya nina maswali mengine kwake.

Kwa kuwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida ndiyo tegemeo kubwa kwa wananchi wa Mkoa wa Singida hususan wanawake katika kupata huduma za afya, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha Hospitali hii ya Rufaa inapata wataalam na madawa ya kutosha pamoja na vifaa tiba kama MRI, *ultra sound* na x-ray pamoja na gari la kubebea wagonjwa. (Makofi)



Kwa kuwa tayari kuna jengo ambalo limeainishwa kwa ajili ya kuanzishwa duka la madawa karibu na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida na kinachokosekana ni fedha za ukarabati wa jengo hilo?

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha za kutosha kwa ajili ya ukarabati wa jengo hilo ili lianze kufanya kazi mara moja?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla kwa kifupi tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe, Mbunge wa Viti Maalum, kwa maswali yake mawili ya nyongeza.

(a) Jibu letu la kwanza ni kwamba Serikali ina mikakati mingi kama ambavyo tulieleza wakati wa kipindi cha bajeti hapa Bungeni, miongoni mwa mikakati hiyo ni pamoja na kuongeza bajeti yetu ya dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kwenye bajeti hii ya mwaka 2016/2017 kutoka takribani bilioni 26 zilizokuwepo kwenye bajeti ya mwaka uliopita mpaka bilioni takribani 252 kwenye bajeti hii mpya. Kwa hiyo, tukishakuwa na fedha za kutosha tutaweza kukidhi mahitaji ya hospitali zote nchini.

Mheshimiwa Spika, pili tunaendelea kuzishauri Halmashauri na Mikoa yote nchini watumie vizuri pesa wanazopata kutokana na *user fees* wanazo-charge kwa wagonjwa wakati wanaenda kupata huduma kwenye hospitali, pia pesa wanazopata kutoka kwenye Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ili waweze kuzitumia vizuri kwa ajili ya manunuzi ya vifaa tiba, kwa sababu tunalenga katika muda mrefu kuhakikisha hospitali zetu za Wilaya na hospitali za Mikoa zinajitegemea zenyewe na ndiyo malengo ya *Decentralisation by Devoluton*.

(b) Kuhusiana na ukarabati, hili nimuachie Mheshimiwa Mbunge akashauriane na Katibu Tawala wa Mkoa wake, waone ni namna gani wanaweza wakafanya ukarabati wa hospitali hii wa jengo hili la *theater* na maabara na vitu vingine.

Mwisho nimtoe shaka Mheshimiwa Mbunge pamoja na Wabunge wote kwamba katika mwaka huu unaoendelea tuna mradi mkubwa wa vifaa tiba unaoitwa *ORIO* ambapo tutaweza kupata vifaa kama *MRI*, *CT Scan*, *ultra sound* na *x-ray machines* ambavyo amevitaja Mheshimiwa Mbunge na tutavigawa kwenye hospitali mbalimbali nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya, majibu ya ziada!

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**  
Mheshimiwa Spika, nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu. Nataka tu kuongeza sehemu ya pili ya swali la Mheshimiwa Aysharose Mattembe kwamba ni lini tutapeleka wataalam.

Mheshimiwa Spika, nataka kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hivi karibuni tutaanza kutangaza nafasi kwa hiyo tutapeleka wataalam katika hospitali za Rufaa za Mikoa.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili tumekubaliana kwamba tunataka kuzifanya kweli hospitali za Rufaa za Mikoa ziwe Hospitali za Rufaa kwa hiyo tumetangaza nafasi tutafundisha wataalam watano katika kila Mkoa kwenye masuala ya usingizi, magonjwa ya akina mama, magonjwa ya watoto, upasuaji na mifupa.

Kwa hiyo niwaombe Waheshimiwa Wabunge kuwahamasisha Madaktari walio katika mikoa yao walete maombi, hatutampeleka mtu ambaye hatoki katika hospitali hizi za Serikali na Mashirika yasiyo ya Kiserikali.(Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana. Swali la mwisho linaenda Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, linaulizwa na Mheshimiwa David Silinde.

Na. 40

### **Kupandishwa Hadhi Barabara ya Kakuzi - Kapele**

**MHE. DAVID E. SILINDE** aliuliza:-

Barabara ya kutoka Kakuzi - Kapele mpaka Ilonga ina kilometa 50.6, pia inaunganisha Mkoa wa Songwe na Rukwa bado ipo chini ya Halmashauri pamoja na maombi ya kuipandisha hadhi kupitia vikao vyote ikiwemo *Road Board* kukubali.

Je, ni kwa nini Serikali inachelewa sana kuipandisha hadhi barabara hiyo ili ihudumiwe na *TANROADS* kutokana na umuhimu wake.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Momba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kupandishwa hadhi barabara unafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007 na Kanuni zake za mwaka 2009. Aidha, maombi ya kupandisha hadhi barabara ya

Wilaya ya Kakozi - Kapele hadi Ilonga kuwa ya Mkoa yamepokelewa na yatafanyiwa kazi na Wizara sambamba na maombi kutoka Mikoa mingine. Mara baada ya kukamilika kwa zoezi hilo taarifa itatolewa na Serikali kupitia kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Songwe.

**SPIKA:** Jibu fupi, zuri kabisa. Mheshimiwa Silinde hujaridhika? Swali la nyongeza.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, ukiliangalia jibu unaona kweli fupi na linaridhisha.

Mheshimiwa Spika, nina maswali madogo mawili ya nyongeza, ni nini kinachochelewesha Wizara kuchukua hatua ya kujibu barabara zote ikiwemo hii ya Kakozi - Kapele mpaka Ilonga, kupata majibu mapema iwezekanavyo tofauti na jibu ambavyo limewekwa hapa?

Jambo la pili, barabara hii tulikuwa tunaiomba kupandishwa hadhi karibu mara tatu kukamilisha vigezo, mwaka 2011, mwaka 2013 na mwaka 2015 kupitia *Road Board* ya zamani tulipokuwepo ya Mkoa wa Mbeya. Wizara mlitushauri tuombe *special funds* kwa ajili ya kuikarabati barabara hii, tumeomba fedha na mpaka sasa hazijaja.

Kwa nini mnatushauri tuchukue maamuzi ambayo hamuwezi kutekeleza? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Profesa Mbarawa majibu.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli inachukua muda mrefu, baadhi ya kati, kupandisha hizi barabara kwa sababu kuna mchakato lazima na tujiridhishe *whether* barabara hiyo imekidhi viwango au sivyoy. Vinginevyo kila maombi tunayoletewa kama tutazipandisha itakuwa hatufanyi sahihi. Kuna utaratibu ambao umewekwa na vigezo ambavyo vimewekwa kuhakikisha kwamba barabara hiyo inakidhi vigezo hivyo ndiyo ipandishwe.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa barabara ya Mheshimiwa Silinde, ni kweli barabara hii inakidhi. Kwanza barabara hii inaunganisha mpaka baina ya Tanzania na Zambia; pili inaunganisha Mkoa wa Rukwa ambao kwa upande wa Mkoa wa Rukwa barabara hii ni ya Mkoa lakini kwa upande wa Mkoa wa Songwe ni ya Wilaya (*District Road*). Kwa vile tutaipandisha na baada ya kuipandisha, fedha hizo tutatoa ili kuikarabati barabara hii.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mtaona kwamba muda wa maswali umeisha kwa kweli, ninawashukuru sana. Sasa tuendeleo na shughuli zilizo mezani kwetu.

Waheshimiwa Wabunge, nitaanza na wageni walioko Bungeni. Wageni watatu wa Mheshimiwa William Lukuvi, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambao ni Ndugu Yamungu Kayandabila, Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Katibu Mkuu pale ulipo karibu sana. Ndugu Michael Luena, Mkurugenzi wa Sheria, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi karibu sana wako *Speaker's Lounge* pale. Ndugu Evelyne Mugasha, Kaimu Mthamini Mkuu wa Serikali, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni watano kutoka Chama cha Waandishi wa Habari za Bunge kutoka Bunge la Ghana. *Those guest of ours from Ghana, it is Ghana Parliamentary Press, you are welcome to Tanzania.* Ni ndugu Andrew Edwin Arthur, Ndugu Stephen Odoi Larbi, Ndugu Francis Kyei, Ndugu George Wilson Kingson na Ndugu Simon Akwatulim Agianab. *You are warmly welcome. (Makofi)*

Tunao pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni watatu wa Mheshimiwa Jumaa Aweso ambao ni ndugu zake kutoka Pangani, Mkoa wa Tanga Ndugu Ramadhani Khalid, Ndugu Nassir Said na Ndugu Dhahiru Maamuni, karibuni sana ndugu zetu kutoka Pangani kule Pwani.

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Maria Kangoye ambaye ni Ndugu Christine Mosore ni Mwanzilishi na Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya *Mosorec International Foundation* iliyopo nchini Marekani. Ahsante sana, karibu sana Christine. *(Makofi)*

Wapo wageni wa Mheshimiwa Juma Nkamia ambao ni walimu watatu pamoja na wanafunzi 30 kutoka shule ya sekondari ya Makole ya Mjini Dodoma. Wanafunzi wa Makole karibuni sana walimu na wanafunzi wa Makole.

Mwisho tunao wageni Tisa kutoka Benki ya Amana ya Jijini Dar es salaam wakiongozwa na Mkurugenzi wa Benki hiyo Ndugu Muhsin Salim Masoud, karibuni sana ndugu zetu wa Amana na niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba keshokutwa, siku ya Jumamosi tutakuwa na semina maalum ambayo tutapata ujumbe maalum kutoka kwa Ndugu zetu wa *Amana Bank*.

**MBUNGE FULANI:** Ni leo.

**SPIKA:** Ni leo eehh? Basi nimepitiwa nirekebishe, ni leo, karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo la semina. Katibu wa Bunge anaomba kuwakumbusheni Waheshimiwa Wabunge kwamba leo Alhamisi tarehe 8 Septemba, kutakuwa na semina kwa Wabunge wote kuhusu kazi za Benki ya Amana Tanzania katika Ukumbi wa Msekwa kuanzia saa 7.30 mchana. Naomba Waheshimiwa Wabunge wote muweze kushiriki pale, hamuwezi kujua kunaweza kukawa na kuhusu utaratibu kule. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wote niwatakie kila la kheri watoto wetu wa darasa la saba ambao wanamalizia mitihani yao leo popote pale walipo nchini, kwa niaba ya Wabunge wote niwahakikishie watoto wetu wanaofanya mitihani kwamba Wabunge hawa wanaahidi kwamba kila mtoto atakayepata alama za ufaulu wa kwenda sekondari, Wabunge tutajitahidi kuhakikisha kwamba anapata fursa hiyo. Kwa hiyo tunawapongeza sana walimu wote, wazazi, Serikali kwa maana ya Wizara ya Elimu, TAMISEMI na wote wanaohusika na jambo hili la mitihani Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi kwa jambo hili linaloendelea katika nchi yetu. *(Makofi)*

Jambo la pili ni la ushauri wa jumla lakini gumu kidogo nitaomba tuvumiliane. Ninaushauri wa jumla kwa baadhi ya Vyama vya Upinzani, narudia tena baadhi.

Kuna utaratibu ambao umekuwa ukiendelea binafsi kama Spika siupendi kidogo, wa kufukuza fukuza Wabunge kienyeji enyeji. Ningependa vyama hivi vijifunze kutoka kwa Chama cha Mapinduzi. Chama cha Mapinduzi sijasikia wakifukuza fukuza Mbunge toka nimeingia hapa Bungeni, sijasikia. *(Makofi)*

Haimaanishi kwamba kwenye Chama hiki cha Mapinduzi hawa wote ni Malaika. Wako watu ni kichwa ngumu kweli lakini hawafukuzani hovy hovy. Kwa sababu kumpata Mbunge wa kuchaguliwa jamani ni shughuli kubwa, pevu na Mbunge huyu siyo lazima awe amechaguliwa na wanachama wa chama chenu ninyi.

Mara nyingi Mbunge huyu anakuwa amechaguliwa na wananchi walio wengi halafu ninyi mnaka wachache mnamfukuza. Pili ni gharama kubwa sana kumpata Mbunge mwingine. Gharama kwa Serikali, gharama kwa chama, ni gharama kubwa na shughuli pevu. *(Makofi)*

Kwa hiyo ushauri wa jumla ndiyo maana nimesema nimeomba radhi mapema msinishambulie nitoe tu mawazo yangu kwamba ni vizuri kwa kweli tukimpata Mbunge tuvumiliane naye, mambo madogo tumalize huko ndani. Kwa hiyo, katika hili naomba mkiige Chama cha Mapinduzi naona ni moja ya mambo mazuri ambayo wanafanya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea kama kuna chochote siyo katika haya niliyosema, naona nimechokoza mjadala hapa. Kwa mengine yoyote lakini siyo katika haya niliyosema. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Taarifa kidogo.

**SPIKA:** Taarifa kutoka wapi?

**MBUNGE FULANI:** Kutoka hapa.

**SPIKA:** Taarifa hapewi Spika.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo.

**SPIKA:** Taarifa unampa Mbunge mwenzako anayeongea huko. Wale wanaotaka miongozo tajeni majina yenu, tumieni vyombo, Mheshimiwa Katani, Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Frank Mwakajoka, Mheshimiwa Pauline Gekul, Mheshimiwa Magdalena Sakaya na Mheshimiwa Susan Lyimo. Kwa kifupi sana kwa sababu muda wetu ni mdogo leo tuna sheria ambayo ni lazima tumalize leo. Tuanze na Mheshimiwa Katani.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Spika, nasimama kwa Kanuni ya 68(7). Kusemea suala la vyama vya upinzani ambavyo vina Katiba zake na kama watu wanavunja Katiba za vyama...

**SPIKA:** Mheshimiwa Katani naomba ukae chini. *(Makofi)*

Nimesema ninatoa mawazo yangu na nimeomba radhi mapema hata kama mtu hayapendi. Tatizo letu Watanzania ni kufika mahali ambapo hatutaki kusikiliza maoni ya mtu mwingine. Kama mtu anatoa maoni tusikilize tu na akishatoa Spika ndiyo *final* huwezi kufungua mjadala, ndiyo Kanuni zetu. Hoja yangu ni kwamba ninyi mmenichagua mimi, uongo au kweli? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kweli.

**SPIKA:** Kwa hiyo, mimi ni Mwakilishi wenu pia! Mnapopata matatizo lazima niwasemee. Mnapofukuzwa hovyoy siwezi kufurahia. Tunaendelea na Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru ingawa hii hoja ilikuwa nzuri sana, sasa nisiende huko, usinyime fursa, siendi kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kupata fursa hii. Ninaomba Mwongozo wako kupitia Kanuni ya 68 (7).....

**MBUNGE FULANI:** *(Hakutumia kipaza sauti).*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Hivi unafikiri mimi ni kilaza kama wewe?*(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kuna mambo ambayo yanaendelea Tanzania hapa, sasa nikataka nipate tu Mwongozo wako kwa niaba ya Bunge hili Tukufu na kwa niaba ya Watanzania wote, kwamba Wizara ya Afya na hasa Muhimbili na maeneo mengine ninayoyafahamu Hospitali ya Amana, Hospitali ya Temeke na Kinondoni. Kumekuwa na utaratibu ambao ukiwa na mgonjwa wanaruhusu anatibiwa halafu baadaye ikitokea bahati mbaya akafariki, unazuiliwa ile maiti mpaka ulipe gharama zote, bila kujali kama ni mtoto, ni mtu mzima ama ni mzee una uwezo au huna uwezo. Sasa nataka nipate tu Mwongozo wako kwamba katika mambo haya kwa Watanzania wenzetu inakuaaje?

Mheshimiwa Spika, hiyo ndiyo hoja yangu. Ninakushuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waitara umetumia Kanuni ya 68(7) ambayo inasema; "Hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema."

Sasa hilo limetokea Bungeni mapema lini tena? Mheshimiwa Gekul

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika nakushukuru nipate nafasi nipate Mwongozo wako.

Mheshimiwa Spika naomba Mwongozo wako kuhusu jambo ambalo limetokea mapema humu ndani, maswali kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nafahamu kwamba huko tulikotoka utaratibu ulikuwa siyo mzuri sana *at least* sasa uko-*modified*, lakini bado haukidhi.

Nilikuwa naomba mwongozo wako ni kwa nini Kiti chako na uongozi wako usitusaidie Wabunge mka-review Kanuni ya 38(3) na 38(7) katika suala zima la dakika 30 kwa siku ya Alhamis, lakini Kanuni 38(7) kuhusu maswali mengine kuendelea siku ya Alhamis, hasa kipindi cha Kikao ambacho ni kifupi kama hiki, siku za Alhamis zinakuwa kama mbili tu. Ni kwa nini siku ya Alhamis isitumike sasa kwa ajili ya Maswali kwa Waziri Mkuu, kwa sababu hata *list* uliyonayo hapo mezani kwako ni wengi sana waliomba na ni wengi wamekosa.

Mheshimiwa Spika, pia Mwongozo ulitoka mapema kwamba tukishatoka jioni, Bunge likiahirishwa kama jana ilikuwa takribani saa 2.30 usiku ndiyo Wabunge waende sasa kule ofisini wajiorodheshe, lakini kwa hali halisi jana watu wamekaa tangu saa sita wakisubiri muda ule wa saa mbili na nusu hata



humu ndani hawakuingia. Unaona ni jinsi gani ambavyo Wabunge wanakaa muda mrefu kule hata humu ndani hawawezi kuingia kuonesha unyeti wa maswali hayo kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako, kwa nini msiangalie upya suala hili la Maswali kwa Waziri Mkuu ilhali Wabunge wameshaongezeka na muda hautoshi? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, hilo halihitaji mwongozo, ni mapendekezo ya mabadiliko ya Kanuni ambayo unaweza ukayaleta katika utaratibu wa kawaida ili tutakapofika wakati wa kuangalia ni mambo gani tuyarekebishe katika Kanuni zetu tuweze kuzingatia wote kwa pamoja tuone kama kuna uhitaji wa jambo hilo.

Tunaendelea na Mheshimiwa Mwakajoka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Na mimi natumia Kanuni ya 68(7) hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo...

**SPIKA:** Endelea tu.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako kutokana na majibu ya Serikali hasa wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu akijibu maswali mbalimbali ambayo yalikuwa yanahusu mambo ya uchumi.

Mheshimiwa Spika, katika majibu ambayo yametolewa ni kwamba, Serikali inaonyesha kabisa kwamba haitaki kupokea ushauri, kwa sababu hapa nina *sample* tu ya Kampuni moja ya Impala ambayo ilikuwa inasafirisha *copper* kutoka Zambia kupitia Bandari ya Dar es Salaam ambayo kwa mwezi mmoja tu ilikuwa inasafirisha karibu tani 35,000 za *copper* kupitia Bandari ya Dar es Salaam na kila tani moja walikuwa wanalipa karibuni dola 600 na sasa hivi kampuni hii inapitia Durban, na sasa hivi ukijaribu kuangalia taarifa ambazo tunazo kutoka Durban ni kwamba wamesafirisha tani 55,000 kwa mwezi huu peke yake.

Mheshimiwa Spika, jambo hili kama Serikali haitaki kupokea ushauri wa Waheshimiwa Wabunge na wadau mbalimbali inaonesha ni jinsi gani tunavyopata athari katika nchi yetu. Kwanza hata wauza mafuta kwenye nchi hii leo...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwakajoka ningekuomba kidogo ukae.

Mimi ningependa tutumie vizuri muda huu ambao tunapata badala ya kuanzisha malumbano, hakuna mahali ambapo Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema Serikali haitaki kupokea ushauri, hakuna mahali kama hapo!

Pili, uchumi wa nchi huwezi kulinganisha na suala la Kampuni moja inayoitwa Impala, yaani unatuweka mahali pagumu tu kidogo. Kwa hiyo nakushukuru kwa mawazo yako Serikali imesikia. Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mwongozo wangu tayari umeshaujibu ilikuwa ni suala la Maswali kwa Waziri Mkuu ambalo kwa kweli limekera sana, kwa hiyo nashukuru kwa Mwongozo wako.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sakaya, mwisho.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nasimama pia kwa Kanuni hiyo hiyo ya 68(7). Tumekuwa tunaomba vitabu vya Kumbukumbu za Wabunge hapa Bungeni kwa muda mrefu na kwa bahati nzuri juzi vimetolewa ila vimetolewa vichache, wengi tumekosa na tunapouliza watumishi wetu huku ndani pia wanakuwa hawana majibu, kwa hiyo, tunaomba tujue vitabu hivyo tunavipata lini kwa wote. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Ofisi yangu ya Katibu imeshapata habari, kesho mtapata maelezo ya kutosha ya nini kinachoendelea, ni nia yetu kuhakikisha kila Mbunge anapata nakala na kama nilivyoeleza mwanzoni nakala zipo nzuri zina picha ya kila mmoja wetu, wengi bado hatufahamiani vizuri vitabu hivi vitatusaidia sana katika kufahamiana vizuri. Tunaendelea. Katibu.

**NDG. ASIA MINJA - KATIBU MEZANI:**

### **MISWADA YA SHERIAYA SERIKALI**

#### **Muswada wa Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini wa mwaka 2016 (*The Valuation and Valuers Registration Bill, 2016*)**

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Ninakuita mara ya pili Katibu tena eeh! Ni hapo tu?

Nawashukuru sana. Kwa hatua hii sasa ninamuomba nimuite Mwenyekiti, Mheshimiwa Najma Giga aje aendelee na utaratibu.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea namkaribisha mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Ardhi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na hatimaye kupitisha Muswada wa Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini 2016 (*The Valuation and Valuers Registration Act, 2016*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii ya pekee kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii na Wajumbe wote wa Kamati hii ya Kudumu kwa ushauri na mapendekezo ambayo yamesaidia sana kuboresha maudhui ya muswada huu kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho litakalotolewa hivi punde humu Bungeni.

Aidha, nawashukuru sana pia Waandishi wa Sheria chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na watumishi wengine wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu pamoja na watumishi wa Wizarani kwangu walioandaa muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada wa Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini wa mwaka 2016, pamoja na Jedwali la Marekebisho unapendekeza kutungwa kwa Sheria itakayosimamia taaluma ya uthamini. Sheria inayopendekezwa kutungwa itasaidia kuratibu shughuli za uthamini nchini pamoja na kuunda chombo cha usimamizi na usajili wa wathamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inayokusudiwa kutungwa itawezesha wanataaluma wa uthamini kutenda kazi kwa kujiamini, kuzingatia maadili pamoja na kulinda haki za watumiaji wa huduma ya uthamini. Sheria inayopendekezwa itapunguza migogoro ya ardhi inayosababishwa na kutozingatiwa weledi katika utendaji wa Wathamini na kupelekea uwepo wa viwango tofauti vya thamani kinyume na miongozo inayokubalika ya uthamini ya Kikanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu ni mwendelezo wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 inayotambua kwamba ardhi ina thamani na itumike katika miamala yote ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inayopendekezwa itabainisha taratibu rasmi za utendaji wa wathamini. Pia itatumika kama mwongozo kwa shughuli zote za uthamini zitakazofanyika kwa madhumuni mbalimbali. Aidha, sheria itarasimisha taratibu za uthamini ambazo awali hazikuwa zimewekewa utaratibu wa kisheria na hivyo kuboresha mazingira ya kiutendaji. Sheria hii pia imezingatia haki za watumiaji wa huduma ya uthamini kama zinavyoainishwa kwenye sheria nyingine na miongozo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inayopendekezwa itatatua migogoro ya matumizi ya ardhi inayotokana na Wathamini kutozingatia maadili ya uthamini pamoja na kazi ya uthamini kufanywa na watu wasiokuwa na sifa za kazi hiyo na hivyo kusababisha ucheleweshaji wa ulipaji fidia, kupanda kwa fidia husika za gharama za miradi na kuchelewa kuanza utekelezaji wa miradi mbalimbali, ikiwemo miradi ya ujenzi na uwekezaji kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muswada huu unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini wa mwaka 2016, itakayoweza kuweka mfumo wa kitaifa wa utendaji na usimamizi wa wathamini nchini, kujenga miundombinu ya utoaji huduma za uthamini, kuanzisha mamlaka za usimamizi pamoja na kuweka mazingira yatakayoweza taaluma ya uthamini kutambulika na kushamiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo muhimu yaliyozingatiwa katika muswada huu ni pamoja na yafuatayo:-

(a) Kuanzisha mamlaka ya usimamizi wa fani ya uthamini nchini kwa ajili ya kuratibu na kusimamia shughuli za uthamini katika sekta ya umma na sekta binafsi;

(b) Kubainisha majukumu ya Mamlaka hiyo, mipaka na mahusiano na taasisi nyingine zenye maslahi na huduma ya uthamini;

(c) Kusimika mfumo wa kitaifa wa kiutawala na kubainisha majukumu ya kiusimamizi katika kila ngazi;

(d) Kuanzisha Bodi ya Usajili wa Wathamini, kubainisha majukumu ya bodi, taratibu za uteuzi wa wajumbe wa bodi na kipindi cha bodi;

(e) Kubainisha aina za madaraja ya Usajili wa Wathamini na taratibu za kufanya kazi katika kila daraja;

(f) Kuanzisha taratibu mpya za kusajili wathamini kwenye madaraja mbalimbali, zitazozingatia ufaulu wa mitihani;

(g) Kubainisha makosa mbalimbali ya kitaaluma na adhabu zake;

(h) Kuweka taratibu za utendaji kwa wathamini ambao siyo Watanzania;

(i) Kubainisha Mamlaka ya Bodi katika kusimamia taaluma ikiwemo kuhakikisha Wathamini waliosajiliwa wamehudhuria mafunzo ya kujiendeleza kama sharti la kuendelea kusajiliwa;

(j) Kuweka taratibu za kuwafuta wadhamini toka kwenye rejesta ya Bodi, hususan kwa kukiuka maadili ya taaluma;

(k) Kubainisha mahusiano yaliyopo kati ya Waziri wa Sekta na Bodi;

(l) Kuiwezesha Bodi kuunda Kamati ndogo kulingana na uhitaji;

(m) Kuiwezesha Bodi kuwa na daftari la kumbukumbu za Wathamini wote nchini litakaloonesha madaraja yao ya usajili na sehemu walipo;

(n) Kuwezesha uwepo wa taratibu za rufaa, kwa wasioridhishwa na maamuzi ya Bodi au maamuzi ya Mthamini Mkuu wa Serikali;

(o) Kurasimisha aina mbalimbali za uthamini, misingi ya uthamini na mbinu za ukadiriaji thamani za mali zinazohamishika na zisizohamishika;

(p) Kurasimisha miongozo na taratibu za uthamini kwa madhumuni mbalimbali kama njia ya kuipa nguvu ya kisheria na kurahisisha utendaji; na

(q) Kuweka kipengele kitakachomwezesha Waziri mwenye dhamana kuandaa Kanuni za utekelezaji wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muswada umegawanyika katika sehemu kuu saba. Sehemu ya Kwanza ya Muswada inahusu masharti ya awali yakiwemo jina la Sheria inayopendekezwa, matumizi yake, pamoja na tafsiri za maneno na misamiati iliyotumika katika muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Pili inahusu Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali. Chini ya Sehemu hii, Ofisi ya Mthamini Mkuu itaendelea kutambulika kama Idara iliyo chini ya Wizara yenye dhamana na masuala ya ardhi. Aidha, sehemu hii itabainisha utaratibu wa uteuzi wa Mthamini Mkuu wa Serikali, Wathamini Wakuu Wasaidizi na Wathamini Waidhinishwa. Muundo huu wa Ofisi ya Mthamini Mkuu utahakikisha kwamba Wathamini Wakuu Wasaidizi watawekwa katika kila Kanda na watakuwa ni wasimamizi wa shughuli za uthamini zinazofanywa na Wathamini wa Serikali na Wathamini Waidhinishwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mikoa na Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tatu inabainisha muundo wa Bodi ya Usajili wa Wathamini, utaratibu wa uanzishwaji wa Bodi pamoja na kufafanua majukumu na mamlaka ya Bodi. Aidha, sehemu hii inapendekeza utaratibu wa uteuzi wa msajili ambaye atawajibika kusimamia utekelezaji wa siku kwa siku wa shughuli za Bodi. Ili kuongeza uwazi, nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi itatangazwa na kila mwenye sifa ataruhusiwa kuomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Nne ya Muswada inahusu Usajili na Uorodheshwaji wa Wathamini. Usajili unapendekezwa kufanyika katika makundi matatu ambayo ni usajili kamili, usajili wa muda na usajili wa mpito. Usajili kamili utafanyika kwa Wathamini wenye uzoefu wa angalau miaka mitatu mbali na kuwa na sifa za msingi za kitaaluma. Usajili wa muda utahusu Wathamini ambao siyo Watanzania. Usajili wa mpito utakuwa ni kwa wahitimu wa masomo ya uthamini na wengineo ambao hawajatimiza muda wa kupata usajili wa kudumu. Kwa upande mwingine, uorodheshwaji wa Wathamini utakuwa ni kwa ajili ya Wathamini ambao wana vyeti au Stashahada katika taaluma ya uthamini. Wathamini walioorodheshwa au Wathamini Wasaidizi wataruhusiwa kusaidia kazi za uthamini chini ya usimamizi wa Wathamini waliosajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala mengine kuhusu kukubali au kukataa maombi ya usajili, uhalali wa cheti, haki na stahili za Wathamini waliosajiliwa au kuorodheshwa, rejesta, ukaguzi wa rejesta na kusitisha kwa muda au kufutwa kwa cheti cha usajili yamefafanuliwa kwa kina.

Sehemu ya Tano inahusu mwongozo kuhusiana na uendeshaji wa shughuli za uthamini, ambapo masuala yote yanayohusu aina za uthamini, madhumuni, misingi na mbinu za uthamini yamefafanuliwa kwa kina.

Aidha, sehemu hii inapendekeza masharti kuhusu uhalali wa uthamini, muda wa ukomo wa uthamini na masuala mengine yanayohusu kuingia katika ardhi au majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Sita ya Muswada inahusu masharti kuhusu fedha, ambapo masuala yanayohusu vyanzo vya mapato ya Bodi, hesabu na ukaguzi wa hesabu pamoja na taarifa ya mwaka kuhusu utendaji kazi wa Bodi yameainishwa kwa ufasaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya Saba inapendekeza masharti ya jumla. Sehemu hii inahusu masuala ya miiko ya maadili ya kitaaluma kwa wathamini wa Serikali na Wathamini Waidhinishwa, ada za uthamini, makosa na adhabu, kanuni (*regulations*) zitakazotengenezwa na Waziri, na *rules* za Bodi na masharti ya mpito na yale yanayoendelea. Aidha, sheria inayopendekezwa kutungwa itakuwa sheria mama kwenye masuala yote yanayohusu uthamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muswada unapendekeza majedwali mawili yanayohusu masharti na taratibu za Bodi na pia marekebisho yatoakanayo ambapo sheria zote ambazo kwa namna moja au nyingine zitaathirika kutokana na sheria inayopendekezwa, zinapendekezwa kufanyiwa marekebisho. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Ardhi, Sheria ya Ardhi ya Vijiji na Sheria ya Usajili wa Wapima Ardhi na Wathamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu taaluma na huduma za uthamini zimekuwa na usimamizi hafifu uliopelekea kuwepo kwa changamoto mbalimbali. Hivyo sheria inayopendekezwa leo kutungwa na Waheshimiwa Wabunge italeta manufaa mengi. Machache kati ya hayo ni haya yafuatayo:-

(i) Sheria hii Waheshimiwa Wabunge mkikubali kuitunga itawaondoa kwenye mateso wananchi wanaothaminiwa mali zao na kuchelewa kulipwa fidia kwa kuweka ukomo wa muda ambao fidia lazima ilipwe na kuwadhibiti wawekezaji wote kulipa fidia kwa wakati. Hii itapunguza kwa kiasi kikubwa migogoro ya fidia ambayo imekuwa ikileta kero kubwa kwa wananchi ambao ardhi yao imekuwa ikichukuliwa kwa ahadi ya kulipwa fidia na hailipwi kwa wakati;

(ii) Sheria hii itawachuja na kuwaondoa sokoni Wathamini wote ambao hawana sifa, matapeli na wadanganyifu ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakilitia hasara Taifa;

(iii) Kuondoa utapeli uliokuwa unafanywa na Wathamini wa kuongeza thamani kinyume cha utaratibu na kuongeza wafidiwa hewa katika jedwali la fidia, ambapo Serikali imekuwa ikipata hasara kubwa kwa kulipa wadai hewa;

(iv) Kudhibiti uthamini wa kifisadi ambao umekuwa ukifanywa na baadhi ya Wathamini kwa kushusha thamani ya mali kwa madhumuni ya kukwepa kodi sahihi na stahili kwa Serikali;

(v) Kuondoa udanganyifu unaofanywa na Wathamini wa kuongeza thamani kinyume cha uhalisia kwa mali zitumikazo kama rehani ya mikopo ili kujipatia mikopo mikubwa kwenye mabenki; Hili limekuwa linafanywa kwa maksudi na wakati mwingine mali za maskini zinapouzwa napo wanafanya mali inakuwa ndogo ili maskini waweze kupunjwa; *(Makofi)*

(vi) Kuwadhibiti baadhi ya Wathamini wanaokula njama na wanaume. Wanawake hapa lazima msikilize; ili kushusha ama kupandisha thamani ya mali za wanandoa kwa nia ya kuwapunja akinamama katika mgawanyo wa mali za wanandoa; *(Makofi)*

(vii) Kwa usajili wa Wathamini chini ya Sheria hii pendekezwa, kutakuwa na mfumo mzuri wa kuwawajibisha Wathamini wote wanaokiuka maadili ya kitaaluma, kutoa adhabu kwa Wathamini wanaokiuka sheria ikiwa ni pamoja na kifungo gerezani, faini, kusimamishwa na kufutiwa usajili. Zamani ilikuwa Wathamini akichezea mahali anafukuzwa kazi lakini anaendelea na kazi ya kuthamini mitaani. Anafungwa anaendelea na kazi ya kufanya uthamini - sasa ukinyang'anywa leseni hutafanya kazi ya taaluma maisha yako yote;



(viii) Kuondoa urasimu katika upatikanaji wa huduma za uthamini kwa kusogeza huduma hizo katika Kanda na Serikali za Mitaa, Mikoa na Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya machache ambayo naamini Waheshimiwa Wabunge mmenielewa na kupitia kwako kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, kuujadili muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho na kuupitisha katika hatua mbili yaani Kusomwa Mara ya Pili na Mara ya Tatu. Nina imani kwamba Bunge lako litaridhia kutungwa kwa sheria itakayosimamia Uthaamini na Usajili wa Wathamini Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti,naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Naona hoja imeungwa mkono na ahsante sana kwa kutumia muda sasa tunamkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa ajili ya kutoa maoni yao.

**MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yafuatayo ni maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Muswada wa Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini wa mwaka 2016 *(The Valuation and Valuers Registration Act, 2016)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utangulizi;kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Muswada wa Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini wa mwaka 2016 *(The Valuation and Valuers Registration Act, 2016)* uliotolewa kwenye Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 84 Sehemu ya Kwanza ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya tarehe 23 Agosti na tarehe 2 Septemba, 2016 Kamati ilikutana na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa William Lukuvi na Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa Angelina Mabula pamoja na Watendaji mbalimbali wa Wizara ya Ardhi katika Ukumbi wa Pius Msekwa uliopo ndani ya Ofisi ya Bunge Mjini Dodoma na kupokea maelezo kuhusu madhumuni na umuhimu wa Muswada wa Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini wa mwaka 2016.

Mheshimiwa Mweyekiti, katika maelezo yake Mheshimiwa Waziri alieleza Kamati kuwa lengo kuu la Muswada huu ni kutunga sheria moja itakayoweza kusimamia taaluma na shughuli za uthamini Tanzania bara, kwa lengo la kupunguza changamoto mbalimbali zinazoikabili jamii na sekta ya ardhi kwa ujumla. Aidha, alitaja mapendekezo mbalimbali yanayokusudiwa kutungiwa sheria, mapendekezo hayo ni pamoja na yale yanayoainisha mamlaka na majukumu ya Mthamini Mkuu wa Serikali yanayoanzisha Bodi ya Usajili wa Wathamini yanayoainisha majukumu na muundo wa uongozi wa Bodi pamoja na eneo linalohusu udhibiti na usimamizi wa taaluma na kazi za uthamini kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kamati kusikiliza maelezo ya Serikali kama nilivyoieleza hapo juu, ilizingatia masharti ya Kanuni ya 84 (2) na 117(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 kwa kuwaadika wadau mbalimbali mbele ya Kamati na kutoa maoni, tafsiri na matokeo ya Sheria inayopendekezwa kwa mazingira halisi ya utekelezaji wake. Wadau waliofika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao siku ya tarehe 25 na 26 Agosti, 2016 ni pamoja na *Tanganyika Law Society, Tanzania Bankers Association, Ardhi University, TANESCO, Tanzania Institute of Valuers and Estate Agents, Contractors Registration Board, Architects and Quantity Surveyors Registration Board, Tanzania Revenue Authority na National Council of Professional Surveyors.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru wadau wote ambao waliwasilisha maoni yao ambayo kwa kiasi kikubwa yamesaidia kuboresha muswada huu hadi kufikia hatua ulivyo sasa. Tunawashukuru kwa dhafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada wa Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini wa mwaka 2016 una Sehemu Kuu Saba zenye jumla ya vifungu 73 pamoja na majedwali ya marekebisho. Kamati iliupitia kwa umakini na kufanya uchambuzi wa kina na kujiridhisha na mambo yote muhimu katika utungaji wa sheria inayokusudiwa. Yapo maeneo ambayo Kamati na Serikali walikubaliana kama yalivyowasilishwa katika jedwali la marekebisho na mtoa hoja. Aidha, yapo maeneo machache sana ambayo Kamati bado inaendelea kulisitiza na kuishauri Serikali kama ifuatavyo:-

(a) Katika sehemu ya kwanza ya tafsiri ya maneno, Kamati ilipendekeza neno *property* litafsiriwe vizuri zaidi kuongeza wigo wa tafsiri halisi ya neno *property* kulingana na ukubwa wa matumizi ya sheria hii ili kuongeza vitu halisi vitakavyofanyiwa uthamini kwa mujibu wa sheria hii.

(b) Aidha, Kamati inapendekeza kuongezwa kwa tafsiri ya neno *Ministry* imaanishe *Ministry responsible for lands* ili kuondoa kujirudia rudia kwa maneno *responsible for lands* ndani ya muswada.

(c) Kamati inapendekeza kuongeza maneno “*immovable assets*” kwenye tafsiri ya *nenoproperty* kwani katika tafsiri ya mwanzo hilo neno halikuwepo. Katika sehemu ya pili inayohusu Mthamini Mkuu, Kamati ilipendekeza na bahati nzuri ilikubaliana na Serikali kwamba kifungu cha 6 kinachohusu mamlaka na majukumu ya Mthamini Mkuu mara baada ya kifungu cha 6(2) kiongezwe kifungu kidogo cha (3) kitakachompa Mthamini Mkuu mamlaka ya kutekeleza majukumu yake chini ya sheria hii kwa uwazi na kutokuwa na upendeleo kwa watu wote bila kujali hali yao ya kiuchumi. Tunashukuru sana tulikwenda vizuri na Serikali.

(d) Kifungu cha 6 (1)(e) kinachohusu kuwasilisha ripoti ya uthamini kwa Waziri, kamati ilikuwa imependekeza ripoti iwasilishwe mara mbili kwa mwaka yaani kila baada ya miezi sita, lakini Serikali iliona kwamba miezi mitatu inatosha naamini imeshajipanga.

(e) Sehemu (c) kifungu cha 8 (2) kikisomwa na kifungu cha 5(2)(b) kinaeleza sifa ya kuwateua Wathamini Wakuu Wasaidizi ni lazima mtu awe na uzoefu wa kwenye tasnia ya uthamini kwa muda usiopungua miaka kumi, Kamati inapendekeza iwe ni uzoefu usiopungua miaka mitano ili kuweza kuwapa fursa vijana kujijenga kiutendaji katika nafasi za uongozi. Tukiweka miaka kumi kwa wasaidizi wakati ndiyo sifa hiyo hiyo ambayo inakwenda kwa mthamini mkuu wa serikali maana yake hatutakuwa na *succession plan* nzuri ya kuwafanya vijana waweze kulitumikia Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sehemu ya Tatu inayohusu Bodi ya Usajili, kifungu cha 13(1)(d) kinachohusu muundo wa Bodi, Kamati inashukuru kwamba walikubaliana na Serikali kwamba pawepo wawakilishi wawili toka chama cha Wathamini na siyo mwakilishi mmoja. Vilevile tunaipongeza Serikali kwa kukubaliana na pendekezo ikiwa ni pamoja na kuingiza mwakilishi toka Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) pamoja na mwakilishi toka Chama cha Mabenki Tanzania kwa kuwa wao ni wadau wakubwawa uthamini wakati wa kutoa mikopo.

Kipengele (b) katika kifungu cha 15 kinachohusu Kamati za Bodi, Muswada unapaswa ufafanue vizuri upatikanaji wa Wajumbe wa Kamati za Bodi, na iwekwe wazi kwamba Wajumbe hao watatoka ndani ya Bodi kama tulivyokubalina na Serikali, aidha, mtu yeyote ambaye siyo Mjumbe wa Bodi au Kamati aweza kualikwa ili kuisaidia Kamati katika jambo mahsus ambalo Kamati imeliainisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, (c) kifungu cha 21(3) kinachohusu upelelezi wa malalamiko Kamati inapendekeza Mthamini anayelalamikiwa apewe nafasi ya kusikilizwa Kifungu hiki vilevile tunashukuru tulikubaliana na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 23(1), kuna kosa la kiuandishi ambalo Kamati ilipendekeza lirekebishwe na Serikali ilikubaliana, Sehemu ya Nne inayohusu Usajili wa Wathamini, Kamati inapendekeza yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 25(1) Kamati inapendekeza adhabu zote ziwe endelevu kulingana na mabadiliko ya thamani ya shilingi. Aidha, kiuandishi, kifungu hiki kinapaswa kiende kifungu cha 67 ambacho kinachohusu makosa ili kuweza kuleta mtiririko mzuri wa kiuandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sehemu ya Tano inayohusu mwongozo kuhusu ufanyaji wa uthamini, Kamati ina mapendekezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kwamba katika Kifungu hiki cha 52(2) kinachohusu uhalali wa uthamini, Kamati ilikubaliana na Serikali na tunaishauri Serikali ikumbuke makubaliano tuliyokubaliana katika Kamati kuwa kwa madhumuni ya fidia, ukomo wa uhalali wa uthamini uwe ni muda wa miezi 24 au miaka miwili kwa uthamini na taarifa ya uthamini uliofanyika chini ya sheria hii. Hii ni kwa sababu ulipaji fidia huchukua muda mrefu na wananchi hulipwa chini ya thamani kwa mali iliyothaminiwa, inapotokea thamani za mali iliyothaminiwa kupanda baada ya ukomo uthamini ufanyike upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya (b) tunaikumbusha Serikali kuwa Katika Jedwali la Marekebisho lililoletwa kwenye Kamati lenye tafsiri ya Kiswahili kifungu 53(3) maneno "mtu ataruhusiwa" inabadilisha maana halisi ya kifungu hiki kwani kwenye tafsiri ya Kiingereza "A person shall not," hii maana yake badala ya neno "ataruhusiwa" lisomeke "hataruhusiwa."

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu (c) kifungu cha 55(1) Kamati inapendekeza kirekebishwe ili kumlazimu Mthamini kuwa na kibali maalum (*warrant*) ambacho kitakuwa kikitolewa na Mthamini Mkuu au Mamlaka ya Serikali za Mitaa kabla ya kuingia sehemu na kufanya uchunguzi wake kwa lengo la kuepuka watu wasiowathamini kutumia nafasi hiyo vibaya kuingia na kufanya uhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tatu, maoni na ushauri wa jumla kutokana na uchambuzi wa muswada huu Kamati inatoa maoni ya jumla kama ifuatavyo:-

(i) Ni vema sheria inayopendekezwa ipitishwe kwani itabainisha taratibu rasmi za utendaji wa Wathamini na hivyo kusaidia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995, ambayo inatambua thamani halisi ya ardhi.

(ii) Kamati inashauri kuwa sheria hii inayopendekezwa iwekewe mfumo imara wa kisheria utakaohakikisha Wathamini pamoja na shughuli zao wanawekewa utaratibu utakaowawezesha kufanya kazi kwa weledi na ustadi ipasavyo.

(iii) Kamati inashauri kuwa sheria hii iweke mfumo wa Kitaifa wa utendaji na usimamizi wa Wathamini nchini, pamoja na kuanzisha mamlaka za usimamizi wa fani ya uthamini katika sekta za umma na sekta binafsi.

(iv) Pamoja na usimamizi wa sheria hii Kamati inashauri kuwa Bodi ya Usajili wa Wathamini inayopendekezwa kuundwa ni vema isimamiwe ipasavyo kwa lengo la kupata Wathamini wenye sifa na vigezo katika kada ya uthamini kwa lengo la kuinua na kukuza taaluma ya uthamini hapa nchini.

(v) Kamati inashauri kuwa katika Bodi ya Usajili wa Wathamini ni vema Wathamini wakasajiliwa katika daftari maalumu litakaloweka kumbukumbu za Wathamini wote nchini kwa sifa, namba, mwaka waliohitimu na kusajiliwa ili kuweka madaraja katika usajili.

(vi) Kamati inaendelea kusisitiza kuwekwa kwenye sheria kipengele kinachoanisha malipo ya riba (*interest*) kwa mtu au taasisi itakayoshindwa kukamilisha malipo ya fidia mapema kipengele kitakacholeta msukumo kwa taasisi au mtu kulipa fidia mapema iwezekanavyo. Hii italeti ukombozi kwa jamii na wote ambao wangeathirika na uthamini. Hata hivyo ni dhahiri kuwa Serikali kwa kizingatia maoni ya Kamati kama tulivyokubaliana, wananchi wetu watafaidika kwani watakuwa wakilipwa malipo ya fidia mapema yaani ndani ya miezi sita tangu Mthamini Mkuu atakapoidhinisha uthamini na baada ya hapo riba italipwa kila baada ya miezi sita ndani ya miezi 24 kabla ya uthamini kufikia ukomo.

(vii) Kamati inashauri baada ya sheria hii kupitishwa ni vema isimamiwe ipasavyo kwani itasaidia katika kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi inayoendelea kuibuka kwa kasi hapa nchini inayotokana na Wathamini wasiozingatia maadili ya uthamini. Aidha, Wathamini watapaswa kuzingatia miiko yote inayopendekezwa katika sheria na kanuni kwa utendaji bora wa kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; moja ya mambo muhimu kabla ya kutunga sheria yoyote ni kujiridhisha na umuhimu wa kuwa na sheria husika. Katika kufanya hivyo, Kamati ilirejea historia ya uthamini na dhana nzima ya uthamini na usajili wa Wathamini katika nchi za Jumuiya ya Madola.

Aidha, Kamati ilifanya mlinganisho wa sheria hizo na namna zinavyotumika na kuona kuwa kuna haja kubwa ya kutungwa kwa sheria

itakayosimamia taaluma na shughuli za uthamini hapa nchini. Tunaipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu mbele ya Bunge lako Tukufu ili tuujadili na baadaye tuupitishie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Napenda pia nimshukuru Waziri wa Ardhi Mheshimiwa William Lukuvi, Naibu Waziri Mheshimiwa Angeline Mabula, Watendaji wa Wizara ya Ardhi pamoja na Watendaji wa Ofisi ya Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria kwa ushirikiano wao hadi kukamilika kwa muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee napenda pia kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Ardhi Maliasili na Utalii kwa ushauri wao ambao umesaidia kuboresha muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashilillah, Watendaji wa Ofisi ya Bunge pamoja na Sekretarieti ya Kamati wakiongozwa na Ndugu Gerald Magili, Ndugu Haika Mtui, Ndugu Elieka Saanya na Ndugu Thomson Shawa na Ndugu Jane Ndulesi kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII  
KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA UTHAMINI NA USAJILI WA WATHAMINI WA  
MWAKA 2016 [THE VALUATION AND VALUERS REGISTRATION ACT, 2016]  
KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

## **1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Muswada wa Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini wa Mwaka 2016 [The Valuation and Valuers Registration Act, 2016], ulioletwa kwenye kamati kwa mujibu wakanuni ya 84 (1) ya Kanuni za kudumu za Bunge toleo la Januari 2016.

**Mheshimiwa Spika**, kati ya tarehe 23 Agosti, 2016 na tarehe 2 Septemba Kamati ilikutana na Waziri wa Ardhi Mheshimiwa William V. Lukuvi (Mb), Naibu Waziri Mhe Dkt, Angeline L. Mabula (Mb), pamoja na watendaji mbalimbali wa Wizara ya Ardhi katika Ukumbi wa Pius Msekwa uliopo ndani ya Ofisi ya Bunge Mjini

Dodoma na kupokea maelezo kuhusu madhumuni na umuhimu wa Muswada wa Sheria ya Uthamini na Usajili wa wathamini wa Mwaka 2016.

**Mheshimiwa Spika**, Katika maelezo yake, Mheshimiwa Waziri alieleza Kamati kuwa lengo kuu la muswada huu ni kutunga sheria moja itakayoweza kusimamia taaluma na shughuli za uthamini Tanzania Bara kwa lengo la kupunguza changamoto mbalimbali zinazoikabili jamii na sekta ya ardhi kwa ujumla. Aidha alitaja mapendekezo mbalimbali yanayokusudiwa kutungiwa sheria, mapendekezo hayo ni pamoja na yale yanayoainisha mamlaka na majukumu ya Mthamini Mkuu wa Serikali, yanayoanzisha Bodi ya usajili wa wathamini, yanayoainisha majukumu na muundo wa uongozi wa Bodi, pamoja na eneo linalohusu udhibiti na usimamizi wa taaluma na kazi za uthamini kwa ujumla wake,

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya Kamati kusikiliza maelezo ya Serikali kama nilivyoieleza hapo juu, ilizingatia masharti ya Kanuni ya 84(2) na 117 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 kwa kuwaadika wadau mbalimbali mbele ya kamati na kutoa maoni, tafsiri na matokeo ya Sheria inayopendekezwa kwa mazingira halisi ya utekelezaji wake. Wadau waliofika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao siku ya tarehe 25 na 26 Agosti, 2016 ni pamoja na Tanganyika Law Society, Tanzania Bankers Association, Ardhi University, Tanesco, Tanzania Institution of Valuers and Estate Agents, Contractors Registration Board, Architects and Quantity Surveyors Registration Board, Tanzania Revenue Authority na National Council of Professional Surveyors.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru wadau wote ambao waliwasilisha maoni yao ambayo kwa kiasi kikubwa yamesaidia kuboresha Muswada huu hadi kufikia hatua ulivyo sasa, tunawashukuru kwa dhati.

## 2.0 UCHAMBUZIWA MUSWADA

**Mheshimiwa Spika**, Muswada wa Sheria ya Uthamini na usajili wa Wathaminiwa Mwaka 2016 [*The Valuation and Valuers Registration ACT, 2016*] una sehemu kuu **saba (7)** zenye jumla ya **vifungu 73**, pamoja na majedwali ya marekebisho. Kamati iliupitia kwa umakini na kufanya uchambuzi wa kina na kujiridhisha na mambo yote muhimu katika utungaji wa sheria inayokusudiwa. Yapo maeneo ambayo Kamati na serikali walikubaliana kama yalivyowasilishwa katika jedwali la marekebisho na mtoa hoja. Aidha yapo maeneo mengine ambayo bado kamati inaendelea kusesitiza ifuatavyo:-

(a) Katika sehemu ya kwanza ya tafsiri ya maneno Neno **“property”** litafsiwiwe vizuri kuongeza wigo wa tafsiri halisi ya neno *property* kulingana na ukubwa na



matumizi ya sheria hii ili kuongeza vitu halisi vitakavyofanyiwa uthamini kwa mujibu wa sheria hii.

(b) Kamati inapendekeza kuongezwa kwa tafsiri ya neno '**Ministry**' imaanishe "**Ministry responsible for lands**" ili kuondoa kujirudiarudia kwa maneno "**responsible for lands**" ndani ya muswada.

(c) Aidha inapendekeza kuongeza maneno "**immovable assets**" kwenye tafsiri ya neno **property** katika tafsiri ili kuongeza wigo wa vitu vitakavyo fanyiwa uthamini kwa mujibu wa sheria hii.

(ii) Katika sehemu ya pili inayohusu Mthamini Mkuu kamati inapendekeza mambo yafuatayo:-

(a) Kifungu cha sita kinachohusu mamlaka na majukumu ya Mthamini Mkuu. Mara baada ya kifungu cha 6 (2) kiongezwe kifungu kidogo cha tatu (3) kitakachompa Mthamini Mkuu mamlaka ya kutekeleza majukumu yake chini ya sheria hii kwa uwazi na kutokuwa na upendeleo kwa watu wote bila kujali hali yao ya kiuchumi. Aidha, kifungu hiki ili kuleta mantiki iliyo sahihi, kisomwe pamoja na kifungu cha 6 (1) (h)

(b) Kifungu cha 6 (1) (e) kinachohusu kuwasilisha ripoti ya uthamini kwa Waziri, kamati inapendekeza ripoti iwasilishwe mara mbili kwa mwaka kwa kuwa miezi mitatu ni muda mfupi sana kwa Mthamini Mkuu kukusanya taarifa zote za uthamini na kuziwasilisha kwa Waziri.

(c) Kifungu cha 8 (2) kikisomwa na kifungu cha 5(2)(b) kinaelekeza sifa ya kuwateua Wathamini Wakuu Wasaidizi ni lazima mtu awe na uzoefu wa kwenye tasnia ya uthamini kwa muda usiopungua miaka kumi, Kamati inapendekeza iwe ni uzoefu usiopungua miaka mitano(5) ili iweze kuwapa fursa vijana kujijenga kiutendaji katika nafasi za uongozi.

(iii) Katika sehemu ya tatu inayohusu Bodi ya Usajili wa wathamini, Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

(a) Kifungu cha 13 (1) (d) kinachohusu muundo wa Bodi, Kamati inapendekeza wawe wawakilishi wawili toka chama cha wathamini na sio mwakilishi mmoja. Tunaipongeza Serikali kwa kukubaliana na pendekezo hili ikiwa ni pamoja na kukubalina na Kamati kuongeza mwakilishi toka Bodi ya Taifa ya Wahasibu na wakaguzi wa Hesabu (NBAA) pamoja na mwakilishi toka chama cha mabanki Tanzania kwa kuwa wao ni wadau wakubwa wa uthamini wakati wa kutoa mikopo.

(b) Katika kifungu cha 15 kinachohusu kamati za Bodi, Muswada unapaswa ufafanue vizuri upatikanaji wa wajumbe wa kamati za Bodi, na iwekwe wazi

kwamba wajumbe hao watatoka ndani ya Bodi, aidha mtu yeyote ambaye si mjumbe wa Bodi/kamati aweza kualikwa ili kuisaidia kamati katika jambo mahsusi ambalo kamati imeliainisha.

(c) Kifungu cha 21(3) kinachohusu upelelezi wa malalamiko kamati inapendekeza Mthamini anayelalamikiwa apewe nafasi ya kusikilizwa (right to be heard) kabla ya Bodi kutoa uamuzi wake. Jambo hili ni nyeti na likumbukwe kuwekwa kwenye kanuni ili kifungu hiki cha sheria kionyeshe kufuata utawala wa sheria.

(d) Katika kifungu cha 23 (1), kuna kosa la kiuandishi kamati inapendekeza kuondoa herufi “a” na kuweka herufi “the” kati ya maneno “with” na “Board”.

(iv) Katika sehemu ya nne inayohusu Usajili wa wathamini, Kamati inapendekeza mambo yafuatayo:-

(a) Katika kifungu cha 25 (1) Kamati inapendekeza adhabu zote ziwe endelevu kulingana na mabadiliko ya thamani ya shilingi. Aidha, kiuandishi, kifungu hiki kinapaswa kiende kifungu cha 67 kinachohusu makosa ili kuweza kuleta mtiririko wa kiuandishi.

(v) Katika sehemu ya tano inayohusu mwongozo kuhusu ufanyaji wa Uthamini, Kamati ina mapendekezo yafuatayo:-

(a) Katika kifungu cha 52(2) kinachohusu uhalali wa uthamini Kamati inasisitiza Serikali ikumbuke makubaliano tuliyokubaliana katika Kamati kuwa kwa madhumuni ya fidia ukomo wa uhalali wa uthamini uwe ni muda wa miaka miwili (2) kwa uthamini na taarifa ya uthamini uliofanyika chini ya sheria hii. Hii ni kwa sababu ulipaji fidia huchukua muda mrefu na wananchi hulipwa chini ya thamani kwa mali iliyothaminiwa, inapotokea thamani za mali iliyothaminiwa kupanda. Baada ya ukomo Uthamini ufanyike upya.

(b) Tunaikumbusha Serikali kuwa Katika Jedwali la marekebisho lililoletwa kwenye Kamati lenye tafsiri ya kiswahili kifungu 53(3) maneno “mtu ataruhusiwa” inabadilisha maana halisi ya kifungu hiki kwani kwenye tafsiri ya kiingereza “ A person shall not”, hii maana yake badala ya neno “**ataruhusiwa**” lisomeke “**hataruhusiwa**”.

(c) Kifungu cha 55(1) Kamati inapendekeza kirekebishwe ili kumlazimu mthamini kuwa na kibali maalum (**warrant**) ambacho kitakuwa kikitolewa na Mthamini Mkuu au Mamlaka ya Serikali za Mitaa kabla ya kuingia sehemu na kufanya uchunguzi wake kwa lengo la kuepuka watu wasio wathamini kutumia nafasi hiyo vibaya kuingia na kufanya uhalifu.

### 3.0 MAONI NA USHAURI WA JUMLA

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uchambuzi wa mswada huu Kamati inatoa maoni ya jumla kama ifuatavyo:-

(i) Ni vyema sheria inayopendekezwa ipitishwe kwani itabainisha taratibu rasmi za utendaji wa wathamini na hivyo kusaidia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 ambayo inatambua thamani halisi ya ardhi.

(ii) Kamati inashauri kuwa sheria hii inayopendekezwa iweke mfumo imara wa kisheria utakaohakikisha wathamini pamoja na shughuli zao wanawekewa utaratibu utakawawezesha kufanya kazi kwa weledi na ustadi ipasavyo.

(iii) Kamati inashauri kuwa sheria hii iweke mfumo wa Kitaifa wa utendaji na usimamizi wa Wathamini nchini, pamoja na kuanzisha mamlaka za usimamizi wa fani ya uthamini katika sekta ya Umma na Sekta binafsi.

(iv) Pamoja na usimamizi wa sheria hii kamati inashauri kuwa Bodi ya Usajili wa wathamini inayopendekezwa kuundwa ni vyema isimamiwe ipasavyo kwa lengo la kupata wathamini wenye sifa na vigezo katika kada ya uthamini kwa lengo la kuinua na kukuza taaluma ya uthamini hapa nchini.

(v) Kamati inashauri kuwa katika Bodi ya usajili wa wathamini ni vyema wathamini wakasajiliwa katika daftari maalumu litakaloweka kumbukumbu za wathamini wote nchini kwa sifa, namba, mwaka waliohitimu na kusajiliwa ili kuweka madaraja katika usajili.

(vi) Kamati inaendelea kusesitiza kuwekwa kwenye sheria kipengele kinachoanisha malipo ya **riba** kwa mtu au taasisi itakayoshindwa kukamilisha malipo ya **fidia mapema**, kipengele kitakacholeta msukumo kwa taasisi au mtu kulipa fidia mapema iwezekanavyo. Hii italeti ukombozi kwa jamii na wote ambao wangeathirika na uthamini. Hata hivyo ni dhahiri kuwa Serikali kwa kizingatia maoni ya Kamati kama tulivyokubaliana, wananchi wetu watafaidika kwani watakuwa wakilipwa “malipo ya fidia mapema” yaani ndani ya miezi sita tangu Mthamini Mkuu alipoidhinisha uthamini na baada ya hapo riba ilipwe kila baada ya miezi sita ndani ya miezi ishirini na nne (24) kabla ya Uthamini kufikia ukomo.

(vii) Kamati inashauri baada ya sheria hii kupitishwa ni vyema isimamiwe ipasavyo kwani itasaidia katika kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi inayoendelea kuibuka kwa kasi hapa nchini inayotokana na wathamini wasiozingatia maadili ya uthamini. Aidha, wathamini watapaswa kuzingatia

miiko yote inayopendekezwa katika sheria na kanuni kwa utendaji bora wa kazi zao.

#### 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, Moja ya mambo muhimu kabla ya kutunga Sheria yoyote ni kujiridhisha na umuhimu wa kuwa na sheria husika. Katika kufanya hivyo, Kamati ilirejea historia ya uthamini na dhana nzima ya uthamini na usajili wa wathamini katika nchi za jumuiya ya Madola, aidha Kamati ilifanya mlinganisho wa sheria hizo na namna zinavyotumika na kuona kuwa kuna haja kubwa ya kutungwa kwa sheria itakayosimamia taaluma na shughuli za uthamini hapa nchini. Tunaipongeza Serikali kwa kuleta muswada huu mbele ya Bunge lako tukufu ili tujadili na baadaye tuupitiche.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya kamati napenda kukushukuru kwa kunipatia nafasi kuwasilisha maoni na mapendekezo ya kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Napenda pia nimshukuru Waziri wa Ardhi Mhe. William V. Lukuvi (Mb), Naibu Waziri Mhe. Dkt. Angeline L. Mabula (Mb), watendaji wa Wizara ya Ardhi pamoja na watendaji wa Ofisi ya Mshauri Mkuu wa Bunge wa mambo ya Sheria kwa ushirikiano wao hadi kukamilika kwa Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee napenda pia kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Ardhi Maliasili na Utalii kwa ushauri wao ambao umesaidia kuboresha muswada huu. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Atashasta J. Nditiye, Mb, Mwenyekiti
2. Mhe. Kemilembe J. Lwota, Mb, M/Mwenyekiti
3. Mhe. Fredy Atupele Mwakibete, Mb, Mjumbe
4. Mhe. Devotha Mathew. Minja, Mb, Mjumbe
5. Mhe. Dkt Godwin Oloyce. Mollel, Mb, Mjumbe
6. Mhe. Grace Sindato Kiwelu, Mb, Mjumbe
7. Mhe. Jaffar Sanya Jussa, Mb, Mjumbe
8. Mhe. Joshua Samweli Nassari, Mb, Mjumbe
9. Mhe. Khalifa Salim Sulemain, Mb, Mjumbe
10. Mhe. Lucy Fidels Owenya, Mb, Mjumbe
11. Mhe. Magdalena Hamisi Sakaya, Mb, Mjumbe
12. Mhe. Mary Pius Chatanda, Mb, Mjumbe
13. Mhe. Musukuma Joseph Kasheku, Mb, Mjumbe
14. Mhe. Omari Abdallah Kigoda, Mb, Mjumbe
15. Mhe. Pauline Philipo Gekul, Mb, Mjumbe
16. Mhe. Richard Mganga Ndassa, Mb, Mjumbe
17. Mhe. Risala kabongo, Mb, Mjumbe
18. Mhe. Shabani Omari Shekilindi, Mb, Mjumbe

- |     |                                  |        |
|-----|----------------------------------|--------|
| 19. | Mhe. Silafu Jumbe Maufi, Mb      | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Sebastian Simoni Kapufi, Mb | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Yussuf Salim Hussein, Mb    | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Zainabu Nuhu Mwamwindi, Mb  | Mjumbe |
| 23. | Mhe. Yussuf Haji Khamis, Mb      | Mjumbe |
| 24. | Mhe. Neema William Mgaya, Mb     | Mjumbe |
| 25. | Mhe. Salma Mohamed Mwassa, Mb    | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, Aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashillilah, Watendaji wa Ofisi ya Bunge pamoja na Sekretarieti ya Kamati Ndugu, Gerald Magili, Haika Mtui, Elieka Saanya, Thomson Shawa na Jane Ndulesi kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Eng. Atashasta Justus Nditiye, (Mb)

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA  
ARDHI, MALIASILI NA UTALII**

08 Septemba, 2016

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa kutumia muda vizuri, sasa namkaribisha Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani ili na wao waweze kutoa maoni yao.

**MHE. WILFRED L. LWAKATARE - MSEMaji MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, chini ya Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Bungeni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini ya mwaka 2016 (*The Valuation and Valuers Registration Act, 2016*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa zawadi ya uhai na kuendelea kunijalia afya njema.

Pili, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote na uongozi wa Ofisi ya Bunge kwa kunifariji binafsi hapa na kunisaidia kwa hali na mali kipindi nilichopata matatizo ya kiafya. Kwenu nyote nasema ahsanteni sana na Mwenyezi Mungu awabariki na kuwakirimia maradufu kwa ukarimu ule mlionitendea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Naibu Waziri Kivuli wa Wizara hii Mheshimiwa Salma Mwassa, Mbunge, ambaye *professionally* ni Mthamini kwa mchango wake wa kitaalamu katika maandalizi ya hotuba yangu hii. Aidha, naishukuru Sekretarieti ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa uchambuzi wa muswada huu, uchambuzi ambao umesaidia sana kuandaa maoni haya ninayoyasoma sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee napenda kutumia fursa hii pia kumshukuru na kumpongeza sana Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, ambaye pia ni Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe pamoja na Kamati Kuu ya CHADEMA kwa kuanzisha Operesheni ya Umoja wa Kupambana na Udikteta yenye lengo la kizalendo la kuirejesha nchi hii kwenye misingi ya utawala wa kidemokrasia, utawala unaoheshimu Katiba na sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tunawapongeza viongozi wote wa CHADEMA katika ngazi zote na wanachama wote kwa jumla kwa kujitokeza na kusimamia bila woga zoezi la maandalizi ya UKUTA, licha ya vitisho vya watawala na vyombo vya dola, pamoja na kuteswa na wengine kuwekwa rumande na kufunguliwa kesi lukuki za uchochezi, kamwe walionesha moyo wa ujasiri na hawakurudi nyuma. Hakika UKUTA umethibitisha kwamba CHADEMA kiko imara pembe zote za nchi na kwa kipindi cha zaidi ya mwezi mmoja nchi ilisimama kusikilizia nini kinachotoka CHADEMA na imethibitisha jinsi tulivyo na viongozi jasiri pembe zote za nchi, wanaoweza kusimamia maelekezo ya chama bila kutetereka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote ni mashahidi na wananchi wameona jinsi Serikali hii ya Awamu ya Tano ilivyoamua kwa makusudi kutupilia mbali Katiba ambayo ndiyo sheria kuu inayotoa haki, uhuru, wajibu na mwongozo wa namna ya kuendesha nchi na badala yake kauli za mtu mmoja zinachukuliwa kama ndio sheria za kuongoza nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fikra za namna hiyo, kwamba kauli za mtu mmoja zinaweza kuwa bora kuliko Katiba na sheria za nchi na hata hii miswada tunayoendelea kuileta Bungeni kujadili, ni fikra potofu, ni fikra za kijima na kamwe haziwezi kuwa na nafasi katika karne hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiachia suala hili la kupuuzwa Katiba liendeleo, kwanza tutakuwa tumevunja kiapo chetu cha kuilinda, kuihifadhi na kuitetea Katiba hiyo, jambo ambalo kila Mbunge alilitoa hapa Bungeni na kushuhudiwa na Watanzania wote na jambo hilo litakuwa ni laana kwetu ikiwa mambo yataharibika kutokana na Katiba hiyo kuvunjwa. Pili na mbaya zaidi nchi hii itaingia kwenye machafuko ya kisiasa ikiwa hatutatimiza wajibu wetu kukemea tabia hii ya kupuuzwa Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika msingi huu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa rai kwa makundi mbalimbali ya jamii na wananchi wote kwa ujumla wanaopenda kuona utawala wa sheria ukidumishwa Tanzania kuunga mkono Operesheni UKUTA Awamu ya Pili (*UKUTA Phase II*) inayotegemewa kuanza tarehe 01 Oktoba, 2016 ambayo inalenga kurejesha nidhamu ya kuheshimu Katiba na sheria za nchi katika kuendesha Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili madhumuni na sababu za sheria inayopendekezwa; ni ukweli usiopingika kwamba kumekuwa na migogoro mingi ya ardhi miongoni mwa wananchi ambayo kwa kiasi kikubwa imekuwa ikisababishwa na uthamini usiokidhi viwango ambao hupelekea kutolipwa kwa fidia stahiki kwa wananchi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeeleza kwamba Muswada wa Sheria inayopendekezwa umeletwa ili kuondokana na changamoto hizo. Kambi Rasmi ya Upinzani haipingi malengo ya kuletwa kwa muswada huu, na ni vizuri Serikali imeleta marekebisho mengi yaliyozingatia hoja za wadau, isipokuwa kuna baadhi ya vifungu ambavyo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni italeta majedwali ya marekebisho kwa lengo la kuifanya sheria hii inayopendekezwa kuwa bora zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matarajio ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba Serikali kupitia Wizara hii iliyowasilisha muswada huu itakuwa *pro-active* kama ilivyofanyia kazi haraka baadhi ya mambo tuliyowasilisha kipindi cha bajeti. Kwa mfano, uanzishaji wa mfumo wa kielektroniki katika usimamizi wa mambo ya upimaji na ugawaji ardhi, lakini pia fidia kwa wananchi wa Kifungwa, Kata ya Kahoro katika Manispaa ya Bukoba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu mahusiano kati ya Muswada wa Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini na Sheria ya Mahakama za Ardhi. Muswada huu una mahusiano makubwa na Sheria ya Mahakama za Ardhi (*Courts Land Disputes Settlement Act*) ya mwaka 2002. Itakumbukwa kuwa sheria inayoanzisha Mahakama za Ardhi (*The Courts Land Disputes Settlements, Act*) ya mwaka 2002 inaweka utaratibu wa thamani ya ardhi na Mahakama au Baraza ambalo litakuwa na mamlaka ya kusikiliza mashauri hayo kulingana na thamani ya ardhi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Baraza la Ardhi la Kata, mathalani Sheria ya Mahakama inayohusika na migogoro ya ardhi kifungu cha 15 imeweka kiwango kisichozidi milioni tatu kuwa ndicho kikomo cha thamani ya ardhi ambayo ikiwa kuna mgogoro Baraza la Ardhi la Kata litakuwa na mamlaka ya kushughulikia jambo hilo. Kwa upande wa Baraza la Ardhi la Wilaya, kifungu cha 33 cha sheria hiyo kinatoa mamlaka kwa Baraza hilo



kushughulikia mashauri ya ardhi ambayo thamani yake haizidi milioni 40 mpaka milioni 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na Muswada huu kuwa na mahusiano na sheria hiyo ya Mahakama za Ardhi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kuwe na uwiano kati ya Sheria hii ya Uthamini na Usajili wa Wathamini na sheria inayoratibu mashauri ya ardhi. Hii ni kutokana na kukua kwa miji na kuongezeka kwa thamani ya ardhi bila kufanya marekebisho katika sheria zetu. Ikumbukwe kwamba mashauri na migogoro mingi iko katika ngazi hizo. Hali hii imefanya Mwakili kuwashauri wateja wao kushusha thamani zao za ardhi ili kukidhi haja ya masharti ya sheria.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kufanya marekebisho ya Sheria ya Mahakama za Ardhi, ili itambue thamani ya ardhi itakayokuwa inatolewa kwa mujibu wa masharti ya Muswada huu, kuweza kuendana na wakati na kuhakikisha kuwa wananchi wanapata haki kulingana na thamani zao za ardhi wakati wa migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu muda wa kuthibitishwa kwa Wathamini, kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kwa Wathamini kuchukua muda mrefu mpaka kuthibitishwa rasmi kuwa Wathamini. Wathamini huchukua muda wa miaka saba au zaidi ukiunganisha na muda waliokuwa darasani. Kozi za Wathamini huchukua miaka minne mpaka miaka mitano na baadae wahitimu hutakiwa kukaa kwa Mthamini aliyesajiliwa kwa muda usiopungua miaka miwili au zaidi kulingana na jinsi atakavyokuwa amekidhi masharti ili kupata uzoefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na umuhimu wa kukaa muda mrefu kwenye mafunzo ya uthamini kwa ajili ya kuwajengea weledi ni wazi kuwa muda wanaokaa kabla ya kuthibitishwa ni mrefu sana. Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kwamba kwa kuwa sasa Wathamini wameundiwa chombo chao, ni vema chombo hicho kikawa na mamlaka ya kusimamia mafunzo ya Wathamini hasa baada ya kumaliza masomo ya Chuo Kikuu ili kuwathibitisha mapema kuliko utaratibu uliopo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni Uthamini na Uhifadhi wa Thamani katika kanzi data moja. Kumekuwa na migogoro kadhaa baina ya wananchi na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kutokana na mamlaka hiyo kufanya ukadiriaji wa thamani ya ardhi na mali nyingine kwa ajili ya malipo ya kodi mbalimbali. Aidha, katika Mahakama za Ardhi nchini kumekuwa na migogoro katika ukadiriaji wa thamani ya ardhi na kujua mahakama ambayo ina mamlaka ya kusikiliza mashauri mbalimbali katika Mabaraza ya Ardhi na Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo taarifa kuwa TRA wanayo kanzi data ya thamani ya ardhi nchini ambayo huitumia katika kukadiria kodi mbalimbali zinazohusiana na masuala ya ardhi. Kwa kuwa Serikali sasa imeleta Muswada huu wa Wathamini ni vema wananchi na mamlaka zingine za Serikali zikawa na uhakika kuhusu thamani za ardhi zao na au kuhakikisha kuwa taarifa za uthamini zinaendana na taarifa za thamani ya ardhi ambazo zipo katika mamlaka zinazotambulika na zilizopewa nguvu na sheria hii na hivyo kusaidia kuepuka migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kwamba, TRA ifanye kazi ya *assessment* na siyo *valuation*. Tunawachanganya sana wananchi kwa kuachia mamlaka mbili tofauti kufanya jambo lile lile na mkanganyiko unakuwa mkubwa zaidi iwapo uthamini uliofanywa utakuwa na matokeo tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sasa nchi yetu inaendelea kukumbwa na migogoro ya ardhi kati wananchi wenyewe kwa wenyewe, wafugaji na wakulima, wananchi dhidi ya Mamlaka ya Hifadhi za Taifa na wananchi dhidi ya Serikali yenyewe hasa wakati wa kutwaa ardhi kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Kifungu cha nne cha Sheria ya Ardhi Namba Tano ya mwaka 1999 inaweka bayana kuwa katika ulipaji fidia ni lazima Serikali au mtu mwingine yeyote kuhakikisha kuwa fidia inatakiwa kuwa ya haki, kamilifu na ilipwe kwa wakati. Ni vema Serikali ikawatumia Wathamini kuhakikisha kuwa taarifa za uthamini zinatolewa na wataalam hawa ili kuepuka malalamiko ya wananchi kuhusu thamani ya ardhi yao pindi inapotwaliwa na Serikali kwa ajili ya shughuli zingine kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uhuru wa Mthamini Mkuu wa Serikali; kwa kuwa Serikali ndiyo mdau mkubwa katika ununuzi wa ardhi, majengo na mali nyingine kutoka kwa wananchi, na kwa kuwa Serikali ndiyo mthamini na mfidiaji, kuna dalili ya Serikali kujipendelea kwa kushusha thamani na kutoa fidia kidogo ili kujinufaisha. Kwa msingi huo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza Mthamini Mkuu wa Serikali awe huru kama alivyo Mhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) au Mkemia Mkuu wa Serikali na asiwe chini ya Wizara ya Ardhi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa bado kuna kazi ya kiporo cha Katiba Mpya, Serikali ijipange kufanya marekebisho ndani ya Katiba kumpa uhuru Mthamini. Muswada huu, tukubaliane, uwe mpito tukiwa tunaelekea kutimiza azma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imetoa mapendekezo hayo kwa kuzingatia pia kwamba Mthamini Mkuu ana wajibu wa kuthamini pia vitu vingine ambavyo siyo ardhi au majengo, ana wajibu mathalani wa kuthamini ndege, meli au mali nyingine zinazohamishika ambazo hazipo katika Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa uthamini na ulipaji fidia kwa wananchi wanaopisha miradi ya maendeleo. Ni bahati mbaya Muswada huu haujazungumzia utaratibu wa uthamini na ulipaji fidia kwa wananchi wanaopisha baadhi ya miradi ya maendeleo kama vile barabara, njia kuu za umeme, mabomba ya maji, gesi na hata ujenzi wa viwanda na taasisi mbalimbali za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na hali ya sintofahamu kwa wananchi ambao nyumba zao za kuishi au za biashara zimekuwa zikiwekewa alama ya 'X' kuashiria kwamba wanatakiwa kutoendesha shughuli zozote katika maeneo hayo ili kupisha miradi ya maendeleo, jambo la kusikitisha ni kwamba, alama hizo za 'X' huwekwa bila uthamini kufanyika na bila fidia kulipwa. Mifano hai ni kule Bukoba, Bukoba Mjini kuelekea Muleba, Bukoba kuelekea Kyaka, kuelekea Karagwe ni jambo ambalo limekuwa la kawaida, nyumba zinawekwa 'X' bila uthamini kufanyika, Wizara ya Ujenzi ina-extend barabara hata mipaka ya vigingi vya zamani bila kufanya uthamini, hili linapaswa liangaliwe kwa karibu na sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupisha miradi ya maendeleo siyo jambo baya ikiwa uthamini unafanywa na fidia inalipwa kwa wakati, lakini uzoefu unaonyesha kwamba alama hizo huwekwa na kuachwa kwa muda mrefu kama ilivyo sasa huko Bukoba, bila uthamini na bila fidia kulipwa, jambo linalowaathiri wamiliki wa maeneo hayo. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kwamba Muswada huu uweke utaratibu wa kufanya uthamini na kulipa fidia katika maeneo ambayo wananchi wanapaswa kupisha miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana nyingine sheria itamke bayana ni muda gani uthamini na ulipaji fidia unatakiwa ufanyike baada ya kuainisha maeneo ambayo wananchi wanatakiwa kupisha miradi ya maendeleo. Ni vema Serikali kupitia muswada huu ikabainisha namna watakavyoyashughulikia maeneo ambayo mpaka sasa yameathiriwa na jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa vifungu mahsus vya muswada. Kifungu cha 8(2) kinaweka masharti ya vigezo au sifa za mtu anayetakiwa kuteuliwa kuwa Mthamini Mkuu Msaidizi kama ilivyoainishwa kwenye kifungu cha 5(2) cha muswada huu. Mojawapo ya sifa zilizoainishwa katika kifungu cha 5(2) ni pamoja na kuwa na Shahada ya Uzamili (*Masters*

Degree) katika masuala ya uthamini katika chuo kinachotambulika na kuwa na uzoefu usiopungua miaka kumi katika shughuli za uthamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama maoni ya Kamati yalivyoeleza, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaunga mkono vigezo au sifa zote zilizoainishwa na muswada huu ili mtu ateuliwe kuwa Mthamini Mkuu Msaidizi, isipokuwa kigezo cha kuwa na Shahada ya Uzamili na uzoefu wa miaka kumi. Sababu kubwa ya kupinga vigezo hivi ni kwamba vitasababisha tuendelee kuwa na uhaba wa Wathamini kutokana na uchache wa Wathamini wenye Shahada za Uzamili na wenye uzoefu wa miaka kumi katika kazi. Pili, hawa Wathamini Wakuu Wasaidizi hawatakuwa na tofauti na Mthamini Mkuu kwa maana watakuwa na sifa zinazofanana na kwa maana hiyo hakutakuwa na haja ya kuwaita Wathamini Wakuu Wasaidizi, wote ni Wathamini Wakuu kwa kuzingatia vigezo vyao. Aidha, hakutakuwa na mantiki ya kuwa na kifungu cha 8(3) cha kuwafanya hawa Wathamini Wakuu Wasaidizi kuwajibika kwa Mthamini Mkuu ikiwa wote wana sifa zinazolingana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi ya kuwa na Wathamini Wakuu Wasaidizi wa kutosha na kwa misingi ya kuepuka kuwa na Wathamini Wakuu Wasaidizi wenye sifa zile alizonazo Mthamini Mkuu na kuleta mkanganyiko wa madaraja ya mishahara na stahili nyingine kwa wahusika, na kwa misingi ya kuepuka kutowaajiri vijana wenye nguvu ya kufanya kazi kutokana na masharti ya kuwa na uzoefu wa miaka kumi, Kambi Rasmi ya Upinzani inakusudia kuleta Jedwali la Marekebisho katika eneo hili ili Wathamini Wakuu Wasaidizi watakiwe kuwa na Shahada ya Kwanza katika masuala ya Uthamini kama kigezo cha elimu na kigezo cha Shahada ya Uzamili ibaki kwa Mthamini Mkuu pekee.

Aidha, tutaleta mapendekezo ya kufuta sharti la kuwa na uzoefu wa miaka kumi kama sifa ya kuwa Mthamini Mkuu Msaidizi ili kuongeza wigo wa ajira kwa vijana wenye sifa. Kimsingi uzoefu wa miaka mitano unatosha kumfanya Mthami awe na sifa ya kuteuliwa kuwa Mthamini Mkuu Msaidizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imepitia Jedwali la Marekebisho la Serikali katika kifungu cha 52; kimsingi Serikali inapendekeza katika kifungu cha 52(2) kwamba uthamini pamoja na ripoti za uthamini zilizoandaliwa chini ya sheria hii kwa minajili ya kulipa fidia utakuwa na ukomo wa miaka mitatu kuanzia tarehe ripoti hiyo ilipoidhinishwa, japo tumepata taarifa kwamba kimererekebishwa na kuwa miaka miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo ukomo wa miaka miwili unaopendekezwa na sheria hii bado tunauona ni mrefu kiasi kwamba mwananchi anayetakiwa kulipwa fidia kutokana na uthamini uliofanyika stahiki zake zitakuwa pungufu kutokana na muda wa kusubiri kuwa mrefu. Miaka miwili siyo mchezo, siku 360 mara mbili siyo mchezo. Kwa vyovyote vile thamani

iliyobainika baada ya uthamini, haiwezi kuwa hiyo kwa miaka miwili mfululizo. Ama thamani itakuwa imeongezeka au itakuwa imepungua kutokana na asili (*nature*) ya mali iliyofanyiwa uthamini na au mabadiliko ya mwenendo wa uchumi (*economic dynamics*). Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inakusudia kuleta Jedwali la Marekebisho katika eneo hili, ili ukomo wa uthamini na ripoti za uthamini kwa minajili ya kulipa fidia uwe mwaka mmoja ambao unatoshia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani pia inakusudia kuleta Jedwali la Marekebisho katika Jedwali la Marekebisho la Serikali katika Kifungu cha 52(5) ili kupunguza wigo wa miaka mitatu wa kulipa fidia na riba hadi kufikia mwaka mmoja na nusu. Hii ni kwa ajili ya kuwabana walipa fidia kulipa fidia na kwa wakati ili kuwaondolea wananchi usumbufu wa kusubiri muda mrefu bila kulipwa fidia yao. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza ukomo wa ripoti ya uthamini uzingatie vipengele vyote vilivyoainishwa katika kifungu cha 49(2) na siyo kwenye fidia peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; kwa ujumla muswada huu kama utatekelezwa ipasavyo chini ya Waziri ambaye kwa kweli ameonesha jitihada kubwa za kusimamia yale anayoyatamka kuwa sheria utapunguza changamoto nyingi katika sekta ya ardhi na nyumba zilizokuwa zikitokana na matatizo ya uthamini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Serikali ni kufanya marekebisho ya sheria nyingine zilizokuwa zinatoa mwongozo wa uthamini ili kuzioanisha na sheria hii kutoleta mkanganyiko katika utekelezaji wa sheria inayopendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwa nimetoa maoni kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. Ahsante sana, nashukuru. (*Makofi*)

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI, MHESHIMIWA WILFRED MUGANYIZI LWAKATARE (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA UTHAMINI NA USAJILI WA WATHAMINI YA MWAKA 2016 (VALUATION AND VALUERS REGISTRATION ACT, 2016)  
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*Inatolewa chini ya Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016*

---

## **1. UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa zawadi ya uhai na kuendelea kunijalia afya njema. Pili nawashukuru sana waheshimiwa wabunge wote na uongozi wa Ofisi ya Bunge kwa kunifariji na kunisaidia kwa hali na mali kipindi nilichopata matatizo ya kiafya. Kwenu nyote nasema asanteni sana na Mwenyezi Mungu awabariki na kuwakirimia mara dufu kwa ukarimu ule mlionitendea mimi.

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Naibu Waziri Kivuli wa wizara hii Mheshimiwa Salma Mwassa (Mb) kwa mchango wake wa kitaalamu katika maandalizi ya hotuba hii. Aidha, naishukuru Sekretarieti ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa uchambuzi wa muswada huu – uchambuzi ambao umesaidia sana kuandaa maoni haya.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekeenapenda kutumia fursa hii pia kumshukuru na kumpongeza Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ambaye pia ni Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe pamoja na Kamati Kuu ya CHADEMA kwa kuanzisha operesheni UKUTA yenye lengo la kizalendo la kuirejesha nchi hii kwenye misingi ya utawala wa kidemokrasia - utawala unaoheshimu Katiba na Sheria. Aidha, tunawapongeza viongozi wote wa CHADEMA katika ngazi zote na wanachama wote kwa jumla kwa kujitokeza na kusimamia bila woga zoezi la maandalizi ya UKUTA licha ya vitisho vya watawala na vyombo vya dola, kuteswa na kuwekwa rumande na kufunguliwa kesi lukuki za uchochezi. Hakika UKUTA umethibitisha kwamba CHADEMA kiko imara pembe zote za nchi na kina viongozi jasiri wenye kuyasimamia maelekezo ya chama bila kutetereka.

**Mheshimiwa Spika**, sote ni mashahidi na wananchi wameona jinsi Serikali hii ya awamu ya tano ilivyoamua kwa makusudi kutupilia mbali Katiba ambayo ndiyo sheria kuu inayotoa haki, uhuru, wajibu na mwongozo wa namna ya kuendesha

nchi na badala yake kauli za mtu mmoja zinachukuliwa kama ndio sheria za kuongoza nchi.

**Mheshimiwa Spika**, fikra za namna hiyo; - kwamba kauli za mtu mmoja zinaweza kuwa bora kuliko Katiba na Sheria za nchi na hata hii miswada tunayoleta bungeni kuijadili, ni fikra potofu, ni fikra za kijima na kamwe haziwezi kuwa na nafasi katika karne hii.

**Mheshimiwa Spika**, tukiachia suala hili la kupuuza katiba liendeleo, kwanza tutakuwa tumevunja kiapo chetu cha kuilinda, kuihifadhi na kuitetea Katiba hiyo jambo ambalo litakuwa laana kwetu ikiwa mambo yataharibika kutokana na katiba hiyo kuvunjwa, lakini pili na mbaya zaidi, nchi hii itaingia kwenye machafuko ya kisiasa ikiwa hatutatimiza wajibu wetu kukemea tabia hii ya kupuuza Katiba.

**Mheshimiwa Spika**, ni katika msingi huu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa rai kwa makundi mbalimbali ya jamii na wananchi wote kwa ujumla wanaopenda kuona utawala wa sheria ukidumishwa Tanzania kuunga mkono operesheni UKUTA awamu ya pili (UKUTA phase II) inayotegemewa kuanza tarehe 1 Oktoba, 2016 ambayo inalenga kurejesha nidhamu ya kuheshimu Katiba na Sheria za Nchi katika kuendesha Serikali.

## 2. MADHUMUNI NA SABABU ZA SHERIA INAYOPENDEKEZWA

**Mheshimiwa Spika**, ni ukweli usiopingika kwamba kumekuwa na migogoro mingi ya ardhi miongoni mwa wananchi ambayo kwa kiasi kikubwa imekuwa ikisababishwa na uthamini usiokidhi viwango ambao hupelekea kutolipwa kwa fidia stahiki kwa wananchi husika.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeeleza kwamba; Muswada wa Sheria inayopendekezwa umeletwa ili kuondokana na changamoto hizo. Kambi Rasmi ya Upinzani haipingi malengo ya kuletwa kwa muswada huu, na ni vizuri Serikali imeleta marekebisho mengi yaliyozingatia hoja za wadau, isipokuwa kuna baadhi ya vifungu ambavyo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni italeta majedwali ya marekebisho kwa lengo la kuifanya sheria hii inayopendekezwa kuwa bora zaidi.

**Mheshimiwa Spika**, ni matarajio ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba Serikali kupitia Wizara hii iliyowasilisha muswada huu itakuwa **'pro-active'** kama ilivyofanyia kazi haraka baadhi ya mambo tuliyowasilisha kipindi cha bajeti ; kwa mfano uanzishaji wa mfumo wa ki-elektroniki katika usimamizi wa mambo ya upimaji na ugawaji ardhi, fidia kwa wananchi wa Kifungwa – Kata ya Kahororo katika Manispaa ya Bukoba nk.



### 3. MAHUSIANO KATI YA MUSWADA WA SHERIA YA UTHAMINI NA USAJILI WA WATHAMINI NA SHERIA YA MAHAKAMA ZA ARDHI.

**Mheshimiwa Spika**, muswada huu una mahusiano makubwa na Sheria ya Mahakama za ardhi [Courts (Land Disputes Settlement Act] ya mwaka 2002. Itakumbukwa kuwa Sheria inayoanzisha Mahakama za Ardhi [The Courts (Land Disputes Settlements) Act] ya mwaka 2002 inaweka utaratibu wa thamani ya ardhi na Mahakama/Baraza ambalo litakuwa na mamlaka ya kusikiliza mashauri hayo kulingana na thamani ya ardhi husika.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Baraza la Ardhi la Kata, mathalani; sheria ya Mahakama inayohusika na migogoro ya ardhi kifungu cha 15 imeweka kiwango kisichozidi milioni tatu kuwa ndicho kikomo cha thamani ya ardhi ambayo ikiwa kuna mgogoro Baraza la Ardhi la Kata litakuwa na mamlaka ya kushughulikia jambo hilo. Kwa upande wa Baraza la Ardhi la Wilaya, kifungu cha 33 cha sheria hiyo kinatoa mamlaka kwa Baraza hilo kushughulikia mashauri ya ardhi ambayo thamani yake haizidi milioni 40 mpaka 50.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na muswada huu kuwa na mahusiano na sheria hiyo ya mahakama za ardhi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kuwena uwiano kati ya sheria hii ya Uthamini na usajili wa wathamini na sheria inayoratibu mashauri ya ardhi. Hii ni kutokana na kukua kwa miji na kuongezeka kwa thamani ya ardhi bila kufanya marekebisho katika sheria zetu. Na ikumbukwe kwamba mashauri na migogoro mingi iko katika ngazi hizo. Hali hii imefanya Mwakili kuwashauri wateja wao kushusha thamani zao za ardhi ili kukidhi haja ya masharti ya sheria. Kambi rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kufanya marekebisho ya sheria ya Mahakama za ardhi ili itambue thamani ya ardhi itakayokuwa inatolewa kwa mujibu wa masharti ya muswada huu ili kuweza kuendana na wakati na kuhakikisha kuwa wananchi wanapata haki kulingana na thamani zao za ardhi wakati wa migogoro.

### 4. MUDA WA KUTHIBITISHWA KWA WATHAMINI

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kwa wathamini kuchukua muda mrefu mpaka kuthibitishwa rasmi kuwa wathamini. Wathamini huchukua muda wa miaka saba au zaidi ukiunganisha na muda waliokuwa darasani.

**Mheshimiwa Spika**, Kozi za wathamini huchukua miaka minne mpaka mitano na baadae wahitimu hutakiwa kukaa kwa mthamini aliyesajiliwa kwa muda usiopungua miaka miwili au zaidi kulingana na jinsi atakavyokuwa amekidhi masharti ili kupata uzoefu.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na umuhimu wa kukaa muda mrefu kwenye mafunzo ya uthamini kwa ajili ya kuwajengea weledi ni wazi kuwa muda wanaokaa kabla ya kuthibitishwa ni mrefu sana. Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kwamba; kuwa kwa kuwa sasa wathamini wameundiwa chombo chao, ni vema chombo hicho kikawa na mamlaka ya kusimamia mafunzo ya wathamini hasa baada ya kumaliza masomo ya Chuo Kikuu ili kuwathibitisha mapema kuliko utaratibu uliopo sasa.

## 5. UTHAMINI NA UHIFADHI WA THAMANI KATIKA KANZIDATA MOJA

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na migogoro kadhaa baina ya wananchi na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kutokana na mamlaka hiyo kufanya ukadiriaji wa thamani ya ardhi na mali nyingine kwa ajili ya malipo ya kodi mbalimbali. Aidha, katika Mahakama za Ardhi nchini kumekuwa na migogoro katika ukadiriaji wa thamani ya ardhi na kujua Mahakama ambayo ina mamlaka ya kusikiliza mashauri mbalimbali katika Mabaraza ya ardhi na Mahakama Kuu.

**Mheshimiwa Spika**, zipo taarifa kuwa TRA wanayo kanzi data ya thamani ya ardhi nchini ambayo huitumia katika kukadiria kodi mbalimbali zinazohusiana na masuala ya ardhi. Kwa kuwa sasa serikali imeleta muswada huu wa wathamini ni vema wananchi na mamlaka zingine za serikali zikawa na uhakika kuhusu thamani za ardhi zao na au kuhakikisha kuwa taarifa za uthamini zinaendana na taarifa za thamani ya ardhi ambazo zipo katika mamlaka zinazotambulika na zilizopewa nguvu na sheria hii na hivyo kusaidia kuepuka migogoro.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kwamba TRA ifanye kazi ya '**assessment**' na sio '**valuation**'. Tunawachanganya sana wananchi kwa kuachia mamlaka mbili tofauti kufanya jambo lilelile na mkanganyiko unakuwa mkubwa zaidi iwapo uthamini uliofanywa utakuwa na matokeo tofauti.

**Mheshimiwa Spika**, kwa muda mrefu sasa nchi yetu inaendelea kukumbwa na migogoro ya ardhi kati wananchi wenyewe kwa wenyewe, wafugaji na wakulima, wananchi dhidi mamlaka za hifadhi za taifa na wananchi dhidi ya serikali yenyewe hasa wakati wa kutwaa ardhi kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha nne cha sheria ya Ardhi namba tano ya mwaka 1999 inaweka bayana kuwa katika ulipaji fidia ni lazima serikali au mtu mwingine yeyote kuhakikisha kuwa fidia inatakiwa kuwa ya haki, kamilifu na ilipwe kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, ni vema sasa serikali ikawatumia wathamini kuhakikisha kuwa taarifa za uthamini zinatolewa na wataalam hawa ili kuepuka malalamiko ya wananchi kuhusu thamani ya ardhi yao pindi inapotwaliwa na serikali kwa ajili ya shughuli zingine kwa mujibu wa sheria.

## 6. UHURU WA MTHAMINI MKUU WA SERIKALI

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Serikali ndio mdau mkubwa katika ununuzi wa ardhi, majengo na mali nyingine kutoka kwa wananchi; na kwa kuwa Serikali ndiyo mthamini na mfidiaji, kuna kila dalili ya Serikali kujipendelea kwa kushusha thamani na kutoa fidia kidogo ili kujinufaisha. Kwa msingi huo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza Mthamini Mkuu wa Serikali awe huru kama alivyo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) au Mkemia Mkuu wa Serikali na asiwe chini ya Wizara ya Ardhi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa bado kuna kazi ya kiporo cha Katiba mpya, Serikali ijipange kufanya marekebishondani ya Katiba. Muswada huu uwe mpito kutimiza azma hiyo

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imetoa mapendekezo hayo kwa kuzingatia pia kwamba Mthamini Mkuu ana wajibu wa kuthamini pia vitu vingine ambavyo sio ardhi au majengo. Ana wajibu mathalani wa kuthamini ndege, meli au mali nyingine zinazohamishika ambazo hazipo katika wizara ya ardhi.

## 7. UTARATIBU WA UTHAMINI NA ULIPAJI FIDIA KWA WANANCHI WANAOPISHA MIRADI YA MAENDELEO

**Mheshimiwa Spika**, ni bahati mbaya Muswada huu haujazungumzia utaratibu wa uthamini na ulipaji fidia kwa wananchi wanaopisha baadhi ya miradi ya Maendeleo kama vile barabara, njia kuu za umeme, mabomba ya maji, gesi na hata ujenzi wa viwanda na taasisi mbalimbali za umma.

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa nahali ya sintofahamu kwa wananchi ambao nyumba zao za kuishi, au za biashara zimekuwa zikiwekewa alama ya **X** kuashiria kwamba wanatakiwa kutoendesha shughuli zozote katika maeneo hayo ili kupisha miradi ya maendeleo. Lakini jambo la kusikitisha ni kwamba alama hizo za **X** huwekwa bila uthamini kufanyika na bila fidia kulipwa.

**Mheshimiwa Spika**, kupisha miradi ya maendeleo si jambo baya ikiwa uthamini unafanywa na fidia inalipwa kwa wakati. Lakini uzoefu unaonyesha kwamba alama hizo huwekwa na kuachwa kwa muda mrefu bila uthamini na bila fidia kulipwa jambo linalowaathiri wamiliki wa maeneo hayo. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kwamba; Muswada huu

uweke utaratibu wa kufanya uthamini na kulipa fidia katika maeneo ambayo wananchi wanapaswa kupisha miradi ya maendeleo. Kwa maana nyingine, sheria itamke bayana ni muda gani uthamini na ulipaji fidia unatakiwa ufanyike baada ya kuainisha maeneo ambayo wananchi wanatakiwa kupisha miradi ya maendeleo. Na ni vyema Serikali kupitia Muswada huu ikabainisha namna watakavyoyashughulikia maeneo ambayo mpaka sasa yameathiriwa na jambo hilo.

## 8. UCHAMBUZI WA VIFUNGU MAHSUSI VYA MUSWADA

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 8(2) kinaweka masharti ya vigezo au sifa za mtu anayetakiwa kuteuliwa kuwa Mthamini Mkuu Msaidizi kama ilivyoanishwa kwenye kifungu cha 5(2) cha muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, mojawapo ya sifa zilizoainishwa katika kifungu cha 5(2) ni pamoja na kuwa na shahada ya uzamili (Masters Degree) katika masuala ya uthamini katika chuo kinachotambulika, na kuwa na uzoefu usiopungua miaka kumi katika shughuli za uthamini.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaunga mkono vigezo au sifa zote zilizoainishwa na muswada huu ili mtu ateuliwe kuwa Mthamini Mkuu Msaidizi isipokuwa kigezo cha kuwa na shahada ya uzamili na uzoefu wa miaka kumi. Sababu kubwa ya kupinga vigezo hivi, ni kwamba vitasababisha tuendeleo kuwa na uhaba wa wathamini kutokana na uchache wa wathamini wenye shahada za uzamili na wenye uzoefu wa miaka kumi katika kazi. Lakini pili hawa wathamini wakuu wasaidizi hawatakuwa na tofauti na Mthamini Mkuu kwa maana watakuwa na sifa zinazofanana na kwa maana hiyo hakutakuwa na haja ya kuwaita wathamini wakuu wasaidizi – wote ni wathamini wakuu kwa kuzingatia vigezo vyao. Aidha, hakutakuwa na mantiki ya kuwa na kifungu cha 8(3) cha kuwafanya hawa wathamini wakuu wasaidizi kuwajibika kwa mthamini Mkuu ikiwa wote wana sifa zinazolingana.

**Mheshimiwa Spika**, kwa misingi ya kuwa na wathamini wakuu wasaidizi wa kutosha, na kwa misingi ya kuepuka kuwa na wathamini wakuu wasaidizi wenye sifa zile zile alizo nazo Mthamini Mkuu na kuleta mkanganyiko wa madaraja ya mishahara na stahili nyingine kwa wahusika, na kwa misingi ya kuepuka kutowaajiri vijana wenye nguvu ya kufanya kazi kutokana na masharti ya kuwa na uzoefu wa miaka kumi, Kambi Rasmi ya Upinzani inakusudia kuleta jedwali la marekebisho katika eneo hili ili wathamini wakuu wasaidizi watakiwe kuwa na shahada ya kwanza katika masuala ya uthamini kama kigezo cha elimu, na kigezo cha shahada ya uzamili ibaki kwa Mthamini Mkuu pekee. Aidha tutaleta mapendekezo ya kufuta sharti la kuwa na uzoefu wa miaka kumi kama sifa ya kuwa Mthamini Mkuu Msaidizi, ili kuongeza wigo wa ajira kwa vijana wenye sifa.

Kimsingi uzoefu wa miaka mitano unatosha kumfanya mthami awe na sifa ya kuteuliwa kuwa Mthamini Mkuu Msaidizi.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imepitia jedwali la marekebisho la Serikali katika kifungu cha 52. Kimsingi Serikali inapendekeza katika kifungu cha 52(2) kwamba uthamini pamoja na ripoti za uthamini zilizoandaliwa chini ya sheria hii kwa minajili ya kulipa fidia utakuwa na ukomo wa miaka mitatukuanzia tarehe ripoti hiyo ilipoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**, ukomo wa miaka mitatu unaopendekezwa na sheria hii ni mrefu mno kiasi kwamba mwananchi anayetakiwa kulipwa fidia kutokana na uthamini uliofanyika stahiki zake zitakuwa pungufu kutokana na muda wa kusubiri kuwa mrefu. Kwa vyovyote vile thamani iliyobainika baada ya uthamini, haiwezi kuwa hiyo hiyo kwa miaka mitatu mfululizo. Ama thamani itakuwa imeongezeka au itakuwa imepungua kutokana na asili (nature) ya mali iliyofanyiwa uthamini na au mabadiliko ya mwenendo wa uchumi (economic dynamics). Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inakusudia kuleta jedwali la marekebisho katika eneo hili, ili ukomo wa uthamini na ripoti za uthamini kwa minajili ya kulipa fidia uwe mwaka mmoja.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani pia inakusudia kuleta jedwali la marekebisho katika jedwali la marekebisho la Serikali katika kifungu cha 52(5) ili kupunguza wigo wa miaka mitatu wa kulipa fidia na riba hadi kufikia mwaka mmoja na nusu. Hii ni kwa ajili ya kuwabana walipa fidia kulipa fidia na kwa wakati ili kuwaondolea wananchi usumbufu wa kusubiri muda mrefu bila kulipwa fidia yao.

Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza ukomo wa ripoti ya uthamini uzingatie vipengele vyote vilivyocainishwa katika kifungu cha 49(2) na siyo kwenye fidia tu.

## 9. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla muswada huu kama utatekelezwa ipasavyo baada ya kupitishwa kuwa sheria utapunguza changamoto nyingi katika sekta ya ardhi na nyumba zilizokuwa zikitokana na matatizo ya uthamini.

**Mheshimiwa Spika**, rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Serikali ni kufanya marekebisho ya sheria nyingine zilizokuwa zinatoa mwongozo wa uthamini ili kuzioanisha na sheria hii ili kutoleta mkanganyiko katika utekelezaji wa sheria inayopendekezwa.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha.

Wilfred Muganyizi Lwakatare  
**WAZIRI KIVULI NA MSEMaji MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI**  
**KATIKA WIZARA YA ARDHI,**  
**NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**  
8 Septemba, 2016

**MWENYEKITI:** Asante sana Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani, ninakushukuru sana kwa kuukubali Muswada, hamkuupinga na mmetoa mapendekezo mazuri sana, ahsanteni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge kwa vile muda uliobaki na dakika ambazo tunatakiwa kila mchangiaji, ni dakika 15, ningeshauri tupunguze angalau dakika 10, ili tupate wachangiaji zaidi. Kwa hiyo, tutaanza moja kwa moja na Mheshimiwa Godbless Lema na baadaye atafuata Mheshimiwa Elias Kwandikwa na baadaye Mheshimiwa Cosato Chumi.

Mheshimiwa Godbless Lema, hayupo. Mheshimiwa Peter Msigwa hayupo pia, basi tunaanza na Mheshimiwa Sabreena Sungura .

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia muswada huu ambao toka nchi imepata uhuru ulikuwa haujaletwa na kusababisha usumbufu mkubwa kwa Watanzania na wapenda mabadiliko kwa ujumla. Ukiangalia muswada huu una lengo zuri, lakini una matatizo makubwa kwenye uteuzi wa Mthamini Mkuu wa kufanya uthamini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia hapa tumesema miaka yote kwamba, Mheshimiwa Rais amekuwa akilundikiwa vyeo kila mara, lakini katika Muswada huu bado tunasema kwamba, mthamini huyu uteuzi wake utafanyika na mamlaka ile ile, hapa kuna tatizo. Mthamini Mkuu ni lazima angepatikana kwa sifa, watu mbalimbali waliopo Serikalini na walioko nje ya Serikali wapeleke sifa zao ili ziweze kuangaliwa, wachujwe, wafanyiwe *interview* na hivyo apatikane Mthamini Mkuu ambaye atakuwa na tija na hatakuwa na upendeleo kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivi! Mthamini Mkuu anapochaguliwa na mamlaka ambayo iko Serikalini, kesho anaambiwa akafanye uthamini katika mali za Serikali, lazima huyu mtu atakuwa *biased*, lakini kama atateuliwa na mamlaka nyingine tofauti na Serikali ileile ambayo anaenda kuifanyia kazi, ataweza kufanya kazi yake kwa uhuru zaidi na hivyo hatakuwa na *conflict of interest*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia suala zima la Muswada huu, ukija kwenye majukumu ya Mthamini Mkuu wa Serikali, tumeona hapa kifungu cha 6(1)(a), atakuwa na kazi ya kuishauri Serikali kwenye masuala yanayohusu shughuli za uthamini ikiwemo uzwaji wa mali za Serikali na ununuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupendekeza kwa kuwa, kumekuwa na tabia ya wanasiasa ikiwemo Mheshimiwa Rais, Mawaziri na viongozi wengine Serikalini kwenda katika Halmashauri mbalimbali nchini na kuwahamisha wananchi wa maeneo hayo kwa sababu za kisiasa bila kupata ripoti ya tathmini ya awali kwamba nani atalipa gharama za fidia ya wananchi hao, ningependa muswada huu uwaonye na uwakanye wanasiasa wenye tabia hizo kwa sababu mmekuwa mnasababisha sintofahamu kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano namba moja; alikuja Mheshimiwa Rais wa Awamu iliyopita katika Manispaa ya Kigoma Ujiji akawazuwia wananchi wanaoishi katika maeneo ya mlima unao-face *railway station* kwamba wanatakiwa wahame kutokana na sababu za kijiografia. Ni zaidi ya miaka kumi mpaka leo hii anatafutwa mtu wa kulipa fidia hapatikani. Halmashauri wanaulizwa, wanasema fidia ile imekuwa ni kiwango kikubwa zaidi ya bilioni moja, hawana uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hamuoni kwamba tabia hizi za wanasiasa kwenda kutamka matamshi ambayo wanajua Serikali haiwezi kutekeleza ni kuwapa usumbufu wananchi wetu? Kwa hiyo, sheria hii i-*declare* kwamba wanasiasa na viongozi wengine wa Serikalini msiwe na mamlaka ya kwenda kuhamisha ama kusitisha shughuli za wananchi, shughuli za maendeleo pale ambapo Wathamini ambao mnawatungua sheria leo hii hawajafanya thamani halisi ya eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba vijana wetu ambao wana uwezo mzuri watahindwa kupata ajira kwa sababu tu watahindwa ku-*meet* hii *condition* ya umri. Hivyo basi, ili liendane sambamba na lile suala zima la miaka mitatu, tunasema kwamba tutakuwa na wasajili wa mpito na wasajili wa muda pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasajili hawa tunawaambia wawe na *experience* ya miaka mitatu, lakini tujaribu kuangalia taasisi nyingine, kwa sababu siyo kwamba Wathamini hawa ndio wawekewe miaka mitatu lakini tunao Wahandisi ambao wanawekewa *experience* ya *one year*, wakitoka hapo wanapewa *certificate* waanza ku-*practice*. Tunao wanasheria ambao wanapewa elimu ya mafunzo kwa kipindi cha miezi nane mpaka mwaka mmoja; wakimaliza hapo wanapewa muhuri wanakwenda kufanya kazi. Kwa nini kwa Wathamini mweke kikomo cha miaka mitatu? Hii siyo *fair*, tupunguze



kikomo hiki tuweze kupata muda ambao ni wa mwaka mmoja wafanye mafunzo ya vitendo na hivyo wataweza kujajiri na kupunguza tatizo la ajira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napendekeza makampuni na biashara ziwe zinafanya uthamini kila mwaka kama zinavyofanya Halmashauri zetu na Manispaa zetu mbalimbali. Tumeona mwaka 2015 Manispaa ambazo hazikufanya uthamini wa mali zake walipatiwa hati chafu, basi ni vyema makampuni na mashirika na taasisi zilizo za Umma ziweze kuwa zinafanyiwa tathmini kila mwaka ili tuweze kupanua wigo wa mapato katika nchi yetu na kuhakikisha kwamba miradi inayopangwa na Serikali inafanikiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika muswada huu sijaona mkazo ukutiliwa kwa wazawa. Tumeona kuna hawa Wathamini wa mpito na wa muda mfupi wakiwemo na wageni. Kwa nini tunakumbatia wageni kwa *condition* ambazo ni rahisi sana? Tunapoingiza watu wengi waweze kusajiliwa hapa nchini kupitia Bodi yetu ya Wathamini inamaanisha kwamba kuna ajira nyingine Wathamini wetu wa Serikali ama binafsi ambao ni wazawa watazikosa na nafasi hizi zitakwenda kwa wageni. Lazima tuweke utaratibu ambao utawabana wageni waweze kuachia nafasi hizi kwa wazawa na kazi hii iweze kufanyika kwa viwango. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutengeneza soko la ajira, ni vyema basi mabanki yetu na taasisi za fedha ziwe na wathamini wenye sifa kwa ajili ya kuangalia thamani ya wakopaji na isiwe ni suala la *short time* pale ambapo mkopaji anaenda benki ndiyo mthamini anatafutwa kufanya thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema katika sheria hii basi tuweke kifungu ambacho kitasababisha taasisi zote za fedha, mabanki na mashirika mengine ya Kiserikali yawe na utaratibu wa kuwa na wathamini wao binafsi pale ambapo wateja mbalimbali watahitaji kwenda kukopa. Pia kuna Mashirika kama ya Bima, wenyewe wana *loss assessors*. Napendekeza kwamba hawa *loss assessors* wa Mashirika ya Bima basi nao wangukuwa wathamini ili pale inapotokea *loss* thamani halisi ya fidia ijulikane. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda kuchangia kwenye muswada huu ni kuhakikisha kwamba ili kufanya uthamini uliokuwa na tija hususan Serikalini, tumeona hapa awamu iliyopita ya Mheshimiwa Mzee Mkapa, nyumba za Serikali ziliuzwa kwa bei ya chini sana na Taifa likapata hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti kuna nyumba ambazo ziliuzwa mpaka shilingi milioni mbili, mpaka shilingi milioni 10; lakini ukiangalia hali halisi, nyumba hizi zilitakiwa ziuzwe kwa gharama ya juu zaidi. Je, ni vipi sasa sheria yetu hii

tunayoitunga leo itawadhibiti watu ambao wataliingizia Taifa hili hasara kama iliyotokea miaka michache huko nyuma na kufanya wafanyakazi wetu wa mashirika mbalimbali na wafanyakazi wetu wa Serikalini kukaa mbali na miji kwa sababu tu nyumba za Serikali ziliuzwa tena kwa bei ya kutupa ama bei ya bure. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema basi sheria hii iweke msisitizo na iweke mkazo wa kuhakikisha ni jinsi gani basi Wathamini wa Serikali watatenda kazi kutokana na hali halisi ya soko na siyo kulitilia Taifa hasara kama ilivyokuwa ikifanyika siku za nyuma.

Pia napenda niseme kwamba lazima tuwe na *appellate jurisdiction*. Mthamini Mkuu wa Serikali amefanya uthamini, labda mtu aliyefanyiwa uthamini, aidha, wananchi ama shirika ama taasisi yoyote haikuridhika na uthamini uliofanywa na Mthamini Mkuu wa Serikali, taasisi hiyo au mtu huyo ama wananchi hao wanakwenda ku-*appeal* wapi juu ya maamuzi yaliyofanyika? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kumwambia Mheshimiwa Waziri hapa mwaka 2015 katika uchangiaji wangu, nilimwambia kwamba kuna maeneo ambayo watu walifanyiwa uthamini. Mtu alihitaji kulipwa shilingi milioni 20, 30 mpaka 40 lakini alilipwa shilingi milioni mbili, tatu, nne, mpaka tano na kuna watu ambao walitumia fursa hiyo kuwahonga Wathamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu ambaye alitakiwa alipwe fidia ya shilingi milioni 10 aliweza kulipwa mpaka shilingi milioni 60. Je, ni hatua gani za makusudi mnazozitokea kuhakikisha kwamba udanganyifu katika uthamini mnaudhibiti hivyo fidia ya haki stahiki iweze kulipwa kwa wananchi wetu na isiwe longolongo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtu ambaye atakayesababisha mtu kupata fidia chini ya kiwango hatua kali ziweze kuchukuliwa chini ya sheria hii, aidha, iwe kufungwa miaka 10 mpaka miaka 20 kwa sababu watu hawa wanalitea Taifa hasara na wanawatia umaskini Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Sabreena, tunaendelea na Mheshimiwa Elias Kwandikwa na baadaye Mheshimiwa Cosato Chumi na Mheshimiwa Sophia Simba wajandae.

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kwenye Muswada huu wa Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini wa mwaka 2016. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu kutujalia afya, nimepata fursa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza Wizara, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam kwa kuja na muswada huu. Kwa kweli huu muswada umekuja ukiwa umechelewa, ulitakiwa uje wakati ule tunaanza kufanya reforms mbalimbali, kwa sababu unakuja sasa kutuondolea matatizo mengi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, muswada huu unajaribu kutoa kielelezo cha utawala bora kwa sababu tutakapokuwa na Sheria hii ya Uthamini kuna mambo mengi yatakuwa kwa uwazi na itaongeza pia uwajibikaji katika usimamiaji wa hizi rasilimali ikiwemo ardhi, nyumba na assets nyingine ambazo zimetajwa kwenye sheria hii. Pia inaongeza dhana nzima ile ya ushirikishaji, kwamba inatoa fursa ya kushirikisha makundi mbalimbali. Kwa hiyo, nilifikiria nianze kwa kuipongeza sana Serikali kuja na muswada huu na nina uhakika kuna mambo mengi yatakaa vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niseme tu faida chache kwa sababu yapo mambo mengi sana, kutokana na muda niseme tu faida chache ambazo ninaona zitaenda kuondolewa na kuwa na muswada huu. Kwanza utaona kabisa kwamba ili kuweza kutoa ile risk iliyokuwepo kwenye assets zetu kwamba wakati mwingine kulikuwa kuna over valuation wakati labda rasilimali au mali za Serikali zikinunuliwa na labda wakati mwingine kulikuwa na undervaluation wakati mali za Serikali zikiuzwa. Kwa hiyo, hii itaenda kutibu na utaona kabisa kwamba kwenye ile section ya 49 inaonesha kabisa kwamba kutakuwa na vigezo vya ukadiriaji kwenye hizi rasilimali. Kwa hiyo, itatoa zike double standards ambazo zilikuwa zinajitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri wakati akiwasilisha hapa, inaenda tena pia kutupa faida kubwa ya kuweka vizuri ule uthamini wa mali na kupatikana kwa haki za wananchi hasa wanavyopata fidia. Utakuja kuona pia kwamba inatoa fursa sasa ya kuwa na assessment nzuri za kodi na ninaamini Wizara na maeneo mbalimbali yataenda kupata kodi iliyostahiki huku ikiwaacha pia wananchi waweze kulipa kile ambacho wanastahili kulingana na sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo ambayo yalikuwa yanasumbua sana. Wananchi walio wengi wakati mwingine wamekuwa wakichelewa kupata mirathi kutokana na tatizo lililokuwepo. Sasa sheria hii inaenda kuondoa na kufanya urahisi wa kuweza kupata thamani hasa kwenye zoezi la usimamizi wa mirathi huko kwa wananchi wetu; lakini pia ku-facilitate zoezi la mauzo na manunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa kilichokuwa kinanitia moyo, utaona lilikuwepo tatizo kubwa sana kwenye reporting framework ya hesabu zetu za upande wa Serikali. Utaona sasa hii inaenda kutibu, kwa sababu ukija

kuangalia, siyo Tanzania tu, lakini nchi nyingi kuna tatizo la uthamini wa ardhi na nyumba, kuweza kuingia kwenye zile hesabu. Kwa hiyo, utaona kabisa kwamba huu ni mwanzo mzuri wa kuweza kufanya tuweze kuja kuwa na taarifa nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nimsahihishe kidogo msemaji aliyenitangulia kwamba tatizo la uthamini halijafika katika hatua hiyo katika Halmashauri zetu. Zoezi ambalo lilikuwa linafanyika kule alivyokuwa anzungumza hapa, hii ni *stock taking, stock count* ambayo ndiyo walikuwa wanafanya mara kwa mara, lakini walikuwa waniacha nje, zoezi la kuthamini mali kama vile ardhi pamoja na nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unaona kabisa kwamba kupitia sheria hii, tunaenda ku-*improve* ile *reporting framework* kuanzia kwenye Halmashauri zetu na pia kwenye Serikali Kuu, vilevile kwenye ile *consolidation* ya *national wealth*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, muswada huu ni muhimu sana, utarahisisha. Kwa sababu ukiuangalia kwa upana, unatoa nafasi sasa wale *ma-valuer* ambao tulikuwano kuanzia kwenye ngazi ya Halmashauri, sasa wanaenda kuwa *authorized valuers*, kwa sababu walikuwa hawajapata ile nguvu ya kuweza kufanya kazi yao. Kwa hiyo, ninaamini kwamba tutaenda kuwa na *improvement* kubwa sana kwenye hesabu zetu. Yapo mambo mengi yanaonekana hapa na zoezi zima ata kuhusu watu kupata haki kupitia Bima, lakini pia kikubwa itaenda kusaidia kwenye soko letu la hisa, soko la mitaji. Kwa maana hiyo, kwamba tunapokuwa tumefanya uthamini kwa maana ya kwamba zile kampuni zitakapokuwa zinakwenda ku-*deal* na hii biashara kwenye soko la mitaji au soko la hisa, kwa hiyo sheria hii inaenda kuweka ubora zaidi katika ku-*facilitate* ili soko liweze kuwa *effective*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu nichangie kwenye suala zimala muundo wa huyu *Chief Valuer*. Nafikiri la muhimu hapa ni upande wa Serikali kuangalia ni namna gani sasa huyu *Chief Valuer* kumwezesha aweze kufanya kazi vizuri. Kwa sababu utakuja kuona kwamba nilitaka nitofautiane na msemaji aliyetangulia kwamba, kumfanya *Chief Valuer* awe kama CAG. Ni kwa sababu *Chief Valuer* ana Bodi. Kwa hiyo, la muhimu ni kuifanya hii Bodi iweze kufanya kazi vizuri. Bodi hii ikiwezesha itamwezesha huyu *Chief Valuer* afanye kazi vizuri. Muhimu ni hicho kwamba tumwone sasa huyu *Chief Valuer* anaweza kufanya kazi yake kwa nguvu tuweze kuwa na mali yetu iweze kujulikana kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nikubaliane kwamba *Chief Valuer* huyu ni mtu ambaye atasimama kwenye nafasi yake, ataweza kusimamia sekta mbalimbali, ni *cross-cutting*. Kwa hiyo, ipo umuhimu tu wa Serikali kuitazama ofisi hii ili itakapoanza kufanya kazi zake aweze kufanya kazi kwa uzuri na kwa

haraka zaidi ili tuweze kuondoa yale mambo ambayo tuliyaona kama ni shida. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nilitaka niseme kidogo kwamba nimevutiwa na kuwa na hii Bodi, kwa sababu utakuja kuona katika sehemu hii ya uthamini tunapokuwa na bodi; hii bodi ikifanya kazi kama tunavyoziona bodi nyingine kama NBAA, tumeona bodi inayoshughulikia hawa Maafisa wa Ununuzi, lakini tumeona pia hata kwenye upande wa sheria kwamba kabla watu hawajaenda ku-*practice* kipo chombo ambacho kinawa-*regulate*. Nimeona kwamba itakwenda vizuri kwa sababu inatoa fursa ya kwamba hawa wathamini kila wakati kuweza kufanya mitihani lakini pia ku-*practice* ili tuone kwamba wanaenda kufanya kazi nzuri. Utaona kabisa imeweka mamlaka ya bodi ili kuwa na labda na *code of ethics*, kuondoa ile hali ya uzembe. Kwa hiyo, yale yote ambayo yalikuwa yanaonekana kwamba kuna *over valuation* na *under valuation* yametajwa kwenye sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaona kabisa bodi hii inapewa fursa ya kusimamia miongozo mbalimbali ya ndani lakini pia miongozo ya Kimataifa. Kwa hiyo, utaona kabisa kwamba tumekuja sasa kuwa na chombo ambacho kitatufanya twende vizuri zaidi. Kwa hiyo, nataka niipongeze sana Serikali kwa kuja na sheria hii, lakini mimi ninaamini kabisa kuna mambo mengi yataenda kukaa vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho tu nilitaka nizungumzie pale kwenye usajili. Kwenye kile kifungu cha 26, ukikiangalia pamoja na kifungu cha 27, ili usajili wa hizi *firm* uzingatie kwamba mtu ambaye anaweza kwenda kusajili *firm* awe *full registered*, iwalazimishe hawa *temporary registered* na *provisional* ili waweze ku-*team up* na huyu ambaye yupo *full registered* ili *firm* ziweze kufanya vizuri. Nakushukuru kwa nafasi hii. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Elias, tunaendelea na Mheshimiwa Cosato Chumi na baadaye Mheshimiwa Sophia Simba na Mheshimiwa Hamidu Bobali, wakae tayari. (Makofi)

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kupata nafasi hii na pia nitumie fursa hii kuishukuru na kuipongeza Serikali kwa kuona haja na umuhimu wa kuja na muswada wa sheria hii ambao utatuongoza katika kuilinda na kuifanya hii taaluma iwe na sheria ambayo inaisimamia. Kwa sababu ni miongoni mwa taaluma zile tunazoita *rare professional*, lakini hii ni kati ya hizo *rare professionals* ambapo peke yake haikuwa na sheria, haikuwa na masuala yoyote yaliyoletwa kama mambo ya kuwa na bodi na kadhalika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba kuna sheria zinazo-govern Bodi za Wahandisi, sheria zinazo-govern masuala ya Wafamasia, Wapima, Wahasibu na kadhalika. Kwa hiyo, ni jambo la kupongeza kwamba sasa tunakuja kuwa na sheria ambayo siyo tu itasimamia taaluma hii ya uthamini, lakini pia sheria hii jambo lingine la kupongeza na la muhimu sana imekuja sasa na muda *specifically* hasa kuhusu toka mtu alivyofanyiwa uthamini mpaka lini atatakiwa kulipwa fidia yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshashuhudia mara nyingi uthamini ukifanyika na fidia kuja kulipwa hata baada ya miaka 10. Katika sheria hii, inabainisha wazi kwamba baada tu ya uthamini kufanyika na baada ya huyu *Chief Valuer (CV)* kuwa amesha-approve ile taarifa ya uthamini maana yake katika kipindi cha miaka miwili waliofanyiwa uthamini watapata kile ambacho kinawastahili. Kwa hiyo, hii ni hatua mojawapo ya kuthibitisha kwamba Serikali inajali na inawathamini wananchi wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, nina *some observation* hapa kutoka katika hii sheria. Kwa mfano, tukienda na suala zima la *observation* ya *code of conduct*, nadhani ni Ibara ya 20 na ile ya 21, inasema kuhusu malalamiko, lakini haisemi *specifically* hatua gani au adhabu gani yule ambaye atakiuka maadili ya taaluma hii atapewa. Nilikuwa nadhani kwamba pamoja na maelezo ambayo yapo katika kipengele hiki, ingekuwa vizuri kama sheria ingeeleza *specifically* kwamba yule ambaye atakuwa amekiuka maadili, basi kuna adhabu fulani ipo *categorically* kabisa itamkumba yule mtu. Sambamba na hii, katika hiki kipengele pia cha yule atakayekuwa analalamikiwa, pamoja na kutosema waziwazi kwamba adhabu gani atapewa katika msingi wa *natural justice*, haijasema waziwazi kwamba itampa nafasi ya kusikilizwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nadhani kwamba haya ni kati ya mambo ambayo pengine baadaye kwenye majumuisho kitaalam ingeweza kutazamwa mara mbili zaidi, kwamba iseme wazi yule atakayelalamikiwa, yale malalamiko kama yatathibitishwa ni adhabu gani itamkumba yule mtu. Pia wakati huo huo iwe imetoa *room* ya yule mlalamikiwa kusikilizwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hiyo, ukienda katika Ibara ya 8 ya Wathamini Wasaidizi, na mimi napenda niungane na baadhi ya wachangiaji kwamba ikiwa yule Mthamini Mkuu elimu yake na uzoefu wake kwamba Shahada ya Pili ina uzoefu wa miaka mitano; kwangu, kwa sababu hii ni *rare professional* ambayo watu wanasoma miaka minne kama sikosei, lakini pia hata wale watakaokuwa wamesajiliwa, ukienda huko mbele utaona kwamba lazima iwe baada ya uzoefu wa miaka mitatu. Kwa hiyo, napendekeza iwe ni shahada moja ambayo ni Shahada ya Kwanza na angalau miaka mitano isiwe sawa na yule ambaye atakuwa Mthamini Mkuu.



Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika Ibara ya 14, tukizingatia kwamba jana tumepitisha hapa Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa (*Access to Information*) kwa nia ya kupanua wigo wa upatikanaji taarifa, nashauri iseme *clearly* kwamba itatangazwa kwenye magazeti yasiyopungua mawili yanayosambazwa kwa wingi, kwa sababu hapa imeeleza kwamba ile orodha itatangazwa katika Gazeti la Serikali lakini pia katika gazeti moja ambalo linasambazwa kwa wingi. Sasa linaweza kuwa hilo moja likaangukia kuwa ni *Daily News* mathalani au Mwananchi. Sasa tukawa tume-*limit* ile *access to information* ya masuala haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mapendekezo yangu, sheria ingesema angalau magazeti yasiyopungua mawili yanayosambazwa kwa wingi pamoja na ile ya Gazeti la Serikali. Hii pia ya upatikanaji wa hii taarifa unaweza kuiona katika Ibara ya 17 na Ibara ya 34 kama kuna masuala ya uchunguzi na kadhalika. Yale yote yanayohusiana na haya ya watu kupata taarifa, napendekeza isiishie tu kwenye Gazeti la Serikali na gazeti moja linalosambazwa kwa wingi, bali angalau hata magazeti mawili kwa maana ya kwamba kama liko moja la Kiingereza, basi moja la Kiswahili ili kupanua ule wigo wa *access to information*. Kwa hiyo, vipengele vyote ambavyo vinahusiana na kutoa hii taarifa, mapendekezo yangu tungepanua huo wigo wa taarifa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika usajili imeeleza hapa kwamba inabidi kuwe na uzoefu wa miaka mitatu. Napendekeza kwa yale yale niliyosema, kama hii ni *rare profession* na ambayo wanataaluma hii katika mafunzo yao wanafanya, nadhani kila mwaka *practical training*, basi angalau tungesema miaka miwili, yaani sifa mojawapo ya mtu kupata usajili isiwe miaka mitatu, iwe ni miaka miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, katika kipengele cha 68 Mthamini Mkuu ni kama sheria inampa haki fulani tu ya kuwa yeye ni mtu wa kukaa ofisini tu, kwamba mthamini yeyote aliyesajiliwa ambaye ripoti yake itakuwa na maelezo au taarifa yenye makisio ya juu au ya chini, ule uzembe utamkumba mwanataaluma mwenyewe, yaani mthamini atakuwa tu ame-*relax* tu na tayari ile *report* pengine ameshai-*approve*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwamba hapa aende *miles away*, kwamba kama atakuwa na shaka, basi kwa gharama zozote pafanyike au atume timu au mthamini mwingine apate kwenda kujiridhisha juu ya lile jambo kwa sababu *otherwise* naona kwamba yeye atakuwa tu amekaa ame-*relax* kwa sababu aliyekosea ni mtu mwingine basi yeye hawajibiki popote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kwa kuwa kengele imeshanipigia, nazungumzia hili la ukomo wa muda. Kwa mfano, tutakapokuwa na uthamini ambao una-*cover* eneo kubwa, kuna ujenzi wa barabara kutoka hapa *let's say*



mpaka Iringa. Sasa ule uthamini, hii *cut-off date* itahesabika wapi? Kwa mfano, uthamini huu unaweza kuchukua hata miezi sita, je, wale watakaoziziwa Dodoma, watakaokutwa Mtera, Isimani, Nyang'oro na kadhalika, wao ile *cut-off date* itasubiri mpaka siku ya *approval* ya ripoti ama tuwe na utaratibu ambao itahesabika ile siku ya kwanza anajaza tu ile fomu ya kufanyiwa uthamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, napenda kwenda kwenye kipengele cha 55 kama muda utaniruhusu, ile inayosema kwamba mthamini ataingia tu kwenye eneo; nashauri kwamba pawepo na *prior information* au hata *notice in advance* kwa sababu *the way* ilivyo inaonekana kwamba huyu mthamini ana access kubwa ya kuingia kwenye eneo na kufanya kazi yake na kama hatapata ushirikiano, yule ambaye hatatoa ushirikiano, kuna adhabu ambayo itamkumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kuwe na *advance information* kwamba kuna hili linakuja kufanyika ili kumwondoa huyu mtu kwenye tahadhari ya kutokuwa na ushirikiano, sasa akiwa kama amekuwa *ambushed*, maana yake ni kwamba atakosa kutoa ushirikiano na akikosa kutoa ushirikiano, huku mbele unakuta kwamba kuna adhabu ya faini au kifungo kisichopungua miezi 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya napenda kushukuru na mimi wananchi wangu wa Lungemba ambao wanasubiri malipo ya fidia, nadhani sheria hii sasa inaenda kuwa-*accommodate* ipasavyo na fedha zile zitalipwa kwa wakati kama ambavyo sheria inaenda kuelekeza. Nakushukuru sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Sophia Simba.

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie suala lililopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kuwapongeza sana Wizara hii ya Ardhi; Waziri na Naibu wake, tumewaona wanavyohangaikia migogoro ya ardhi na leo wamekuja na sheria ambayo itawasaidia zaidi katika kupunguza migogoro hii ya ardhi. Kabla sijaendelea, naomba nichukue nafasi hii nimpongeze sana Rais wetu mpenzi kwa jinsi alivyoshughulikia tatizo la pale Dar es Salaam kwenye *quarter* za Magomeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais pale ameonesha ubinadamu wake na utu wake, kwa kweli lile tatizo lilikuwa kubwa, lakini wananchi tunamwambia hongera sana na aendeleo hivyo. Ameonesha jinsi anavyowajali

watu wa pale Magomeni, karibu nusu ya wale ni *civil servants* wa siku nyingi sana ndiyo wako pale. Kwa hiyo, kama wenzao waliuziwa nyumba, kwa nini wao wasipewe wakae pale miaka mitano? Nashukuru sana kwa hatua ambayo imefikia. Namshukuru Mheshimiwa Waziri ambaye amelifikisha mpaka limefika kwa Mheshimiwa Rais; sisi Wabunge wa Dar es Salaam tumekuwa tukipata taabu sana kwa malalamiko yao. Pia namwomba Mheshimiwa Waziri, hebu asogee kidogo afike Ilala pale *quarter* tumalize lile tatizo ili mambo mazuri yaonekane pale. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye sheria hii. Sheria hii imekuja wakati muafaka; pamoja na kwamba imechelewa, lakini ni sheria ambayo nadhani itatusaidia sana. Inakwenda kupunguza migogoro ya ardhi na kubwa zaidi ninaloliomba Mheshimiwa Waziri, elimu ifike kwa wananchi, hawajui haki zao. Wananchi wengi wamepoteza haki kutokana na kutokujua, inakuja Manispaa, anakuja Mthamini wa Manispaa, anathamini, analipa anavyotaka au halipi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, kule Dar es Salaam ile *Avic City*, wananchi wamedhulumiwa vibaya sana pale, kama kungekuwa na kitu kama hiki. Kungekuwa na sheria kama hii, nadhani wengi wamekufa pale wameondolewa, tunaona kuna *Avic City* lakini wenyewe waliokuwepo pale sasa ni maskini kabisa. Haya mambo kwa Dar es Salaam yamekuwa makubwa kwa sababu kumejitokeza Wathamini wengi sana ambao wanaenda wanachukua ardhi analipwa mtu shilingi milioni moja yeye anakwenda kutengeneza shilingi milioni 100 bila hata huruma. Kwa hiyo, nadhani wananchi wakijua kuna sheria hii, kabla hawajauza watakuwa wanathaminisha ardhi yao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii pia itatusaidia hasa kutakapokuwa na uthamini ambao uko *registered*, vizuri kabisa, wakati tukitaka kutoa *collateral* kutafuta mikopo mbalimbali, wakati mwingine thamani inathaminishwa inakuwa ndogo kumbe ni kubwa. Kwa hiyo, kwa sababu sasa itatengenezwa na wenyewe kabisa, nadhani itatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo limekuwa likiwakuta hawa Wathamani, anaweza akaenda akathamini jengo la mtu, siku benki inataka kwenda kuchukua mkopo wake, wanauza nyumba ya mtu kwa thamani ya chini sana. Nyumba ambayo imejengwa kwa pesa nyingi lakini kwa sababu benki inataka pesa zake, hawajali yule Mthamini anaithaminisha kwa pesa kidogo, matokeo yake wewe mwenye nyumba hupati kitu chochote. Nadhani hapa tumepata mwarobaini sasa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, akina mama wakati tunajaribu kugawana mali tukiachana, *matrimonial assets*, hivyo hivyo akina baba walikuwa na mchezo

anakwenda anaongea na Wathamini wanathamini nyumba kwa pesa ndogo, mashamba kwa pesa ndogo; kwa hiyo, akina mama walikuwa wanaonewa pale. Kwa hiyo, akina mama nadhani tulielewe hili sisi kama Wabunge wanawake tukawaelimishe akina mama wasikubali vitu hivi vithaminiwe na Wathamini vishoka. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho nimekipenda ni kwamba hii ardhi ikishathaminiwa baada ya miezi sita inaanza ku-*attract* riba na miezi sita mingine ina-*attract* riba zaidi tena, lakini baada ya miezi 24 (miaka miwili), basi uthamini ule umekwisha na inarudi kwako. Nimeona hilo ni jambo zuri na litaifanya Serikali au yule ambaye anatakiwa awalipe alipe haraka tofauti na ilivyokuwa Kipawa. Kipawa watu wamekaa miaka 28 hawafanyi jambo lolote. Waliokuwa na hoteli wengine walishazivunja baadaye hakuna kulipwa fidia, wamekaa muda mrefu sana mpaka wamekuja kulipwa, wengine wameshakufa. Kwa hiyo, nadhani kwa hali ilivyo kutakuwa na *speed* ya kulipa. Wengine kama kule Kigamboni pia wamepata hasara sana kwa sababu ya kusubiri subiri mambo kama haya ingawa sasa hivi naona mambo yanakuwa mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sheria hii mnazungumzia kutoa *notice* pia, ni jambo zuri kwa sababu wale ambao nyumba zao kulikuwa na miradi inapita, zile alama, zile "X" nyeusi, "X" nyekundu, kijani, zilikuwa zinawapa hofu sana wananchi. Naamini kwamba sasa zile "X" zitaenda baada ya maelewano; baada ya kuzungumza, wananchi waelewe, wakubaliane, baadaye ndiyo hizo "X" ziwe pale tofauti na ilivyokuwa huko nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza na ninaomba tu kwa hapa tulipofikia, sheria mbalimbali ziwe *harmonized*. Maana yake huko kwenye *Local Government* wana sheria zao, kila mahali wametengeneza sheria zao ili hii sheria iweze kutumika ipasavyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Sophia Simba kwa kulinda muda. Tunaendelea na Mheshimiwa Hamidu Bobali na baadaye Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile na Mheshimiwa Pauline Gekul wajiandae.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Na mimi niungane na baadhi ya wazungumzaji hapa kwamba sheria hii ni nzuri na dhamira inaonekana ni nzuri na ukisoma maelezo ya Waziri wakati anatoa hoja pia uchanganuzi wake ni mzuri. Napata shida katika baadhi ya maeneo tu ambayo ningeomba sasa nichangie ama nimshauri Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, inaonekana hii sheria kama inakwenda kuwa *mother law*; inatengeneza *contradiction* na baadhi ya sheria nyingine. Kwa mfano, wakati Waziri anawasilisha, alizungumzia suala la fidia ambalo kimsingi kabisa ni kweli watu wanakandamizwa, wananyonywa, lakini pia hii nchi ina Sheria ya Fidia. Sasa sijui hii sheria inawezaje kwenda *ku-cut across* na Sheria ya Fidia ambayo tunayo kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia umezungumzia suala la ndoa, ni jambo jema kwamba kuna *tendency* ya wanaume kuwadhulumu wanawake, lakini huko kwenye sheria huko kuna mambo haya ya Sheria za Mirathi na Sheria za Dini ambazo zinaongoza masuala mazima ya ndoa, naona pia inaweza kutengeneza *contradiction*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nishauri jambo lingine. Katika *definition* ya *property* ambayo Kamati ilishauri na mimi pia ningeweza kushauri kwamba tuongeze baadhi ya maneno kwa sababu siyo tu nyumba na majengo ambazo watu wanadhulumwa, leo watu wanadhulumwa hata mashamba yao yanaliwa na tembo, lakini thamani inayofanyika ni thamani dhalili kabisa kwa wananchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimboni kwangu hivi sasa tembo wamekula vyakula vya wakulima, wamemaliza mashamba, sasa hivi wanaingia kwenye kuharibu mikoroshu. Sasa mtu anaharibiwa shamba lake la mikoroshu ekari 10, ekari 15, halafu anakwenda kulipwa shilingi 100,000, *this is unfair*. Kwa hiyo, naomba kama kuna uwezekano, *definition* ya *property* iongezeke na haya mengine, uharibifu unaofanywa na tembo nchini kwetu, pia iingie huko ili nao wafanyiwe tathmini au uthamini na hawa wathamini tunaokwenda kuwatungia sheria. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine naomba *decentralization* ya huyu mtu anayeitwa Mthamini, isiwe makazi yake yanaendelea kuwa mjini; sisi watu tunaotoka kwenye majimbo ya vijijini na wananchi wangu wa pale Mchinga akitaka kukutana na Mthamini, aende Lindi na akifika kule wakati mwingine pia anaweza akamwambia mimi sina mafuta ya kujia huko Mchinga. Kwa hiyo, ni kwamba kuwe na *decentralization*. Hawa watu wawe wanapatikana kwenye ngazi za Halmashauri, wawe wa kutosha ili waweze kwenda vijijini ambako Watanzania wengi ndiko waliko; kusiwe tena na urasimu kwamba sina mafuta, ama nashindwa kuja kwa sababu ya umbali na mambo mengine. Tufanye *decentralization* ya uhakika, wasiwe *centralized*, ni jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningeweza kushauri ama kuchangia, naona hapa kwenye kifungu cha 52 cha *compensation* kweli mmeweka kwamba kutakuwa na riba, lakini inaonesha kwamba ule ukomo ni zaidi ya miaka mitatu, ukiangalia vile vipindi vya miezi sita, sita ni zaidi ya miaka

mitatu, bado hatuondoi tatizo la watu ambao watakuwa wanachukua mali zao hawa wananchi iwe Serikali ama wawekezaji ku-*delay* kwenye kulipa. Kipindi cha miaka mitatu ni kikubwa sana na mtu anaweza akaamua tu kwamba uwezo wa kulipa riba ninao, kwa hiyo, anaweza kukaa, akachelewa na baadaye sheria inasema kwamba lile eneo linaweza likarudi kwa mwenyewe. Tayari tumeshamharibia malengo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa yeye anakuwa ameshajiandaa kwamba hili eneo limeshafanyiwa uthamini, nitalipwa. Unapokuja ukasema kwamba sasa kwa sababu ameshindwa kukidhi vigezo, tunalirudisha tena, bado changamoto iko pale pale kwamba badala ya kuwa tumemwondolea shida na kero huyu mwananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine ambalo nimeona Mheshimiwa Waziri kama litampa mamlaka kubwa sana, kuna kifungu kilitakiwa kuwepo kwenye sheria, naona siyo vyema kukipeleka kwenye *regulation* kama mlivyopendekeza, kwamba kuna mambo ya msingi ambayo yalipaswa yawe kwenye sheria yenyewe. Ukisoma kifungu cha 49 na kifungu cha 52(6) kinaeleza kwamba baadhi ya vitu ambavyo vitafanyiwa uthamini, maelezo yake yatatolewa na *regulations* za Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini vitu hivi vyote visingetajwa kwenye sheria badala ya kusubiri Mheshimiwa Waziri sasa kwenye mwongozo wake hivyo vitu avitaje kwenye mwongozo? Ni vema kwa sababu haya mambo yanahusu maisha, *property* za watu na za wananchi, ni vizuri yangewekwa kwenye sheria ikabaki ni utaratibu wa kisheria, siyo tena utaratibu wa kikanuni kwamba tusubiri kanuni za Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine niendeleo tu kusema kwamba sheria imechelewa, kuna *contradiction* kubwa ya namna watu wanavyolipwa, mkanganyiko mkubwa upo. Sisi kule Lindi tuna miradi ya *LNG* ambayo Mheshimiwa Waziri hapa alikuwa anajibu swali, leo unakuta kuna *contradiction* *TPDC* wanasema wao wanalipa kiwango hiki, Manispaa wanalipa kiwango hiki, kumekuwa na *contradiction* kubwa. *Contradiction* hii inachelewesha baadhi ya miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati wakati anajibu hapa alishindwa kueleza sijui kwa sababu haijui ama ni kwa sababu ya muda, kwamba pamoja na mambo mengine ambayo mradi wa *LNG* unaweza ukawa unachelewesha pale Likong'o ni kwamba uthamini unaofanywa, wananchi bado wanaendelea kugomea kwa sababu kile kiwango kinacholipwa wao wanakiona ni kidogo zaidi, lakini pia *TPDC* wana kiwango chao, Manispaa wana kiwango chao. Kwa hiyo, ni vyema kama hii sheria

ingekuwa imewahi ingekuwa labda ni mwarobaini kwa haya ambayo leo yanakwamisha kuendelea kwa miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme kwamba sheria kama ilivyo ina malengo mazuri, wasiwasi wangu ni kwenye usimamizi, kwa sababu shida ya nchi hii siyo tu kuwa na sheria nzuri, usimamizi wenyewe wa sheria ni changamoto. Kwa hiyo, kama kutakuwa na usimamizi mzuri, kutakuwa na *political management* nzuri ambayo imejipanga kuja kutatua kero za wananchi, tunaweza tukapiga hatua kwa namna moja ama nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Bobali kwa kulinda muda. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, hayupo. Tuendeleo na Mheshimiwa Richard Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza namshukuru Mungu kwa siku ya leo, lakini pia naipongeza Serikali kwa ujumla na hasa Wizara husika kwa kuweza kuwasilisha muswada huu. Mazuri mengi ambayo tutafaidika kwenye muswada huu yameelezwa ikiwa ni mambo ya fidia, watu kufanya kiutaalam, mambo ya mikopo, wawekezaji na kupunguza utapeli kwa ujumla. Naipongeza sana Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Waziri Mkuu alifanya ziara Mkoa wa Katavi na Rukwa, aliweza kutatua kero ya ardhi kuhusu utapeli wa wanakijiji waliokuwa wanatapeliwa. Pamoja na hayo kuna masuala madogo ambayo naomba Mheshimiwa Waziri akija aweze kutupa ufafanuzi au kuelewa kwa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ni ukataji wa rufaa kama ambavyo ameeleza kwenye hotuba yake, lakini kwa haraka haraka sijaona kifungu cha kisheria ambacho kinamwezesha mtu aliyefanyiwa thamani au kuthaminiwa kwamba atakitumia kwa ajili ya kukata rufaa na endapo hajaridhika na Mthamini Mkuu hiyo rufaa yake anaweza kuipeleka wapi? Tutaomba Mheshimiwa Waziri aweze kutufafanulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile endepo Mthaminiwa atakuwa haridhiki na uthamini uliofanywa na Serikali, je, kuna uwezekano wa kumweka Mthamini wa binafsi (*independent valuer*) halafu iingie kwenye Bodi? Hilo nalo Mheshimiwa Waziri tutaomba utusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika muswada huu Kifungua cha 25 kinazungumzia adhabu kwa lugha nyepesi tuiite vishoka, lakini pia ukienda Kifungu cha 62 kwenye masharti ya jumla kinazungumzia adhabu.



Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Kifungu cha 25 kwamba mtu atapewa adhabu kati ya shilingi milioni tano mpaka shilingi milioni 20 ikiwa ni mtu, lakini kama ni kampuni ni shilingi milioni 20. Ukienda kwenye masharti ya jumla Kifungu cha 62 kinazungumzia adhabu itakuwa kima cha juu ni Shilingi milioni tano au kifungo cha miaka miwili au vyote kwa pamoja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naona hivi vifungu viwili kama vinaoana kutokana na makosa; kwa sababu kifungu cha 25 ni mtu ambaye hana cheti; lakini ukienda kifungu cha 62 ni mtu ambaye anafanya kazi, mtu ambaye hajasajiliwa, kwa hiyo, wanafanana na wanaoana kwamba mtu ambaye hajasajiliwa ni sawa sawa na mtu ambaye hana cheti. Kwa hiyo, hizi hesabu tusiwe na *double standard* na kuondoa katika maamuzi ya mahakama kutokuweka mazingira ya rushwa, basi adhabu iwe ya aina moja kati ya kifungu cha 25 na 62.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu taarifa ya utekelezaji, kwamba Bodi ikishafanya kazi yake baada ya mwaka, itatakiwa ndani ya miezi mitatu itengeneze taarifa ya utekelezaji. Sasa katika kifungu cha 61 inaelekeza Bodindani ya miezi minne wapeleke taarifa kwa Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Waziri copy ataipeleka katika Bunge, ikiwa Bunge maana yake ni Kamati husika. Sasa wasiwasi wangu ni kwamba taarifa hii itakuwa ni taarifa ambayo haijakaguliwa na Mkaguzi wetu, CAG.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri kwenye kifungu hiki, taarifa iende kwa Mheshimiwa Waziri wakati imekwishakaguliwa ili anavyoileta katika Bunge iwe ni taarifa ambayo imeshapita kwa Mkaguzi Mkuu. Ukiangalia zile *timing* ni mwezi Septemba na mpaka mwezi wa tatu ambapo Mkaguzi Mkuu anatoa taarifa zake. Kwa hiyo, hilo nalo tutaomba Mheshimiwa Waziri aweze kuliangalia, ikiwezekana basi alete *schedule of amendments* nyingine baada ya mapendekezo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 57, inazungumzia masuala ya adhabu. Sasa kuna lugha pale imenitatiza kidogo, inasema Bodi itakavyoona. Kwa hiyo, tumeacha uhuru, Bodi iangalie ni adhabu kiasi gani. Sasa ni bora kwamba Waziri atakapotengeneza kanuni kwa kurejea kifungu hiki cha 57, aangalie ni adhabu gani ambazo Bodi itaweza kuzitoa kuliko kuacha mazingira ya Bodi kufanya uamuzi wakati kosa limetokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kingine ambacho ningependa kuchangia ni kifungu cha 49 kwamba Mthamini anavyoandika *report* anatakiwa aandike sababu za kufanya huo uthamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni bora Waziri katika upande wa zile kanuni aoanishe hizo sababu, tuwe na sababu ambazo ni *standard* ili watu wetu



wanavyoandika hizi *report* za huu uthamini ambao wameufanya, mtu asitoe sababu zake na lugha zake ambazo zinakuwa hazieleweki; tuwe tayari na sababu zionyeshwe kwenye kanuni ambazo zitakuwa ni *standard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu wengi tunahitaji kuchangia, nishukuru kwa leo, ni hayo tu. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa kujali muda. Tunaendelea na Mheshimiwa Pauline Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuweka mawazo yangu katika muswada huu muhimu kwa maslahi ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze kwenye muswada nikihitaji ufafanuzi labda ni-*declare* tu *interest*, mimi ni Mjumbe wa Kamati hiyo, lakini kwa sababu hiyo sikatazwi pia kuweka mawazo yangu katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate ufafanuzi. Suala la kwanza, mwanzoni tulikuwa na utaratibu kwamba taarifa zie za uthamini zinapokuwa zimeshakwenda kwa ngazi za juu, kunakuwa na nafasi za Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa inaporudi wana-*verify* pia, lakini katika muswada huu hawajatajwa popote. Sambamba na hilo, naomba nifahamu tu kama sasa nafasi zao pia hazipo, lakini pia huyu mwananchi akate rufaa wapi pale ambapo anakuwa hajaridhika na uthamini ule?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba Wizara itusaidie kujibu; kuna wananchi wengi ambao kwa muda mrefu sasa leo tunatunga hii sheria wao wamekuwa wakisubiri fidia zao hazijalipwa kwa muda mrefu na hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani imesema kwamba kuna wale ambao wanasubiri fidia katika maeneo ambayo yametengwa kwa akiba ya barabara na maeneo mengine; hawa watu wamekaa kwa muda mrefu hawajalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya sheria hii kupitishwa, sawa mtapata ule muda ambao unapandekewa na baadaye Bunge tutapitisha, hao wengine wanachukuliwa wapi au wanakuwa wamesahaulika? Napenda kufahamu kwa sababu wako wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze kwenye vifungu vya Muswada huu, katika kifungu cha 7(1). Kifungu hiki kinasema; "Iwapo Mthamini Mkuu ameridhika kwamba uthamini haukufanyika ipasavyo, atapendekewa kwa mamlaka husika nidhamu na hatua zinazopaswa kuchukuiwa dhidi ya Mthamini aliyesajiliwa."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mawazo yangu, ni vizuri sasa kwa sababu tunatunga sheria, tukaweka adhabu wazi wazi. Mheshimiwa Waziri ulikuwa umeeleza katika hotuba yako kwamba nia ni njema, kulikuwa na Wathamini wanafanya ndivyo sivyo na vitu kama hivyo, ndiyo lengo mahususi la muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa nini mnataka kumwachia Mthamini Mkuu apendekeze hatua na kwa nini tusiweke sasa kwenye muswada huu au kwenye sheria hii kwamba huyu ambaye amekuwa akifanya *under valuation* kwa watu wetu na mali zao; huyu mtu adhabu yake iwe ni kiasi hiki? Kwa nini tumwachie Mthamini Mkuu yeye apendekeze? Hiyo mamlaka husika inaweza isimwadhibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napendekeza tu au nashauri kwamba hii adhabu tuiweke kwa sababu tunatunga sheria hii pia kulinda watu wetu ili zile thamani za majengo yao na hadhi zao zisichezewe hovy hovy na hawa Wathamini. Kama lengo ni kuwabana hawa Wathamini, basi tupendekeze adhabu na tusiache hivi ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye kifungu cha 52; Mheshimiwa Waziri amependekeza kutoka kile ambacho mwanzoni kiko kwenye kifungu cha 52 kwamba muda Waziri atabainisha, lakini umeenda kwenye miaka mitatu katika suala zima la kulipa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba huu muda ambao wananchi wetu wanasubiri fidia usiwe zaidi ya mwaka mmoja na tunafahamu kwa muda mrefu sana kwamba wananchi wamekuwa wakitwaliwa maeneo yao, lakini wanasubiri kwa muda mrefu, hawapati hizo fidia; tuwasaidie pia kwa sababu hii ardhi ndiyo rasilimali pekee Mtanzania anayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapomwacha kwa miaka mitatu akisubiri fidia hiyo, anaweza akawa amesha-mess-up na hajui kwamba afanye nini. Baadaye unakuja kusema kwamba unamlipa au haumlipi, wakati huo umeshampotezea muda kama hao wa *reserve* ya barabara tumewaacha sasa, hawajalipwa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napendekeza kwamba endapo ardhi imetwaliwa, lakini huyu mtu baada ya mwaka mmoja hahitaji tena ardhi hiyo, basi alazimike kama ni ile *interest* ambayo ina-*accrue* baada ya miezi sita, ilipwe hata kama haihitaji ile ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri hivi kwasababu zifuatazo: kuna baadhi ya watu binafsi ambao labda wanataka kujenga shule au taasisi fulani,

wanataka kuwekeza kitu fulani, anahodhi ardhi ya wananchi kwa miaka miwili, mitatu au minne kama tutapitisha mwaka mmoja au kama mtapitisha pia kwa wingi wenu hiyo miaka mitatu mnayoipendekeza, lakini kuna watu watatumia ardhi hizo, atakaa nayo, hajalipa fidia, baadaye anasema siihitaji tena ardhi hiyo. Huyu mwananchi anakuwa katika hali gani? Miaka mitatu umempotezea muda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashawishi Bunge hili kwamba pia tuweke charge fulani kwa mtu atakayehodhi hiyo ardhi kwa lengo la kutaka kuendeleza, lakini baadaye aka-reject, akawarudishia wananchi, asiseme tu ardhi yenu hiyo hapo, siihitaji kuwalipa tena fidia kwa sababu siihitaji na siitumii tena. Tuwalinde hawa wananchi ambao watakuwa wamapotezewa muda, angalau awajibike hata some amount aweze kulipa ili tuempushe wimbi kubwa la watu ambao watahodhi ardhi, baadaye wanawarudishia wananchi wakati wameshawapotezea muda na wameshindwa kuendeleza ardhi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwamba miaka mitatu ni miaka mingi sana, kama lengo ni kuwasaidia Watanzania, Mheshimiwa Waziri akubaliane na maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba isiwe zaidi ya mwaka mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niende kwenye kifungu cha 55; hiki kifungu kinasema, Mthamini aliyesajiliwa endapo atataka kuingia kwenye eneo lolote au kwenye jengo lolote lile, hatakiwi kukataliwa. Pia Mheshimiwa Waziri akaleta marekebisho katika jedwali lake kwamba aweze kutoa taarifa; inaweza ikawa ya maandishi au taarifa yoyote ile. Niongezee kwamba iwe ni kwa ridhaa ya yule anayehodhi eneo hilo, iwe ni ardhi au jengo, kwa sababu taarifa inaweza isimfikie kama hajatoa ridhaa kwamba nakubali tukafanye uthamini wa haya niliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Waziri, kuna Wathamini watakwenda watasema mmiliki anafahamu, lakini hawa wamiliki hawafahamu. Nitoe mfano mzuri wa wananchi wa Jimbo langu la Babati Mjini eneo la Bagara Ziwani, Mheshimiwa Waziri analifahamu sana. Wale wananchi walithaminiwa maeneo yao bila wananchi wengi kufahamu hata kama Wathamini wameingia kwenye maeneo hayo, wakabaki kuwafukuza kwa silaha. Maana yake ni nini? Wakaja wakatoa taarifa ya uthamini ekari ifidiwe kwa shilingi 240,000. Wananchi wengi wakakataa kuchukua zile fidia kwa sababu haikuwa ridhaa yao pia na hawakushirikishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika kifungu hiki cha 55, iwe pia pamoja na taarifa ya maandishi, pawepo na ridhaa ya mwenye mali hiyo, iwe ni ardhi au jengo kwamba sasa hili lifanyike. Tusipofanya hivyo, taarifa zitapikwa

mezani na baada ya hapo wananchi watakataa na mchakato wa fidia utachukua muda mrefu sana na matatizo yatakuwa mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upesi upesi kifungu 55(2), nipendekeze kwamba hiki kifungu tukifute kabisa na tufanye vice versa. Kinataka mtu ambaye amekataa kwamba eneo lake lisithaminiwe, hajatoa ushirikiano, kifungu 55(2)(d) inapendekeza adhabu, kwamba atatozwa *fine* isiyopungua shilingi milioni moja na isiyozidi shilingi milioni tatu au kifungu kwa kipindi kisichopungua miezi 12 na kisichozidi miezi 24 au vyote kwa pamoja; *fine* na kifungu. Naomba hii adhabu iwe nikwa hao Wathamini. Watakapokuwa wamekosea...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru nitaleta *amendment*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Gekul. Kwa vile muda umebaki kidogo, nampa nafasi Mheshimiwa Mary Chatanda kwa dakika tano ili aweze kumalizia. *(Makofi)*

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi angalau kwa dakika tano hizo, lakini naanza kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kusimamia utawala wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania sasa hivi wanazijua mbivu na mbichi, wala watu wengine wasipoteze nguvu bure kwa ndoto za alinacha, wala wasijenge ukuta usiokuwa na matofali. Wamwache Mheshimiwa Rais atekeleze majukumu yake kwa mujibu wa Katiba ya nchi na jinsi ambavyo waliweza kumpa kura wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma kwenye hiki kitabu chao, ni kumzungumza yeye tu kwenye ukurasa wa kwanza, wa pili na wa tatu. Sasa naomba wajue kwamba Rais wetu anasema Hapa Kazi Tu, wala hahitaji ukuta ambao hauna matofali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake kwa kuleta Muswada huu ambao unahusu Mthamini Mkuu, Uthamini pamoja na ...haya sasa! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza kwa kuletwa Muswada wa Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini wa mwaka 2016. Naungana na mawazo ya

Kamati ambayo tumezungumzia na kukubaliana na mapendekezo yaliyoletwa na Serikali. Kwa mfano, katika kifungu cha 5 ambacho kinazungumzia suala la Mthamini Mkuu, kwenye sheria inasema Mthamini Mkuu atateuliwa na Rais, lakini ni miongoni mwa Watumishi wa Umma. Sisi kama Kamati tumekubaliana na wenzetu upande wa Serikali kwamba tupanue wigo zaidi kwa maana ya kuacha nafasi hii iweze kuwa na wigo mpana ili kusudi aweze kupatikana Mthamini Mkuu ambaye ana sifa na vigezo vya kuweza kuteuliwa. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kifungu cha 6 kinachohusu mamlaka ya majukumu ya Mthamini Mkuu, tumeangalia tukaona kwamba ni vizuri kikaongezwa kifungu cha (3) kitakachompa Mthamini Mkuu Mamlaka ya kutekeleza majukumu yake chini ya sheria hii kwa uwazi bila kuingiliwa na kutokuwa na upendeleo wowote. Vilevile tulifikiri ni vizuri basi kifungu hiki kikaendana na kifungu cha 6(1)(h) mbacho kinasema; “Kuandaa na kusababisha kuandaliwa, kusimamia na kuidhinisha taarifa zote za uthamini.” Kwa hiyo, kikiungana na hiki ndiyo kitaleta maana nzuri katika muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia tena kwenye kile kifungu cha 6(1)(e) kinachohusu kuwasilisha *report* ya uthamini kwa Waziri; nakubaliana na Kamati kwamba *report* ni vizuri iwasilishwe mara mbili kwa mwaka badala ya miezi mitatu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia sehemu ile ya tatu inayohusu Bodiya Usajili wa Wadhamini, Kifungu kile cha 13(1)(d) kinachohusu muundo wa Bodi; muundo wa Bodi umefanyiwa marekebisho makubwa. Tumeangalia na tumeona kwamba kuna taasisi ambazo zilikuwa zimeachwa, sasa sisi tumefikiri ni vizuri tukaingiza Wawakilishi toka Bodiya Taifa ya Uhasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) na Wawakilishi toka Chama cha Mabenki Tanzania kwani hawa ni wadau wakubwa namba moja wa uthamini wakati wa kutoa mikopo na wanao uwezo wa kushauri na kutoa mawazo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi ya kushukuru tena kwa kunipa nafasi, niseme kwamba naungana na mawazo ya Kamati na vilevile naungana na mawazo ya Serikali. Ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsanteni sana Waheshimiwa wote ambao mmechangia. Kwa vile muda wetu umemalizika kwa mchana wa leo, kabla sijaitisha Bunge niseme kwamba jioni tutaendelea kwa kuanza na Mheshimiwa Salma Mwassa baadaye tutakuwa na Mheshimiwa Fredy Atupele, Mheshimiwa Silafi Jumbe na Mheshimiwa Omary Mgumba.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge kwa mchana huu hadi saa 11.00 jioni ya leo.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. ASIA MINJA - KATIBU MEZANI:**

### **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**(Muswada wa Sheria ya uthamini na Usajili wa Wathamini wa mwaka 2016  
(The Valuation and Valuers Registration Bill, 2016)**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na wachangiaji niliowataja pale mchana. Tunaanza na Mheshimiwa Salma Mwassa na baadaye tutaendelea na Mheshimiwa Fredy Atupele.

**MHE. SALMA M. MWASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza kabisa napenda kuishukuru Serikali kwa kuona uzito wa jambo hili la tatizo la uthamini katika nchi yetu. Kwanza ni-*declare interest*, mimi ni mthamini na mwenye usajili wa kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudi kwenye kuchangia muswada. Kwanza napenda kuipongeza Serikali kwa kuona kwamba hili tatizo limekuwa ni kubwa na linapotezea Serikali mapato na linafanya wananchi kuwa katika hali mbaya kutokana na mali zao kuthaminiwa aidha kwa kutokukidhi viwango au kuthaminiwa kwa wathamini ambao hawana uhakika au siyo wanataaluma hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri na wafanyakazi akiwemo *Chief Valuer* kwa kumshauri Waziri kwa ushauri wake wa kitaalamu na kuuleta huu muswada Bungeni. Faida za muswada huu ni nyingi kwa kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa muswada huu utaongeza mapato ya Serikali kwa maana *valuation* nyingi zilikuwa zinafanyika chini ya kiwango, hivyo Serikali ilikuwa inapoteza mapato makubwa kwa uthamini. Kwa mfano, kukadiria kodi ya majengo, kukadiria *land rent* au kodi ya ardhi. Kwa sababu Wathamini wengi hawakuwa na ile sheria ambayo inayoeleweka, kwa

hiyo, walikuwa wakijichomeka kwenye sheria mbalimbali ambazo hazikuwa zinakidhi hivyo viwango.

Vilevile sheria hii itawaondoa wananchi kwenye mateso makubwa ya fidia ambayo imekuwa ni tatizo kubwa hasa katika sekta yetu hii ya ardhi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile itahamasisha uwekezaji, kwa sababu wawekezaji watakuwa tayari wana ile kanzi data ya ardhi ya kila eneo katika Tanzania. Kwa hiyo, anapokuja hapa, anaelewa kabisa kwamba nikitaka kuchukua shamba labda Kilombero au nikitaka kuchukua eneo labda Dar es Salaam, nitalipa kiasi gani? Ni kwamba tu kwenda kwenye Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali na atazikuta hizo kanzi data zote. Kwa hiyo, hayo ni mafanikio ya huu muswada na faida kama Waheshimiwa Wabunge tutaupitisha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na faida zote hizo, kuna vipengele vya kuweza kurekebisha. Kwa mfano, kipengele cha 28, Usajili wa Wathamini, pamoja na *section 26(2)*. Sifa alizotajwa kwenye 26(2) ni sawa kabisa lakini 28(b) inasema kwamba Mthamini awe na uzoefu au afanye kazi chini ya Mthamini aliyesajiliwa kwa muda wa miaka mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyeti wa taaluma hii na kwa upungufu wa Wathamini uliopo kwa sasa, nasema kwamba miaka mitatu ni mingi, haina sababu ya kuwa chini ya Mthamini au chini ya mafunzo ya huyo Mthamini kwa muda wa miaka mitatu. Kwa sababu mkumbuke huyu mtu tayari ana *degree* ambayo amechukua kwa miaka minne. Sasa kwa nini tena akae chini ya mtu kwa miaka mitatu apate uzoefu halafu ndiyo asajiliwe? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo, tutaweka urasimu wa kuwasajili hawa Wathamini. Mheshimiwa Waziri mwenyewe ni shahidi, kuna Wilaya nyingi sasa hivi hazina Mthamini kabisa. Kazi za Wathamini zinafanywa tu na watu wengine ambao sio wataalam wa taaluma hii kwa sababu ya upungufu uliopo. Sasa tukiweka hii asome miaka minne, akae tena chini ya mtu miaka mitatu, yaani tutaona kabisa hatutaweza kwenda haraka kwa kasi hii ya uthamini ambao unaotakiwa katika taifa letu. Kwa hiyo, napendekeza uwe mwaka mmoja badala ya miaka miwili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niende kwenye *section 52* kuhusu ukomo wa uthamini. *Section 52(2)* inasema kwamba uthamini huu wa fidia uwe miaka mitatu, lakini vilevile ukisaidiwa na *section 52(4)*, ya *amendment* inasema kwamba huo uthamini wa fidia, naomba ni-*quote*; “A person or an entity which fails to effect prompt payment of compensation shall, in addition to the principal sum, be liable to pay interest to be chargeable at the average



*percentage rate of interest offered by commercial banks on fixed deposit until such compensation is paid."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwamba miaka mitatu ni mingi sana kwa uthamini huu wa fidia, kwa sababu huu muswada unatakiwa zaidi uwasaidie au umekuja kukomboa wananchi juu ya fidia, lakini kama tutaweka miaka mitatu, tunarudi kule kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, itakuwa yaani ni kelele zile zile, tutakuwa tumebadilisha tu muziki. Kwa sababu kelele nyingi, hata Mheshimiwa Waziri mwenyewe hapa atakuwa ni shahidi kwamba kwenye ofisi yake malalamiko anayopokea kwa siku, asilimia 80 yanakuwa ni ya fidia. Sasa kama tutasema kwamba miaka mitatu halafu tu iongezeke tu hii *interest* ya *fixed deposit*, hiyo naona haitakuwa sahihi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nyumba yenyewe ukumbuke kifungu cha 53(3) inasema hivi, *once* tu *valuation* itakapofanyika huyu mtu hataruhusiwa ku-*add* chochote wala kuongeza chochote kwenye jengo lake au kwenye ardhi yake. Sasa unapoendelea kuchelewa kumlipa kwa miaka mitatu, hiyo nyumba si itakuwa imeanguka? Maana haruhusiwi kufanya *modification* yoyote, anapigwa *stop order* toka pale *valuation* inapokuwa *affected*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba badala ya miaka mitatu, iwe mwaka mmoja halafu *valuation* inaenda kwenye *yearly basis* ambao ni *financially*. Sasa kama tunai-*term financially* ya *Commercial Bank* kwa nini isiwe kwenye mwaka mmoja, iwe kwenye *fixed deposit* wanayosema ya *Commercial Bank*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niende kwenye kipengele cha muundo wa Bodi, *section 13*. Wajumbe wa Bodi wameorodheshwa pale, lakini kwenye *schedule of amendment* imesema kwamba itazingatia *gender*. Kwenye wale Wajumbe tisa na *gender* itakuwemo. Ni 13(4), naomba ninukuu: "*In appointing members of the Board under this section (1), the Minister shall consider skills, experience and gender presentation.*" Naomba kwanza itaje uwiano, kwamba wanawake watakuwa wangapi na wanaume watakuwa wangapi katika hawa Wajumbe wa Bodi, kwa maana wanawake nao wana taaluma, *experience* na huo uzoefu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napendekeza iwe ya *ratio* ya 5:4. Kwa hiyo, kama wanaume watakuwa watano, basi wanawake wawe wanne. Kwa hiyo, hata Mheshimiwa Waziri anavyowa-*appoint* hao watu ni lazima a-*consider*

hiyo *gender*. Tukiendelea tu kusema tuta-consider *gender*, kuna hatari hapa ya kuajiri wanaume, yaani ku-appoint wanaume watupu.

Kwa hiyo, lazima iseme uwiano wa *gender* inakuwaje katika hiyo *section* ya 13 ya muundo wa Bodi, ituambie kabisa. Kama huyo Mjumbe ni Mwanasheria, labda atakayetoka kwa Mwanasheria Mkuu, aseme kama atakayetoka labda kwa *Chief Valuer* atakuwa nani? Kwa hiyo, uwiano usemwe kabisa, siyo tu useme *gender*, hapana. Hiyo *gender* iwe ngapi kwa ngapi? Kwa hiyo, nilikuwa nashauri iwe 5:4. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda niende kwenye kifungu cha 49, madhumuni mbalimbali ya kufanya uthamini. Tukija kwenye kifungu cha 52(6) wanasema kwamba hizo *purpose* nyingine zilizotajwa kwenye kifungu cha 49 ni kwamba kumetajwa hapa uthamini wa *rating*, uthamini wa *capital gain*, uthamini wa bima, uthamini wa kodi ya ardhi, lakini anasema kwamba ukomo wa uthamini huo atasema Mheshimiwa Waziri kwenye kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu utajwe kwenye sheria kwa sababu tukisema kwamba atasema Waziri kwenye kanuni, leo anaweza akawa kama hivyo Mheshimiwa Lukuvi, siku nyingine atakuwa mwingine yeyote. Kwa hiyo, naomba hii sheria itaje kabisa ukomo wa *valuation*, kama ni mwaka mmoja iwe kwa *valuation* zote; ziwe za fidia, ziwe za bima, kodi ya ardhi, kodi ya majengo, zote zitajwe hapa kwenye sheria kwamba ziwe mwaka mmoja, yaani ziwe *yearly basis*; siyo ziseme kwamba itakuwa kulingana na kanuni, ziseme kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niongelee tena *section* 8(2) kuhusu uteuzi wa Wathamini Wasaidizi. Uteuzi wa hawa Wathamini Wasaidizi, naomba niungane na wenzangu kwamba uzoefu wa miaka 10 uliotajwa kwenye *section* 5(2) cha kwamba lazima awe na *master's degree*, lazima uzoefu wa miaka kumi, naona kabisa hii itanyima fursa ya hawa vijana na watu watazeeka bado hawajawa *appointed*; na kuna hatari hapa ya kuteua wazee tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa vijana hawatakuwepo, kwa maana mtu anasoma zaidi ya miaka 21 kwanza, *degree* yenyewe miaka minne, *masters* miaka mitatu, halafu tena akae tena chini ya uangalizi wa mtu ili asajiliwe, miaka mitatu, halafu tena anakuja kuwa na uzoefu, miaka kumi. Ukijumlisha toka aanze kusoma huyu mtu kwenye taaluma, mpaka aje kuwa na sifa za kuwa *appointed* kama Mthamini Msaidizi tunakuwa na miaka 21.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo ukijumlisha na ile ya kusoma ina maana tutakuwa tuna-appoint watu kuanzia miaka 55 na kuendelea. Kwa hiyo, hapa tutakuwa tunafanya tu leo Mthamini Msaidizi atateuliwa leo, baada ya miaka minne atastaafu. Atateuliwa kesho, miaka minne atastaafu, maana watakuwa wazee watupu hapa, vijana watakuwa hawapo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napendekeza iwe miaka mitano. Naungana na wenzangu waliokuwa wamechangia mwanzo kwamba miaka mitano inatoshia kabisa kwa huyu Mthamini Msaidizi kuteuliwa kama Mthamini Mkuu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Salma. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Silafu Jumbe na baadaye atafuatiwa Mheshimiwa Omary Mgumba na Mheshimiwa Richard Mbogo ajiandae.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia katika suala zima katika suala zima la Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuendelea kumwomba heri na baraka na apate wepesi Mheshimiwa Spika wetu, afya yake iendelee kuwa njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani za dhati kwa Wizara ya Ardhi, kwa Waziri mwenyewe, Naibu Waziri na Kaimu Kamishna Mkuu ambaye ni Mthamini Mkuu wa Wizara hii kwa kazi nzito waliyoifanya na kukubaliana kwamba sasa ni wakati muafaka wa sheria hii kuweza kuletwa katika Bunge hili ili kuweza kujadiliwa na hatimaye kupitishwa ili iweze kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 52 cha uhalali wa uthamini wa masuala kwa wananchi wetu ilikuwa ni kazi nzito sana na ikajenga kero miongoni wa wananchi, lakini kwa sasa kutokana na *speed* aliyonayo Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, wakifuata *speed* ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Magufuli, ni dhahiri kusema kwamba sheria hii itaweza kuwa-*push* na kuifanya kazi yao katika ukamilifu tunaouhitaji na unaotarajiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nazungumzia suala la ulipaji wa fidia. Hili suala la ulipaji wa fidia ndani ya miaka miwili na ulipaji wa ribandani ya miezi sita litaweza kutoa ufafanuzi mzuri kwa wananchi wetu na kuleta muafaka wa kuweza kuona kwamba Serikali yao ni kweli ni Serikali ya wanyonge. Hili suala la thamani; uthamini ulikuwa ukifanyika toka huko awali, ulikuwa upo, lakini walikuwa wamechanganywa pamoja na ma-*surveyor*. Sasa hivi hii sheria itakuwa ni ma-*valuer* peke yao ambao watakuwa wanaitumia kwa maana ya kuweka ufanisi na weledi katika kazi yao ya uthamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi ninachoomba na ninaamini ya kwamba katika taarifa hiyo uliyotuletea ni dhahiri kusema kwamba Wizara imekubaliana na mapendekezo ya Kamati ya kuzungumza kwamba huyu

Mthamini Mkuu awe huru. Hapa imethibitisha wazi ya kwamba ni huru kwa sababu atateua wenzie wa kumsaidia kazi kwenye eneo la kanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Sheria hii ni nzuri, ninaiomba Serikali katika kifungu cha 5 kinachuhusu kuteua Wathamini Wasaidizi, ni vyema suala hili likafanyiwa kazi na hizo sifa ni sahihi kwa sababu hao Wathamini wapo tokea awali isipokuwa Bodi ndiyo ilikuwa haipo. Sasa Bodi ya Wathamini imepatikana; na katika mchanganuo na ushirikiano uliowekwa kwa kila sekta inayotakiwa katika suala zima la uthamini, wamo katika Bodi. Kwa maana hiyo ndiyo kusema ya kwamba wale Wathamini walioko wa miaka mitano hawatakuwa wazee peke yao, watakuwa ni pamoja na vijana watakaotimiza hivyo vigezo vinavyohitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema kwamba katika kipengele hiki cha namba 5 kwa utaratibu chini ya Sheria ya Utumishi wa Umma wangepanya haraka iwezekanavyo kuwateua hawa Wathamini Wakuu Wasaidizi ili Mthamini Mkuu aweze kufanya kazi yake kwa weledi mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia suala zima katika Ibara ya 8(1) mpaka (4) ambacho kinapelekea kwamba Wathamini Wasaidizi wa Kanda watakuwepo katika Kanda. Naomba katika uteuzi wa Wathamini hawa, naomba kila Halmashauri ya nchi hii wapate Wathamini angalau wawili, watatu kwa sababu migogoro mingi ambayo imeorodheshwa na Wizara ya Ardhi, iliyopo katika orodha ya migogoro, migogoro mingi iko kwenye Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunawaomba Wathamini wawepo katika Halmashauri zetu ili wale Wathamini Wakuu Wasaidizi wa Kanda waweze kusaidiana nao katika ile migogoro inayowahusu kutatuliwa mmoja baada ya mwingine; ili migogoro ile ikianza kutatulika ni dhahiri ya kusema kwamba hii miaka miwili ya uthamini kuanzia sasa itakwenda vizuri na hatimaye tutakuwa tumefuta migogoro yote na hatutakuwa tena na migogoro mingine mipya itakayooana ama kushahibiana na ile ya zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachokiomba ni kwamba Sheria hii ya uthamini ni nzuri na kuweza kumpatia Mthamini Mkuu kuweza kuteua Wathamini Wakuu Wasaidizi na Wathamini ambao wataidhinishwa katika maeneo yetu. Hii inamaanisha ya kwamba katika kifungu cha 11(1), kinampa mamlaka ya kuweza kukasimu mamlaka yake, kinampa mamlaka kuteua. Katika kuteua mamlaka ile, anaweza akafikia kutoa agizo la jukumu lake yeye la kusaini hati. Sasa akimtafuta mtu ambaye sio wa ngazi yake itakuwa ni tofauti na sheria ambayo tumeitunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachokiomba ni kwamba wale Wathamini Wasaidizi wabakie vilevile kwa sifa zile zile za kifungu cha 5 ili waende sambamba na Mthamini Mkuu na ili atakapowakasimia madaraka ya kazi zake, ziwe zinakwenda kwa mtu muafaka anayehitajika kuifanya kazi ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza mafungu hayo matatu, napenda kusema kwamba hii sheria ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, naomba tukubaliane kwamba itatatua matatizo yaliyopo na itafuta kabisa matatizo haya kujirejea tena kwa wananchi wetu. Hivyo, naomba tuiunge mkono kwani *speed* ya Mheshimiwa Waziri na *speed* ya Mheshimiwa Rais na *speed* ya Naibu Waziri katika kutatua matatizo ya hawa wananchi nina imani kabisa ya kwamba itaweza kwisha na sisi tutakuwa tumepumua na hii sheria itatoa pumzi kwa wananchi wetu wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile itamuunga mkono Mthamini Mkuu kwa sababu sasa hivi Wizara hii ina Mthamini Kaimu; yaani Kaimu Mthamini Mkuu. Kutokana na hali hii ya sheria hii ya kumpa uhuru wa kufanya kazi hii, nina imani kabisa ya kwamba katika kifungu 52 atakitimiza kwa kazi ngumu hiyo, ataitimiza kwa weledi mkubwa na uaminifu mkubwa ili aweze kujithibitishia yeye mwenyewe kwa Mheshimiwa Rais aweze kumteua na kuwa Mthamini Mkuu wa Serikali katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa naomba Waheshimiwa Wabunge tukubaliane kabisa kwamba sheria hii imefika wakati muafaka wa kutatua matatizo ya wananchi wetu na kwa hiyo, tuiunge mkono iweze kupita tuondokane na matatizo kwa wananchi wetu, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Silafu. Tunaendelea na Mheshimiwa Omary Mgumba na baadaye tutaendelea na Mheshimiwa Hassan Suleiman na Mheshimiwa David Silinde ajiandae.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami nichangie kwenye muswada uliokuwa mbele yetu.

Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa uhai na uzima wa siku ya leo. Pia na mimi naungana na Wajumbe wenzangu wengi ambao michango mizuri iliyotolewa, kwanza nianze kwa kuunga mkono hii hoja kwa asilimia mia moja kwa sababu ni muswada ambao ni mzuri na umekuja wakati muafaka ambao utatua changamoto kubwa zilizokuwepo kwa Wathamini ambao walikuwa baadhi yao wengine ni wadanganyifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nasema ni muswada mzuri kwa sababu mpaka taasisi kwa mfano kama za kifedha zilikuwa zinakosa hata uaminifu kwa

baadhi ya wathamini wengine na ndiyo maana walikuwa wanachagua hata Wathamini maalum wa kufanya kazi zao. Sasa hii ilikuwa inakosha fursa kubwa sana kwa wananchi wetu kupata kile walichokuwa wanatarajia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, wenzangu wameshachangia mengi lakini naomba tu kwenye kile kifungu cha 52(2) na tumeona hapa kwenye *amendment* ametuletea Mheshimiwa Waziri leo; kama tunavyojua tarehe ya uthamini ni siku ile ya uthamini na ardhi mara nyingi huwa inapanda bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *valuer*, ule muda ambao *valuation* inakua kwa miaka miwili tunakubaliana ni sawa, lakini sasa inaanza kutumika mpaka pale *valuer* anapotia saini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba katika kipengele hiki tu hata huyu *Valuer* Mkuu baada ya kuthibitishwa ile, uwekwe muda maalum kuliko kuacha hivi hivi tu. Ni vizuri kupendekeza iwekwe kama miezi sita hivi, kwa sababu tukiacha hivi hivi kuna athari, wakati mwingine *valuation* inaweza ikafanyikakwa nia njema kabisa ikafika kwake na wakati huo labda hana uwezo au hana fedha ya kulipa akaucheleweshwa kwa makusudi hata miaka mitatu, minne, mitano, matokeo yake itamwathiri yule mwananchi au yule ambaye ni mnufaika wa *valuation* ile, kwa sababu anakuja kulipwa wakati ile *value* ya *land* au *the property* imeshapita muda wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri hata huyu *valuer* akawekewa muda maalum aseme kwamba, yaani ikifika mezani kwake ile *document* basi izungumze kabisa ndani ya miezi sita anatakiwa asaini, ili tusije kuondoa maana nzima ya ile *evaluation report* ambayo ilikuwepo mbele yetu. Nisema tu, ilikuwa mchango wangu leo ni huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na ahsante sana kwa kunipa nafasi. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Omary Mgumba. Tunaendelea na Mheshimiwa Hassan Suleiman, hayupo, tuendeleo na Mheshimiwa David Silinde.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa na mimi fursa ya kuchangia Muswada wa Sheria ya Uthamini na Usajili wa Thamani ya mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, nami niseme tu kwamba muswada umekuja mahali pake na ni muswada ambao utakuja kulisaidia sana



Taifa ikiwa baadhi ya mambo ambayo nitakwenda kuyazungumza vilevile yatapewa kipaumbele hususan kwenye utekelezaji wa hii sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia utathimini, maana yake tunajadili jambo linalohusu mali; thamani ya jambo fulani, hapo ndipo tunapokuwa tunajadili maana ya utathimini. Mara nyingi kwenye masuala yanayohusu utathimini hususan kwenye Taifa letu, ndilo eneo ambalo limekuwa likijenga migogoro mingi sana kwa wananchi pamoja na Serikali, hususan kwenye hii miradi ambayo tumekuwa tukiisikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka jambo la kwanza ambalo nilitaka nipate majibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, wameainisha sifa za mtu kuwa Mtathimini wa ardhi; na pamoja na kwamba wameainisha mtu anayepaswa kusajiliwa kuwa *valuer*, inaonesha kwamba sasa hivi kumekuwa na *contradiction* nyingi sana huko tunakoelekea. Kwa mfano, jibu ninalotaka ni kwamba endapo kutakuwa na ripoti mbili za watathimini wawili kuhusiana na jambo moja ripoti ipi ndiyo itachukuliwa na kufanyiwa kazi? Kwa sababu kuna haya makampuni ambayo yanafanya kazi ya kutathimini na vilevile kuna watathimini wa Serikali. Sasa kwenye mradi ukiwaleta watu wawili tofauti kwenye mradi mmoja, watakupa ripoti mbili za thamani tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa ninachotaka kufahamu kutoka kwako Mheshimiwa Waziri, endapo kutatokea *contradiction* hii kwa Watathimini wenye vigezo vinavyofanana, je, ripoti ipi ndiyo itakayotumika kwa ajili ya tathimi ya thamani ya hilo eneo? Kwa hiyo, nilitaka nilifahamu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Mheshimiwa Waziri ameeleza hapa kwamba kwenye utathimini huu wamesema hawa Watathimini wamepeva mamlaka ya kufanya tathimini kwenye mambo mengine. Sasa hivi umejua kabisa kwamba kumekuwa na tathimini, kabla hujachukua mkopo hususan kwa watu wa kawaida kule mtaani, unafanyiwa tathimini; una-*mortgage* labda nyumba, shamba ama gari. Kwa mfano, unawekeza nyumba yako kwamba nyumba yangu ni shilingi milioni 800 na unalipa deni baada ya kufanyiwa tathimini labda shilingi milioni 700 na mwisho wa siku unaposhindwa kulipa shilingi milioni 100, benki inakuja kuuza nyumba yako kwa thamani ya shilingi milioni 100 na wewe unakuwa umepoteza ilhali katika kipindi chote cha mkopo wako umejitahidi kulipa shilingi milioni 700 na umeshindwa shilingi milioni 100 tu ambayo imebaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitaka nijue hapa, Serikali na yenyewe kwenye maeneo kama haya, inawezaje kuwasaidia hawa watu ambao watakuwa wanakutana na adha kama hii ili kuondokana na kero ambazo zimekuwa zikitokea?



Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba moja ya changamoto kwenye masuala ya tathmini kwenye nchi yetu ambayo mimi nimekuwa nikayashuhudia ni kwamba sisi kama Taifa la Tanzania, kwa mfano, mtu anakuja anaomba kibali cha ujenzi, tunashindwa kupata thamani, yaani kujua thamani ya nyumba mtu anayokwenda kujenga? Ukienda kwa mfano nchi za Uarabuni pale Saudi Arabia na nchi zote za Uarabuni, pale mtu anapotaka kujenga cha kwanza unaleta ramani, unatoa thamani ya ile nyumba ambayo unataka kujenga. Labda unasema, hii nyumba yangu kabla sijapata vibali, nategemea hii nyumba kuanzia mwanzo mpaka mwisho itatumia shilingi milioni 600. Wao tayari kwenye *database* yao wanaweka ile dhamani ya mali. Kwa hiyo, mwisho wa siku ni kwamba hata ikitokea baadaye Serikali inataka kutumia eneo lile inakuwa inajua thamani ya kitu ambacho kiko eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la nchi yetu ni kwamba sisi hatuna huo utaratibu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, moja ya mapendekeo ambayo ningetaka ni kwamba sasa hivi mnapotoa vibali vya ujenzi kwa nyumba ya aina yoyote ile, jambo la kwanza watu waainishe na thamani ya nyumba anayotaka kujenga. Kwa hiyo, mnakuwa mnajua. Kwenye kutathimini ni kwamba kila hatua ya ujenzi, ramani inatakiwa ifuatiliwe, hatua ya msingi mnafuatilia mpaka nyumba inapokuwa inakamilika ama mradi husika unapokuwa unakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mkifanya hivi, maana yake sasa hata hao Watathimini wenyewe tutawapunguzia gharama. Kwa mfano, kama sasa hivi tumekuja na hii sera ya *Property Tax* ambayo inakwenda kukusanywa na TRA. Hao watu wa TRA watakuwa na urahisi wa kukusanya mapato kwa sababu watakuwa wanajua thamani ya kila nyumba ama ujenzi, ama jambo lolote ambalo limefanyika katika eneo husika. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri naye atakapokuja ajue namna gani wanaweza kuja kuliweka ili kuweza kusaidia hii tasnia ya Watathimini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba kuna ulazima sasa wa kupima ardhi nchi nzima, hili tumekuwa tukililia kila siku. Tukipima ardhi, tukapanga miji vizuri, maana yake ni kwamba migogoro hii ambayo inatokea, haitatokea tena. Leo ukiangalia Serikali inapotea fedha nyingi sana kwenye kulipa fidia. Kila mradi unaotolewa ni kwamba watu wanadai fidia kubwa na wakati mwingine inazidishwa mara tatu tofauti na thamani ya kitu ambacho kiko pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri, jambo la kwanza ni lazima tukubali kupima ardhi; ni lazima tukubali kupanga maeneo, hii itarahisisha suala la utathimini; lakini tukubali kuweka *reserve* ya maeneo ya miradi. Sasa hili sisi linatushinda. Leo watu wengi mnaweza kuwa na mifano mizuri. Ukitembea ukaenda Marekani leo, ukitembea ukaenda hata *South Africa*, nchi ya jirani kabisa hapo, utakuta wenzetu kwenye barabara, kwanza barabara ziko nane,

lakini bado wana *reserve* ya kutengeneza barabara nane nyingine. Sasa hapo unaona kabisa kwamba *vision* ya nchi ni ipi?

Kwa hiyo, sisi tunachotakiwa kukifanya sasa hivi ni kuhakikisha na hapo tunapokwenda kufanya hii miradi tuhakikishe tunatenga hayo maeneo ili kupunguza hizi gharama ambazo zinatokea. Niseme tu kwamba sasa hivi moja ya changamoto kubwa ambayo tunaipata kwa upande wa Serikali, ni kushindwa ama niseme kung'ang'ania kutumia maeneo; hao Watathimini wanatumia maeneo ambayo watu wanakaa, yaani kuna wakazi. Mfano, mdogo ni mradi wa Kinyerezi, umekwenda maeneo ambayo tayari wakazi wako pale. Sasa leo Serikali inabidi itumie gharama kuwaondoa wale watu.

Kwa mfano, kama sisi kama Serikali tungekuwa tumetenga ama tumefuata maeneo ya maporini, maeneo ambayo hayana wakazi wengi, ninaamini hii gharama ambayo tunaiingia sasa kupitia kwa hawa Watathimini Serikali isingepata na hii fedha ingetumika kwa ajili ya miradi mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashukuru sana, hayo ndiyo yalikuwa maoni yangu katika huu muswada. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Silinde. Tunaendela sasa na Mheshimiwa Atashasta Nditiye, hayupo, tuendeleo na Mheshimiwa Japhet Hasunga.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mawazo yangu machache juu ya sheria hii ambayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda niipongeze Serikali kwa kuleta muswada huu kwa wakati ambao ni muafaka. Naamini kabisa muswada huu utatupunguzia matatizo mengi sana ambayo yamekuwepo maeneo mengi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza nijikite katika maeneo machache. Eneo la kwanza ambalo ningependa kulisemea ni kuhusu huyu Msajili ambaye anatajwa katika sheria hii. Nimeona muda wa Msajili huyu ambaye ametajwa kwamba atateuliwa na atapewa miaka mitatu na baadaye anaweza akateuliwa tena kwa kipindi cha miaka mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nadhani Msajili ndio mtendaji mkuu. Kipindi cha miaka mitatu ni kipindi kifupi sana. Bodi ina miaka mitatu, Msajili miaka mitatu. Sasa mara nyingi hapa kwa sababu Msajili ndio mtendaji, panaleta mvutano kidogo. Wakati mtakapokuwa mnafanya uteuzi wa Bodi

tutajikuta hata Msajili mwingine tena atakuwa anateuliwa, kiasi kwamba mwendelezo wa ofisi utakuwa unakosekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kushauri, kama inawezekana, Msajili angekuwa anateuliwa kwa kipindi cha miaka angalau minne au mitano. Hiyo ingesaidia kwamba wakati bodi inateuliwa lakini kunakuwa na Mtendaji ambaye tayari yuko pale na ofisi inaweza sasa ikawa na mwendelezo wa kuweza kutekeleza majukumu yake. Tumeona katika Bodi nyingi, Wasajili wanakuwa na muda mrefu kidogo, wanakuwa na miaka minne au mitano, hii inasaidia sana katika kuweza kuimarisha utendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo napenda kulizungumzia ambalo linaelezwa katika sheria hii ni hili suala ambalo sheria inamtaka Msajili kuwasilisha taarifa kwa Waziri kwa miezi mitatu na Waziri baadaye ataiwasilisha hiyo taarifa katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi wangu ni kwamba taarifa ambayo atakuwa anaiwasilisha ambayo itawasilishwa na bodi hii miezi mitatu baada ya mwaka kumalizika, hiyo taarifa naamini itakuwa bado haijakaguliwa. Ili taarifa iweze kuwasilishwa hapa Bungeni ni vyema basi taarifa hiyo ikawa imekaguliwa na mtu mwingine ameiona, ameiangalia kwa undani na akaona hii taarifa sasa inafaa kabisa kuja kuwasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naona kabisa hii taarifa ya miezi mitatu itakuwa ni taarifa ambayo ni *unaudited* na hivyo haitaweza kutoa picha halisi ya utendaji wa taasisi inayohusika au wa bodi yetu inayohusika. Kwa hiyo, napendekeza kwamba kwa utaratibu mzuri kabisa, inafaa taarifa hiyo iwe ni ile ambayo itatolewa labda ni miezi sita baada ya kufunga mwaka ambapo sasa hiyo taarifa itakuwa imekaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu; taarifa hiyo itakuwa sasa ni taarifa ya mwaka mzima ambayo itakuwa na majukumu mbalimbali ambayo yametokeleza na hiyo Bodi pamoja na huyo Msajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hiyo taarifa itakuwa sasa inakidhi mahitaji yetu ambayo tunayahitaji, kuliko hivi sasa ambapo taarifa yenyewe inakuwa ni ya miezi mitatu itakuwa bado haijakamilika kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nilikuwa nataka kulizungumzia, zipo njia nyingi ambazo zinatumiwa katika kufanya uthamini. Njia hizi zinategemea na lengo hasa la uthamini ni nini. Lengo ni kupata mkopo, lengo ni kutoa fidia au lengo ni sababu gani? Zipo sababu nyingi.

Sasa nilikuwa nafikiri kwamba umefika wakati hizi njia ili kusiwe na migongano, Mthamini mmoja anaweza akaleta taarifa fulani halafu ikagongana na Mthamini mwingine, ni vyema basi tukawa tunachagua njia,

zikaelezwa katika kanuni zitakazotolewa na Mheshimiwa Waziri, tukaeleza kama ni mkopo kwamba tutatumia kigezo fulani; tutatumia njia fulani kwa ajili ya kuthaminisha. Kama ni fidia, basi lazima tuainishe kwamba ni njia hii ambayo ndiyo inafaa zaidi, hivyo hii ndiyo itakayofaa kuweza kuthaminisha mali zilizoko katika eneo fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hiyo itatusaidia katika kupunguza migongano ambayo inaweza ikajitokeza kutokana na Wathaminishaji kuwa wawili au watatu ambao wote wana sifa lakini wanatoa ripoti zinazotofautiana. Nadhani ni muhimu sana tukaziangalia hizo njia ambazo tunazitumia katika kufanya hizo *valuation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna njia nyingi zimetajwa katika hii sheria na vigezo vingi vimetajwa, kama tutazingatia labda gharama za soko, kama tutazingatia soko, yaani mali hiyo ina thamani kiasi gani, yaani *market value* au tutazingatia gharama (*cost recovery program*) au *historical cost* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa vigezo hivi viendane na sababu hasa ya kufanya uthamini. Naamini kabisa kama zikiendana na sababu ya kufanya uthamini, inaweza ikasaidia sana na inaweza ikapunguza migogoro ambayo imekuwa mingi sana katika hii sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nashukuru, naona kabisa kwamba hii sheria ni nzuri na ni sheria ambayo itaweza kukidhi mahitaji yetu, itasaidia sana kupunguza migogoro ambayo imekuwepo katika maeneo mengi sana.

Kwa hiyo, naomba itakapokuwa imepitishwa, basi Mheshimiwa Waziri mwiharakishe katika kuitangaza na kuhakikisha kwamba inaanza kutumika ili kusudi kule kwenye kanda na kwenye Halmashauri zetu ziweze kuanza kuitumia hii sheria na iweze kutatua matatizo ambayo yapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na hayo machache, ahsante sana.  
(Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

Tunaendelea na Mheshimiwa Maulid Mtulia na baadaye Mheshimiwa Daniel Mtuka, ajiandae.

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa salama kuonana na wenzangu hapa lakini pili nishukuru kwa kupata fursa hii adhimu kabisa ya kuchangia katika sheria hii muhimu sana kwa mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli sheria hii ni miongoni mwa sheria zilizokuwa zinahitajika sana katika ustawi wa Taifa letu. Hata ukisikiliza michango ya wenzangu waliotangulia wote wanaonesha umuhimu wa sheria hii. Kubwa kuliko yote wanajaribu kuonesha sehemu ambapo kuna upungufu ili yafanyiwe marekebisho hatimaye tupate sheria ambayo italeta ustawi kwa jamii yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijakwenda mbali, nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Waziri kwa hili lakini nataka nirudi nyuma zaidi. Jumatatu tulikuwa Dar-es-Salaam pale na Mheshimiwa Waziri, tulikuwa na shughuli moja kubwa sana ambayo ilimjumuisha na Mheshimiwa Rais, ilikuwa ni kuja kuzindua mpango wa kuhakikisha zilizokuwa nyumba kongwe za Magomeni zinajengwa na wananchi wale ambao walikuwa hawana mahali pa kukaa, wanakaa kwa shida, wanarudishwa katika nyumba zao zile kongwe. Kwa hili nasema nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa sababu wanufaika ni watu wa Jimbo langu moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nataka niongeze hapa kwamba wale wananchi wa Magomeni wa zilizokuwa nyumba kongwe, nyumba zao zilivunjwa kwa lengo la kuboresha zile nyumba, wajengewe nyumba nzuri na ikiwezekana Manispaa waweke miradi pale kwa ajili ya mapato. Kilichofanya nyumba zile zisijengwe hakisemwi ni kwamba baada ya kupatikana yule mwekezaji TAMISEMI hawakutoa ridhaa ya ule mradi kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa namna moja ama nyingine isije ikaonekana ni Manispaa ya Kinondoni ilikuwa haitaki wale watu wajengewe nyumba kumbe ilikuwa ni mipango kutoka TAMISEMI haijakamilika. Sasa mambo kama haya ya watu wa TAMISEMI kuzuia jambo halafu *burden* yake au hasara yake kwa Manispaa ya Kinondoni na juzi Meya wangu amesulubiwa sana kwamba alishindwa kuwatetea wananchi wale, napenda *record* ziwekwe wazi kwamba TAMISEMI ndiyo ilikuwa haijatoa idhini au ridhaa ya kuendelea kwa ule mradi, ndiyo maana wananchi wale wameshindwa kupatiwa zile nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine niseme kwamba, wakati tunawarudisha wale waliokuwa wapangaji wa nyumba kongwe walikuwa wanaishi kwa kulipa kodi tukumbuke tuna wananchi tumewavunjia nyumba zao mabondeni. Kwangu mimi hawa kama ni wapiga kura wangu vilevile naiomba Serikali na Mheshimiwa Waziri amshauri Rais kwamba nyumba zile zinazojengwa Magomeni kipaumbele cha pili baada ya wale waliokuwa wamevunjiwa nyumba zao hawajarudi kiende kwa wale wakazi wa mabondeni waliovunjiwa nyumba zao. Ikiwa tunaona huruma kwa wapangaji wetu kurudi kwenye nyumba zetu, basi kwa hisia hiyo hiyo tuwaonee huruma na wale tuliowavunjia nyumba za kwao wenyewe ili nao warudi pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika shughuli ile kwa masikitiko makubwa na Mzee wangu Lukuvi, nampenda sana baba yangu anatumielekeza, sisi vijana tunajifunza kazi kutoka kwa wakubwa, lakini kuna tukio limetokea pale sikulipenda kwa kweli. Sisi tumekwenda pale wawakilishi wa wananchi na mimi ni mwakilishi wa Kinondoni na tukio linafanyika Kinondoni, lakini Wizara ya Mzee wangu Lukuvi na uongozi uliokuwepo pale umeshindwa kutambua uwepo wa mwakilishi wa Jimbo husika, hii inatukatisha tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisafiri umbali mrefu kwenda kushiriki shughuli ile nikifahamu kiongozi wetu wa nchi atakuwepo pale na viongozi wetu watakuwepo pale. Kwa sababu mimi ni mwakilishi wa wananchi na nilivyolelewa kwenye chama changu kwamba natakiwa niheshimu uongozi, sasa inapofika wenzetu wakubwa hawa ambao tunategemea tujifunze kutoka kwao anafika Mbunge wa Jimbo husika, Mheshimiwa Lukuvi yeye ni mgeni pale, anashindwa ku-recognise kuwepo kwa Mbunge, imenisikitisha sana. Nafikiri sio namna nzuri, itatukatisha tamaa sisi kama vijana, itatukatisha tamaa sisi kama wapinzani kushirikiana na Serikali katika matukio ya Kitaifa. Kwa kweli, sikulipenda nimeona nieleze. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukirudi sasa kwenye jambo letu hili, sheria hii pamoja na uzuri wake lakini kuna mambo yanayotakiwa yafanyiwe marekebicho. Siku za nyuma kulikuwa na kawaida, mfano, hawa wathamini wanaweza wakathamini jengo au mali inayotaka kuuzwa na baada ya kuthamini TRA wanapokuwa wanataka kwenda kuchukua kodi yao nao huwa wanapeleka watu wengine kwenda kufanya tathmini. Hii ni *repetition* isiyokuwa na maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba sasa itambulike kwamba huu uthamini utakaokuwa unafanywa na hawa Wathamini wetu, ile *document* itakayotokea iwe ni *document* ya kisheria asitokee mtu mwingine tena akamtafuta mthamini wake, tafsiri yake itakuwa wale waliofanya kazi ile hawaaminiki na tutakuwa tunapoteza nguvu bila sababu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, katika huu Muswada kuna suala la Wajumbe wa Bodi, tumeambiwa kutakuwa na Wajumbe wa Bodi tisa na Kamati nne. Muswada haujieleza moja kwa moja wajumbe wa Kamati hizi nne wote watakuwa wanatoka kwenye ile Bodi ya watu tisa? Kama itakuwa ndivyo, idadi yao itakuwaje? Kila Kamati itakuwa na Wajumbe wa Bodi wawili au vipi? Kwa hiyo, naomba ufafanuzi ili tujue hawa wajumbe wa hizi Kamati nne ni walewale wa Bodi tu peke yao au wengine wanatoka wapi kwa sababu sheria haijieleza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, kuna hii *stop order*. Mara nyingi wananchi wetu wanapowekewa *stop order* wanatakiwa wasifanye

maendelezo yoyote. Hii *stop order* ni kwa muda gani kwa maana ni muda gani mwananchi anatakiwa asiendeleze? Tukisema hiyo miaka mitatu maana yake mwananchi huyu atapata athari kubwa. Kwa hiyo, mawazo yangu mimi ni bora basi ile *stop order* isizidi miaka mitatu kwa sababu mwananchi akishapewa ile haruhusiwi kufanya maendeleo yoyote. Kwa hiyo, tuipunguze irudi angalau iwe mwaka mmoja badala ya miaka mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napata tabu sana, ardhi Tanzania imekuwa mali ya Serikali au mali ya Rais. Sisi Kinondoni pale tuna eneo letu kubwa sana, Mheshimiwa Waziri amemshauri Rais walichukue, nilitegemea TAMISEMI kuwa chini ya Rais hata ile ardhi angeweza kuisimamia akiwa kulekule TAMISEMI, sasa hivi imeporwa imepelekwa Serikali Kuu, sasa hii ardhi maana yake inakuwa haina mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar-es-Salaam unapowapora ardhi Manispaa, leo Manispaa ya Kinondoni ikiamua kufanya maendeleo, ikiamua hata kubadilisha ofisi yake inabidi ikamwombe Mheshimiwa Lukuvi kuchukua ile ardhi, nafikiri hili si sawa. Ifike mahali hizi Manispaa ziachiwe ziwe na ardhi na ifike mahali hata wananchi ardhi za kwao ziwe ni za kwao. Isiwe leo mwekezaji anaenda Wizarani anachagua eneo halafu mwananchi hapewi taarifa analazimishwa tu kufanyiwa tathmini.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtulia muda wako umemalizika. Kwa vile muda unakaribia kwisha mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa ni Mheshimiwa Daniel.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami naomba nitoe mchango wangu kwenye huu Muswada ulio mbele yetu wa Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitoe furaha yangu kwa Muswada huu kwa sababu kwa muda wa miaka 22 ya taaluma yangu hii ya uthamini nimekuwa nikifanya kazi katika mazingira magumu sana. Hili ni wazo ambalo linawakilisha wathamini wote katika nchi nzima, nimekuwa nikipokea simu nyingi, wamefurahi sana, wanaomba tu jioni hii tuipitisha sheria hii ili na sisi tufanye kazi katika mazingira mazuri na tuweze kutoa mchango wetu katika Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza wenzangu ambao wametangulia wamesema karibu yote ambayo nilikuwa nafikiria lakini niguse kidogo maeneo machache.



Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, kifungu cha 28 ambacho kinazungumzia usajili kamili wa Mthamini. Naungana mkono na wenzangu kwani mapendekezo yangu na mimi ni hayohayo kwamba uwe mwaka mmoja huyu mtu au Mthamini aweze kupata usajili kamili kuwa mthamini. Ninazo sababu mbili, tatu. Hatuwezi kwenda miaka mitatu kwa sababu huyu anapokuwa mwaka wa kwanza mpaka anapomaliza kila mwisho wa mwaka anakuwa na *practical training*, anaenda *field*, tayari anaanza kupata uzoefu. Pia kutakuwa na mitihani ya usajili kama ambavyo tumeelezwa kwenye Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi kutakuwa na *continuing professional education*, mafunzo ya kuendelea ambayo Mthamini Mkuu katika majukumu yake ya kazi anatakiwa aandae na haya tumekuwa tukiyafanya miaka yote. Pia hatuwezi ku-*guarantee* huu mwaka mmoja unaweza ukaongezeka, anaweza akafanya mitihani aka-*fail*, ni jambo la kawaida kwenye taaluma nyingine zote hata wahasibu wamekuwa wakirudiarudia, CPA mtu anaweza akafanya miaka zaidi ya mitano, sita hata kwenye uthamini ni hivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anaweza asiende mwaka mmoja huu, anaweza akashindwa kwenye mitihani akarudia kwa hiyo miaka ile itaongezeka tu. Mtaani kuna vijana wengi sana tunataka wawe Wathamini kamili waweze kutoa mchango wao katika nchi hii lakini pia ni ajira. Kwa hiyo, naunga mkono usajili kamili uwe mwaka mmoja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele kingine, nimejaribu kupitia makosa ambayo sisi Wathamini tunayatenda na ambayo tunatarajia labda yatakuwa yanatendeka. *Section 67*, nimeona mengi yameorodheshwa lakini kuna kipengele naomba kama ni kuongezwa kiongezwe au kama ni ku-*rephrase* tu-*rephrase*. Kuna kitu kinaitwa kula njama kutenda kosa (*conspiracy*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye uthamini, yamekuwa ni malalamiko ya muda mrefu. Unakwenda kufanya uthamini wa fidia, mwenye nyumba na mthamini wanakula njama kwa pamoja, bwana niongezee thamani ya hii nyumba yangu badala ya shilingi milioni 10 iwe shilingi milioni 20, tutagawana hapo katikati. Hili kosa limekuwa likitendeka, nadhani tungeongeza hii *conspiracy* iwe moja ya *offence* kwenye hili eneo kujaribu kudhibiti mtindo huu kwani Serikali inapoteza pesa nyingi sana, *value* zinakuwa juu sana, tudhibiti *conspiracy*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele kingine ambacho pia naomba nikichangie ni kifungu cha 15 cha Muswada huu, uundwaji wa Kamati za Bodi. Sijajua hao wengine watatoka wapi kwenye hizi Kamati maana naona Wajumbe wa Bodi wako tisa lakini hizi Kamati ziko karibu nne au tano. Ukipiga

hesabu unakuta kila Kamati itakuwa na wajumbe wawili. Napata mashaka kama Kamati itakuwa na wajumbe wawili. Kama kuna wengine wataongezeka nadhani ni vema isemwe wazi hao wengine watatoka wapi aidha kwenye *regulations* zitakapokuwa zinatengenezwa kwenye kifungu kile cha 70. Tunataka kukimbia kule ambako tumetoka kwa watu wengine ambao siyo *professional* hii kuingilia taaluma hii. Naomba suala hili lisemwe wazi kwenye *regulations* wanatoka wapi hawa wajumbe wengine kwa sababu naona ni wajumbe wawili tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kinaitwa *approval fee*, unapokuwa umefanya kazi una-*submit* ile taarifa yako kwa Mthamini Mkuu kuna hela inalipwa Serikalini. Humu haijaoneshwa lakini najua ipo, naomba kwenye *regulations* ioneshwe na ikishaoneshwa naomba kuwe na *exemption* ya baadhi ya taasisi za Serikali ambazo zinafanya uthamini wa kazi hizi. Kwa mfano, taasisi mojawapo inayofanya *valuation* sana kwa wingi sana na inalipa *approval fee* fedha nyingi ni TAKUKURU. TAKUKURU ni chombo ambacho pia kina Wathamini ambao wanafanya *valuation* nyingi sana, kwa hiyo, kwa bajeti za kawaida kama watakuwa wanalipa *approval fee* watahondwa kufanya kazi yao na watahondwa kuwasaidia watu. Naomba ioneshwe kwenye *regulations* lakini kuwe na hiyo *exemption* ya *approval fee* kwa taasisi kama TAKUKURU. *Approval fee* ni fedha nyingi sana kwa taasisi hii kwa sababu wanafanya *valuation* nyingi sana. Nataka nishauri pia hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uteuzi wa *Assistant Chief Valuer*, naomba niungane na wenzangu kusema uzoefu wa miaka mitano unatosha. Sitaki kuzungumza mengi, wenzangu wamezungumza, hatuwezi kusema uzoefu wa miaka 10, hii hapana! Kwa uzoefu wangu ninavyofahamu kwa sababu haya ninayoyasema tumekuwa tukiyatenda sijasoma tu kwenye *document* hii, ndio maisha yangu ya *profession*. Miaka mitano ni mingi inatosha kwa *Assistant Chief Valuer*.(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho, kuna msemaji mmoja alitaka kutuchanganya kidogo, labda tu nimpe...

*(Hapa kengele ililia kuashiria  
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, muda wako umemalizika.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono sana na nawaomba Wabunge tuiptishe sheria hii ili na sisi tuwe miongoni mwa wataalam ambao wanaweza wakaisaidia nchi hii. Ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa vile muda wa wachangiaji umemalizika, sasa tunaenda moja kwa moja kwa Mheshimiwa mtoa hoja. Ataanza Mheshimiwa Naibu Waziri halafu baadaye atamalizia Mheshimiwa Waziri. Karibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru kabisa kwa kunipa fursa ya kuja kutoa mchango wangu lakini wakati huohuo kuweza pengine kujibu baadhi ya hoja ambazo wachangiaji wamezisema. Napenda tu nianze kwa kuwashukuru wachangiaji wote ambao wametoa hoja zao tukianza na Waziri mwenyewe mtoa hoja, Mwenyekiti wa Kamati na Mwakilishi wa Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote katika taarifa zao wamesema vizuri na karibu sehemu kubwa wanaunga mkono Muswada huu. Pia wachangiaji wote kila aliyesimama alikuwa anapongeza maana yake ni kwamba Muswada huu umekuja wakati muafaka ambapo pengine imekuwa ni kero ya muda mrefu, lakini sasa ndiyo muda wake wa kuweza kuitungia sheria ili wanataaluma hawa waweze kufanya kazi zao kwa weledi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kupitia hoja za Waheshimiwa Wabunge ambazo wamezitoa na zile ambazo pengine sitazizungumzia hapa basi nina imani Mheshimiwa Waziri atakuja kuzizungumzia. Msemaji wa kwanza Mheshimiwa Sabreena alizungumzia suala la uteuzi wa Mthamini Mkuu akasema usifanywe na Mheshimiwa Rais. Hata hivyo, tunasema kwamba kutokana na uzito na umuhimu wa nafasi yenyewe bado kama Serikali tunaona ni muhimu Mheshimiwa Rais aweze kuteua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo tumepanua wigo badala ya kuteua kutoka ndani ya watumishi wa umma peke yake anao pia wigo mpana wa kuweza kuangalia pia hata walioko nje ya Serikali. Kwa maana hiyo, bado kuna nafasi kama kuna Mthamini aliyebobea nje ya Serikali kwa maana ya mtumishi wa umma basi atapata fursa hiyo. Jedwali la Marekebisho limepanua wigo huo na nadhani litakuwa limeshapita huko na mtakuwa mmeliona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia akazungumzia uzoefu wa Mthamini Mkuu kuwa wa miaka 10 kuwa ni mingi sana hivyo kusababisha pengine vijana kukosa nafasi hii. Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge niseme nafasi tunayoizungumzia ni ya Mthamini Mkuu na ni nafasi moja. Sasa ukimpa muda mfupi wakati nafasi hii ni nyeti na Taifa linamtegemea zaidi katika zoezi la uthamini haitakuwa sawa. Ukipunguza miaka hii na sisi tunahitaji mtu mwenye weledi mkubwa na nafasi yenyewe ni moja, kidogo tutakuwa hatujatenda haki sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunasema kwamba kutokana na umuhimu wa nafasi yenyewe na majukumu ya Mthamini Mkuu wa Serikali jinsi yalivyo anahitaji kuwa na uzoefu wa kutosha ili kuweza kusimamia eneo hilo, uzoefu ni kigezo cha yeye kupewa nafasi hiyo. Sasa anavyosema vijana watakosa ajira au muda ni mwingi bado tunasema kwamba ile nafasi inahitaji mtu aliyebobea katika nafasi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwenye suala la usajili, kigezo cha uzoefu wa miaka mitatu Mheshimiwa Sabreena alipendekeza ipungue iwe mwaka mmoja. Ili mtu aweze kusajiliwa kuwa mthamini ni lazima awe na uzoefu wa kutosha wa kumudu majukumu yake. Sheria inayopendekezwa imepunguzwa muda kutoka miaka mitano na kuweka miaka mitatu. Tukumbuke pia tuna taaluma zingine kama za wenzetu watu wa CRB ambazo pia ni taaluma kama hii ambayo tunakwenda kuizungumzia, hizi ni *rare professional*, tunahitaji watu ambao wamefanya kazi kwa weledi chini ya watu na wamesimamiwa na wanaweza wakajisimamia wenyewe baada ya kuwa wamepata uzoefu wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tulipunguza kutoka kwenye hiyo miaka mitano na kuleta mitatu baada ya wajumbe ndani ya Kamati pia kusema kwamba huu ni muda mwingi sana. Sasa ukiupunguza ukawa mmoja maana yake pia tunakuwa hatujapata yule mtu tunayemtaka na tukumbuke kazi hii ni kazi ambayo imeleta migogoro mingi sana na bado kuna migogoro mingi kwa hiyo, hatuhitaji kufanya majaribio katika hili. Mfano, nimetoa kwa wenzetu hawa wa *engineering registration*, nao wanakwenda kwa miaka mitatu na hii ni *rare professional*. Kwa hiyo, kwa nini tunasema miaka mitatu na siyo mwaka mmoja ni kutokana na unyeti wa kazi yenyewe wanayokwenda kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Sabreena amezungumzia pia suala la kwamba wazawa hawakupewa kipaumbele au kutiliwa mkazo bali wageni ndiyo wamependekezwa. Nadhani katika pendekezo hili kifungu cha 25 kwenye huo Muswada kimetoa muda wa mtu asiye mzawa kutokana na kazi anayoifanya ambayo ni ya muda usiozidi mwaka mmoja, ana *limit* ya kufanya kazi hiyo siyo kwamba wamependelewa. Vilevile leseni anayoipata ni ya mwaka mmoja tu, baada ya hapo tena hatuko naye. Kwa hiyo, hakuna upendeleo isipokuwa tumejaribu kuweka muda wa mwaka mmoja kwa wale ambao siyo wazawa wa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameuliza Muswada wa Uthamini utakavyodhibiti hasara iliyosababishwa na wathamini. Katika kifungu cha 67 cha Muswada huu kimeorodhesha adhabu kutokana na makosa mbalimbali ya uthamini na hasara iliyofanywa kwa vitendo na mthamini. Kwa hiyo, tuna imani kama wataisoma sheria vizuri siyo rahisi kwenda kinyume na kile ambacho kimepangwa na ndiyo maana na adhabu zake ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Elias Kwandikwa yeye amezungumzia mkanganyiko uliopo katika Ibara ya 26 na 27 katika suala zima la usajili. Tunachosema hapa ni kwamba sheria hii inasomeka sambamba na sheria nyingine, hivyo lazima hizi sheria tuziangalie. Unapoangalia vigezo vilivyowekwa huyu mwingine ni mtu aliyesajiliwa lakini mwingine ni mtu ambaye bado yupo kwenye *practical* anahitaji kusajiliwa, yupo katika matazamio, kwa hiyo, huwezi kuwalinganisha katika makosa yao. Huyu mwingine yupo *full registered* na tayari ameshaanza ku-*practice*, huyu mwingine anajitangaza tu bado hajaweza kupata ile *full registration* ya kuweza kufanya kazi hizo maana yake akifanya kosa lile anapewa adhabu. Kwa hiyo, adhabu za hawa watu wawili haziwezi kulingana, lazima yule mmoja ambaye anatambua sheria inaambana namna gani akifanya kosa lazima adhabu yake iwe kubwa kuliko huyu mwingine ambaye anajitangaza kwamba yupo kati ya wale wathamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Chumi yeye amezungumzia Ibara ya 20 na 21 haisemi adhabu gani itatolewa kwa watakaokiuka maadili ya sheria iliyopendekezwa. Adhabu zote zinatokana na taaluma ya uthamini na zimeainishwa katika Ibara ya 67 kama nilivyozungumza hapo juu, kimeorodhesha adhabu zote kulingana na kosa alilofanya. Kwa hiyo, hapa hakuna mkanganyiko wowote ambao upo, hasara itakayofanyika pale lazima itakwenda sambamba na ukiukwaji wa maadili ya taaluma, ataadhibiwa kwa mujibu wa Ibara ya 67.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameomba pia Muswada uweke kifungu kitakachoweka haki ya mlalamikaji. Utaratibu wote kuhusu malalamiko dhidi ya Wathamini waliosajiliwa utainishwa katika kanuni. Ukitaka kuweka kila kitu katika sheria tungekuwa na Muswada mkubwa sana ambapo sasa inakwenda kutokea sheria ambayo imejaa mambo mengi, lakini kuna mambo mengine ambayo yataainishwa kwenye kanuni. Kwa hiyo, hayo anayoyazungumzia yatakwenda kuonekana katika kanuni zitakapokuwa zimeandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumzia pia Ibara ya 8 kuhusu Wathamini Wakuu Wasaidizi ambapo anapendekeza wawe na shahada moja na uzoefu wa miaka mitano isiwe sawa na sifa ya Mthamini Mkuu. Tukumbuke huyu Mthamini Msaidizi atakwenda kufanya kazi katika Ofisi za Kanda na tunatarajia atafanya kazi sawasawa na zile anazofanya Mthamini Mkuu aliyeko pale Wizarani. Kwa hiyo, ili aweze kufanya kazi yake vizuri na kwa uhakika ni lazima na yeye sifa zake zifanane na yule Mthamini Mkuu kwa sababu kule kwenye kanda atafanya shughuli zote za uthamini kulingana na majukumu atakayokuwa amepewa. Kwa hiyo, ukisema yeye awe na sifa za chini kidogo maana yake tutakuwa tunazishushia pia hadhi kanda zetu ambazo tumesema tuna kanda nane na kila kanda itafanya kazi zote kama ambavyo zitafanywa Wizarani. Kwa hiyo, bado sifa ya yeye kuwa sawasawa na Mthamini Mkuu tunasisitiza ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Chumi pia ameongelea suala la Ibara ya 68 Mthamini Mkuu awajibike kwa uzembe wa kitaalam utakaosababishwa. Mthamini Mkuu kwa makosa ya kitaaluma atawajibishwa na Bodi na ndiyo maana katika uundaji wa Bodi pia wao watakwenda kuweka kanuni (*rules*) ambazo zinawasimamia hawa wathamini. Kwa hiyo, yeye adhabu yake itatokana na Bodi ambayo imemsajili na katika utendaji wake wa kazi yupo chini ya Bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumzia suala la utata wa ukomo wa muda pale ambapo siku itakapoanza kufanyika maendelezo au katika muda wa miaka miwili iliyoelekezwa toka siku ya kujaza fomu na ni lini kipindi hicho kitaanza kuhesabika. Tumesema kipindi kitahesabika baada tu ya taarifa ya mthamini kuidhinishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali, hapo ndipo tunapohesabu ile miaka miwili. Baada ya hiyo miaka miwili kwisha kama bado malipo ya fidia hayajafanyika maana yake ule uthamini tena hauhesabiki, utakwenda kuanza uthamini mwingine mpya lakini kwa kuzingatia ile hali halisi iliyokuwepo kwa wakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama viwango vya malipo vitakuwa vimebadilika, basi tutachukua vile vilivyopo lakini kwa kuangalia ile hali halisi iliyokutwa wakati uthamini wa kwanza unafanyika. Hapatakuwa na zoezi la kurudi kule *site* kufanya uthamini upya isipokuwa uthamini ule ule uliofanyika mara ya kwanza ndiyo huo huo utakaorudiwa tena, lakini kwa kutumia viwango vipya ambavyo vimewekwa katika utaratibu wa bei zile za fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Chumi kaongelea pia suala la *notice* kabla ya mthamini hajaingia kwenye eneo la wananchi na nini kifanyike. Tuseme hili limezingatiwa kwenye Jedwali la Marekebisho katika Ibara ya 55(1).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Sophia Simba yeye ameongelea habari ya elimu itolewe kwa wananchi kuhusu haki zao juu ya sheria hii. Serikali inasema tumezingatia ushauri huu na utakwenda kufanyika kwa sababu kwa vyovyote vile unapokuwa na sheria mpya ni lazima pia elimu itolewe ili watu waweze kutambua. Kwa sheria hii kila mmoja nadhani atakuwa anaisubiri kwa hamu kwa sababu tayari watu wameumizwa sana, watu wamelia sana. Kwa hiyo, ushauri wake tumeuzingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwenda Ilala ili kuweza kumaliza tatizo nalo tumelizingatia tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia amezungumzia sheria zinazogusa masuala ya uthamini zihuishwe ili kuondoa masuala ya mgongano. Hili nalo tumelizingatia katika Jedwali la Marekebisho katika Ibara ya 72.



Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali yeye amezungumzia tafsiri ya *property* kwamba iongezwe baadhi ya maneno. Tafsiri inayopendekezwa haitofautiani sana na iliyopendekezwa kwenye Muswada. Hivyo Ibara ya 2 imetoa tafsiri kwamba ni mali zinazohamishika na zile zisizohamishika na aina za mali ambazo zinafanyiwa uthamini na pia inakuwa imezingatia matakwa ya tafsiri ambayo imependekezwa. Kwa hiyo, imeguswa hatuhitaji pengine kuweka ufafanuzi mwingine zaidi ya ule ambao upo kwa sababu unapozungumzia mali zinazohamishika na zisizohamishika tayari unakuwa umegusa aina nyingi ya mali ambayo ipo pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumzia pia suala la ugatuzi wa madaraka katika huduma inayotolewa na Mthamini Mkuu iwe inapatikana hadi vijijini kwenye Halmashauri. Muswada unaopendekezwa Waheshimiwa Wabunge umezingatia suala hili katika Ibara ya 10, kutakuwa na Wathamini Wateule katika kila Halmashauri. Hawa wathamini siyo kwamba watakuwa chini ya Wizara ni sawasawa na kwenye Halmashauri zetu ambapo tunao Maafisa Ardhi Wateule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo na kule kutakuwa na Mthamini Mteule kwa sababu Wathamini watakuwepo wengi, lakini lazima wawe na kiongozi wao ambaye atakuwa anawajibika pia katika kutia saina zile fomu za uthamini unapokuwa umefanyika uthamini. Kwa hiyo, hawa wapo kule kwenye Halmashauri siyo kwamba watakuwa Wizarani. Kwa hiyo, hili limezingatiwa pia katika muundo mzima ulivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 52 kuhusiana na ukomo wa miaka mitatu ni mingi. Jedwali katika Ibara ya 52 limerekebisha na tumezungumzia miaka miwili kama hapo juu nilivyozungumzia nini kinakwenda kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Richard Phillip Mbogo yeye anasema hajaona kifungu cha kukata rufaa kwa mtu ambaye hajaridhika. Sheria hii siyo kwamba itakwenda kusimama peke yake bali itakwenda kusomwa sambamba na sheria zingine na Sheria ya Ardhi imeweka utaratibu wa ukataji rufaa kwa watu ambao hawajaridhika na uthamini. Kwa hiyo, sheria hii siyo kwamba inakwenda kusimama peke yake. Katika maeneo ambayo pengine hayakutajwa hapa, basi kuna sheria ambayo inakwenda kugusa wapi mtu anaweza kwenda kukata rufaa au kulalamika pale ambapo anakuwa hajatendewa haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 57, Mheshimiwa Phillip amezungumzia habari ya kwamba inaipa Bodi mamlaka makubwa na kufanya Bodi kusema itakavyo. Kwa hiyo, yeye anashauri kanuni ya Waziri itaje adhabu ambazo Bodi itazitoe. Muswada huu umefafanua taratibu na mamlaka kati ya Bodi na Waziri, kwa hiyo, hilo litazingatiwa katika utaratibu huo.



Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumzia Ibara ya 49 anasema sababu za kufanya uthamini ziwe *standard* na zitajwe katika kanuni zitakazotolewa na Waziri. Waheshimiwa Wabunge Ibara ya 49 imetaja madhumuni mbalimbali ya uthamini yanayotambulika kitaaluma. Kwa hiyo, haya yote yameorodheshwa na yatakwenda kufanyika kulingana na sheria itakavyokuwa, hatuhitaji tena kutaja moja baada ya nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Pauline Gekul yeye amezungumzia kwamba Wakuu wa Wilaya hawakutajwa. Hili litazingatiwa katika kanuni kwa sababu hata ile ya awali walivyokuwepo walikuwa wametajwa katika kanuni, hawakutajwa katika sheria. Kwa hiyo, bado wapo watafanya kazi zao, lakini watatajwa kwenye kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akauliza kwa wananchi ambao bado hawajalipwa fidia mpaka leo sheria hii ikishapita hatma yao ni ipi? Sheria hii itaanza kutumika pale itakapokuwa imetangazwa, kwa hiyo, kwa ile migogoro mingine yote ya nyuma ambayo ipo sasa, sheria ya zamani iliyopo itaendelea au tuseme sheria zilizopo za ardhi bado zitaendelea kusimamia hilo. Kwa hiyo, hapatakuwa na hitaji lolote la kuweka pale kwa sababu kuna sheria. Kama kuna mtu pengine anaona kwamba hajatendewa haki basi itashughulikiwa kwa njia ya kimahakama, anaweza akachukua hatua ya kwenda kulalamika lakini bado anaweza akatendewa haki kwa mujibu wa utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 7(2)(a), anasema kifungu kitaje aina ya adhabu. Hii imezingatiwa katika Ibara ya 67 ambayo imeainisha adhabu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumzia ukomo wa mwaka mmoja, hii imezingatiwa katika Ibara ya 52 ambapo tumetaja miaka miwili na siyo mmoja kama ambavyo anapendekeza na nimeshaliongelea hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akauliza endapo mtu alichukua ardhi kwa ajili ya maendelezo akaamua kuiachia ardhi hiyo nini hatma yake. Tunasema basi endapo mtu alisimamishwa kuendeleza shughuli zake halafu mtu akaamua tena kusema kwamba hafanyi tena hii kazi, akaamua kuachia basi huyu mtu anayo haki pia ya kushtaki kwa maana kwamba sheria zingine zitachukua hatua. Kwa sababu ni kitu ambacho alikisema anataka kukichukua halafu kaacha kuchukua na huyu kamkwamisha katika maendelezo yake na katika shughuli zake, basi anayo haki pia ya kulalamika katika vyombo vya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezingatia yale yote aliyoyazungumza Mheshimiwa Maufi, nadhani amezungumzia Ibara ya 52 ukomo wa miaka, akazungumzia suala la Wathamini Wasaidizi kuepusha migogoro lakini kazungumzia pia suala la CV aliyepo, yeye anadhani anatosha. Basi vyombo

vinavyohusika kwa uteuzi vitakuwa vimesikia kilio chako pengine inaweza ikawa kama unavyoomba lakini tuseme *Inshallah* Mwenyezi Mungu atabariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Omary Mgumba naye kazungumzia Ibara ya 52 ambayo tayari tumeshalizingumzia. Katika suala la CV kukaa na ule uthamini, tumesema ikishafika kwa CV haitakiwi izidi siku saba na itawekwa kwenye kanuni kwa sababu ni lazima izingatiwe kwa maana kama kazi yote imeshafanyika kazi yake yeye ni kujiridhisha, hatutarajii kwamba atakaa nayo muda mrefu. Kwa hiyo, ndani ya siku saba lazima awe amemaliza na ameitoa kwenda kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Silinde ameongea mambo mengi ambayo yana ushauri pia tunashukuru lakini kwa suala la uthamini kufanywa na makampuni mawili hilo ni kosa, hakuna mahali ambapo makampuni mawili yatafanya uthamini kwa wakati mmoja halafu useme ni uthamini umefanyika, hilo ni kosa tayari. Hiyo inaweza ikafanyika pengine kuona kwamba kuna kitu hakikwenda sawa, mtu ame-*appeal* basi inateuliwa kampuni nyingine au watu wengine kwenda kufanya lakini haiwezekani wathamini kutoka makampuni mawili kufanya kazi moja halafu tulinganishe kazi zao nani kasema vipi, hilo ni kosa pia katika taaluma ambayo wanakwenda kuifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini akasema anataka kujua pia thamani ya nyumba kabla ya mambo ya uthamini kuendelea. Tukumbuke kwamba unapotaka kujenga nyumba kuna mtu anayeitwa *Quantity Surveyor* ambaye anakuwa ameshaonesha kwenye *bill of quantity*. Kwa hiyo, masuala ya *bill of quantity* yale yale ndiyo yatakayokuwa yamechukuliwa kama thamani ya kile ambacho kimejengwa pale kwa maana ya nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Japhet Hasunga yeye amezungumzia muda, tayari tumekwishalizingumzia. Pia mengi aliyoyazungumzia masuala ya Bodi kujulikana kabla na kadhalika mengine yatazingatiwa kwenye kanuni kwa sababu huwezi kuya-*mention* yote kwa wakati mmoja. Kwa hiyo, katika hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge sehemu kubwa tumezizingumzia kwa sababu karibu yote yanajirudiarudia katika maeneo yale yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Salma Mwassa kwa kuchangia na ameonesha Mheshimiwa ni mbobezi katika taaluma hiyo kama Mthamini na ali-*declare interest* na tumepokea ushauri ambao amezungumza. Pia napenda tu kumfahamisha yale aliyopendekeza tayari Jedwali la Marekebisho limeshayazingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muundo wa Bodi amesisitiza kutaja habari ya wanne kwa watano lakini hakusema sasa wanne ni wanawake au wanaume,

kasema tu nne kwa tano, kwa hiyo, inaweza ikawa wanawake watano wanaume wanne. Niseme hili ni katika zile barua za kutaka yale mashirika au zile taasisi kuleta majina yao. Kwa hiyo, Waziri anapowaandikia kuleta majina maana yake ni kwamba atakuwa ametaja pale kwamba angalau apendekezwe mwanamke lazima aseme. Unaweza ukakuta majina yaliyoletwa au yaliyopo karibu yote ni ya wanawake, tunaweza tukawa na Bodi ya wanawake watupu, tunaweza tukawa na Bodi ya mchanganyiko lakini hii pia inakwenda na sifa, lazima wawe na sifa zile zilizotajwa kwa maana lazima awe *registered* na anaweza kufanya kazi hii. Kwa hiyo, suala la *gender* litazingatiwa na linaendelea kuzingatiwa kutegemeana tu pia na *qualification* za watu ambao wapo. Hili tunalipokea na litafanyiwa kazi pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengine yalijirudia, kwa hiyo nisingependa kuyazungumzia. Suala la muda wa *valuation*, Mheshimiwa Mgumba alikuwa anapendekeza hizi *valuation* zifanyike kwa muda wa miaka miwili. Huwezi kuwa na *valuation* ya muda mrefu namna hii, lakini hapa pia tunaangalia na *scope* yenyewe ya *valuation*. Unaweza ukawa na magari yako mawili, matatu huhitaji kuwa na muda mrefu. Kwa hiyo, muda utakuwa-*determined* pia na ukubwa wa kazi yenyewe wanayokwenda kufanya. Ukiweka miaka miwili kuna mingine ambayo unakuta ndani ya siku moja imefanyika, huhitaji kuwa na muda mrefu. Kwa hiyo, hili huwezi kulipangia kwamba baada ya muda huu iwe imekwisha kwa sababu ukubwa wa kazi yenyewe pia unategemea na namna ambavyo kazi inakwenda kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Japhet Hasunga ameongelea habari ya taarifa kuletwa hapa kwamba miezi mitatu ni kidogo. Hilo tumeliona na tumepokea ushauri wako. Ni kweli kwa sababu unapomaliza mahesabu ndani ya miezi mitatu yanatakiwa yawe yamekwenda kwa Mkaguzi wa Hesabu. Mkaguzi wa Hesabu huwezi ukampangia muda kwamba ndani ya mwezi mmoja awe amemaliza vinginevyo hesabu zitakuja hapa hazijakaguliwa. Kwa hiyo, tumeliona hili na tumeangalia pia taasisi nyingine zinafanyaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa *NIMR* wana miezi sita kwa sababu tunajua kwamba ukishamaliza ndani ya miezi mitatu umepeleka kwa Mkaguzi Mkuu kule naye ana muda wake wa kufanya hesabu na siyo kwamba ana ya kwako tu na taasisi nyingine zimepeleka pale, kwa hiyo tumeweka muda wa miezi sita...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu Bungeni tafadhali tumsikilize mtoa hoja, tafadhali sana naomba mtulie.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Ndani ya miezi sita tuna imani kazi ya ukaguzi itakuwa imekwisha na Waziri atapata fursa

nzuri ya kuzileta hesabu hizo Bungeni zikiwa zimekaguliwa. Kwa hiyo, tumechukua ushauri wake Mheshimiwa Japhet Hasunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Mtuka kwa sababu yeye pia ni mwana taaluma wa uthamini, ushauri alioutoa tumeuchukua tutaufanyia kazi. Sehemu kubwa ambayo amezungumzia ni pale ambapo anasema kwamba Wajumbe wa Bodi wako tisa na zipo kama Kamati nne, sasa wakiunda Kamati zile ina maana Kamati moja inaweza ikawa na watu wawili au watatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia ile Ibara ya 13 imeongelea kama Bodi itahitaji mtu pengine kwa taaluma yake kutakuwa na wale *co-opted members* kutoka nje ambaye atakuja tu pengine kwa ajili ya kutoa uzoefu wake katika taaluma fulani. Unaweza ukawa unafanya shughuli ya mambo ya mahesabu, unahitaji pengine mtu aliyebobea, kwa hiyo, atakuja kama *co-opted member* kuweza kutoa ushauri wake pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, habari ya kuwa na Wajumbe wa Bodi tisa hilo lipo kisheria, huwezi kusema kwamba utakuwa nao wengi zaidi ili uweze kuwa na Kamati zilizo na watu wengi, kwa hiyo, wanaweza wakawa watatu. Wala siyo vibaya mtu mmoja kuwa na Kamati mbili lakini bado wata-*co-opt members* kutoka nje pale wanapoona kwamba wanahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumzia suala la *exemption* ya fee kwa taasisi za Serikali na hasa zile zinazofanya uthamini wa mara kwa mara. Kama Serikali tumelichukua hilo na nadhani litakwenda kuwekwa katika kanuni kwa sababu ni kweli kuna maeneo ambapo unapofanyika uthamini wa mara kwa mara unaweza ukakuta kwamba ile taasisi haiwezi kulipia hizo fee ambazo unaziweka lakini *nature* ya kazi yake inataka aende kwenye shughuli ya uthamini. Kwa hiyo, hili tumelichukua litazingatiwa wakati wa kuweka kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hoja zile ambazo zimetolewa nadhani karibu sehemu kubwa tumezizungumzia na sehemu kubwa pia zitaonekana kwenye Jedwali la Marekebisho ya Serikali ambalo limeletwa. Changamoto kubwa ambayo inakuwepo katika kazi hii na ambayo imesababisha Muswada huu kuwepo, tulikuwa na makanjanja wengi ambao wanajiita Wathamini lakini ni Wathamini hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke pia taasisi zetu nyingi hasa za fedha zimeibiwa sana na hawa vishoka, sasa Muswada huu unakwenda kuweka nidhamu kwa taaluma husika. Kama wanataaluma wamekuwa wakitajwa na sheria nyingine na walikuwa kwenye Bodi ile ya ma-*Quantity Surveyor* lakini ukiangalia kazi zao zinavyofanyika wanahitaji kuwa na sheria yao ya kuwasimamia, kwa sababu sehemu kubwa pia hata Serikali imeingia hasara

sana kwa watu ambao hawazingatii sheria na wakati mwingine hawana chombo kinachowabana au kinachowaongoza katika kazi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jinsi Muswada huu ulivyokuja tunaomba sana Wabunge wote walione hili na wote ni mashahidi huko tuliko watu wanavyolalamika, wanavyoonewa na wanavyolalamikia ule uthamini ni kwa sababu tu baadhi ya watu siyo wote walikuwa hawafanyi kazi zao kwa weledi. Kwa hiyo, inabidi kuwaweka katika mfumo ambao watadhibitiwa na Bodi yao, lakini watadhibitiana wenyewe kwa sababu pia wana *association* zao lakini wataheshimu ile kazi ambayo wanakwenda kuifanya. Ili waweze kufanya kazi zao kwa weledi, waweze kuheshimu taaluma yao, ni lazima kuwe na chombo ambacho kinawafuatilia na kuangalia namna ambavyo wanatekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue fursa hii pia kushukuru tena kwa mara nyingine na nikiwaomba Waheshimiwa Wabunge waone umuhimu wa kupitisha Muswada huu ili tuweze kufanya kazi katika taratibu ambazo zipo kisheria na watu wanabanwa, wanaheshimu na tupunguze pia migogoro ambayo imekuwa ikiwakwaza watu wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Waheshimiwa Wabunge, naomba ikitolewa hoja mtulizane, ongeeni taratibu angalau tusikilizane. Sasa hivi namkaribisha Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Lukuvi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo na majibu yote ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwanza nampongeza sana kwa kusimamia kwa muda mrefu sana Muswada huu na kutoa majibu ya uhakika. Nadhani hata wenzangu waliotoa hoja wataridhika kwamba amesema kitu anachokifahamu na nampongeza sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muhimu ni kwamba kama tulivyosema Wabunge wengi jambo hili halikuwepo, kila jambo lina mwanzo. Kwa hiyo, naomba niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia lakini nawapongeza sana mlioleta *amendments*, leo nafikiri tutafika saa nane maana ziko *amendments* 20 hapa lakini bahati nzuri wengi wameandika mambo yanayofananafanana muhimu ni kwamba sheria ipo na mtakubali tuanzie mahali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anazungumza kuna mwingine alichangia mwisho hakumsikia, Mheshimiwa Mtuka. Mheshimiwa Mtuka alikuwa amependekeza juu ya masuala ya makosa yaliyopo kwenye Ibara ya 67. Maoni aliyopendekeza yapo kwenye sheria nyingine za nchi, lakini mengine aliyosema yamejibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri. Ni kweli kwamba taasisi za Serikali zitakapokuwa zinafanya tathmini yake mara nyingi huwa tunatumia Wathamini wa Serikali kwa sababu tunao Wathamini kwenye Halmashauri na kwenye Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sheria hii hatuwezi kutoa *exemption* kwa sababu *exemption* ni suala la Wizara ya Fedha. Kwa hiyo, *exemption* itatolewa wakati wa tathmini ya kazi ya Serikali kwa kutumia Sheria nyingine ya Fedha siyo kwa sheria hii maana mimi siyo Waziri anayehusika na *exemptions*. *Exemption* kwa shughuli kama hizi kwa *non-profit making organisations*, kwa Serikali, itatolewa kama inavyotolewa siku zote na sheria nyingine. Kwa hiyo, tathmini za binafsi zitalipiwa na Bodi itatengeneza *fee* lakini za Serikali zitapewa *exemption* kwa mujibu wa sheria ya *exemption*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, karibu yote ambayo mmechangia yamejibiwa lakini nataka niseme moja. Nimewasikiliza sana, nataka nifanye marekebisho kidogo kwenye jambo la sifa za Wathamini Wasaidizi. Waheshimiwa Wabunge, tukipitisha Muswada huu mambo yatakuwa kama yafuatayo:-

Kule Wilayani watu wa Serikali kutakuwa na Wathamini lakini Wilaya moja inaweza kuwa na Wathamini watatu, kila Wilaya kuna mtu atapewa uteule na *Chief Valuer* anaitwa Mthamini Msaidizi Mteule ambaye ndiye atakuwa na uwezo wa kuidhinisha na *ku-sign* nyaraka zote za tathmini ndani ya Wilaya ile, atapewa ile kofia ya uthamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ardhi mnao hawa watu wanaitwa Afisa Ardhi Mteule, hata kama mna Maafisa Ardhi watano lakini ndani ya Wilaya kuna mtu anaitwa Afisa Ardhi Mteule ambaye ndiye anayeidhinisha hati na zinakwenda kwa Kamishna. Kwa hiyo, Mthamini Msaidi Mteule ndiye atakuwa muidhinishaji wa tathmini kabla hazijakwenda kwa *Chief Valuer* hata kama Wathamini wako wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa uzoefu tulionao ni kwamba tathmini za nchi nzima, ziwe za watu binafsi kutoka Kibondo au Rombo au za Serikali kutoka Rombo au Kibondo lazima zifike Dar es Salaam alipo *Chief Valuer*, ni mtu mmoja tu peke yake ndiyo anaruhusiwa kuthibitisha au kuidhinisha tathmini yoyote ya nchi nzima.

Waheshimiwa Wabunge, Muswada huu mnaotunga leo hawa Wathamini Wasaidizi watafanya kazi hiyo ili kupunguza mzigo kwa wananchi na taabu



wanayoipata na muda unaopotea kwa Serikali au wananchi kusubiri tathmini eti kwa sababu makabrasha yako kwa *Chief Valuer*. Wakati mwingine zinaweza kuja tathmini za mashamba ekari 100,000, 10,000, vitabu 100, 200, vyote vinajaa kwenye chumba cha mtu mmoja, inachukua muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini katika Muswada huu tunasisitiza uzoefu ufanane na *Chief Valuer* ni kwa sababu hawa ma-*Valuer* Wasaidizi tunawaweka kwenye kanda zile, tunayo Kanda ya Kaskazini (Moshi), Nyanda za Juu (Mbeya), tunayo Tabora na Mwanza, kule hatukuwa na hawa watu ndiyo maana *valuations* zilikuwa zinakuja Dar es Salaam, mkitupa hawa watu kwenye sheria hii tunawaweka kule kwa hiyo *valuation* ya kila kanda haitakwenda kwa *Chief Valuer*, itaishia kwa huyu wa kanda kama ilivyo kwa hati zenu. Tumefanikiwa sasa hati zote zinatolewa kwenye kanda na zinasajiliwa kwenye kanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungependa sasa hata *valuation* ripotizisije Dodoma anapohamia *Chief Valuer* ziishie kwenye kanda. Kanda ya Kasakazini *Chief Valuer* Msaidizi wa Moshi awe na uwezo sawa na yule kwa sababu ndiye atakayegonga mhuri wa mwisho na hatahojiwa na *Chief Valuer*. Ndiyo maana tunasema angalau hawa watu wawe na sifa na uzoefu unaofanana kidogo kwa sababu itafika mahali huyu atakuwa anachunga nidhamu ya hawa, wakati mwingine itafika huyu hana kazi ya kugonga muhuri kwa sababu kazi nyingi zitakuwa zinafanywa kwenye kanda. Kwa hiyo, tusiwapuuze sana hawa ni watu muhimu, ndiyo watakaofanya kazi na ninyi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninachotaka ku-*compromise* hapa, tumejadiliana sana na AG na tume-*research*, miaka mingi nchi yetu haikuwa hata na *degree* za *valuation*. Chuo cha Ardhi kimetoa *advanced diploma* kwa miaka mingi, tukilazimisha kwamba *Assistant Valuers* wawe na *masters* hatutawapata, hawapo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka nikubaliane kwa jumla na wote mnaosema angalau uzoefu uwepo lakini watu wenye shahada ya kwanza au elimu inayofanana na shahada ya kwanza wawe na sifa hiyo ya kuwa ma-*Valuer* Wasaidizi. Kwa sababu wote tunajua vyeti havifanyi kazi, hii kazi anayofanya *valuer* ni ileile katika maisha yake yote, kwa hiyo uzoefu ni muhimu kuliko cheti. Maana kila siku kukicha uzoefu na utaratibu uliowekwa kwenye kanuni na Bodi ya namna ya kufanya *valuation* ni uleule, ni kazi ya mazoea, kazi ya mazoea inahitaji uzoefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakubaliana na ninyi kwamba kwa kazi hizi *bachelor* inatoshia au elimu inayofanana na hiyo. Zamani tulikuwa na *advanced diploma* ambazo zinafanana na hizo, zimefundishwa sana na Chuo cha Ardhi na *Valuers* wengi ndiyo wanazo hizo, tukisema *masters* hapa



watasajiliwa wachache sana. Kwa hiyo, hilo nakubaliana na ninyi, tutakapofika kwenye marekebisho nimeona mtu fulani ameleta, tutafanya masahihisho juu ya suala hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwamba uzoefu ni muhimu katika kazi hii. Leo huyu mtu Halmashauri nzima kule ndani kuna *private sector* kuna Serikali, Serikali inataka kufanya *valuation* ya *property tax* kwenye majengo, kuna mambo ya *mortgage*, hata wewe tu unaweza kuwa na dhahabu yako unataka kujua thamani yake ili ujue tu una mali kiasi gani siyo kwa maana ya *mortgage* au nini, ni huyuhuyu atafanya. Ili aweze kujua namna ya kufanya tathmini ya mambo yote haya, maana ndiyo mnayemtegemea, lazima awe na uzoefu, *degree* peke yake haitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasema naweza ku-*compromise* habari ya cheti kwamba vijana hawa waliosoma *degree* ya kwanza akipata uzoefu huo anaweza kuwa na ngazi hiyo, lakini uzoefu ni muhimu kwa sababu kama mlivyoona *valuation* hii inahusu mambo mengi sana. Kwa hiyo, ndugu zangu nafikiri hapo tunaelewana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sasa kutakuwa na mnyumbuko. Mnajua Wathamini wa Wilaya wako chini ya TAMISEMI, wale wa Kanda wako chini ya Wizara lakini leo hakukuwa na mahusiano kati ya Mthamini Mkuu na Mthamini wa kwenye Wilaya. Kwa kumweka Mthamini kiungo pale au mteule maana yake umemuunganisha *Chief Valuer* na huyu *Valuer* wa Wilaya. Kwa hiyo, sheria hii imekamilika kutokana na *structure* iliyowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwassa hapa amesema tuorodheshe maeneo, si rahisi kuorodhesha yote hapa ndani, nafikiri ni rahisi zaidi tukitulia tukaorodhesha kwenye kanuni kwa sababu maeneo haya yanaongezeka, *technology* inaongezeka sasa, mahitaji ya maeneo mapya ya *valuation* yanaweza yakaongezeka, kurudi Bungeni hapa kuyaongeza kila mara kwenye sheria itakuwa ngumu. Kwa hiyo, tukubaliane tu Mheshimiwa Mwassa kwamba twende kwenye kanuni ili kuorodhesha haya mambo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi mmezungumza hapa kuhusu *Valuers* wawili katika mradi mmoja, haiwezekani! Kama *Valuer* mmoja tathmini yake inapingwa, inafutwa, anateuliwa mwinginehuwezikuajiri kampuni mbili zinafanya *valuation* ya kitu kimoja, lazima itakuwa *valuation* moja *at a time*. Kwa sababu kama kweli huyu amesajiliwa na inapita kwenye Bodi ileile, haziwezi kuwa *valuation* mbili, unataka nini? Au huyu unaikata, una-*appeal*, unatafuta mwingine hii inafutwa, kwa hiyo, *valuation* itakuwa moja tu haziwezi kuwa mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kidogo juu ya ndugu yangu Mheshimiwa Mtulia, ameunganisha hili na mambo ya Magomeni Kota. Haya mambo hayahusiani lakini basi wacha niseme tu. Kwanza kama alivyompongeza Mheshimiwa Rais nami nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa uamuzi huu wa kibinadamu na upendo wa Kitanzania kwa kuwahurumia wale maskini na kufanya uamuzi mgumu sana. Nilifikiri Mheshimiwa Mbunge wa eneo lile asingeongeza yale mengine yanayoonesha kuna kasoro, angempongeza moja kwa moja, angeishia pale pengine wananchi wake wangemwelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna kasoro katika hili, hili jambo lililofanywa na Mheshimiwa Rais ni jema na asilinganishe jambo hili na yaliyopita na asifiche. Sisi tunaojua historia pale kulikuwa na harufu ya ufisadi, halikuwa jema, wala asisingizie ya juzi, habari ya TAMISEMI kazuia, kwa nini TAMISEMI kazuia, huo uendelezaji ulitaka kufanywa na nani? Mnataka niseme hapa hao waendelezaji mliotaka kuwapa pale?

**WABUNGE FULANI:** Sema.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Tuishie tu kusema Mheshimiwa Rais amefanya uamuzi mgumu lakini wa busara, kwa upendo na kwa kuzingatia maadili aliyonayo. Jambo hili ni baya, lilikosewa na ndiyo maana amesema halifai kurudiwa tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu walipewa ahadi...

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Muulizeni Mheshimiwa Mtulia anayetetea kwamba TAMISEMI ndiyo imechelewesha.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kumwambia Mheshimiwa Mtulia jambo hili ni jema na halikuwa na makosa. Nataka wale wananchi wa Magomeni Kota waendeleo kumwomba Mheshimiwa Rais ili Mwenyezi Mungu amjalie nia njema hii ikamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni jema kabisa na wala asilinganishe na la mabondeni. Hilo la mabondeni nalijibu kabisa, nyumba hizi 644 zitakapojengwa watapewa tu wale waliovunjiwa nyumba waliokuwa wakazi wa Magomeni Kota. Watu wa mabondeni waliovunjiwa wana sababu nyingine

zaidi ya hii, nyumba hizi haziwahusu. Wale wameondoshwa kwa sababu walikuwa wanakaa kwenye maeneo hatarishi, kwa hiyo, hawatapewa nyumba hizi. Siwezi kuendelea zaidi kwa sababu Mheshimiwa ana kesi mahakamani, nafikiri aendelee na ile kesi kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa amelaumu kidogo kwamba hakutambulishwa na angefikiri kwamba mimi ningemtambulisha. Sasa wewe na mimi, wewe si ulikuwepo pale juzi, mimi si uliona nimewekwa kwenye ratiba kama mgeni ulionona mimi ni MC? Mimi nimetangazwa pale nimepewa nafasi yangu, Mheshimiwa Waziri njoo mbele, waliopewa kazi ya kutambulisha wamemaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Meya pale ametambulishwa na Mheshimiwa Rais mwenyewe na wengine wametambulishwa na mimi na nimepewa nafasi yangu moja tu ya kusema. Sasa lawama hizo rafiki yangu kutoka kule Dar es Salaam mpaka kuja Bungeni kwa kutokutambulishwa tu na Waziri na mimi nilikuwa mgeni na MC ulimwona! *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Nafikiri ungeangalia maudhui ya sherehe yenyewe. Nafikiri maudhui ya sherehe yenyewe na mafanikio ya sherehe yalikuwa makubwa zaidi kuliko kutambulishwa mtu mmoja. Kwa hiyo, mzee mimi nilikuwa mgeni kama wewe nisingeweza kuchukua jukumu la kutambulisha watu kwa sababu sikupewa kazi hiyo. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimjibu kwa sababu amesema, hata kama wengine hampendi lakini mtu anayesema lazima ajibiwe maana mimi siyo bubu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kwa kuwashukuru sana wachangiaji wote waliochangia hoja hii kuanzia Kamati yetu ya Ardhi, Msemaji wa Kambi ya Upinzani na wachangiaji wote waliochangia humu ndani wa vyama vyote pamoja na wale walioandika *amendments*. Nataka kuwahakikishia kwamba baada ya Muswada huu kupita Serikali itajitahidi kukamilisha kanuni zilizoahidiwa ili kuhakikisha kwamba sheria hii inatekelezwa kwa malengo yaliyokusudiwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Naona hoja imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, kutokana na *schedules of amendments* kuwa nyingi, namwomba Mheshimiwa Anthony Mavunde, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu aweze kutengua Kanuni ya 28(4) ili tuweze kuendelea na shughuli zetu hadi pale tutakapomaliza.

### **HOJA YA KUTENGUA KANUNI**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 153 kutengua Kanuni ya 28(4) ili Bunge hili liendelee na kazi ya kupitia Muswada mpaka kazi itakapokamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa nitawahoji kuhusu uamuzi wa kutengua Kanuni.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*  
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya Kutengua Kanuni iliridhiwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Katibu tuendelee.

**NDG. ASIA MINJA - KATIBU MEZANI:**

### **KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu tuendelee.

Ibara ya 1

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 2

Ibara ya 3

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 4

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 5

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tibaijuka.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante. Kwanza naomba kabisa wakati naleta *amendments* yangu niseme kwamba naunga mkono hoja na kuwapongeza Waziri na timu yote kwa kukamilisha kazi hii. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika azma nzima ya kuboresha Muswada huu, mapendekezo yangu ni kwamba baada ya neno ‘*President*’, utaratibu huu wa kumtafuta *Chief Valuer* ambao nimeona umekwenda vizuri na Serikali imeleta marekebisho ambayo na yenyewe yameboreshwa lakini ya kwangu nilikuwa naenda hatua kidogo kwa kuelewa undani wa jambo lenyewe, napendekeza tuongeze maneno:-

*“Upon receiving a recommendation of three candidates who fulfill conditions to be fully registered Valuers from the Minister”.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu mtu ateuliwe kama ambavyo Serikali imeleta *amendments* kutoka kwenye *profession* zote, nimemsikia Naibu Waziri ameeleza vizuri lakini kuna zaidi, kwamba, inabidi kazi hii itangazwe. Kama tunataka kuleta kweli weledi na ufanisi katika kazi hii inabidi itangazwe. Waziri ajiwekee utaratibu watangaze kazi ili watu wa ndani na wa nje ambao wana *qualifications* waombe. Pia kama ilivyo utaratibu wetu hapa, majina matatu yanateuliwa, basi Mheshimiwa Waziri ajiridhishe *a-select* majina matatu ndiyo sasa yaende kwa Mheshimiwa Rais aweze kuchagua jina moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya wakati mwingine yanatawaliwa na sheria nyingine kwa maana uteuzi wa Watendaji kama hawa huwa wanateuliwa vilevile na

Sheria nyingine ya Utumishi wa Umma. Haiwezekani kila Wizara ikajitangazia kivyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na maoni ya Mheshimiwa Profesa kwamba anatakiwa mtu mwenye uzoefu nafasi hii itangazwe lakini nafikiri tutumie utaratibu na Sheria nyingine ya Utumishi wa Umma ya namna ya kuwapata watendaji hawa. Uko utaratibu umewekwa wa namna ya kuwapata *Ma-Chief Executive* kama hawa. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tibaijuka.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimemsikia Mheshimiwa Waziri anavyosema, lakini jamani hapa tunatunga Sheria ya Uthamini, hatuwezi kujificha nyuma ya sheria nyingine ambazo hatuzijui. Sheria hii imesubiriwa katika sekta hii kwa muda mrefu na mimi mwenyewe wakati niko kwenye Wizara nilifanyia kazi hata kabla sijaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili pendekezo halipingi sheria nyingine zitasemaje, lakini linaleta *clarity* kwamba Bunge linaagiza kazi hii ifanyikeje, lakini ukivaa mwavuli wa sheria nyingine tunaondoka hapa bila kujua sasa huyu mtu anakwenda kupatikanaje. Kwa hiyo, ombi langu ni kwamba narudisha kwa Waziri aweze kupeleka *recommendations* kwa Rais lakini ameongozwa kwamba amefanya *selection* kwa *profession*, sioni ukakasi wowote, ila nasema ni muhimu. Lazima niseme kwamba kuna sheria nyingine zinatawala siyo jibu la tatizo letu. Kwa hiyo, haya ndiyo mapendekezo yangu kwa Mheshimiwa Waziri nadhani iko *straight forward* hata na AG anasikia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwa mawazo yake mazuri, lakini Ibara hii anayoizungumzia inahusiana na *qualifications* za mtu na siyo *procedure* za uteuzi. Kwa hiyo, hoja yake aliyoileta haina uhusiano na hii Ibara yenyewe. Tunaongelea *qualifications* za mtu anayestahili kushika nafasi hiyo na siyo *procedure* ya uteuzi.

**MWENYEKITI:** Sasa nitawahoji.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Hapana.

**MWENYEKITI:** Hajasema hoja yake ichangiwe jamani.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niseme sikumwelewa Naibu Waziri alivyofafanua. Hapa tunasema huyu mtu anapatikanaje, kwa hiyo kama naelewa *unless* kuna kitu kinanichenga hapa, *the Chief Valuer shall be appointed by the President*, huo ndiyo utaratibu wa kumpata huyu mtu au siyo? Kwa hiyo, siwezi kujua Mheshimiwa Naibu Waziri alikuwa anamaanisha nini alivyoniibu kama alivyojibu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini itoshe kusema kwamba tunachofanya hapa ni maslahi ya umma wala hakuna *challenge* ya mtu yeyote. Pendekezo langu, naomba basi nitoe hoja kama nashindwa kulieleza vizuri lakini siwezi kukubali twende hivi hivi kwa kujificha nyuma ya sheria nyingine ambazo siyo tunazozishughulikia sasa hivi, hatutaeleweka huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba hoja yangu ijadiliwe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge lakini mwanzo hukusema kama unatoa hoja. Umeshazungumza mara tatu kwa hiyo nitawahoji tuendelee.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 6

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 7

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Upendo Peneza.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwenye hiilbara ya 7(1), napendekeza kutoa neno '*issatisfied*' na kuweka maneno baada ya *Valuer*, '*in his own opinion or upon receiving a complaint in a prescribed form*' na napendekeza sasa kiweze kusomeka:-

*"Where the Chief Valuer in his own opinion or upon receiving a complaint in a prescribed form that the valuation was not properly conducted he may..."*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Peneza naomba urudie hawajakuelewa vizuri.



**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katikalbara ya 7(1) baada ya neno *Chief Valuer* kuna neno *'is satisfied'*, napendekeza neno *'is satisfied'* litolewe na badala yake baada ya neno *Valuer* yaje maneno, *'in his own opinion or upon receiving a complaint in a prescribed form* halafu mabadiliko yasomeke:-

*"Where the Chief Valuer in his own opinion or upon receiving a complaint in a prescribed form that the valuation was not properly conducted he may-*

*(a) Disapprove the valuation report..."*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yake ni nzuri na Serikali inaipokea lakini hii inaweza ikawekwa kwenye kanuni na siyo lazima iingie kwenye sheria. Itawekwa kwenye kanuni kwa sababu ni hoja ya msingi ambayo ameizungumza kwa hiyo siyo lazima iingie humu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Upendo Peneza.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni ya msingi napenda ionekane hapa ili iweze kutoa huo mwongozo ambao nimeutoa ili iweze pia kuwasaidia ufanyaji wa kazi. Kwa sababu kama tunategemea *Chief Valuer* ataweza kuifutilia mbali ripotina vitu kama hivyo, basi ingekuwa ni vizuri kukawa na utaratibu kama hizo *form* kujazwa. Naomba kama nilivyopendekeza kwenye hizi *amendments* basi iwe hivyo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali hoja yake ni ya msingi na hata kama itaachwa kwa maana kwamba hatutaihusisha kwenye sheria haitakuwa na madhara lakini bado kwenye kanuni itaingizwa na itafanyiwa kazi siyo lazima uiweke huku. Hoja yake ni ya msingi lakini haina madhara hata kama haitabadilika kama anavyopendekeza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Peneza.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara imetambua umuhimu, naomba hii kitu iweze kuingizwa lakini kama bado kuna

kusuasua basi naomba Waheshimiwa Wabunge waweze kuniunga mkono ili waweze kujadili suala hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Peneza hakuna ambaye anaunga mkono hoja yako. Mheshimiwa Naibu Waziri ametoa maelezo kwamba itaingia kwenye kanuni.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutekeleza hilo analolisema kwamba kuwe na *form* maalum ndiyo maana tunasema tutakwenda kwenye kanuni ili angalau hata hizo *form* anazopendekeza hapa ambazo mtu anaweza akazijaza kulalamikia ni lazima zionyeshwe ni aina gani ya hiyo *form*. Kwa hiyo, ndiyo maana tunasema hii tumekubali lakini tutaenda kuifafanua vizuri zaidi kwenye kanuni.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Antony Komu.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Katika msingi huu huu wa kuboresha sheria hii ambayo kwa kweli ni muhimu hasa wakati huu ambapo nchi yetu inakwenda kwenye uchumi wa soko huria, naomba baada ya ile *clause 7(2)(b)* tuongeze kifungu (3) ambacho kitakuwa na maneno:-

*“Notwithstanding the provisions of subsection (1) paragraph (a) of section 7, any person aggrieved by the decision of the Chief Valuer may appeal to the Board”.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu ukiangalia kuanzia ile *clause 7(1)(2)(a)* na (b) utaona kwamba *Chief Valuer* anaweza aka-*disapprove* taarifa na baada ya kuikataa taarifa hiyo hatua zingine zozote zinazofuata anazichukua yeye mwenyewe. Jambo hili si la afya sana kwa sababu inawezekana kukawepo na *conflict of interest* kwa sababu huyu ndiyo Mshauri Mkuu wa Serikali kwenye mambo yote yanayohusiana na uthamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ninayopendekeza yatasaidia kuleta ushirikishi zaidi wa wadau wengine. Pendekezo hili linaweza kuiepusha sana Serikali na kesi ambazo siyo za lazima kwa kutoa fursa kama nitakavyokuja kupendekeza tena huku mbele ya kuwepo na chombo kingine ambacho kinaweza kikawa na jicho la pili kwenye jambo ambalo *Chief Valuer* hakuridhika kwa namna moja ama nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu ili twende mbele.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati natoa majibu ya baadhi ya hoja za Wajumbe nilizungumzia suala hili ikiwa ni pamoja na hili analolizungumzia Mheshimiwa Mbunge. Pamoja na hayo kifungu hiki bado hakitoi fursa ya rufaa kwa mtu asiyeridhika, yeye ana haki ya kwenda Mahakamani kwa njia ile ya mapitio yaani kuomba ile *judicial review* ili aweze kwenda ku-*appeal* zaidi. Kwa sababu Bodi inahusika na usajili na usimamizi wa Wathamini na taaluma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, masuala mengine ambayo yapo. haki ya kwenda kukata rufaa katika vyombo vingine ipo. Tunachoweza kufanya kingine pengine ni kupendekeza tu kifungu hiki cha rufaa kwenda kwa Waziri kwa sababu bado anayo fursa nyingine ya kuweza kufanya mapitio ya kosa lile ambalo linazungumziwa kwa sababu hajaridhika likaenda Mahakamani lakini siyo kuweka kwenye hii kifungu hapa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Antony Komu.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema kabisa kwamba nia yangu ni njema sana na naiomba Serikali na Waheshimiwa Wabunge walione hili kwamba tunataka kuiepusha Serikali yetu na kesi zisizokuwa za lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Waziri alivyokuwa anatoa hoja alisema kwenye ukurasa wa 41, *objects and reasons* za kuleta huu Muswada sasa hivi, ni kwamba kumekuwa hakuna sheria moja ambayo ni *comprehensive* inayoweza kushughulikia masuala yote yanayohusiana na masuala ya uthamini. Sasa huu ni wakati muafaka wa kuwa na kitu ambacho ni *self*, maana haya maneno yanasema, *lack of one comprehensive and self-contained legislation covering the valuation practices in the country has culminated into serious challenges within the societies.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunataka kuondokana na changamoto ya namna hiyo kwa kuwa na *a comprehensive legislation* ambapo tukiwa na kifungu hiki hapa ni kwamba mambo hayo yote yanaanzia kwenye Wizara na yanaishia hapo hapo bila kuingiza Serikali kwenye migogoro ambayo siyo ya lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi zaidi na kama hawatatoa ufafanuzi unaofaa basi nitaomba Bunge zima lisaidie katika kutatua jambo hili kwa kulijadili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwelewa sana Mheshimiwa Komu, lakini ukisoma kifungu hiki hayo anayoyasema tayari yameshafanyika. Kifungu kinasema:-

*“Iwapo, baada ya uhakiki wa uthamini chini ya kifungu kidogo cha (1), Mthamini Mkuu ameridhika kwamba uthamini haukuzingatia miongozo ya uthamini, Mthamini Mkuu anaweza-*

*(a) Kupendekeza kwa mamlaka husika ya nidhamu, hatua zinazopaswa kuchukuliwa dhidi ya Mthamini aliyesajiliwa”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake tayari imeshakwenda Bodi. Mthamini Mkuu (*Chief Valuer*) tayari ameshapeleka kule. Kwa hiyo, kuna nidhamu hapa, inaweza kuwa kwa mwajiri au kwa Bodi kutokana na usajili maana hii Bodi inasimamia usajili wa hawa wanataaluma lakini kwa sababu hakuridhika, kazi hiyo anaagiza irudiwe na Mthamini mwingine aliyesajiliwa. Kwa hiyo, keshampa haki yule mtu ambaye ameonewa, kazi imeshakwisha. Baada ya hapo hatuwezi kuzuia watu kwenda Mahakamani maana hata ukimwambia huyu mtu binafsi aende Bodi, Mthamini tayari keshaipelekea Bodi ile hoja yake na bado anaruhusiwa kwenda Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri ukisoma vizuri hapa kazi hii ambayo imevurugwa tayari hawa watu waliovurugwa Mthamini Mkuu ameshawapeleka kwenye Bodi hiyo ambayo Mheshimiwa Komu anataka wapelekwe. Sema tu sasa upelekaji wenyewe kwamba yeye anataka yule mtu mwenye tathmini yake apeleke lakini *Chief Valuer* ndiye aliyegundua udhaifu huu, kwa hiyo, ameamua huyu mhusika achukuliwe hatua. Kwa hiyo, nafikiri kifungu hiki kinajitosheleza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Komu umeridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri?

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika na majibu kwa sababu Waziri...

**MWENYEKITI:** Basi kama hujaridhika usichangie tuone nani watajadili suala hilo, Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Dkt. Ndugulile.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULIE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata fursa ya kuchangia katika hoja ya Mheshimiwa Komu. Hoja ya Mheshimiwa Komu ina mantiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachoongelewa hapa katika kipengele hiki ni pale Mthamini Mkuu wa Serikali anapoona kwamba ile *valuation* ina kasoro

lakini tuangalie vilevile upande mwingine wa shilingi pale yule ambaye amethaminiwa naye ana malalamiko yake, hajaridhika na ule uthamini aliofanyiwa, je, yeye anafuata taratibu gani kupata haki yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie na upande mwingine wa shilingi pale yule mthaminiwa anapoi-*query* au anapokuwa anapata wasiwasi na anapingana au hauamini ule uthamini uliofanyiwa, *remedy* yake inakuwa ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kile kifungu ambacho Mheshimiwa Komu amekisema naona bado kina mantiki kwamba kipokelewe na kiingizwe kama ni sehemu ya sheria hii. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naungana na Mheshimiwa Komu na Mheshimiwa Dkt. Ndugulile. Kwanza, ni muhimu Waziri aelewe Mheshimiwa Komu anachozungumzia hapa ni mamlaka ya rufaa hazungumzii Kamati ya Nidhamu yaani ni vitu viwili tofauti. Kamati za Nidhamu zimeundwa kifungu cha 15 na ziko Kamati tano mbalimbali za kuisaidia Bodi na kila Kamati ina majukumu yake, tusichanganye haya mambo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu Serikali ikaelewa kwamba kwa kutunga sheria hii hatutaki tena tuanzishe urasimu wa Mahakama. Ninyi mnafahamu kwamba kwanza kuomba *judicial review* ni mchakato mrefu na una usumbufu wa hali ya juu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, ukiangalia majukumu ya Bodi kama yalivyoainishwa kwenye kifungu cha 14(g),(h),(m) na (n) utaona kwamba aina ya kazi wanazozifanya zitaruhusu kabisa mapendekezo ambayo Mheshimiwa Komu ameyatoa. Kwa hiyo, nadhani ni muhimu Serikali iangalie nia njema hii na tuweze kutafuta chombo kingine cha rufaa, tusiache mtu mmoja awaumize watu na mamlaka nyingine ni kwenda kuelekeza chombo ama kitoe adhabu ama kumpa mtu mwingine, sasa unakuta kwamba haki ya mtu kusikilizwa haijapatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani ni muhimu Waziri aliangalie vizuri, asiangalie haraka haraka ni hoja nzuri tu ambayo anaweza akaichukua na ikasaidia. Kwa sababu tumeitunga hii sheria inakuwa kama ni sheria mama ya masuala ya *valuation*, kwa hiyo, tunataka vitu vingi kwa kadri inavyowezekana viweze kuwa *sorted out* huku. Ndiyo maana hoja ya Mheshimiwa Profesa Mama Tibaijuka mmeamua kuichinjia baharini lakini ilikuwa ni hoja ya msingi sana ili hiki kitu kimoja kiweze kushibisha na kuwa na nyama mbalimbali ili hata ufanisi wake katika utekelezaji uwe mzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba hoja ya Mheshimiwa Komu waichukue kwa sababu ina mantiki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua umuhimu wa michango ya Waheshimiwa Wabunge, lakini hapa tunatunga sheria na naomba Waheshimiwa tuzingatie mambo haya yafuatayo:-

Moja, ile hoja aliyoisema Mheshimiwa Dkt. Ndugulile kwa mtu ambaye hakuridhika na uthamini uliofanywa yaani aliyekuwa anathaminiwa, Ibara ya 14(g) kama alivyosema Mheshimiwa Mdee inamhusu, ataenda kulalamika. Kwa sababu hiyo, hoja ya Mheshimiwa Dkt. Ndugulile haiwezi kuwa ya msingi ku-*justify* hili pendekezo la Mheshimiwa Komu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja niwashauri Waheshimiwa Wabunge, ni mamlaka gani unayompa *Chief Valuer* kama anashindwa hata kupendekeza kwamba amenipa kazi mimi *valuer*, nimekiuka zile taratibu za *valuation* halafu ashindwe hata kushauri tu kwamba bwana eeh sasa napendekeza mamlaka ya nidhamu imchukulie hatua? Anaweza akawa ni mwajiriwa Serikalini na mamlaka ya nidhamu yenyewe ndiyo hiyo Bodi, kama akimpeleka kwenye Bodi si huko huko atajitetea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwashawishi tu, hiyo mnayopendekeza ndiyo inayoleta urasimu kwa sababu hatimaye itamfanya huyo ashindwe kutekeleza wajibu wake ambao leo tunakusudia kumpatia huyu Mheshimiwa anapotekeleza majukumu yake. Kwa hiyo, hoja hizo za rufaa nazifahamu lakini hapa tunatunga sheria. Sasa unamwambia kwamba kama amekuta amelipua kazi unasema aah, aah asimpe mtu mwingine, unamwanzishia sheria halafu hana mamlaka lakini kama akipeleka kwenye Bodi atajitetea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwanza Waheshimiwa wengi wameunga mkono sheria hii na wamesema imekuja kwa wakati muafaka. Sasa tunapoitunga pia tumpe fursa huyu bwana aitekeleze kuleta nidhamu katika masuala ya *valuation*, ndiyo ushauri wangu. Kwa hiyo, napendekeza Wabunge wakubali mapendekezo ya Serikali kama ilivyo kwenye Muswada.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Komu hitimisha hoja yako.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mkanganyiko hapa, mimi nachozungumzia ni mamlaka ya rufaa. Hali ilivyo sasa hivi kama mtu atakuwa hakuridhika na uamuzi wa *Chief Valuer* atafanya nini kwa sababu yaliyoko kwenye Bodi ni *normal functions* za Bodi. Je, mtu aliyefanyiwa uthamini

au aliyefanya uthamini anafanya nini? Ni lazima aende Mahakamani kama Serikali inavyotaka kitu ambacho tunasema siyo afya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Bunge liamue kwa sababu lengo hapa ni kuboresha na kupata kitu kizuri ambacho kitatupeleka kwa spidi hii ambayo wote tunaitamani. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Unataka kuongeza Mheshimiwa Waziri?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naongeza hili la Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, Mheshimiwa Halima Mdee ameisoma hapa 14(g), kazi ya Bodi hii ni pamoja na kupokea hayo malalamiko Mheshimiwa Komu. Bodi hii itapokea na kushughulikia malalamiko yanayowasilishwa, au kwa sababu tu haikusema rufaa? Inasema Bodi itapokea malalamiko yanayowasilishwa na Wathamini waliosajiliwa mmoja mmoja. Anaweza kuwa haridhiki tu na uamuzi au jambo lolote ambalo ametendewa na mkubwa wake *Chief Valuer* lakini itapokea malalamiko ya Wathamini waliosajiliwa, Mthamini Mkuu naye anaweza kulalamika kwa Bodi au mtu mwingine yeyote. Labda msembe huyo mtu mwingine yeyote na utaratibu tukafafanue kwenye kanuni, lakini mtu mwingine yeyote ana fursa ya kulalamika pale ambapo hakutendewa haki, *unless* mnasema neno hili halifanani na neno linaloitwa rufaa lakini rufaa ni malalamiko tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri hii imekaa vizuri na kwenye kanuni tutakwenda kufafanua vifungu vingi zaidi ambavyo havina maelezo ya kutosha.

**MWENYEKITI:** Haya, nitawahoji kuhusu hoja ya Mheshimiwa Komu.

*(Hoja ilitolewa iamulie)  
(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 8

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lwakatare.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli niliwasilisha *schedule of amendment* katika Ibara hii. Nimshukuru sana Waziri amefafanua kwa kiasi cha kutosha na kwa kweli ame-*accommodate* hilo jambo ambalo nilikuwa nimeli-move. Kwa hiyo, sina sababu ya kuchelewesha kikao hiki, naomba tuendeleo. Ahsante. (Makofi)



(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 9

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Peneza.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika Ibara hii ya 9 ningependa pia kuongeza kifungu kidogo cha (3) ili viweze kuwa vitatu hapa. Katika kifungu kidogo cha (1), naomba nikisome:-

*“There shall be Government Valuers who shall be appointed or employed in accordance with the Public Service Act, and who shall undertake valuation functions in the public sectors”.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hiki kimezungumzia mambo ya *valuation* ndani ya *public sectors*. Napendekeza tuwe na kifungu kidogo cha (3) katika hii Ibara ya 9 ambacho kitasomeka:-

*“Without prejudice to subclause 9(1), the Government valuer may also conduct valuation in private sector upon request by the private individual or entity”.* (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tutafafanua hivyo kwa sababu ndiyo *practice*.

**MBUNGE FULANI:**Sawa.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Huko Wilayani yupo *Valuer* mmoja tu Halmashauri, anafanya zote. Kwa hiyo, huyo *Government Valuer* anaweza kufanya na ya *private* maana anakuja kufanya tathmini hata nyumba yangu binafsi kwa ajili ya *property tax*, lakini hata mauziano ya watu binafsi anafanya isipokuwa tu wale watu binafsi wanapofanya watalipa, ya Serikali inakuwa *exempted* kwa Sheria ya Fedha. Kwa hiyo, tutafafanua hivyo. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Peneza umeridhika?

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nimemwelewa vizuri ni kwamba amekubali hiki kifungu kiingie, ni sawa?

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Okay,ahsante. (Makofi)

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 10

Ibara ya 11

Ibara ya 12

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 13

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya Serikali yame-capture nilichokitaka. Kwa hiyo, nakubaliana na mabadiliko ya Serikali.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 14

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Antony Komu.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 14, naomba kile ambacho Serikali imesema kizingatiwe sasa kwa sababu nilikuwa nimependekeza kwamba tuongeze kifungu cha (p) ambacho kitasema:-

*“Consider appeals from the decisions of the Chief Valuer”.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tunataka kuwe na uwazi na hiyo *function* ya kuzingatia *appeals* ambazo zinatokana na uamuzi wa Mthamini Mkuu wa Serikali basi hii *provision* iwepo pale. Kwa sababu kwenye ile Ibara ya 7 ukiangalia mchakato ulivyo pale ni kwamba *Chief Valuer* anakataa taarifa, akishakataa taarifa anachukua hatua mpaka hata za kuteua mtu mwingine wa kufanya hiyo kazi ambayo ilishafanywa na mtu mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kufika mahali ambapo umeshatoa taarifa maana yake ni kwamba umeshaingia gharama, umeshakamilisha kila kitu, umeshakamilisha kazi na ndiyo maana una-*submit report* ambayo ikiwa

*disapproved* huna mahali pengine popote pa kwenda kulingana na ile Ibara ya 7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sasa hiyo nia ambayo Serikali imeonesha kwamba ingeenda kufanya kwenye kanuni basi iwe wazi hapa kwa kuwepo na (p) kinachosema kuwepo na *consideration* ya *appeals* kutokana na maamuzi ya Serikali. Naomba majibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Possi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, worry yetu hapa ni kwamba hii inaweza ikaleta *confusion*. Mheshimiwa Komu anasema kwamba bodi pamoja na mambo mengine *will consider appeal from the decision of the Chief Valuer*. Bodi itasikiliza rufaa kwa tafsiri ya haraka haraka kutokana na maamuzi ya *Chief Valuer* lakini sasa, moja ya maamuzi ya *Chief Valuer* katika kifungu cha saba, ni kupendekeza *to the relevant disciplinary authority on measures to be taken against such registered*. Kwamba yawezekana pia moja ya hayo maamuzi ya *Chief Valuer* ni kupeleka suala kwa bodi halafu wewe hujaridhika na maamuzi ya *Chief Valuer* kupeleka maamuzi kwa bodi halafu una-*appeal* kwa bodi hiyo hiyo. Inaleta *confusion*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Komu.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kama tunafanya ligi ambayo haina sababu. Kwa sababu kama hiyo bodi inaweza ikasikiliza malalamiko sasa ni kwa nini tunakataa malalamiko haya, huyo *Chief Valuer* ambaye na yeye anaruhusiwa kwenda kulalamika kwenye bodi, asilalamikiwe na mtu mwingine kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba labda nashindwa kujieleza vizuri, sasa niombe Wabunge wengine waniunge mkono kwenye hili kwa sababu naona kama tunataka kuminya haki za watu kwa kumlinda mtu mmoja ambaye kwa kweli katika hali ya kawaida kabisa anaweza kuwa *mislead* na taarifa labda alizonazo na vitu kama hivyo. Kwa hiyo, naomba iungwe mkono Wabunge wajiadili ili tuweze kuwa na muafaka mzuri zaidi.

**MWENYEKITI:** Haya wangapi wanakubaliana na kutaka kujadili, wawili na hapa; mwingine nani, Mheshimiwa Sabreena na Mheshimiwa Gekul. Wawili wanatosha kwanza hao, Mheshimiwa Sabreena tunaanza.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kama tulivyosema hapa kwamba mthamini mkuu ndiye anayelalamikiwa na kwa maana hiyo basi *appellate jurisdiction* yake iwe ni bodi. Sasa mthamini yeye

ndio analalamikiwa, kwa nini malalamiko haya sasa mtu hajaridhika na uthamini wake asiruhusiwe kwenda kwenye bodi ku-*appeal* ili sasa bodi iweze kuangalia Mthamini Mkuu wa Serikali alikosea wapi, kuliko kwamba yeye ndiye amelalamikiwa, halafu yeye ndio achukue malalamiko hayo ayapeleke tena kwenye bodi. Hapo kutakuwa hakuna *transparency*, lazima mtu ambaye ameonewa yeye ndio aka-*appeal* badala ya Mthamini Mkuu ambaye ndiye aliyelalamikiwa aka-*appeal* kwa niaba. Kwa hiyo, kifungu hiki ni kizuri, ni vyema tu Serikali ikaridhia ili tuweze kuendelea na vifungu vingine. Nashukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mhe. Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, hoja ya Mheshimiwa Komu ina mashiko kwa sababu zifuatazo:-

Huyu *Chief Valuer* anapeleka au anashauri, anapendekeza kwenye bodi adhabu ambazo zinaweza zikachukuliwa dhidi ya huyu Mthamini ambaye kazi yake haijaenda vizuri. Sasa Mheshimiwa Komu anachopendekeza ni kwamba nafasi hii ya bodi isitumike tu na *Chief Valuer* lakini pia yule mtu ambaye kazi yake haijapitishwa au *Chief Valuer* hajaridhika, apate nafasi ya ku-*table* kwamba nilichopeleka kwa *Chief Valuer* ni hiki lakini adhabu ambayo inapendekezwa dhidi yangu ni hii. Kwa hiyo, bodi izingatie yale ambayo mimi nimeyafanya. Kwa hiyo, tusitoe nafasi kama nia njema, tusitoe nafasi kwa *Chief Valuer* kusikilizwa kwenye bodi wakati yule ambaye ameathirika hapati nafasi. Kwa hiyo, niombe na niungane na Mheshimiwa Komu kwamba mapendekezo yake yazingatiwe kwa ku-*provide a fair play game* isiwe upande mmoja, iwe pande zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wangekubali tangu mwanzo alivyokuwa amependekeza maana yake hiki wala tusingerudia. Kwa hiyo, athari ya kukataa tangu mwanzo ndiyo hii. Ni vizuri tukawa *fair* pande zote badala ya kupendelea upande mmoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tuangalie utaratibu wa uandishi wa sheria, huwezi kuwa na rufaa kwenye mamlaka mbili kwa wakati mmoja. Kwenye sheria hii mkisoma Waheshimiwa Wabunge ile Ibara ya 33 rufaa zinaenda kwa Waziri kutoka kwenye bodi. Kwa hiyo sasa, huwezi kuwa na rufaa maana rufaa inatoka huku inaenda huku, lakini huyu mtu ambaye ni mthamini aliyesajiliwa hakukosa fursa yeye atalalamika ndio msingi Waheshimiwa Wabunge wa kifungu cha 14(1)(g) kimeorodheshwa pale na naomba nikisome na Mheshimiwa Waziri alizungumza hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu mtu atakapolalamika si atakuwa analalamikia maamuzi mabovu ya huyu *Chief Valuer* ambaye haridhiki naye na hatima yake, ile bodi itafanya maamuzi kwamba anakata rufaa au ni malalamiko ya kawaida. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge hili tulifikirie tu, hajakataliwa kabisa, lakini nisome kwa Kiswahili kifungu hiki kinavyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinasema hivi: Kazi za Bodi ni zifuatazo (g) kupokea na kushughulikia malalamiko yaliyowasilishwa na Wathamini waliosajiliwa ambayo huyo sasa amefanya kazi hovy hovy, Mthamini Mkuu anasema anapendekeza labda kwenye jina lake kwenye mamlaka ya mtu mwingine au ya nidhamu au anasema hii kazi nimpatie mtu mwingine, halafu Wathamini waliosajiliwa, Mthamini Mkuu au mtu mwingine yeyote. Kwa hiyo, kila mtu hapa amepewa fursa. Waheshimiwa Wabunge naomba sana mliangalie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu matumizi ya neno rufaa, ninyi ndio mnawakilisha wananchi kule mnajua. Neno rufaa lenyewe linaogopesha, mtu anaanza kufikiria hapa sijui nitaweka kwa mwanasheria, nawaambie tu, lakini cha msingi hapa ni kwamba *whether* unatumia jina malalamiko au unatumia jina rufaa, *the board consider this complaintor that particular* rufaa na kufanya maamuzi ya haki. Kwa hiyo, wote hawa wana haki hapa, Mthamini Mkuu ana haki, Msajili aliyesajiliwa, Mthamini aliyesajili na mwananchi yeyote yule kama ni yule ambaye alikuwa anathaminiwa, wote wana haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba tuendelee kutumia neno malalamiko, huyu aliyeathirika alalamike kwenye bodi na mamlaka yale, lakini sasa kama ilivyo kwenye Ibara ya 33, rufaa inatoka kwenye bodi, ambaye haridhiki na maamuzi ya bodi ndio anakwenda kwa Mheshimiwa Waziri, ni utaratibu tu Waheshimiwa Wabunge wa namna ya kuandika hizi sheria vizuri. Cha msingi hapa ni kwamba hakuna ambaye amekosa hiyo fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwashauri Waheshimiwa Wabunge najua haya mapendekezo mnaleta kwa nia njema kabisa, lakini sheria jinsi ilivyo kwa maana ya Muswada huu, pia mapendekezo ya Serikali yamezingatia fursa ya kila mtu, hakuna ambaye ananyimwa hiyo fursa. Kwa hiyo, naomba tukubaliane na mapendekezo yaliyopo kwenye Muswada kama yalivyoletwa na Serikali Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri huna la kuongeza. Mheshimiwa Komu umeridhika?

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kwelikweli, kwa sababu...

**MWENYEKITI:** Hujaridhika au umeridhika?

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Sijaridhika.

**MWENYEKITI:** Haya basi naomba nilihoji Bunge. Hoja imekataliwa.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 15

Ibara ya 16

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 17

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika kifungu hiki wasiwasi wangu ni ule ambao anausema Mheshimiwa Komu kwamba hapa ni lazima tuone kwamba mtu anaweza aka-*appeal* kwa sababu tuko katika hatari ya kuweka watu ambao wanaweza wakageuka Miungu watu, wakawatesa watu wanaotafuta huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili wala halina ubaya, nataka niamini kwamba hii Miswada inaletwa Bungeni kusudi wote tuboreshe kwa nia njema na walioandika huu Muswada wamefanya kazi kubwa sana. Ni *very complex exercise*, wamefika hapo walipofika na sisi tunajaribu kuboresha kwa nia njema. Sasa hapa ninachokipendekeza ni kwamba, ukiangalia na kwa bahati nzuri Mwanasheria Mkuu anaweza akanisaidia katika hili kwa sababu hapa wanasema kwamba uamuzi huu wa Bodi utakuwa na mamlaka kama ya *High Court*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimeangalia hii Bodi ambayo inapewa mamlaka ya *High Court* ina mwanasheria mmoja tu, ina *valuers very important profession*, lakini sio katika *profession* ya ku-*dispense* haki. Kuna watu wengine ambao wana taaluma hii. Kwa hiyo, sielewi labda kutueleza maana yake hapa sisi tunatafuta tu ufahamu kusudi twende mbele, lakini wanahistoria wasije wakasema hivi Wabunge walikuwepo au walikuwa wamelala usingizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa nasema kitu cha kwanza ni *clarification*, lazima nikiri mimi sio Mwanasheria sikuelewa hapa mamlaka

ambayo sasa wanasema *High Court*. Kwa hiyo, wanapewa sasa mamlaka ya *ki-high court*, sasa nikaona kwamba labda angalau Waziri wa sekta, angalau ahusike kabla watu hawa hawajapata haya mamlaka ya *high court*, *in case* kuna mtu ana *grievance*, unajua mambo haya...

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hiyo ndio hoja yangu na isije ikawa kama ile *first case*, kama hata kubaliana nitaomba iwe hoja, usije ukaniambia kwamba siku-raise hoja. Hata hivyo, naamini kwamba Mheshimiwa Waziri anaweza akaliweka sawa au mwanasheria tukapata ufahamu tukaenda mbele. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *section* aliyokuwa anaisema Mheshimiwa Tibaijuka, tunapata tabu kuipata kwa sababu *clause* namba 17(4)(4) haipo kwenye huu Muswada sasa atuambie hiyo (4)(4) iko wapi? *Unless* amekosea kuandika maana hapa tunatafuta (4)(4) haipo.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Samahani nimekosea ni 4(b), *sorry*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima unasema zinafanana hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria haikufunga na ndiyo maana rufaa zinazotoka kwenye bodi zinaenda kwa Waziri. Yule mwananchi ambaye hakuridhika ana haki yake hiyo ya kwenda mahakamani, wala hiyo haihitaji kutajwa hapa, isipokuwa hawezi kwenda mahakamani kama rufaa yake hajapeleka kwa Waziri. Kwa hiyo, kule mahakamani watamwambia *no sir, exhaust the remedies*.

Kwa hiyo, hii wala hakuna haja ya kuiandika hapa Mheshimiwa Profesa Tibaijuka, ndiyo utaratibu hakatazwi kabisa lakini kwanza ambaye haridhika na uamuzi wa bodi aende kwa Waziri. Asiyeridhika kwa Waziri ataenda mahakamani kwa *judicial review* au wale wengine wanaita *prerogative orders, mandamus* na vitu vingine, sitaki kuwachanganya hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba, fursa iko hapo na hapa uzuri ni kwamba, kifungu hiki Waheshimiwa Wabunge hakijafunga kabisa kwamba hiyo ya maamuzi ya Waziri ndiyo *final*. Kwa hiyo, naomba tukubaliane na mapendekezo haya jinsi yalivyo.



**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tibaijuka.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu anisaidie ku-address concern yangu ya *high court*. Kwamba sasa hii bodi inatoa uamuzi ambao order yake una *declaratory order* ambayo ina hadhi ya *ki-high court*, kwa hiyo sasa akienda kwa Waziri, nilipokuwa Waziri tulikuwa tunashtakiwa mara nyingi tu, maana yake na Waziri anaweza akashtakiwa *high court* hiyo hiyo. Sasa kama hii bodi tayari yenyewe ni *high court*, mimi ni suala la kisheria tu, utupe elimu tuweze kwenda pamoja. Labda unayoyasema ni kweli lakini elimu haijatoka. Hii *issue* ya *High Court* inakwendaje?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nisome kwanza hii kifungu halafu nitoe jibu langu. *Sub four* inasema *for purpose of proceedings at any inquiring to be held by the Board (b) the Board shall have powers to make any such order as to payment by any part of any costs or witness expenses as it may think fit, and any such order shall be enforceable to the same extent and in the same manner as an order for costs made by the High Court.*

Sasa hii *amendment* ya Profesa hapa inasema *subject to any revision that may result from an appeal lodged to the Minister*. Kwa maana hiyo, kwa mfano inasema Bodi itakuwa ina power kwa mfano za kutoa yale maamuzi ya gharama za mashahidi na kadhalika. Sasa *let think of it inpractical manner*, kuna *inquiring* inaendelea board imeamua kutoa kuhusiana na gharama za mashahidi then kuna *appeal* lakini tunaposema *as it may think fit* ni katika *discretion*, wigo wa ile bodi kutoa hizo gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haina maana kwamba *the decision* ya Bodi ni *final*. *As it may think fit* pale haina maana kusema Bodi inaweza ikatoa gharama hata za mabilioni kadhaa. Imewekwa kuwekwa tu *flexibility* ya namna gani Bodi inafikia maamuzi yake *and it has nothing to do* na ku-restrict powers of *the high court of the Minister* kuhusiana na hayo maamuzi ya Bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ya Mheshimiwa Mdee *its fine*, nilikuwa nazungumzia hii ya Profesa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ya Halima Mdee bado, Mheshimiwa Tibaijuka umeridhika na majibu hayo.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe, hapo jamani mimi nimeuliza maswali ya kawaida, kwamba hii *High*

Court hii huyu mtu anakuja kukubambikizia kwamba wewe bwana unatakiwa ulipe sasa hivi *charges* na *witness* ni milioni 50 na wanasema kwamba ni *declaration* kama ya *High Court*, hilo ndilo swali langu. Swali hili naliuliza kwa niaba ya wananchi ambao watakwenda wote kwa ujumla, tutakwenda kukumbwa na sheria hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tu nipate maelezo, jamani! Ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Haya, basi naomba watu wawili waweze kuchangia ili tupate maoni ya pamoja halafu tumpe Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Komu na Mheshimiwa Halima Mdee.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimepata *concern* ya Profesa! Ni hivi... (Kicheko)

*Wait!* Ni hivi, Mahakama inaposikiliza kesi huwa inaamua kuhusu gharama, uamuzi wa gharama wa Mahakama siyo *final*. Mtu anapokuwa *aggrieved* na *decision* ya *Tax Master* Mahakamani anafanya *special application* kwa *procedures, according to the normal procedures* ambazo zipo katika *civil procedure*, maana yake nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *for that matter* maamuzi yoyote ya Bodi kuhusiana na gharama yataweza kuwa *taxed* na *Tax Master* vile ambavyo *procedure* za kawaida za sheria zime-determine, lakini haimaanishi kwamba, huu uamuzi ukitokea hapa ndiyo *final*.

**MWENYEKITI:** Haya, Waheshimiwa bado mnataka kuchangia hoja hiyo? Haya, Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Komu, tuanze mmoja mmoja.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wakati nachangia niingize na hoja yangu kwa sababu, inafanana na hoja ya Profesa ili tumalize kwa pamoja. Na nashukuru Mheshimiwa Waziri Pansi, amesema amenielewa, kama amenielewa naamini vilevile amemwelewa Profesa kwa sababu, dhamira ni moja lakini inawezekana *approach* ni tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mosi nataka niseme hivi; huu mtindo wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kila tukisema hoja anasema mamlaka ya rufaa ni ya Waziri, siyo sahihi. Mamlaka ya rufaa ya Waziri yaliyoainishwa katika Kifungu cha 33 yanaanzia Kifungu cha 31 ambacho kinahusiana na *Granting and Refusal of Application, Granting of Practising Certificate*. Wala ilikuwa haihusiani na hoja ambayo Mheshimiwa Komu alii-raise kuhusiana na hoja ya yule Mthamini Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, tusikimilie kichaka cha Waziri ambaye

amepewa mamlaka *limited* uliyoinisha wewe kwenye hiyo Sheria kama Mamlaka ya Rufaa. Hiyo ni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, tukisoma hiki kifungu cha 17(4)(b) ambacho Profesa amerejea na ambacho na mimi narejea, naomba nikisome na Mwanasheria Mkuu ujue sisi tunajua Kiingereza, biashara ya kusema unatusomea Kiswahili, tunajua Kiingereza!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nisome hivi, *the Board*, na ni muhimu mkaelewa huu ni uchunguzi wowote ambao Bodi inafanya, naomba mnisikilize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawanisikilizi hawa.

**MWENYEKITI:** Wanakusikiliza Mheshimiwa, endelea tumalize.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 4(b) kinasema, baada ya kufanya huo uchunguzi wa masuala mbalimbali ambayo inaweza ikaletewa, *the Board shall have powers to make any such order as to payment by any part of any costs or witness expenses as it may think fit, and any such order shall be enforceable to the same extent and in the same manner as an order for costs made by the High Court.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hapa ni kwamba, kwa kuwa, hiki chombo kimepewa mamlaka makubwa lazima kuwe na mamlaka ya rufaa, ili kama haki haijatendeka huku chini, hiyo mamlaka iweze kuangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana kwenye mapendekezo yangu nilisema hivi, katika 17(4)(b), nikasema (a) *By deleting paragraph (b) and substituting the new paragraph*, ambayo itakuwa ni (b) sasa ambayo inasema hivi; *the Board shall have power to make any such order as to payments by any part of any costs or witness expenses as it may think fit*, ikaishia hapo.

Halafu nikasema (b) *By adding immediately after (b) a new paragraph* ambayo itakuwa ni (c) ambayo itasomeka hivi: *“Any person who is not satisfied with the decision of the Board may within 21 days from the date of the decision, appeal to the High Court. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii ni mamlaka ya rufaa. Kwa hiyo, hoja yangu na hoja ya Mheshimiwa Profesa. Tibaijuka zinafanana, dhana hapa ni rufaa ili hii mamlaka moja isipewe mamlaka makubwa ambayo hayapimiki! *That is the concept. (Makofi)*

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo ya Mheshimiwa Halima, nibaki tu kushangaa kama Profesa Tibaijuka

anavyoshangaa, kama hii Bodi inapewa uzito sawasawa na uamuzi wa *High Court!* Maana yake sasa hata tukiacha haya maneno ya Profesa Tibaijuka, basi tuweke hata maneno basi kwamba, *Court of Appeal* iwe na uwezo wa ku-revise haya maamuzi. Maana ukisema yaende kwa Waziri, yaani haya maneno yote ambayo Serikali imekuwa ikizungumza yanakuwa *defeated!* Yaani ile *purpose* ya kwamba, unaweza uka-appeal sijui kwa Waziri au kwa nani, *it will be defeted* kwa sababu, unawezaje kupeleka kitu ambacho kina hadhi ya maamuzi ya Mahakama Kuu kwa Waziri? Ni kitu ambacho hakina nanihii! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali awe *sober* na wakati anajaribu kutushauri ajaribu sana kuwa *very considerate* na asome kwa mapana na marefu kwa sababu, anatumia tu kujifichaficha na kujaribu kuleta *terminologies* hapa ambazo kimsingi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa umeshaeleweka, acha tumsikilize Mwanasheria Mkuu!

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wa siku...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda umekwisha, lakini umeshaeleweka, acha tuwasikilize wanasemaje!

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba kushauri hili Bunge, sisi tu-*address issue* tusiende kwenye *personality*, hilo la kwanza. Kama mmetumwa mje mumshambulie Mwanasheria Mkuu wa Serikali muache, mimi nitajikita kwenye *personality*.

**WABUNGE FULANI:**Aaah! We.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, moja niseme hivi, hilo la Mheshimiwa Halima umepotosha Bunge. Kifungu cha 33 kiko wazi tu kwamba mamlaka ambayo, wala hata hakikuainisha kimesema tu kwamba, ambaye haridhiki na maamuzi ya Bodi atakata rufaa kwa Mheshimiwa Waziri, hilo la pili! Sio kama ulivyoainisha wewe hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu; ambacho tumekibaini baada ya majibizano haya ya muda mrefu ni kwamba, Waheshimiwa wote wawili hawa hawataki neno Mahakama Kuu pale. Hicho ndicho angesema, sisi tunakielewa na hapa Mahakama Kuu limewekwa kwa namna tu ya taratibu, *procedure* za

ku-enforce hayo maamuzi ya hiyo Bodi, lakini kama Waheshimiwa Wabunge mnakubali kwamba, tulitoe neno Mahakama Kuu, sisi tunakubali. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tibajijuka, naomba uhitimishe hoja yako.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu mfikirie baada ya kulitoa hili mtatekeleza namna gani hiyo order ya Bodi?

**MBUNGE FULANI:** Ya gharama?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ya gharama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ambacho ningeshauri ni hivi, wao ukakasi uko kwenye ile kwamba, hii itakuwa *enforceable* kama order ya Mahakama Kuu, inazungumza tu utaratibu, *procedure*. Ambacho Waheshimiwa Wabunge hawataki ni kuweka kwamba, ile *status* ile ya namna ya ku-enforce iwe kama ya order kama ya Mahakama Kuu ya kukaza hukumu, ndicho hawataki! Sasa mnataka tuweke utaratibu upi wa kutekeleza hiyo order ya Bodi au hamtaki itekelezwe! Aah, mimi nimeshashauri vya kutosha, inatosh!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndiyo maana tulisema kwamba, kwa jinsi tulivyoleta mapendekezo haya ni sawa. Hii si sheria ya kwanza tuncitunga ikiwa na utaratibu ule na ushauri wetu sisi ni kwamba, *the comfort* ambayo tunayo pale ni kwamba, huyu mtu kabla hawajamkamatia ana fursa ya kwenda kwa Waziri kuomba rufaa. Maamuzi ya Waziri hapa, sheria haijasema ni *final*, anaweza tena huyu mtu asiporidhika na maamuzi hayo akaenda Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, kama hoja hizo mnaona zinafanana na Mheshimiwa Mdee, mmoja ahitimishe ili tuweze kumaliza.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mosi, tutaomba Bunge liamue. Naamini yale makofi yale hayatabadilika kwa sababu ya hizi *story* za Mwanasheria Mkuu, naamini hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, Dkt. Possi, Mwalimu wa Sheria na mdogo wangu, wakati Profesa anazungumza alisema amelewa hoja yangu. Kwa hiyo, *expectation* yangu ilikuwa ni kwamba, angechangia kama ambavyo anachangia ili awasaidie hiyo Meza Kuu hapo mbele, yeye alielewaje ili tuweze kuboresha kwa kutumia hoja zetu mbili mimi na Profesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tatu, narudia kumwambia Mwanasheria Mkuu wa Serikali, sijalipotisha Bunge. Kifungu cha 33 ambacho anakisema wewe anzio lake ni kipengele (c) ambacho kinasema *granting and refusal of application*. Hiyo *application* ni ya *practicing certificate*! Kwa hiyo, *applicant* ndio anakata rufaa kule, lakini hoja yetu hapa ambayo iko *very straight* ni kwamba, hii Bodi ambayo imepewa mamlaka ya kufanya uchunguzi wa masuala mbalimbali imepewa mamlaka makubwa mno yasiyo na kipimo, ndiyo hoja hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukasema kwa sababu, hii Bodi ina binadamu na mamlaka yanaweza kuwa *abused*, tena amekwenda amepewa mamlaka Mahakama Kuu, wao watatoa maamuzi yao kama anavyodhani...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa imetoshia, acha nilihoji Bunge!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie!  
Mheshimiwa Mwenyekiti, kama anavyodhani, *then* Mahakama Kuu itasik...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mdee, umeeleweka. Naomba nilihoji Bunge, kama itakubaliana, tutaelewana. Kwa hiyo, sasa nalihoji Bunge kuhusu hoja zote mbili ambazo mnasema zinafanana; hoja ya Mheshimiwa Tibaijuka na Mheshimiwa Mdee!

Wanaokubaliana na hoja hiyo ambayo ni ya...

*(Hapa Wabunge walimwomba Mwenyekiti  
ahoji hoja moja moja)*

**MWENYEKITI:** Haya, mmoja mmoja basi haya! Wanaokubaliana na hoja ya Mheshimiwa Tibaijuka waseme ndio. Ambao hawakubaliani wasema sio. Sasa tunaenda kwenye hoja ya Mheshimiwa Mdee; wanaokubaliana na hoja ya Mheshimiwa Mdee waseme ndio. Ambao hawakubaliani waseme sio. (Makofi)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti... (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Haziwezi kwenda mbili!

**MBUNGE FULANI:** Kifungu kinachofuata! (Makofi)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haziwezi kwenda zote mbili! *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kitaandikwa nini sasa? Zinaji-*contradict!* *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Tunaandika nini sasa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaomba tusikilizane jamani Waheshimiwa Wabunge, Kifungu ni kimoja, watoa hoja ni wawili. Anachosema Mwanasheria Mkuu hawajui waweke nini hicho ambacho mnsema ninyi. Yule anasema vyake na wewe unasema vyako.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na ndicho ambacho Waheshimiwa Wabunge tunaomba sasa hapa...

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunaomba Waheshimiwa Wabunge, mchague katika haya mawili aidha kama tunaenda na ya Profesa Tibaijuka...

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ya Mheshimiwa Halima Mdee ndiyo iende mbele. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, aah, basi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa, tumeelewana kwa hiyo, hoja ya Mheshimiwa Halima Mdee ndiyo inaingia huku kwenye Serikali. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 18  
Ibara ya 19  
Ibara ya 20

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 21  
Ibara ya 22

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*



Ibara ya 23  
Ibara ya 24

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 25

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hapa pendekezo langu ni kuondoa maneno ya adhabu. Pale mwishoni nasema *delete neno or both*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa mantiki ni kwamba, hizi adhabu ambazo zimewekwa kwa kweli, ndiyo zinastahili kwa sababu, mambo yenyewe ni muhimu, lakini hii ya kusema mtu afungwe na alipe faini, kidogo nafikiria kwamba, ni *over kill*, kwa sababu, ina ukakasi. Aidha, mtu ana faini au anafungwa! Sasa hii ya faini na kufungwa kwa wakati mmoja! Haya mambo ya kufungafunga watu haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni pendekezo dogo kwamba, aidha, Hakimu ataona ataamua itakavyofaa, aidha ataamua kukufunga au ataamua kukupa faini. Naomba kuwasilisha. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Upande wa Serikali, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 25 hiki, *unless* nimekosea Profesa utanisahihisha! 25(2)(a) ndicho hicho eeh? Umesema tuondoe ile *or both*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri tulifanya haya makusudi kwamba, mtu anaweza akatozwa faini au akafungwa au yote mawili, hii sasa ni *discretion* ya Mahakama. Badala ya kuilazimisha Mahakama ichukue faini au kifungo peke yake, kunaweza kuwa na kosa ambalo linastahili adhabu zote mbili za kifungo au faini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiria hili jambo si baya, kwa sababu, Mahakama zile zinatenda haki. Tumempa *option* Jaji aamue kumfunga au kumtoza faini au yote mawili; hii ni *choice* ya Mahakama na sheria nyingi zinaandikwa namna hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tibaijuka.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa nimemsikia Mheshimiwa Waziri, nimesikia maelezo yake. Naweza nikaishi nayo, lakini hiyo

hainizuwii kusema kwamba, maana hapa tunazungumzia *professionals*, mtu amefanya kosa kama ameshapigwa faini, sasa unasema pia afungwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eeh, mambo haya ndio hivyo, ndio wataalam wanakwenda kuishia jela huko. Kwa hiyo, kwa maelezo hayo na lazima niseme hapa itaokoa muda kwa sababu, nilikuwa nimejaribu kurekebisha vipengele vyote vinavyotaka kufunga na faini kwamba, waamue maana na faini yenyewe kama ni kubwa ni adhabu ya kutosha, lakini twende mbele tuokoe muda. Nakubaliana na Waziri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa. Kifungu kinakubaliwa kama kilivyo?

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 26

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 27

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 28

**MHE. SALMA M. MWASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu cha 28(b) kinachosema kwamba, Mthamini ili asajiliwe awe na uzoefu wa miaka mitatu. Napendekeza iwe mwaka mmoja kutokana na uhaba wa Wathamini na unyeti uliopo na upungufu uliopo hasa kwenye wilaya nyingi. Huduma ya Mthamini ilivyokuwa ni muhimu, naomba ili tusiweke urasimu kuwapata hawa Wathamini, miaka mitatu ni mingi mno, napendekeza iwe mwaka mmoja.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliangalie hili kwa makini kidogo. Huyu Mthamini aliyepo Wilayani ambaye hajasajiliwa siyo kwamba, anazuiwa kufanya kazi katika Wilaya, atafanya kazi lakini chini ya msimamizi mwenye sifa na uzoefu unaozidi. Tusiangalie wingi wa kuzalisha Wathamini tu bila kuwa na uzoefu. Jamani, uthamini unahitaji uzoefu mkubwa. Mheshimiwa Mwassa mwenyewe umesema tuorodheshe vitu vyote vinavyotakiwa kutathminiwa katika sheria, hatuwezi ni vingapi? Kila kitu katika kila sekta kinahitaji kutathminiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri uzoefu huu wa miaka mitatu ni muhimu ili aweze kusajiliwa kwa sababu kazi hii ni pana, tusije tukalipua hapa

tukampeleka mtu amekaa mwaka mmoja halafu ukafikiri kwamba yeye ni *competent* kwenda kufanya uthamini wa masuala ya *banking mortgage*, sijui *rent* kila mahali; inahitaji mtu apate uzoefu wa kupitia maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kazi hazitasimama kwa sababu tunao Wathamini wasajiliwa angalau kila Wilaya, hawa wapya wanaojiriwa watafanya kazi zao, lakini ili ziende sasa kupitishwa na *Chief Valuer* lazima zipate *endorsement* ya huyu aliyesajiliwa. Kazi hazitasimama na ajira watapata, lakini ili mtu huyu afanye kazi yenye tija kwetu sisi tunaomtuma hebu apate uzoefu miaka mitatu. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwassa.

**MHE. SALMA M. MWASSA:** Nashukuru kwa majibu ya Waziri, lakini badi sijaridhika kwa sababu huyu Mthamini yeye tayari ana miaka minne ya *professional* ile ambayo anasomea utaalam tu kwenye Chuo cha Ardhi, utaalam peke yake ni miaka minne au mitano, inawezekana kabisa ikafika hata mitano kama atachelewa ku-*submit* vile vitabu vya mwisho. Sasa kuna haja gani tena ya kuwa chini ya mtu miaka mitatu, anapata saba ya utaalam tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri akumbuke kuna kama hawa mainjinia mwaka mmoja, Madaktari ambao wana-*deal* na uhai wa mtu, lakini wana mwaka mmoja wa *internship*, kwa nini *Valuer* awe miaka mitatu ndiyo asajiliwe? Naomba nitoe hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukilinganisha na *professional* ya Madaktari, Daktari anahusika na mwili ule ule na mara nyingine anakwenda na *speciality* wa macho ni jicho tu anashinda na jicho, ni jicho, lakini huyu wa *valuation* hana *speciality* yeye ni *valuation* ya kila jambo litakalomfikia. Unataka kuchimba madini, kufanya tathmini utamkuta huyu huyu, unataka kuchukua shamba la bibi kizee ni huyu huyu, kuhesabu miti na *valuation* ya mimea na kila kitu, unataka kufanya *valuation* ya gari ufanye *mortgage* utamkuta huyu huyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusilinganishe na *Engineers, Engineer* unaweza kuhesabu kazi zake; huyu anaweka nondo anaweka kokoto, kila siku ni kazi hiyo hiyo, lakini *Valuer* huwezi ku-*assume* kesho kutatokea kitu gani. Jamani *valuation* ni pana kidogo kuliko hizi anazosema. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema miaka minne ile ya kusoma, leo tumeona wanafunzi wengine wakisoma miaka minne hawajapata hata *practical*, hawajaenda hata mahali ku-*practice* namna ya kufanya kazi hii ya

*valuation*. Tunasema akienda kufanya kazi hii ya uthamini halisi basi apate uzoefu wa miaka mitatu na orodha ya kufanya uthamini haina mwisho. Kwa hiyo, tukitaka tufanye lakini natoa uzoefu wangu na ninavyofikiri iwe kwa sheria nzuri maana tusitunge sheria kama tuna haraka hivi; nchi hii inatuhitaji leo na kesho. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwassa.

**MHE. SALMA M. MWASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijamwelewa kabisa Waziri kwa sababu nimesha-*declare interest* kwamba mimi ni Mthamini, naelewa ugumu uliopo na mimi mwenyewe nimesajiliwa, pia nimeona tabu ninayoipata, sitaki wenzangu wapate. Naomba nitoe hoja Bunge lijadili. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Sasa naomba nilihoji Bunge...

**WABUNGE:** Aaah!

**MWENYEKITI:** Kumbe mpo eeh haya basi wawili hao, Mheshimiwa Susan na Mheshimiwa Waitara.

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mwassa na ni ya msingi sana. Namshangaa sana Waziri anaposema kwamba Madaktari sijui macho, *specialization* ni baada ya *first degree* lakini hawa *valuers* wanafunzi wanasoma miaka minne lakini pamoja na kusoma hiyo miaka minne ya *professional* bado wanaenda kwenye *field* kila mwaka *from first year* mpaka *fourth year* wanaenda *field*. Kwa maana hiyo wanakuwa na *experience* tayari, lakini vile vile tunaangalia uhaba mkubwa uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono kabisa kwamba, tuondoe hili tatizo, hiyo *experience* ya miaka mitatu kwa nini wasiseme mitano, *why mitatu and why not one?* Kwa hiyo, huo mwaka mmoja unatosha kabisa kwa sababu hawa watu wameshaka chuoni, wameshaenda kwenye *field* kila mwaka, kuanzia mwaka wa kwanza mpaka wa nne wanaenda *field* na wanakwenda kufanya hizo kazi. Kwa nini iwe miaka mitatu? Kwa hiyo, naunga mkono na naomba Waziri alielewe hilo.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinitaja, kwa hiyo, usije tena ukaelekeza macho kule.

**MWENYEKITI:** Anza Mheshimiwa Cosato.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleee eeh?

**MBUNGE FULANI:** Wewe endelea.

**MHE. MWITA M WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono...

**MWENYEKITI:** Nimesema aanze Mheshimiwa Cosato halafu utakuja wewe.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi nilipokuwa natoa maoni yangu nilipendekeza iwe miaka miwili lakini baadaye mchana nimefanya utafiti wa ziada na ku-check na bodi zingine. Kuna mchangiaji amesema kwamba tunao wachache sasa hapa tuangalie sio suala la *quantity* ni suala la *quality*. Kwamba tupate hawa Wathamini ambao kweli wapo *qualified* na *competent*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala la miaka mitatu kwenye fani kama hii naona ni suala sahihi hata kama mtu anakwenda miaka minne. Angalia kitu kama Bodi ya Wahasibu kuna mtu anakaa hata miaka saba bado hajapata ile sifa kutokana na ile mitihani na kadhalika. Kwa hiyo, miaka mitatu kwa mtu anayekwenda kufanya kazi ya maisha ya watu kama hii ni muhimu awe na huo uzoefu. Naomba kuwasilisha. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikubaliana kwamba tunazungumza *professionals* na mtu aliyetoa hii hoja ni mtu ambae ana uzoefu na ni *professional* yake, kwa hiyo ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, la pili mimi pia nimesoma sayansi lakini sikusoma uthamini huu, hao watu wanapokuwa shuleni tangu *firstyear* mpaka *fourth year* wanafanya *field work* na hii miti ambayo umetathmini kama ilikuwa ni Tarime wakija Dar es Salaam wala haibadiliki, kama Waziri ambavyo umesema hiyo hoja kwamba daktari ana-*deal* na nini na hizi nanihii hazibadiliki. Hapa unaweza ukaona ndani ya miaka minne amekuwa akijifunza kwa vitendo, lakini sasa umetoa mwaka mmoja ambao sasa atakuwa yupo *site* pale anapata *experience* mbalimbali, *document* mbalimbali chini ya mtu mwingine na *reference* zipo. Kwa hiyo, atakuwa na uzoefu wa kutosha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri tusitengeneze *bureaucracy* ya kuzuia watu kupata fursa hizi. Kama kutakuwa na shida kama nilivyosema kwa nini kwanza kunakuwa na ugumu, tunapoteza mapendekezo ambayo ni kuongeza watu wapate nafasi za kufanya kazi, mnazuia, mnakuwa wagumu kukubali Mheshimiwa Waziri, kuna shida gani hapo? Maana yake hakuna hoja ambayo inatolewa ya kwa nini miaka mitatu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kuna Mheshimiwa amezungumza hapa amefanya utafiti, yaani wewe angalia hii ni *professional*, mtu amechangia asubuhi ameenda ndani ya masaa mawili hapa, huu ni utafiti wa wapi, hiyo ni sayansi ya wapi? Hiyo siyo sayansi huo ni uongo. Nilifurahi ile hoja ilipokuja ya maana tukaunga mkono, mimi nimefurahi sana leo. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Haya asante.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Kwahiyo, mimi nadhani hii hoja ya mwaka mmoja inatosha vijana wapate kazi hii, tuongeze wataalam...

**MWENYEKITI:** Sawa, sasa naomba nilihoji Bunge. Wanaokubaliana na hoja..., Mheshimiwa Mwigulu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja zilizotolewa na Mheshimiwa Waziri ni za msingi kabisa kabisa. Nilichotaka kulishauri Bunge na kwa kweli ningeomba tukubaliane na hoja zilizotolewa na Waziri. Tusifanye uamuzi wa kudumu kwa sababu za mpito, kwa hiyo tunaposema tuna wataalam wachache huu uchache hautakuwa kitu cha kudumu; tutakachokwenda kukitumia miaka ijayo ni *qualifications*, tutahitaji nani ame-*qualify* zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakaporundika watu wote wana *experience* ya mwaka mmoja mmoja tutakuwa tunajipa ugumu katika kupata watu walio-*qualify* zaidi. Kwa hiyo, tusifanye uamuzi wa kudumu kwa jambo la mpito. Tunayo-*experience* ya maeneo mengi kwamba katika hivi vitu ambavyo tunaviamulia kwa vitu vya mpito ndiyo baadaye vinatupa matatizo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwashawishi wameshimiwa Wabunge tutumie hoja ambazo amezitoa Waziri na ana dhamana na ameleta mapendekezo na hiki kitu kitalisaidia Taifa, twende kwenye maslahi mapana, sio hii kuwaza kwamba labda nina mtu ambaye ndani ya mwaka mmoja awe ameshapata hiki. Tusifanye hivyo, tusingalie tu jambo la fursa, fursa zitapatikana kwa Watanzania ambao wapo *qualified* na yeyote ambaye yupo *qualified* kwenye miaka hiyo atakuwa ametimiza wajibu ambao anatakiwa na hicho ndicho ambacho kitamfanya apate sifa hiyo. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwassa unakubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri?

**MHE. SALMA M. MWASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani sikubaliani kabisa kwa sababu... (Makofi)

**MWENYEKITI:** Kama hukubaliani basi, naomba nilihoji Bunge, wanaokubalina na hoja ya Mheshimiwa Mwassa...

**MHE.SALMA M. MWASSA:** Kwa sababu hizo *field work* kila baada ya miezi miwili kila *semester* zinafanywa...

**MWENYEKITI:** Umeshaeleza mengi Mheshimiwa ameelewa na wao wamekueleza, sasa naomba tu nilihoji Bunge tafadhali.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na kukataliwa)

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 29

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba haya mapendekezo yangu niyachukue yote kwa ujumla wake kuokoa muda. Kimsingi hapa maelezo yangu yanataka sasa kuboresha tu hiki kifungu ambacho *clause* ni nzuri lakini ilivyokaa, nimeona kwamba *temporary registered Valuers* hawa ambao watakuwa ni wageni labda wapo hapa; nafikiria kwamba katika kuboresha *drafting* ya sekta ambayo naielewa sana even *professionally* ni kwamba tumepitisha sheria hapa kwenye *Finance Act* kwamba kazi hizi zina-*fall* kwenye *category* ya *consultancy*; ni kama *consultancies*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumepitisha hapa *Finance Bill* inayosema hizi kazi za kitaalam ni lazima pia tuwe na Mtanzania *side by side* na hawa wageni. Sasa nimeona nia njema kabisa ya Muswada kujaribu kulinda maslahi ya wataalam wetu. Sasa hapa mapendekezo yangu yamekuja ku-*rationalize* hilo lengo ambalo ndiyo lengo la yaliyoandikwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikaona badala ya kuzunguka sijui kumpa mwaka mmoja au nini, kwanza *registration* inatoka mwaka mmoja. Kwa hiyo, ninachopendekeza ni kwamba haya mapendekezo nimeyaleta yapo manne yanalenga kuhakikisha kwamba tunamlinda huyu mtu wetu, wataalam wetu lazima waingie kwenye *partnership* na hao wageni. Tusiwazuie wageni kufanya kazi, lakini wafanye kazi *in partnership* kama *Finance Bill* ilivyosema, *then* tutakuwa na *logical frame work*. Kwa hiyo, tunaweza tukajikuta kwenye sheria moja inasema hivi, nyingine inasema vile sasa tukashindwa kutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndio mapendekezo yangu kwa ujumla wake. Naomba sana Mheshimiwa Waziri na Mwanasheria waiangalie na lazima nikiri kwamba mimi siyo Mwanasheria, naandika *logic* tu.



**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha naomba u-conclude tafadhali.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Haya. Kwa hiyo, hayo ndiyo mapendekezo yangu. Nawasilisha kwa nia njema kabisa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Profesa ni nzuri kwa sababu inataka kulinda maslahi ya *Valuers* wa Tanzania, lakini inatuletea tatizo moja, tukiondoa hiyo hapo *for purposes of carrying out specific valuation assignment for a period not exceeding one year*, sasa tutashindwa kum-define huyu atakayekuja kuwa *registered* kama *temporary Valuer* kwa sababu itakuwa imeondoa muda na itakuwa imeondoa dhumuni la yeye kufanya kazi nchini, kwa hiyo, itatuletea *confusion*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tibaijuka.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona tupo pamoja na Waziri tunakwenda vizuri, lengo langu ninam-define. Lengo langu ni kwamba huyu ambaye yupo hapa *temporary* ana *professions*, anatafuta kazi lakini sasa kwa sababu siyo raia, hawezi kwenda peke yake bila ya kuwa na huyu ambaye tunamlinda *inpartnership*. Kwa hiyo, nataka kusema kwamba nadhani *concern* ya Waziri, Mheshimiwa Pansi pale anaposema kwamba haoni anam-define, anakuwa *defined*, nimeangalia vifungu kwa sababu ya kuokoa muda naviunganisha kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nataka kusema kwamba huo mwaka mmoja una ukakasi mmoja, naweza kusema kwamba uzoefu wangu wa watu hawa wageni usiposema *specialized assignments*, ile mikataba mikubwa, kazi nzuri watazi-put under one year. Nasema hakuna sababu, sababu ni kusema kwamba bwana lazima uwe na *partner* kama tulivyosema kwenye *Finance Act*, kwakweli hilo ndio lengo langu. Asante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE WALEMAVU:** Okay, sawa endelea.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwelewa sana dada yangu pale na ndiyo maana tumekiandika kwa kirefu sana hiki kifungu, nia ni hiyo hiyo ya kulinda wageni. Hata hivyo, hiki peke yake hakijitegemei, huyu mgeni haji lazima awe na vibali, hizi ni sifa kwa kazi hii lakini haji na kuna sheria nyingine ya wageni. Kama

anataka kuajiriwa na kampuni lazima hiyo kampuni iwe na usajili na bila shaka hiyo kampuni haitakuwa na wazungu peke yake, tunajua kampuni usajili wake siyo kwetu. Kwa hiyo, hiki kifungu peke yake hakijetegemei wala idhini hii ya kumleta mgeni haitafanywa na Bodi kwa kukiuka Sheria nyingine ya *Immigration* na Sheria ya Usajili wa Wageni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sheria ile ya usajili wa wageni hata yenyewe inahimiza kwamba, huyo mgeni anayekuja katika nchi hii na kupata hiyo *work permit* lazima awe na sifa inayozidi Watanzania waliopo. Kwa sababu kazi hizi hutangazwa na kuna chombo kinachotoa *permits*, yote haya yatakwenda pamoja. Kwa hiyo, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Tibaijuka, Sheria ya Makampuni itatumika, Sheria ya Usajili wa Wageni kufanya kazi itatumika, pamoja na hii kwa pamoja. Hii tumeorodhesha iwe ndefu ili angalau wanaotoa *permit* wale wajue na sisi huku tunajilinda kwa mgeni anayekuja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tibaijuka umeridhika na maelezo ya Mheshimiwa Waziri?

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nimeridhika tuendeleo. (Makofi)

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 30

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 31  
Ibara ya 32

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 33

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 34  
Ibara ya 35  
Ibara ya 36  
Ibara ya 37

Ibara ya 38

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 39

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 40

Ibara ya 41

Ibara ya 42

Ibara ya 43

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 44

**MHE.PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hapa nilikuwa natafuta haki ya mtu kukata rufaa, lakini kwa maelezo ambayo Mwanasheria Mkuu ameshatoa hapa na Waziri, naondoa mapendekezo yangu mezani, maana yake wanasema kwamba bado mtu kama hakubaliani na Waziri anaweza akaenda mbele, kwa hiyo tunaendelea.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 45

Ibara ya 46

Ibara ya 47

Ibara ya 48

Ibara ya 49

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 50

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba tu niseme kwamba, hapa kwa uelewa wangu wa sekta hii nimeweka maneno, kwamba tu-*insert* maneno katika hiyo *section* two kati ya neno '*section*' na '*bases*' *taking into account the scale of the exercise*. Ni suala la

kitaaam kwa sababu fani hii ya *valuation* ina pia uchumi ndani yake na nilivyokuwa Wizara ya Ardhi kitu nilichokiona ni kwamba ukiendesha bila kuzingatia misingi ya uchumi inaweza ikaleta ukakasi mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji wengi leo nilikuwa nasikia wanagusia suala la thamani ya *valuation*, atakupangia kiasi gani. Sasa nataka kusema kwamba kwa upande wa Serikali ni lazima anakuwa na, tunaziita *mass valuations*, anaweza kuwa ana labda eneo zima anataka labda kufanya uthamini wa eneo zima, ni tofauti na *market value*, sasa mtu anaweza akafanya kosa *conceptual error* akasema kwamba hapa nyumba zinazwa labda milioni 10, wakati ni nyumba moja inazwa, kama unauza nyumba 20 huwezi kupata milioni 10 na kwa ardhi ni hayo hayo. Kwa hiyo, ili sheria iwaongoze vizuri hawa wataalam wetu, nimeweka hayo maneno, ni suala la kitaalam tu kusudi sheria iende vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu anaimarisha tu hili mimi sina matatizo nalo, nafikiri tunalikubali tutaongeza hapo. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 51

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 52

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Kwenye hicho kifungu pendekezo langu ni punguzo kutoka miaka miwili ya Serikali ambayo wamependekeza mpaka mwaka mmoja na nusu kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia nilizungumzia suala la ule mchakato, kwamba uwekwe kwenye sheria, kwamba zile taarifa za uthamini mpaka zimfikie *Chief Valuer* na ngazi zile zote isizidi muda mrefu sana, kuweka miaka miwili ni kuwaweka wananchi kwa muda mrefu na washindwe kuendeleza ardhi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu alisema kwamba ule mchakato wa Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya upo

kwenye kanuni, tangu mwanzo nilishauri kwamba haya mambo mngeweka kwenye sheria hii itasaidia ku-*justify* pia kwa nini mnapendekeza miaka miwili na kwa nini sio mwaka mmoja au mwaka mmoja na nusu. Hivyo basi, ili kuwasaidia wananchi hawa au yeyote ambaye anahusika katika suala zima la kupata haki yake katika eneo lake ambalo limetwaliwa, basi isizidi mwaka mmoja na nusu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzo tulikubaliana tuweke miaka mitatu, tulivyokwenda kwenye Kamati kukawa na mapendekezo ya Mheshimiwa Dkt. Ndugulile na wengine ndiyo tukafika katikati miaka miwili. Labda niseme kwamba, kwa nini tumefikia miaka miwili, kwa sababu *process* hii ya uthamini si kazi ndogo, ni ndefu na ni shirikishi. Unaweza kuwa na *process* hata ya siku moja katika miaka miwili. Nataka kufanya tathmini ya gari yangu nitamaliza siku moja, nataka kufanya tathmini ya cheni yangu nikaweke *mortgage* nitamaliza siku moja, lakini nataka kufanya tathmini ya reli ya kati kutoka Dar es Salaam kwenda Kigoma siwezi kumaliza siku moja, mle ndani kuna nyumba, kuna mazao, kuna mimea, kuna miti, kuna mashamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuna *process* ya kufanya uthamini, kuna *identification*, lakini pia kabla hujafanya hivyo lazima na wenyewe wenye mali zao katika yale maeneo hata hayo makubwa kuna *process* pengine unaweza kuwa unafanya uthamini wa ekari 100,000 kwa mara moja. Kila mtu aingie kwenye eneo lake mhesabu mimea na miti, michungwa na hivi, kila mmoja lazima utathmini na aridhike na a-*sign*, si kazi ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa tusifikiri kwamba uthamini wote unafanana, iko siku uthamini utakuwa wa mahitaji mapana zaidi kwa hiyo ndiyo maana tumeweka miaka 10. na kwa sababu ni shirikishi, maana kila mwananchi anayethaminiwa lazima ashirikishwe katika zoezi hili. Sasa kwa sababu hiyo, ndiyo tumeona iwe miaka miwili hii. Kwa nini tunasema baada ya miaka miwili uthamini urudiwe, kwa sababu *process* yenyewe ya uthamini ni ya muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunafikiri kwamba miaka miwili inatosha kwa kuzingatia kwamba huyu mtu anaweza kuwa ameshalipwa miezi sita na kama hakulipwa miezi sita ana *interest* anapewa. Yaani hapa ni mwisho, kwanza mtu kama hajalipwa miezi sita analipwa *interest* lakini tumesema kama atakuwa hajathaminiwa baada ya miaka miwili, basi uthamini huo urudiwe. Kwa sababu katika miaka miwili hii si suala la kusubiri tu, kuna *process* ya uthamini hapa imeshafanyika, si suala la kusubiri miaka miwili tu. Kwa hiyo, nafikiri tumetoka kwenye miaka mitatu, twende miaka miwili. Anaweza akalipwa katika mwezi mmoja, miwili, sita na akapata na riba. Kwa hiyo, Mheshimiwa Gekul nafikiri miaka miwili inatosha. (Makofi)

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishawishika kupendekeza mwaka mmoja na nusu kwa kuwa pia Serikali imekuwa ikitoa kauli kwamba sasa hakuna eneo ambalo linaweza likatwaliwa bila huyo mwenye *intention* hiyo kutokuwa na fedha za kulipa fidia. Hata hivyo, nafahamu kuna miradi mikubwa na midogo, miradi haitafanana kwamba Serikali inataka kutwaa eneo lina ukubwa fulani au mtu *private*. Haya matatizo yamejitokeza kwa muda mrefu sana, watu wamesubiri kwa muda mrefu na haya mambo yamejitokeza. Kama Serikali ina wataalam sasa kwa nini isiwe mwaka mmoja na nusu ili kuepusha mlolongo huo mrefu, lakini pia nishauri, kwa sababu pendekezo hili haliko kwangu peke yangu, tuwasikie na wengine mwisho wa siku tufikie *concensus*.

**MWENYEKITI:** Hakuna aliyekuunga mkono tuendeleo Mheshimiwa Dkt. Ndugulile.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipongeze Muswada huu kuletwa na Serikali na uamuzi wa Serikali kuingiza ukomo wa fidia ndani ya *Principle Act* kwa sababu imekuwa ni kilio cha muda mrefu sana. Kimsingi sina matatizo na mapendekezo ya Serikali, nataka nikazie tu maeneo ambayo, kwa sababu kifungu kinasema miaka miwili itaanza kuhesabika pale Mthamini Mkuu wa Serikali atakapokuwa ameidhinisha zile *valuation reports*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa inawezekana Mthamini Mkuu wa Serikali, pamoja na *comfort* ambayo ametoa kwamba anaweza akaifanya ndani ya siku saba, lakini haya ni masuala ya kibinadamu. Sasa nataka kupendekeza tuiweke kisheria zaidi, kwamba, kwa maana ya ku-*endorse* zile *valuation reports* haitazidi miezi sita baada ya kukamilisha zoezi la uthamini ili sasa tuifunge vizuri ili mapendekezo yote ambayo yametolewa na Serikali yaweze kukaa vizuri.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui kama nimemwelewa ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Ndugulile. Unataka ripoti zikifika kwa *Chief Valuer* ile *endorsement* yaani sahihi yake ile isizidi miezi sita? Sawa, lakini sisi *efficiency* yetu imevuka hapo. Ukisoma kwenye sheria tulisema wiki moja. Kama mambo yote na wananchi wameshasaini na kila kitu wamesharidhia, huu mhuri wa *Chief Valuer* pale isizidi miezi sita bila ukomo, unajua anaweza kwenda miezi sita kweli? Miezi sita ni mingi sana, ukisema isizidi miezi sita anaweza kwenda miezi sita. Nafikiri labda tuje katikati tupunguze, lakini miezi sita Dkt. Ndugulile ni mingi sana. Sasa tukiandika hii inampa *room* huyu *Chief Valuer* kwenda miezi sita, itachelewesha na sisi tunataka kwenda kwa kasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda sikumwelewa, labda anifafanulie tena tafadhali.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu kwa Mheshimiwa Waziri, ukiangalia kile kifungu kipyua ambacho amekitoa pale, mimi hapa narejea tuseme ule ukomo unaanza lini na ukomo unaanza kuhesabika pale *Chief Valuer* atakapokuwa ameidhinisha, ninachokitaka sasa na sisi tumbane, wewe ni sawa nakubaliana na wewe sasa hivi katika utendaji wako Mheshimiwa Waziri, ndani ya wiki moja wanaweza wakakamilisha ile kazi, lakini inawezekana huyu *Chief Valuer* ameanza zoezi la tathmini, amemaliza, kwa sababu Serikali haina fedha akachelewesha kuidhinisha lile ili ku-buy time ile miaka miwili isianze kuhesabika. Sasa sababu ya kuleta mapendekezo haya Mheshimiwa Waziri, ni kumbana *chief valuer*, mimi ukiniambia hata wiki tatu, kwamba baada ya zoezi kwisha tukakubaliana sina shida na hilo, lakini tunataka tuweke muda maalum wa *Chief Valuer* kukamilisha ripoti zake.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana naye, isizidi miezi sita. (*Makofi*)

**MHE.PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu naona limeshasemwa na Serikali, ilikuwa ni miaka miwili sasa imeshakuwa *two years, sawasawa, two years.*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi labda niseme, wasiwe na wasiwasi. Japo sheria itasema miezi sita lakini Waziri kwenye *regulations* atakazia kidogo ili isifikie huko miezi sita, maana yake sisi hatuendi kwa uvivu huo. Tunasema isizidi miezi sita, lakini sisi tutaweka utaratibu, sasa tumeshapitisha ile Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, sina *problem.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi *in house* tutaweka utaratibu wa kubanana ili tufikie hii lakini haitazidi miezi sita.

**MHE. SALMA M. MWASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hoja yangu ilikuwa kwenye 52(2) na 52(5), kutoka miaka mitatu kuja mwaka mmoja, lakini nimesikiliza maelezo ya Mheshimiwa Waziri kwamba kutokana na *process* ya *valuation* ameondoa kwenye miaka mitatu sasa inarudi miwili, angalau nakubaliana naye. Kwa maana nilikuwa napata tabu kwenye miaka mitatu hiyo nyumba ingekuwaje. Kwa hiyo, kwa maelezo yake nimeondoa hoja. (*Makofi*)

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)



Ibara ya 53

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti samahani, 52 mimi nina marekebisho bado.

Ibara ya 54

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna marekebisho...  
Ibara ya 55

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru, lakini kwenye kifungu cha 52 nilikuwa nimeongeza kijifungu kidogo cha 52(8), sijui hapo mezani hamkuona na karatasi langu mnalo.

**MWENYEKITI:** Ulipewa nafasi Mheshimiwa, tumemaliza. Tuendeleo na kifungu cha 55.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipewa nafasi kwa 52(2) lakini 52(8) ilikuwa bado.

**MWENYEKITI:** Ilikuwa kwa pamoja zote zile Mheshimiwa, kwa hiyo sasa hivi tuko kifungu cha 55.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana hatuendi hivyo, kwa sababu inaonesha vijifungu vidogo.

**MWENYEKITI:** Tulikuwa tumefanya kwa pamoja vyote na tulikubaliana hivyo na hakuna aliyeunga mkono hoja...

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** hatuendi hivyo.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo naomba tuendeleo kifungu cha 55.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru, naomba tu niendeleo na 55(1). Napendekeza katika 55(1)(a) kwamba hawa *Valuers* watakapoingia kwenye *premise* au maeneo ya watu hao ambao wanataka kufanyiwa *valuation* basi pawepo na *consent* ya wale ambao maeneo yao yanafanyiwa *valuation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekubaliana na marekebisho ya Serikali lakini nikaongeza tu neno dogo la ridhaa ya wale watu ambao wanafanyiwa uthamini na nilisema haya kwa sababu kwa suala la kwamba mtu anahitaji kupata mkopo benki au maeneo mengine inaweza ikawa rahisi lakini kwa ardhi ya wananchi ambayo inataka kutwaliwa, wale watu, pamoja na *notification* ambayo tumeandika kwenye sheria hii lazima pia waoneshe kwamba wako tayari ili kuepusha hawa *Valuers* wasifukuzwe na wananchi kwa sababu lilishatokea na nika-cite mfano katika eneo langu. Kwa hiyo, naomba hili neno tuliongeze kwa sababu pia mapendekezo ya awali ambayo mmetoa kwenye jedwali la marekebisho nimeona hayana tatizo.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hoja ya Mjumbe ni ya msingi kama anavyoizungumza, lakini tukumbuke tu kwamba ukishaweka kifungu hiki sidhani kama kuna mwananchi ataridhia na wakati huo unakuwa na shughuli ya muhimu ambapo unataka kutwaa lile eneo, sasa ukitaka mpaka upate *consent* yake, akikataa maana yake utakwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, pengine limetokea janga la mafuriko, unataka kwenda kutwaa eneo uwape watu waweze kuishi pale, kwa hiyo ni lazima ufanye uthamini wale watu wakakae, huyu akikataa hawa watu unawapeleka wapi. Kwa sababu lazima tuangalie na *situation* ambazo zinafanya watu waende kufanya uthamini kwenye eneo. Sasa ukitaka kusema kwamba mpaka ridhaa yake maana yake hakuna mahali ambapo mwananchi ataridhia tu kwamba lazima ufanye hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo lazima tuchukulie kitu kutegemeana na shughuli unayokwenda kuifanya. Kile kitendo tu cha kumpa taarifa ya kwenda kufanya inatosha yeye kum-*alert* kwamba kuna hiki kitu kinafanyika ili awepe wakati uthamini unafanyika, aweze kushuhudia kile kinachofanyika. Ukitaka mpaka akuruhusu na kwa hali halisi ambayo wananchi wameumia kipindi cha nyuma, hakuna mwananchi atakayekuwa tayari kuridhia ukafanye uthamini kwenye eneo lake halafu uweze kulitwaa, haiwezekani. Kwa hiyo, lazima pia tuangalie na *nature* yenyewe ya *valuation* inayokwenda kufanyika.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru tu sjaridhika na majibu ya Naibu Waziri kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa vitu ambavyo vimekosekana huku nyuma tulikotoka ni pamoja na *Valuers* au taasisi inakwenda kwenye maeneo ya wananchi wanakwenda kufanya *valuation* wananchi hawafahamu. Nikatoa hata mfano wa wananchi katika jimbo langu, naamini pia maeneo mengine haya yamejitokeza, kwamba eneo linakuwa *valuated* wananchi hawafahamu. Kuna taratibu zetu na sheria zetu, kwamba kama

eneo ni la taasisi Serikali inahitaji kwa ajili ya taasisi ama shule au zahanati au hospitali, maana yake ile ni huduma ya jamii ambayo wananchi lazima turidhie, wananchi hawa wakipewa elimu hawakatai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nasema hawa pamoja na *procedure* ambazo zimetumika kuwa-*notify* kwa maandishi au kwa njia yoyote ile, lakini wao wakubaliane na wafahamu kwamba kuna kitu kinaendelea katika maeneo yao ili wawape ushirikiano. Kwa sababu hili linagusa maslahi ya wananchi, naomba niombe Wabunge wenzangu ambao wameelewa waweze kujadili ili tuone kwa sababu tunachohitaji hapa ni ridhaa tu, kwamba nakubaliana njooni mfanye uthamini, baada ya hapo na wao watawapa ushirikiano hata katika ulipaji wa hizo fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ambao wako tayari tafadhali waniunge mkono.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, *amendment* ya Serikali kama anaisoma pale kifungu hicho tumekiandika kwenye *paragraph (p)* pale, *in clause 55 (1) by inserting the word upon prior notice to the owner or occupier of the land, building or premises between the word Act and enter appearing in the paragraph (a)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tukiangalia, akikataa kufanyiwa uthamini kwenye sheria atakuwa ana-*commit offence* katika taratibu nzima hizi. Kwa hiyo, kama atakuwa ana-*commit offence* maana yake yuko *liable* kuweza kupata *fine* ambayo imezungumzwa pale *less than one million shillings but not exceeding three million*, kwa sababu hii *valuation* inapokwenda kufanyika anapewa *notice* ili ajue nini kinafanyika na yeye anakuwepo, sio kwamba itafanyika hayupo. Sasa umeshamwomba, umempa taarifa, halafu bado anakataa, sheria bado inakuja inambana na pia tuangalie *valuation* inakwenda kufanyika kwa ajili ya kitu gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Gekul bahati nzuri ni Mjumbe wa Kamati, lazima tuangalie kwamba *implication* yake itakwenda kuwaje, hakuna kazi itakayofanyika kwa ridhaa tunayotaka watu waipate, lakini sheria ikiwa bayana tayari tutakuwa tumempa *notice* na tunafanya nanihii. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul, umekubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri?

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi kuna tofauti kati ya *notification* na *consent* ya mtu lakini nimeliweka hili ndiyo maana hata katika kifungu cha 55(2), ninyi mmeshauri kwamba mwananchi huyuhuyu akikataa apewe adhabu na mkapendekeza mpaka na miaka ambayo anaweza akafungwa. Ndiyo maana nimeleta marekebisho kwamba hii adhabu isiwe kwa

yule mtu ambaye ana-own eneo lake, iwe ni kwa yule *Valuer* ambaye ameingia na kufanya hayo bila wananchi hao kushirikishwa. Siongei kutoka tu hewani, naongea kutoka kwenye uzoefu na Mheshimiwa Waziri yanafanyika...

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo umekataa au umekubaliana na Mheshimiwa, umekataa?

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijakubaliana nae.

**MWENYEKITI:** Haya basi tumpe fursa Mheshimiwa Mwigulu halafu...

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo analisema Mheshimiwa Mbunge kwa nadharia linaweza likawa jambo jema, lakini haliko *practical* kwenye utendaji na sisi hapa tunatengeneza sheria kwa maana tunataka kupeleka kitu kwenye utekelezaji wake. Aina ya watu anaowaongelea kwamba watoe ridhaa sijui anatumia *reference* ya wapi, lakini watu wengi ninaowajua hata eneo ambalo walikuwa hawajapanda chochote wakiambiwa tunataka kupitisha nyaya za umeme kwenda katika eneo hili wanakwenda kuweka viminyaa, wanaenda kuweka vinyasi kutaka kukwamisha miradi, tuna mifano ya aina hiyo. Ukitaka *consult* hata ya *valuation* tu tutakuwa tunaweka urasimu ambao haustahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania na Serikali na Mamlaka mara zote zinawajali wananchi wake na lengo la *valuation* kimsingi ni kwa ajili ya kujali wananchi walioko katika eneo lile. Nadhani itoshe hiyo ya kutaka kuwajali kwa namna ya kufanya *valuation* na kum-*notify* kwamba tunataka kufanya kitu cha aina hii ili tutunge kitu ambacho kitakuwa *practical*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtakumbuka hata kuna wakati tulikuwa tunatunga sheria tukasema tukiweka sheria ya aina hii kila siku watu watakuwa wako mahakamani wakiishtaki Serikali sasa na hili kwa sababu ya kutengeneza kitu ambacho kiko *realistic* ambacho kitatekelezeka, tuweke kwamba watakuwa *notified* na hizo ni hatua za kwanza za Mtanzania kuweza kupewa haki yake na tunaongelea maslahi mapana ya Kitaifa, hatuongelei mtu mmoja kujitokeza kupora eneo la watu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza hili hebu tujulize sisi ni Wabunge au tujishushe kidogo Madiwani. Vijijini kabla hatujajenga shule, hatujafanya lolote tunapanga mpango wa matumizi bora ya ardhi. Mkutano Mkuu wa Kijiji umekaa, umeamua kwamba hapa tunajenga barabara, hapa ndiyo mahali pa kujenga shule, tumeamua Mkutano Mkuu lakini hapa tunapoamua kama Kijiji hili ni shamba la

Lukuvi tutamfidia atoke tutajenga shule, huyu jamaa hataki mnafanyaje? Mnataka aridhie Mkutano Mkuu wa Kijiji umekaa na mmepanga mpango wa matumizi bora ya ardhi ya kijiji chenu na mmeridhia?.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kwa akili ya kawaida, sheria zipo za *property tax*. *Valuers* wanakuja kwenye nyumba yako umefunga siku ya kwanza, unajua *notification* Mwenyekiti wa Mtaa akishakuletea mara mbili, mara tatu unafunga na sheria mmetunga hapa kwamba kila nyumba ilipiwe kodi halafu haiwezi kuwa hiari ya namna hiyo Mheshimiwa Gekul, haiwezi kuwa kwa sababu hakuna hata mtu mmoja anayechukua ardhi kwa makusudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hairuhusu, usisome hii sheria peke yake, hakuna sheria ya uporaji wa ardhi katika nchi hii, inatwaliwa kwa madhumuni maalum na iko sheria nyingine Rais anaweza akatwaa hivi hivi tu kwa manufaa ya umma bila hata hiyo milolongo yote hii na mjue sheria hii ukisoma sheria namba nne maana yake nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Gekul nasema midhali tumempelekea *notice* na mara nyingi *notice* hizi tunapeleka kwa viongozi wa mitaa au wa vijiji wanapeleka *notice* ya maandishi, mtu amepokea bwana mkaribishe huyu jamaa, mpe taarifa afanye tathmini. Sheria ya kwetu ya ardhi inasema mtu utalipwa thamani halisi, utalipwa fidia inayostahili tena kwa bei ya soko sasa ni kitu gani hicho maana yake vinginevyo Gekul maendeleo yatakuwa magumu sana ku-*perform*. Kufanya kazi za maendeleo itakuwa ngumu.

Angalia hata Babati yako ile unatengeneza *master plan* nimesaini juzi. *Master plan* ile itabadilisha sana muundo wa mji wako wa Babati nimesaini juzi kabla sijaja hapa. Kuna watu utawaondoa pale ili ufanye hayo unayoyataka. Utapangaje mji kwa hiari?

**MWENYEKITI:** Kwa vile Serikali imeshatoa maelezo ya kina, Mheshimiwa Gekul kama hujaridhia basi naomba nilihoji Bunge.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru binafsi sijaridhia kwa sababu pia nina uzoefu na hata hayo yameshajitokeza.

**MWENYEKITI:** Kama hujaridhia basi naomba nilihoji Bunge kwa vile maelezo ya Serikali yamekuwa ni marefu.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)

**MWENYEKITI:** Tuendelee na Mheshimiwa Tibaijuka.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja zangu kwa sababu Mheshimiwa Waziri ameshazijibu, hoja ya Serikali imekidhi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Upendo Peneza.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika hii hoja yangu kwanza nakubali marekebisho ya Serikali ambayo yameletwa lakini katika mapendekezo yangu nafuta maneno ambayo *without liability for trespass*, hilo nafuta, halafu kuna maneno ambayo yanaingia hapo ambayo ni *by in such the word and upon the consent and presence of the owner*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo ambayo yametolewa na Mheshimiwa Gekul lakini pia kutokana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri katika maelezo yake alisema pia kwamba hata mwananchi mwenyewe atakuwepo wakati wa kufanya tathmini, lakini sheria haijataja, haijaruhusu uwepo wa huyo mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tukirudi kwenye upande wa *consent* na upande wa sheria anayoisema labda tuseme kwamba Serikali haitaki kupeleka wananchi Mahakamani, tuseme hivyo kwa sababu suala la *consent*, Serikali ikiwa inatoa *notice* kwa ajili ya kufanya tathmini ya kitu kama hicho ni vizuri pia katika *notice* hiyo ikaandikwa kama mtu hata kubaliana basi mtu huyo atapelekwa Mahakamani na hizi ndizo zitakazokuwa katika *notice*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukisema kwamba, leo hii tunasemea nia njema hii ambayo mnasema labda kumetokea mafuriko katika eneo fulani ama kumetokea shida fulani. Kwa nini tusifikirie katika misingi ambayo mtu anataka kuchukuliwa eneo lake hayupo ni shamba labda kuna uwekezaji unataka kufanyika katika hilo eneo na lazima tukumbuke kama uwekezaji unavyokuja kufanyika...

**MWENYEKITI:** Naomba ufupishe Mheshimiwa Upendo.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa. Mheshimiwa Waziri alivyokuwa anazungumzia *market value* katika maelezo ya awali anavyoelezea *market value* huku katika sheria hii samahani, inaelezea pia kwamba lazima mwananchi aweze kukubaliana, hiyo sentensi pia ipo, kwa hiyo kama kwenye *market value* lazima mwananchi akubaliane, mtu anakuja shambani kwangu ananihesabia anasema nina migomba 10 kumbe in *actual*

sense nina migomba 20, si sawa. Kwa hiyo, ni lazima tuweke *presence* ya mtu ionekane. Hivyo, napendekeza katika hayo marekebisho isomeke hivi:

“When necessary for the purpose of carrying out his functions under this Act, and upon....

**MWENYEKITI:** Muda umekwisha Mheshimiwa Peneza.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naisoma ili aweze kuelewa nataka marekebisho gani?

**MWENYEKITI:** Wanayo tayari pale

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Aaah! Nasoma ya kwangu sisomi yake. Nasoma ya kwangu

**MWENYEKITI:** Hiyo yako wanayo.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Ok, Sawa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anachotaka kukisema ni kwamba, anataka kuondoa *immunity*, niseme hivyo *impliedly* kwa wafanyakazi wa Serikali wanaokwenda kufanya *valuation* kwa maana hiyo ile dhana ya kumlinda Mtumishi wa Serikali kwa kitu ambacho kinaweza kikaonekana ni kosa, lakini kumbe ni jambo ambalo ni lazima alifanye katika utekelezaji wa wajibu wa kila siku, itakuwa haina tofauti sana. *Well*, siwezi nikafananisha na Polisi lakini Polisi anakuja nyumbani kwako huhitaji *consent* halafu unasema *ame-trespass*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu ili kurahisisha utendaji wa wafanyakazi hawa *Valuers* wanapofanya kazi zao na ili kuondoa huu urasimu usiokuwa wa maana tuondoe hiyo. Hata hivyo, kuna kitu kimoja, kwa sababu hii ilikuwa na maana hapa alikuwa amezungumzia; *and upon the consent*, tumeshasema mwanzo labda niliweke mwanzo kwamba ukikataa mtu kuingia kwenye eneo lako kufanya *valuation* ni kosa la jinai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiweka hapa *upon consent* ina maana unampa mtu ridhaa ya kukubali au ya kukataa. Kwa maana nyingine, unampa mtu ridhaa ya kukubali au kutenda kosa la jinai. Sasa sijui unataka ku-*protect* kitu gani kwamba umwambie mtu kubali au tenda kosa la jinai *that's the meaning of consent here*. Kwa hiyo, kwa upande mwingine utakuwa unawauza



wananchi, unawaambia watende makosa ya jinai wakati kumbe *bynotice* kila kitu kingekuwa kimeshamalizwa. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Upendo Peneza.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui Serikali inachokimbia ni nini kwa sababu mwisho wa siku mtu akifanya tathmini katika eneo langu lazima nikubaliane kwamba kile alichokikuta ndani ya shamba langu ndicho, lazima nikubali hicho, sasa sheria haihitaji *my presence* kwenye hiyo *situation*. Kwa hiyo, hapa ninachoongelea ni kwamba *presence of the owner* wa hilo eneo ili mwisho wa siku tusirudishe Serikali kwamba mtu ameshanihesabia vitu nilivyonavyo shambani, unaniletea karatasi nisaini ili basi huo mji au *whatever the project* unataka kuleta pale ili iendelee nikaikwamisha kwa sababu nimekataa kusaini kukubaliana kwamba hiki ulichokihesabu ndicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tu Serikali tuweze kukubaliana kwenye hili kwamba *consent* iwepo na kama kwenye suala zima la *consent* mtu akikataa, kwa hiyo dhana nzuri mnayoiongelea, shida ikitokea kuna sheria ipo, kifungu kidogo cha (2) hapo 55 kinasema Serikali mnaweza mkampeleka Mahakamani, *then* kwa nini tusikubaliane hiki? Yaani *why not?* Yaani kwa kweli...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Upendo hivyo ndivyo inavyofanyika hata sasa. Hiyo *procedure* ya kuwepo, wiki iliyopita nimetoka Ruangwa, kuna tathmini ya madini inafanyika kule tena hawa wawekezaji siyo tu wanataka *presence* ya mtu hata akienda siku ya kuhesabu na kuthibitisha mimea yake wanamlipa shilingi 15,000. Unakuwepo na bado wanakulipa. Hii mnahesabu pamoja na unasaini kwamba nina mikorosho 10, minazi, halafu kwenye orodha ya thamani inaonekana kila mmea na kila mtu na kila kitu kina thamani kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa asifananishe vitu viwili, sisi tunachosema hapa, alichokuwa anasema Mheshimiwa Gekul, kabla ya kufanya *process* yenyewe lazima uridhie, hapana ila nilisema mwanzo katika *process* yenyewe ya uthamini kuna ushirikishwaji na ndiyo maana mtu mwenyewe yule halipwi kama asiposaini kukubali ule uthamini, utalipwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tutenganishe vitu viwili. Narudia hapa tutengenishe vitu viwili. Kwenda kufanya tathmini ukishapewa *notice* lazima uwepo na lazima ushiriki. Hakuna swali hapo. Usipofanya unaadhibiwa, lakini katika zoezi lile la tathmini mpaka kufikia hesabu unashirikishwa tena si wewe tu

hata viongozi wa mitaa wanashirikishwa, hata sasa inafanyika hivyo, *Valuers* wako hapa wanajua.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ni...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Peneza, kwa vile Serikali ilishatoa maelezo marefu naomba tu nilihoji Bunge kama hukubaliani nayo.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba basi uruhusu watu waweze kujadili hili suala.

**MWENYEKITI:** Ndiyo muda umekwisha na umeshazungumza mara mbili hujasema kama unatoa hoja, kwa hiyo, naomba nilihoji Bunge ili tukubaliane tumemaliza.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti ni suala la muda kwisha ama ni suala la mimi kuomba watu wajadili? Kwa sababu alishatengua kanuni ili tuweze kujadili.

**MWENYEKITI:** Muda wako umemalizika kwa sababu hukutoa fursa ya kusema kwamba unatoa hoja. Kwa hiyo, sasa kwa vile Serikali ilishatoa maelezo marefu naomba nilihoji Bunge.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 56

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 56, Mheshimiwa Tibaijuka.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naondoa mapendekezo mezani yameshazungumziwa ni kuhusu zile adhabu tumeshakubaliana kwamba ni kufungwa na *fine*.

**MWENYEKITI:** Sawa.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 57

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 58

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 59

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 60

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 61

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 62

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 62, Mheshimiwa Tibaijuka.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Yanaondolewa mezani, tunaendelea.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 63

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 64

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 65

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 66

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 67

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu yanaondolewa.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 68

Ibara ya 69

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 70

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 70, Mheshimiwa Tibaijuka.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hapa nimeangalia vipengele ambavyo Mheshimiwa Waziri ataviandikia na nimependekeza kwamba katika zile kanuni napendekeza kanuni zifuatazo nazo zifafanuliwe vizuri. Inawezekana ziko chini ya zile *headings* walizoweka lakini kwa ushauri wangu itakuwa vizuri tupate *procedures for assessing land and buildings while conducting valuations*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hiki ambacho tumekizungumzia sana na tumekubali marekebisho ya Serikali kwenye *Principle Act* imeingia lakini katika vitu ambavyo sheria inamtaka Waziri sasa afafanue zaidi maana yake *Principle Act* imeweka sasa hivi, lakini nimesema kwamba pia Waziri katika kanuni zake aifanyie kazi zaidi na pili *procedures for assessing land and property rates under singular and mass valuations*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tumekubaliana kule kwamba suala la *scale* liingizwe, hii nayo inakuwa muhimu kwamba Waziri aweze kuwasaidia

wale wataalam *procedure* watakazotumia *under mass valuation or singular valuation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kuandaa hii kanuni tutazingatia mapendekezo ya Mheshimiwa Profesa.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 71  
Ibara ya 72  
Ibara ya 73  
Ibara ya 74

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali la 1  
Jedwali la 2

*(Majedwali yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ASIA P. MINJA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imekamilisha kazi yake.

*(Bunge Lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea Waheshimiwa. Waheshimiwa Wabunge tukae. Mheshimiwa mtoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limeridhia Muswada huu pamoja na marekebisho yake naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge sasa naomba nilihoji Bunge. Naona hoja imekubaliwa.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:** Muswada wa Sheria kwa ajili ya kutunga Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini, Kuainisha Mamlaka na Majukumu ya Mthamini Mkuu wa Serikali, kuanzisha Bodi ya Usajili wa Wathamini, Kuainisha Majukumu na Muundo wa Bodi, Kusimamia na Kudhibiti Taaluma na Kazi za Uthamini Pamoja na Mambo Yanayohusiana na hayo.

*A Bill of an Act to provide for Powers and Function of Chief Valuer of the Government, Establish Valuer's Registration Board, Functions and Management of Board, provide for Regulations and Control of Valuation, Professional and Practice and to provide for the related matters.*

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sina budi kutoa pongezi za dhati kwa Serikali pamoja na wale wote waliohiriki kwa njia moja ama nyingine kuchangia na kuboresha huu Muswada na hasa Waheshimiwa Wabunge kwa ustahamilivu wenu na uzalendo wenu mpaka saa hizi tumeweza kukaa hapa na mkaweza kuchangia vizuri kabisa hadi Muswada huu ukaweza kupitishwa. Kwa hiyo, niwapongeze sana Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kupitia Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake. *(Makofi)*

Kwa hivyo, sasa natangaza kwamba Muswada huu umepitishwa na Bunge na kwamba sasa utapelekwa kwa Mheshimiwa Rais ili atoe kibali.

Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge, tuna matangazo kidogo tu hapa. Kuna Mheshimiwa Joyce Biti Sokombi anatangaza kupotelewa na cheni yake ya mkononi leo akiwa katika maeneo ya Bunge. Kwa hivyo, yoyote ambaye ameokota anaomba amrejeshee. *(Makofi)*

Pia Mheshimiwa Jasson Rweikiza anawaomba Waheshimiwa Wabunge wote wa CCM kuwa kikao cha caucus kimeahirishwa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, niwatakie kila la kheri na Mungu awabariki sana. Sasa naliahirisha Bunge hadi kesho siku ya Ijumaa saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 3.04 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 9 Septemba, 2016, Saa Tatu Asubuhi)*